Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Kumi na Tisa – Tarehe 5 Julai, 2011**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:**

Randama za Makadirio ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

Taarifa ya Mwaka ya Utendaji kazi na Hesabu za Mamlaka ya Elimu Tanzania kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 *(The Annual Report of Activities and Accounts of Tanzania Education Authorities for the Financial Year 2009/2010).*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 175

**Ubovu wa Barabara ya Mombasa – Kivule**

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA** aliuliza:-

Barabara ya Mombasa – Mazizini – Kivule ni mbovu kwa kipindi kirefu sasa na imekuwa kero kubwa kwa watumiaji wa barabara hiyo licha ya kwamba Mheshimiwa Rais aliahidi wakati wa kampeni zake za uchaguzi mwaka 2010 kwamba barabara hiyo itajengwa:-

(a) Je, ujenzi huo wa barabara utaanza na kukamilika lini?

(b) Je, Serikali itawalipa fidia wananchi waiojenga pembezoni mwa barabara ili kupisha ujenzi wa barabara hiyo?

**NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU,TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, ELIMU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eugen Elishiringa Mwaiposa Mbunge wa Ukonga lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, barabara ya Mombasa – Mazizini – Kivule yenye urefu wa kilomita 6 ni mojawapo ya barabara muhimu inayohudumia idadi kubwa ya wakazi wa Kata ya Ukonga na Kivule. Mwishoni mwa mwezi wa Mei mwaka 2011, Halmashauri ya Manispaa ya Ilala ilifanya matengenezo ya dharura kwa kuweka vifusi vya changarawe kwenye barabara hiyo kuanzia eneo la Mombasa hadi Moshi – bar urefu wa kilomita nne kwa gharama ya shilingi milioni 19.5 ili iweze kuhudumia vizuri wananchi wa eneo hilo. Aidha, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Serikali kupitia wakala wa barabara(TANROADS) Mkoa wa Dar es Salaam imetenga jumla ya shilingi milioni 105 kwa ajili ya matengenezo ya maeneo korofi ya barabara hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais, Serikali kupitia Halmashauri ya Manispaa ya Ilala imeshafanya tathimini ya fidia kwa ajili ya kupisha ujenzi wa barabara hiyo ambapo nyumba sabini na nne zilifanyiwa uthamini na gharama ya fidia hiyo kufikia shilingi bilioni 2,209,551,375. Aidha utekelezaji wa ahadi ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kwiango cha lami utafanyika mara fedha hizo zitakapopatikana.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa barabara hiyo anayozungumzia Waziri na kiasi hicho cha shilingi milioni 105 zilikuwa zimetengwa kwa kipindi cha bajeti ya 2010/2011 na hazikuweza kutumika na zimepelekea sasa kupelekwa kwenye bajeti ya mwaka 2011/2012 uliotajwa hapa katika majibu yake.

Je, Waziri anaweza au Serikali inaweza ikawaeleza wananchi wa Jimbo la Ukonga kwamba ni ka nini fedha hizo hazikuweza kutumika kwa kipindi hicho na jambo ambalo limepelekea sasa fedha hizo zipelekewe katika bajeti ya 2011/2012?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana na Naibu Waziri, naomba niongezee tu kwa kusema Wizara ya Ujenzi nayo inachangia kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri katika kusimamia ukarabati wa barabara hii.

Ningependa tu nimWeleze Mheshimiwa Mbunge kwamba pamoja na shilingi milioni 105 ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri amesema tumetenga kwa ajili ya

ukarabati katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara ya Ujenzi kuanzia mwaka 2004 mpaka mwaka jana anaouzungumzia Mheshimiwa Mbunge, tumetumia zaidi ya shilingi nusu bilioni kwa ajili ya ukarabati ya barabara hii, kuchonga tuta, kuweka changarawe, kuweka makaravati (*box caravats*) na hata kuinua matuta.

Na. 176

**Upungufu wa Shule za A - Level Mbulu**

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY** aliuliza:-

Sera ya Serikali ni kujenga shule za sekondari katika kila Kata au hata kila kijiji, sehemu kubwa ya shule hizo zimejengwa kwa nguvu za wananchi. Kuwepo kwa shule hizo katika kila kata kumeleta hitaji la kujenga shule za *A – level* zisizopungua sita katika kila Wilaya.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga shule za *A – Level* katika Wilaya na hasa Wilaya ya Mbulu ambayo pamoja na kuwa na shule za sekondari 33 ina shule moja tu ya *A- Level*?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay Mbunge wa Mbulu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, shule za sekondari za kidato cha tano na sita ni za kitaifa na hivyo ni lazima ziwe za bweni kwa kuwa zinadahili wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali ya nchi isipokuwa shule chache za kutwa zilizopo katika maeneo ya miji.

Mheshimiwa Spika, ili kutimiza adhima ya kuwa na shule za kidato cha tano na sita kwa kila tarafa Serikali kupitia mpango wa maendeleo ya Elimu ya Sekondari Awamu ya II(MES) imelenga kujenga shule mpya na kupandisha hadhi shule zilizopo ili kupanua elimu katika ngazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wilaya ya Mbulu ina shule za sekondari 32 za kidato cha kwanza hadi cha nne na shule moja tu ya kidato cha tano na sita na kwa kuwa azma ya Serikali ni kuwa na shule za aina hii kwa kila tarafa nashauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, ubiani shule zinazoweza kupandishwa hadhi kuwa za kidato cha tano na sita kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa na Wizara yangu. Wizara yangu itakuwa tayari kutoa kibali cha kuanzisha mikondo ya kidato cha tano na sita kwa shule zitakazopendekezwa iwapo zitakuwa zimekidhi vigezo vilivyowekwa.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswalimawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Wilaya ya Mbulu ina tarafa sita na kwa kuwa tayari katika hizo tarafa sita shule tano tayari zina bwalo na mabweni. Je,Serikali iko tayari katika mwaka huu wa fedha kutuma wataalamu wa kutazama kama vigezo hivyo tayari na kupanga bajeti ya chakula na kuleta walimu ili shule hizo zianze, angalau hata shule tatu?

(b) Kwa kuwa hata hii shule moja iliyoko sasa hivi haina walimu hasa wa sayansi, Je katika mwezi huu wa Julai 2011, katika wanafunzi wanaotoka chuoni, Mheshimiwa Waziri, Serikali itapanga walimu wa kwenda kwenye shule hii ya Haidom?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mustapha Akunaay,Mbunge wa Mbulu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la kupandisha hadhi ndani ya Halmashauri ya Mbulu, shule moja au mbili kuwa za *A level* ni suala la Halmashauri yenyewe, namshauri Mheshimiwa Mbunge wafanye mawasiliano na Ofisi ya Ugazuzi Kanda, pale kanda ya kaskazini ili waweze kutuma maafisa wakaguzi pale wakagague shule hizo, kama zitakidhi vigezo, Wizara yangu haina matatizo juu ya kutoa kibali kwa kuanzisha A leve, lakini vigezo vyenyewe ni pamoja na mabweni, kwa sababu kama nilivyosema kwamba shule hizi ni za Kitaifa lazima watoto watoke Mikoa yote ya Tanzania wafike pale, maana yake watakaa pale, watakula pale, watalala pale.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala lingine la walimu wa *A level* katika shule ambayo iko moja pale Mbulu, namuakikishia tu Mbunge kwamba tayari mwezi huu wa Julai 2011, Wizara yangu inafanya utaratibu wa kuwapanga walimu kwenda kuripoti kwenye shule ambazo ziko mbali na maeneo hayo na walimu wataripoti na tayari programu za Wizara kwamba tuna vyuo vingi sana sasa hivi ambavyo vinatoa kada hii ya uwalimu, MUSE, DUSE, TEKU kama ni vyuo binafsi na vyuo vyote nchini vinatoa mafunzi haya ya uwalimu, kwa hiyo tutasambaza walimu kwenye shule za Mbule.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Kwa sababu kwa harakaharaka uzoefu uliopo umeonyesha kwamba ongezeko hili la shule hasa za kidato cha tano na sita kwenye shule kwa ngazi ya tarafa, zina tatizo la kukosa wanafunzi kama ilivyojitokeza Wilaya ya Tandahimba ambayo tayari ilikuwa na shule, lakini ikakosa wanafunzi wa kuingia pale kuanza masomo ya kidato cha tano.

Je, Serikali imejiandaa aje kuongeza ufaulu wa wanafunzi ili shule hizo zisikose wanafunzi na kuacha majengo tu yakiwa yao pale wakati nguvu ya wananchi imetumika?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mhehsimiwa Juma Njwayo, Mbunge wa Tandahimba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la kukosa wanafunzi katika baadhi ya shule za *A level* na hasa limejitokeza sana katika mwaka huu (2011), hilo ni suala la ufaulu wa wanafunzi kutoka kidato cha nne kwenda kidato cha tano.

Sasa suala hili ni suala la kitaaluma ambavyo kama nilivyosema kwamba tamko litakuja hapa Bungeni juu ya ufaulu wa wanafunzi uliokuwa umetokea mwaka huu, lakini mambo mengi yaliyojitokeza huko ni pamoja na upungufu wa vitabu pamoja na walimu ambapo nimesema kwamba Serikali tayari  ina juhudi za kusambaza walimu kwenye shule zetu za kata ili kuweza sasa kubaini tatizo ni nini.

Lakini suala la ufaulu ni suala la baraza la mitihani, tuone na mwaka huu mambo yatakuejе, lakini nawashauri Wabunge wote tuhamasishe vijana wetu wasome, wasichezecheze na wala wasiwe na mambo mengine ya mitahani. Wasiangalie mambo ya miziki na mambo mengine, wasome ili ufaulu uongezeke and then tutapata wanafunzi wengi sana wanaojiunga na *A level*.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. nina swali dogo moja la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi imejitahidi sana ikishirikiana na wananchi kujenga kwa kiasi kikubwa sana kwa maeneo mengi sana hasa ya Katani shule hizi za sekondari za kata na kwa kuwa Serikali inaahidi hapa kwamba inapeleka kwa wingi sana sasa walimu katika shule hivi.

Kikwazo kikubwa kimekuwa mazingira mazuri ya walimu hawa kuishi na hasa nyumba.  Serikali imejiandaa kiasi gani kuhakikisha kwamba pengo kubwa la nyumba za walimu ambazo ndiyo tatizo kubwa la walimu hao kuishi vijijini linazibwa?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Said Nkumba, Mbunge wa Sikonge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anachotaka kujua hapa ni namna gani Serikali imejipanga kuboresha mazingira ya walimu hasa upande wa nyumba.

Jibu ni kwamba katika mpango wa maendeleo ya elimu ya sekondari yani MES II, Serikali katika muda wa miaka minne imejipanga kujenga nyumba 1200 ambazo zitakuwa ni two in one kwa ajili ya kuboresha mazingira ya nyumba za walimu, lakini kwa mwaka huu wa fedha, Serikali kwa kupitia mpango huu itajenga nyumba 264 kwa baadhi ya Halmashauri ambazo zitaonekana zina mazingira magumu sana kwa masuala ya nyumba.

Na. 177

**Hatma ya Mjuzi Mkuu wa Tanzania Aliyeko Ujerumani**

**MHE. HENRY D. SHEKIFU (K. n.y. MHE. SAID MTANDA)** aliuliza:-

Ni dhahiri kwamba mjusi mkubwa aliyepatikana huko Tandeguru Kata ya Mipingo katika Jimbo la Mchinga na kuchukuliwa na Wajerumani miaka mingi iliyopita anachangia mapato makubwa Serikali ya Ujerumani hata sasa:-

(a) Je, ni lini Serikali ya Tanzania itasaini Mkataba na Serikali ya Ujerumani ili nchi yetu hususan wananchi wa Mnyangara na Mipingo waweze kufaidika na mapato yatokanayo na mjusi huyo kama hatuwezi kumrejesha nchini?

(b) Je, Serikali inaweza kueleza ni kwa kiwango gani itanufaika na mkataba huo, hususan kwa wananchi wa Mipingo katika Jimbo la Mchinga?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Mtanda Mbunge wa Mchinga lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika,ni kweli kuwa masalia ya mifupa ya mjusi (*dinosaur*) aliyechimbuliwa mwaka 1912 huko Tendaguru kata ya Mipango katika Jimbo la Mchinga ambapo amehifadhiwa katika Makumbusho ya *Humbolt* huko Ujerumani.

Licha ya kuwepo maombi kutoka kwa wadau mbalimbali ya kurejesha masalia ya mjusi huyo nchini Tanzania, hadi leo bado nchi yetu haijawa na miundombinu inayofaa kama vile majengo na maabara katika makumbusho zetu kwa ajili ya kuhifadhi masalia ya mjuzi huyo. Kwa upande wao uongozi wa makumbusho ya Ujerumani wako tayari kuturuhusu kuyachakua masalia hayo tukiwa tayari.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kuzingatia mazingira hayo, imefanya mazungumzo na makumbusho ya Taifa ya *Humbolt* kuhusu kuanzisha ushirikiano katika masuala ya utafiti na ujenzi wa makumbusho au kituo cha utafiti kwenye eneo la Tendeguru.

Kupitia ushirikiano huo, Tanzania itapata fursa ya kuwafunzo watalaam wake katika fani ya shahada ya uzamili na uzamifu. Mazungumzo hayo yaliyofanyika kupitia ujumbe wa Tanzania uliotembelea makumbusho hayo mwaka jana Aprili, 2010 na rasimu ya mkataba imeshakubaliwa na pande zote mbili na sasa tunategemea ku-sign kwa ajili ya kuanza ushirikiano huwo.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa mjisu huyu ni muhimu sana na anatambulika dunia nzima kwamba ni kati ya mijusi mikubwa kuliko mijusi yeyote mingine akiitwa *dinosaur*. Je,

Serikali pamoja na juhudi za kumrudisha hapa nchini, inachukua hatua gani kulitangaza lile kama eneo la kitalii ambalo eneo hilo lina fukwe nzuri sana ambazo zingeweza kutangazwa hivyo?

(b) Kwa kuwa ziko kumbukumbu nyingi kutoka Tanzania au Tanganyika ambazo zimechukuliwa na Wajerumani, ukiangalia kwenye maeneo ambayo Wajerumani hupenda sana kuishi kama Lushoto, kumbukumbu hizo anazo. Ni muhimu sana kwa historia ya nchi yetu, Serikali inachukua juhudi gani kurudisha kumbukumbu hizi pamoja na huyo *dinosaur?*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli lile eneo la Tendeguru ambalo masalia ya mjusi huyu yaligundulika ni eneo ambalo ni zuri sana kiutalii. Lakini kwa bahati mbaya au tuseme katika mpango wa utangazaji wa utalii mara nyingi huwa tunapenda zaidi kutangaza eneo ambalo limeshakuwa tayari kwa ajili ya watu kwenda kutembelea.

Kwa sasa hivi kilichokuwa kinafanyika ni kuandaa mazingira ya eneo lile liweze kutangazika, mojawapo ni kujenga kituo cha utafiti ambacho ndiyo hicho tumekubaliana na hawa wenzetu wa Makumbusho ya Humbolt Ujerumani kwa ajili ya watu watakaokuwa wanatembelea eneo hilo. Lakini na miundombinu mingine ikiwemo barabara ya kwenda maeneo hayo kwa miaka ya nyuma haikuwa nzuri sana. Kwa sasa hivi haya yamekamilika kwa hiyo tunaingia awamu ya pili ambayo itakuwa ni kutangaza eneo hilo.

Kuhusu kumbukumbu mbalimbali ambazo zimechukuliwa na Waherumani na hata Waingereza na kuzipeleka sehemu mbalimbali. Kimsingi kuna sheria za kimataifa zinazohusu utunzaji wa vitu vya kale zinazoruhusu kuzirejesha vitu vyote vilivyochukuliwa na wakoloni kurejesha kwenye nchi ambazo walivitoa. Moja ya sababu ambayo imekuwa ikitupa tabu ni ukosefu wa eneo la kutunza. Ndiyo maana katika ukamilishaji au upanuzi wa makumbusho yetu tuliamua kutafuta fedha kujenga makumbusho pale Dar es Salaam, *House of Culture* kwa ajili ya kuweza ku-*accommodate* vitu mbalimbali ambavyo vilichukuliwa.

Tunategemea mwezi ujao wa nane kuna vitu ambavyo vimetunzwa kwenye makumbusho ya Nairobi nchini Kenya tutaweza kuvirejesha kwenye makumbusho yetu kwa sababu nafasi ya kuviweka ipo. Kwa hiyo tutaendelea kufanya hivyo kadri nafasi inavyoweza kupatikana.

**MHE. MURTAZA ALLY MANGUNGU:** Nashukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Ningependa kujua Mheshimiwa Waziri hili suala limechukua muda mrefu sana. Ni nini ambacho analiahidi Bunge hili na wananchi wa Mchinga pamoja na Mkoa wa Lindi kwa ujumla mkataba huu utakamilika na watanufaika na masalia haya ambayo ni muhimu kwa nchi yetu?
*(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa kifupi tu ni kwamba tunategemea baada ya kuwa makubaliano yamekwisha kufanyika yaani rasimu imekubalika na pande zote mbili katika muda mfupi usiozidi miezi mitatu utakuwa umesainiwa. Kwa upande wetu sisi tumeshasaini, tumewapelekea na wao waweze kusaini na kwa sababu rasimu tulishakubaliana tunategemea hapatakuwa na tatizo lolote. Kwa hiyo katika kipindi kisichozidi miezi mitatu pande zote tutakuwa tumekamilisha usainiaji.

Na. 178

**Maeneo yaliowekwa mabango ya JWTZ**

**MHE. AMINA ANDREW CLEMENT** aliuliza:-

Katika maeneo ya vijiji vya Unguja Ukuu, Tindini, Kaebona na Kikungwi yamewekwa mabango ya JWTZ tangu mwaka 1965 kwa ajili ya mazoezi ya kijeshi, na mengine yamewekwa mwaka 2010 yenye neno HATARI ili wananchi wasifike katika maeneo hayo wakati huyatumia kwa kilimo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwarudisha wananchi maeneo hayo?

(b) Kama mpango huo haupo, je, Serikali imejipanga vipi kuwalipa fidia?

**MAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina Andrew Clement, Mbunge wa Koani lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, JWTZ lilikabidhiwa eneo hili tangu mwaka 1965 kwa madhumuni ya kufanyia mazoezi ya kijeshi. Jeshi liliruhusu wananchi kutumia maeneo hao kwa kilimo cha mazao ya muda mfupi.

Kutokana na matukio ya ajali zilizotokea katika kambi za jeshi, mwaka 2010 ulitolewa uamuzi wa kuweka mabango yenye neno HATARI katika maeneo ya jeshi ili kutahadharisha umma juu ya hatari zinazoweza kutokea wakati wa mazoezi na pia kuzuia wananchi wasianze kujenga katika maeneo hayo.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali itafanya uchunguzi na kufuatilia watu waliokuwepo wakati eneo hilo linatolewa kwa jeshi mwaka 1965 kubaini kama walilipwa fidia. Aidha, ikibainika kuwa kuna wananchi ambao hawakulipwa fidia wakati eneo hilo linatolewa kwa jeshi, taratibu zitafanywa za kutathimini mali zao na kuwalipwa kwa mujibu wa sheria.

**MHE. AMINA ANDREW CLEMENT:** Asante Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini napenda kumwuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa katika Kijiji cha Tindini kuna nyumba tayari ilishawahi kupigwa mabomu wakati

wa mafunzo ya kijeshi. Je, Serikali itachuikua hadhari gani ili janga kama hili lisiweze kutokea tena?

Swali langu la pili, je Mheshimiwa Waziri je utakuwa uko tayari kufanya ziara ya makusudi twende tukakitembelee kijiji hicho cha Tindini? Asante Mheshimiwa Spika.

**MAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kama tulivyosema tahadhari nyingi zinachukuliwa kwa sasa, zipo tahadhari za muda mfupi muda wa kati na muda mrefu. Nitapata nafasi ya kuelezea vizuri suala hili wakati wa bajeti yangu, kwa sababu nitachukua muda mrefu kuelezea kwa sasa. Isipokuwa tu moja ya tahadhari ni kuhakikisha kwamba maeneo hayo ya karibu na wananchi hawajengi makazi ya kudumu. Ndiyo maana tunapenda kwamba eneo linalozunguka maeneo ya jeshi ya mazoezi au kambi angalau kuwe kuna kilomita moja kati ya maeneo hayo na pale wananchi wanapoishi.

Kuhusu kufanya ziara. Mheshimiwa Spika, niko tayari kufanya ziara hiyo na ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakwenda katika maeneo hayo ili tuweze kutoa maamuzi kwa maslahi ya jeshi letu pamoja na wananchi wa maeneo hayo.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE :** Asante Mheshimiwa Spika kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa tatizo linalowakabili wananchi wa Koani huko Unguja linafanana sawasawa na tatizo linalowakabili wananchi wa Tarime hasa katika vijiji vya Ronzoti na Nyandoto.

Je, Waziri anatoa kauli ipi ili aweze kutatua tatizo hili kwa sababu limewakabili sana wananchi wa Tarime na hususani ujenzi wa shule ya Sekondari ya Nyamisangura na wananchi wananyimwa kufanya fursa shughuli za maendeleo kujenga nyumba za kudumu na ile kambi ya jeshi imekuwa katikati ya vijiji hivyo? Waziri unatoa kauli gani ya uhakika ndani ya Bunge hili tukufu. *(Makofi)*

**MAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, matatizo ya mipaka kati ya makambi ya jeshi na wananchi yako maeneo mengi sana katika nchi yetu. Ni kweli yako kwenye maeneo ya Tarime. Lakini vile vile yako katika maeneo mengine mengi katika nchi yetu. Wizara yangu ilichofanya iliunda Kamati ya kwenda kuchunguza matatizo yote hayo. Tayari wameleta ripoti yao. Yako maeneo ambayo jeshi watakuwa tayari kuyaachia yako maeneo ambayo wananchi itabidi walipwe fidia waondoke. Kwa hiyo, kuna hatua mbalimbali ambazo tutazichukua, na kama bajeti yangu itapita basi tutaeleza hatua ambazo tutachukua kwa maeneo mbalimbali kuhusu migogoro katika nchi yetu.

Na. 179

**Mgogoro wa ardhi kati ya kikosi cha 601**
**KJ na 663 KJ na wananchi**

**MHE. HIGHNESS S. KIWIA** aliuliza:-

Mgogoro wa ardhi kati ya kikosi cha jeshi cha 601 KJ na 663 KJ Ihale ni wa muda mrefu sasa na haujapatiwa ufumbuzi, na kwa hali ilivyo sasa inaweza kuhatarisha usalama wa wananchi kwa sababu kikosi 663 KJ kimeweka mizinga ya kivita kwenye makazi ya wananchi wa Nyagungulu mwaka 1978 wakati wa vita ya Uganda na Tanzania na mara baada ya vita waliiondoa na kuirudisha tena tarehe 15/12/2009 bila taarifa na kuwataka wananchi wa maeneo hayo kusimamisha shughuli zao zote kwa ajili hiyo, bila kujali kwamba sialaha hizo zinaweza kusababisha madhara kwa wananchi.

(a) Je, Serikali iko tayari kuliagiza jeshi kuondoka kwenye makazi ya wananchi wa Nyagunguru na kuondoa mizinga yake na kuwaruhusu wananchi zaidi ya 800 waendeleze makazi yao?

(b) Je, Serikali iko tayari kuunda Kamati maalum ikishirikisha wananchi na viongozi wa maeneo ya Buyombe, Hukobe na Ilemela katika kuangalia upya mipaka ambayo imelalamikiwa ili kutatua tatizo hilo?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Samson Highness Kiwia, Mbunge wa Ilemela lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna mgogoro wa ardhi kati ya jeshi na wananchi wa vilima vya Ilemela. Mgogoro huo umeanza baada ya watendaji wa Idara ya Ardhi kutoa vibali vya ujenzi kwa wananchi katika eneo ambalo hutumiwa na jeshi katika ulinzi wa anga na majini kwa jiji la Mwanza ikishirikiana na vilima vya Bugando na Nyamshana. Aidha, eneo hilo pia ni kituo cha ulinzi wa uwanja wa ndege ikishirikiana na vilima vya Nyamilolelwa na Ihale. Kituo hiki ni muhimu sana kwa ulinzi wa jiji na uwanja wa ndege, kukiondoa kuna maana ya kuacha jiji la Mwanza na uwanja wa ndege wake bila ulinzi. Kutokana na hali hiyo:-

(a) Serikali haiko tayari kuondoa kituo hicho kwa manufaa ya ulinzi wa wakazi wa jiji la Mwanza.

(b) Serikali imechukua hatua ya kuunda Kamati ya kufuatilia mgogoro huo kupitia kwa Mkuu wa Wilaya ya Ilemela. Inashauriwa wananchi waelimishwe kuhusu umuhimu wa ulinzi wa nchi. Wizara yangu inaangalia uwezekano wa kuwalipa fidia wakazi wa eneo hilo baada ya majengo yao kuthaminiwa.

**MHE. HIGHNESS S. KIWIA:** Nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa mgogoro huu sasa ni wa muda mrefu na ni dhahiri kwamba hata majibu ya Mheshimiwa Waziri kwa upande mwingine haiendani sambamba na hali halisi ilivyo.

Wananchi wa maeneo hayo sasa imefikia hatua ambayo hata ukuta wa choo hawawezi kuujenga na ni dhahiri kwamba Mkuu wa Wilaya hata ukuta wa choo ukianguka hawawezi kuujenga na ni dhahiri kwamba hata Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa

Mkoa wameshindwa kuleta muafaka katika mgogoro huu wa muda mrefu na hali ya wananchi wa maeneo hayo inazidi kuwa mbaya.

Ningeomba kufahamu kama Mheshimiwa Waziri sasa atakuwa tayari kuambatana na mimi katika maeneo aliyoyataja ili kuweza kupata muafaka unaotosheleza kulingana na hali ya wananchi wa maeneo hayo?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwamba Wizara yangu iliunda Kamati hiyo Kamati imeenda katika maeneo yote ya jeshi ambayo yana migogoro, wametayarisha ripoti yao na wametoa mapendekezo. Baadhi ya mapendekezo yale yanahitaji fedha kwa sababu kuna fidia ambayo inahitajika.

Kwa hivyo nilichosema ni kwamba tutaratibu taarifa ya Kamati ile, tutachukua ushauri wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Ilemela ili hatimaye tuweze kutatua mgogoro huu kwa maslahi ya jeshi na ulinzi wa maeneo yale pamoja na wananchi wanaoishi pale.

Kwenda kutembelea pale siyo tatizo naweza nikamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba nikiwa na Wajumbe wa ile Kamati iliyofanya ile kazi kutoka Wizarani pamoja na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya niko tayari kutembelea eneo lile ili kujionea mimi mwenyewe na hatimaye tuweze kutoa maamuzi kwa maslahi ya pande zote.

Na. 180

**Gharama ya kuunganisha umeme**

**MHE. DKT. SEIF S. RASHIDI** aliuliza:-

Ingawa mpango wa kusambaza umeme vijijini umeshaanza lakini asilimia 36 – 39 ya wananchi wana pato la chini ya dola 2 za Marekani kwa siku, kiwango ambacho hakitoshi kuwawezesha kufikia lengo la kuunganisha umeme:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa nafuu ya gharama za kuunganishwa umeme ili wale wa pato la chini kabisa wakiwemo walioomba huduma hiyo kutoka Rufiji waweze kuunganishwa umeme kwa gharama nafuu?

(b) Kwa vile umeme wa Somangafungu ni MW 7.5 kwa Wilaya ya Rufiji na Kilwa, lakini hadi sasa matumizi ni MW.2.5.

Je, Serikalii inaweza kugharamia usambazaji wa umeme kutoka Ikwiriri hadi Mloka na kutoka Nyamwage hadi Nambanjo ili kutimiza kusudio la kuwapa umeme sehemu ambazo bomba la kusafirisha gesi kutokea Kilwa hadi Dar es Salaam linapita?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Seif Selemani Rashidi, Mbunge wa Rufiji lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali katika jitihada za kutoa nafuu ya gharama za kuunganishiwa umeme wananchi, inatoa punguzo la kuunganisha umeme katika baadhi ya miradi inayofadhiliwa na washirika mbalimbali wa maendeleo pamoja na miradi inayofadhiliwa na wakala wa Nishati Vijijini (REA) na kutekelezwa na wakandarasi mbalimbali kama *(tumkey projects).*

Baadhi ya maeneo yaliyofaidika na unafuu huu ni pamoja na jimbo la Rufiji la Mheshimiwa Mbunge, ambapo wananchi wanaohitaji umeme wamepewa punguzo maalumu la kulipia asilimia 18 tu ya gharama za kuunganishiwa umeme kwa ajili ya kodi ya VAT. Aidha, TANESCO inaruhusu kulipia gharamia za kuunganishia umeme majumbani kwa awamu tatu kwa miezi mitatu mfulululizo ili kila mwenye nia ya kuunganisha umeme nyumbani kwake aweze kufanya hivyo.

(b)Mheshimiwa Spika, Serikali imedhamiria kuhakikisha kwamba, umeme unaozalishwa katika kituo cha Somangafungu unatumika wote. Kwa sasa uwezo wa uzalishaji wa umeme Somangafungu ni MW. 7.5 na matumizi ya umeme maeneo hayo kwa sasa ni MW.2.5. Gharama za kupeleka umeme Mloka kutokea Ikwiriri umbali wa kilomita 146.5 inakadiriwa kufikia shilingi bilioni 5.1 na kupeleka umeme Nambunjo kutokea Nyamwage umbali wa kilomita 19 inakadiriwa kuwa shilingi milioni 656.

Serikali imepokea ombi hili na inafanya tathmini ya kuangalia namna bora ya kupatia utekelezaji miradi hii kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa. Ninamuahidi kumpatia Mheshimiwa Mbunge matokeo ya tathmini hiyo kadri itakavyopatikana.

**MHE. DKT. SEIF S. RASHIDI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Ya kwanza kwa sababu suala lilikuwa ni kutoa unafuu wa gharama za kuunganishiwa na majibu yametaja miradi ambayo ina ukomo.

Je, baada ya miradi hiyo kipindi chake kwisha Serikali itatoa au inaendelea kutoa unafuu upi kwa wale ambao bado hawajaanza kuunganishiwa umeme? *(Makofi)*

Swali la pili ni kutaka kujua na kupata kauli ya Serikali ni lini sasa maeneo ya kutokea Ikwiriri hadi Mloka yatapatiwa umeme. Tathmini kama ilivyoelezwa na gharama zake ni vizuri kuelewa. Lakini ni jambo zuri zaidi kwa Warufiji kuweza kufahamu Serikali itajipanga angalau kwa awamu na kwa hatua ipi na ni lini mradi huo unaweza ukaanza kutekelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa bahari nzuri miradi hii mimi naifahamu vizuri, Tumefanya ziara pamoja na Mheshimiwa Dkt. Seif mwenyewe kwenye jimbo lake mwezi wa kwanza na tatizo la kuunganishwa umeme tunalifahamu vizuri.

Mheshimiwa Spika, miradi hii iko kwenye mikoa 16 na baadhi ya miradi mingine ikiwa Ukerewe, Simanjiro kule kwa Mheshimiwa Ole-Sendeka na kadhalika. Lengo lake ni kutoa unafuu kwa wale watakaounganisha umeme wa kwanza, wengine wanakuwa wateja wa kwanza 200, wengine 300 wengine 250 kulingana na ukubwa wa ule mradi wenyewe.

Sasa pale Rufiji waliunganishiwa umeme kwa kupitia utaratibu huu. Ni wateja 816, lazima tuwe na ukomo kwa sababu ni kama ka-*promotion* fulani hivi kwa muda fulani siyo hauwezi kuwa moja kwa moja *endless.*

Kwa hiyo tumetoa nafuu hiyo nadhani wateja waliokusudiwa ni 1,200. Lakini kwa sababu mradi ulichelewa kuanza na wateja hawakuitikia *promotion* ile ilisitishwa kidogo. Lakini Serikali itaangalia uwezekano wa unafuu kulingana ufadhili uliopatikana kuangalia kama kuna wateja wengine zaidi ya hao 816 wa upande wa Dkt. Seif wanaweza kuunganishwa umeme huo.

Hili swali la pili, Mheshimiwa Spika, pia tumelizungumza jimboni kwake suala la kutoka Ikwiriri kwenda Mloka. Mloka pana uwekezaji mkubwa wa hoteli za kitalii. Lakini ni mbali ni kilomita 100, pana kama gharama ya bilioni 3 za kupeleka umeme huo.

Tutafanya kulingania kujua kama je, bilioni 3 hizo zinaleta *commercial viability* au kama tutapeleka majenereta na ndiyo maana kwenye swali langu majibu ya swali la msingi nimesema tutaangalia namna nafuu kama ni kutoka Ikwiriri ama kupeleka umeme kutokea vyanzo vingine. Lakini suala hili linafanyiwa kazi, tunalifanyia tathmini nitamjibu Mheshimiwa Mbunge kadri tunavyopata majibu.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Kwa kuwa hata wateja ambao tayari umeme upo kwenye maeneo yao na wana uwezo wa kulipa gharama za kuingiziwa umeme. Lakini wanakaa muda mrefu toka wanapotuma maombi kuingiziwa umeme. Je, tatizo ni nini na kama kuna tatizo litaisha lini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, tatizo la kuunganisha umeme hata pale umeme ulipofika ni tatizo ambalo tumekuwa tunalishughulikia kwa muda mrefu. Tumewahimiza *TANESCO* lina sura nyingi, lina sura

ya vifaa kupatikana. Lakini pia lina sura ya umeme ule uliyofika pale uwezo wake wa kugawa. Mara nyingine unafikisha pale umeme lakini mmeweka *transforma* ya 50 KV.

Mheshimiwa Spika, mkifika pale inaonekana kwamba wateja wengi wameitikia mahitaji ya umeme kwa hiyo, *transformer* ile inahitajika ipatikane *transformer* kubwa zaidi, inawezekana kwa kipindi hicho haipo inabidi itafutwe.

Kwa hiyo, ni matatizo ambayo tumeyapokea, *TANESCO* tumeshawaagiza wayafanyie kazi ili pale ambapo umeme, wateja wanaonekana ni wengi, wote wapatiwe umeme kwa kadiri itakavyowezekana.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kuniona. Tatizo la Mloka ni sawasawa na tatizo la Somanga Fungu. Wakati Mheshimiwa Rais, anazindua mradi wa Somanga Fungu, alitoa ahadi ya kuwa wananchi wa Somanga Fungu, waunganishiwe umeme bure, lakini mpaka sasa hivi hawajaunganishiwa.

Mheshimiwa Spika, Je, Mheshimiwa Waziri anatoa tamko gani?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Nyongeza la Mheshimiwa Riziki Lulida kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hoja ya Serikali, haikuwa kuunganisha umeme bure, hata kwa pale Somanga Fungu mpaka Nangurukuru pale, Njia Nne na Kilwa yenyewe yote kwa maeneo ya pale. kwa sababu ule mradi wote ndio huo pamoja na huu wa Rufiji mpaka Bungu, utaratibu ni uleule kwamba kwa baadhi ya wateja watakaounganisha umeme kwanza, watapata nafuu ya *VAT,* ambayo ni 18% ya gharama zote.

Kwa kiasi cha sasa ambacho ni kama laki nne na kitu hivi kwa ggharama, *VAT* yake inakuwa kama 72,000/=. Kwa hiyo, utaratibu huo ambao ulikuwa umekusidiwa mpaka kule Mtwara, ni kulipa kiasi cha 70,000/= mpaka 73,000/= ili uweze kuunganishiwa umeme. Unalipa *VAT* peke yake lakini sio iwe ni bure kabisa.

Na. 181

**Kusuasua Kwa Mradi Wa Umeme Ikimba – Bukoba Vijijini**

**MHE. DEOGRATIUS A. NTUKAMAZINA K.n.y. MHE. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza:-

Mradi wa kupeleka umeme eno la Ikimba, Bukoba Vijijini, Kata za Kemondo, Katerero, Ibwera, Buterankuzi, Rubale, Izimbya, Buturage, Nyakimbili, Kaibanja na Katoro ulishaanza tangu mwishoni mwa mwaka 2010, lakini bado unasuasua:-

(a) Je, kwa nini kazi hiyo inakwenda taratibu sana?

(b) Je, mradi huo unategemea kukamilika lini?

(c) Je, kuna mpango gani wa kuwasaidia wananchi ambao hawana uwezo wa kuingiza umeme katika nyumba zao hata umbali wa mita 10 kutoka katika njia ya umeme iliyojengwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huu unafanywa na *REA* na unahusisha kupeleka umeme katika Kata za Kemondo, Katerero, Ibwera, Buterankuzi, Rubale, Izimbya, Buturage, Nyakimbili, Kaibanja na Katoro. Mradi huu umechelewa kutokana na kuchelewa kufunguliwa kwa barua za malipo *(Letters of Credit).* Hata hivyo, malipo kupitia barua hizo yameshakamilika na kwa sasa tayari utekelezaji wa mradi huu umeanza. Hatua zilizofikiwa hadi sasa katika utekelezaji wa mradi ni pamoja na uchimbaji wa mashimo na kusimamisha nguzo za umeme wa msongo wa *Kilovolt 33* kwa 30% ya mradi ulivyokusudiwa. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2011 kwa makubaliano yaliyofikiwa baina ya *REA* na Mkandarasi.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali imetoa ruzuku kwenye mradi huu ya gharama za kuunganisha umeme. Wateja watakaounganishiwa umeme watatakiwa kulipia gharama za fomu pamoja na gharama ya ongezeko la thamani *(VAT)* ya gharama za kuunganishiwa umeme tu.

**MHE. DEOGRATIUS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

(i) Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mradi huu mazao au mimea ya mazao mengi ya wananchi yamefyekwa ili kupisha ujenzi wa njia za umeme. Je, wananchi hawa watalipwa fidia kiasi gani na ni lini?

(ii) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo la umeme la Bukoba Vijijini ni sawa na lile lililopo Wilaya ya Ngara. Wananchi wa Ngara wanahamu ya kusikia ni lini Serikali italiwezesha Shirika la umeme la *TANESCO* ili liweze kuupatia umeme mradi wa *Kabanga Nikel,* mradi ambao ni tajiri sana ni wa pili duniani baada ya ule wa Canada?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ntukamazina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, popote ambapo tunaweka miradi hii ni lazima pawe na kazi fulani inayohusisha kuweka njia za umeme. Sasa kama pana mazao na kadhalika, huwa yanafyekwa lakini utaratibu wa fidia upo, ambao unasimamiwa na *REA* kwa nchi nzima. Kwa hiyo, kusema kweli kabla ya utekelezaji wa miradi hii ni lazima suala la fidia liwe limejadiliwa na liwe lim ekubaliwa na wananchi pamoja na viongozi, wawakilishi wa wananchi kwa maeneo yale.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kama suala hili halijashughulikiwa na mradi unakaribia kutekelezwa ninamsihi Mheshimiwa Mbunge awasiliane na wananchi wake katika upande ule unaotekeleza mradi huu ili na mimi nipate taarifa hiyo, tuangalie suala hili la fidia litakavyokamilishwa kabla hatuyafika hatua za utekelezaji au kukamilika kwa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, katika swali la pili ni kweli kabisa kwamba pale pana mgodi wa *Kabanga Nikel* ambao ninadhani utakuwa ni mradi mkubwa kabisa wa *nikel* kwa Afrika nzima. Mahitaji yake ya umeme ni kama *Mega Watt 15.* Tumeshakubaliana na muendelezaji wa mradi huo kwamba atakapokuwa anaweka mradi wake wa umeme pale, kwa ajili ya mgodi wa Kabanga *Nikel,* ni lazima ahudumie vijiji vinavyozunguka.

katika eneo lile mradi tunaoutarajia ni mradi wa maji wa Rusumo ambao ni *Mega Watt 90* kwa Rwanda, Burundi na Tanzania 30, 30, sasa kwa maeneo yale yote *mega watt* zile 30 zinazotokana na Rusumo, zinatarajiwa zihudumie wilaya ya Ngara, maana ndiko unakoingia kwanza na wilaya za maeneo mengine yote. Kwa hiyo nadhani hili la Rusumo ambalo tumekaa Kigali juzi tumekubaliana, ndio ufumbuzi mkuu wa matatizo ya umeme Ngara.

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, umeme hata wakati unatoka Dodoma kupelekwa Makao Makuu ya Wilaya ya Bahi, ulipita barabarani ukiacha vijiji na vijiji hivyo viliahidiwa kuwa umeme huo ungeshuka, na kwa kweli baadhi ya vijiji umeme umeshuka, isipokuwa katika kijiji cha Kigwe na Kijiji cha Mpamantwa. Je, Mheshimiwa Waziri, atawahakikishia wananchi ambao tayari waliandaliwa wa kijiji cha Kigwe na Kijiji cha Mpamantwa kwamba umeme huo utashuka hivi karibuni?

**SPIKA:** Swali jipya kabisa, lakini mradi tuko karibu hapa bila ya shaka utalijua. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Badwel, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 2009 Septemba, mimi nilikwenda Bahi kukagua mradi huu wakati ule ulikuwa unasuasua.
Tulikwenda na wataalamu wa *TANESCO* na baada ya ziara ile tukapata ufumbuzi wa kufikisha umeme Bahi, Makao Makuu. Maelekezo yalikuwa ni kwamba, popote ambapo mradi ule utapita na kuna vigezo vya kiuchumi na vya kijamii vya ku-*justify* kwamba umeme ule ufike, tulikubaliana kwamba umeme utashuka. Mheshimiwa Mbunge, naomba nikuhakikishie tu kwa sababu, ahadi ile ilitolewa na Serikali na kama haijapata utekelezaji, tutakwenda tena Kigwe na tutawahimiza *TANESCO* ili lipate utekelezaji kwa sababu ni sehemu ya ahadi ya utekelezaji ndani ya mradi huo.

Na. 182

**Chanzo Cha Umeme Wa Maji – kilombero**

**MHE. DKT. MCH. GETRUDE P. RWAKATARE** aliuliza:-

Wilaya ya Kilombero ina chanzo kikubwa sana cha umeme wa maji huko Boma Ulanga na kinaweza kuzalisha umeme wa *Megawatts 2000.*

Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza chanzo hicho?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dokta Mchungaji Getrude Pangalile Rwakatare, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, chanzo kikubwa kabisa cha umeme unaotokana na nguvu ya maji karibu na Boma Ulanga katika Mto Kilombero, kitatokana na kujengwa kwa Bwawa kubwa pale Kingenenas katika mto Kilombero, umbali wa karibu kilomita 35 Mashariki mwa Ifakara. Mradi huo unahusisha kujenga mitambo ya kuzalisha umeme kutokana na maporomoko ya shuguri *(Shuguri Falls)* katika Mto Kilombero.

Mheshimiwa Spika, utafiti wa kitaalamu wa chanzo hiki cha umeme, upo kwenye ripoti ya mwaka 1984 iliyofanywa na kampuni ya *Norconsult* ya *Norway* kwa niaba ya *RUBADA*, ambao uliitwa *Rufiji Basin Hydropower Master Plan*, yanaonesha kwamba mradi huu unahusisha kujenga miundo mbinu *(transfer canal)* ya kuhamisha maji ya mto Ruaha Mkuu *(Great Ruaha River)* baada ya maji hayo kuzalisha umeme pale Kidatu na baada ya kupita mashamba ya sukari ya Kilombero na kuyapeleka mto Kilombero ili kuongeza wingi wa maji katika mto Kilombero na hivyo kuzalisha umeme mwingi zaidi kutokana na maporomoko pale Shuguri *(Shuguri Falls).*

Mheshimiwa Spika, mradi unaotokana na maporomoko ya Shuguri *(Shuguri Falls)* haumo katika miradi iliyomo katika mpango kabambe kwa sasa kwa sababu ya gharama kubwa ya mradi inayohusisha ujenzi wa bwawa kubwa la maji, kuhamisha maji ya mto Ruaha Mkuu kwenda mto Kilombero na athari nyingine za kimazingira. Miradi

inayoingizwa kwenye mpango kabambe ni ile iliyo na unafuu zaidi wa gharama katika utekelezaji wake *(Least Cost Development Plan).* Na kadiri miradi yenye unafuu zaidi inapotekelezwa ndiyo hivyo na mingine kama huu wa maporomoko ya Shuguri inapata nafasi ya kuingia kwenye orodha ya mpango kabambe nafuu.

**MHE. DKT. MCH. GETRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, asante. Nashukuru kwa majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kilombero ina vyanzo viwili vya umeme Kidatu na Kihansi, ambavyo vinapita katika vijiji vyote au kata mbalimbali za Wilaya hiyo ya Kilombero. La kushangaza sana ni kwamba Kata Muhimu sana za uzalishaji wa kilimo ziko gizani. Zinabaki kuangalia waya na nguzo za umeme zikipita pembezoni ya nyumba zao.

Je, Mheshimiwa Waziri, anawaambia nini wananchi hawa au anatoa ahadi gani kwao ili na wao waweze kufaidi umeme huu? *(Makofi)*

(i)Mheshimiwa Spika, wenzetu ambao wanakaa katika mikoa, mahali ambapo kuna migodi mbalimbali, hupewa mrahaba mwaka hadi mwaka. Sisi wananchi wa Kilombero, tumekuwa tukilinda vyanzo vya maji haya na mifugo ili hewa isiweze kuharibu na hakika kabisa sisi wenyewe hatupati hata senti moja.

Je, Mheshimiwa Waziri, atawaambia nini wananchi wa Kilombero, kwamba wao pia watapata huu mrahaba kuanzia sasa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Dokta Mchungaji Getrude Rwakatare, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli kwamba pale pana Kidatu na Kihansi ambavyo kwa ujumla vinazalisha kama *Mega Watt 300* katika mfumo wa gridi, pale tunapokuwa na uzalishaji wote wa ujumla. Ni umeme ambao ni kama 30% ya mahitaji yetu yote.

Mheshimiwa Spika, lakini umeme unapozalishwa Kidatu na unapozalishwa Kihansi, ukitoka pale unaondoka katika mfumo wa *high tension cables.* Kwa hiyo, mara nyingi kusema kweli utakaa pale utauona umeme unapita juu, lakini ni umeme wa *high tension.*
Sasa wakati wa kutengeneza miradi hiyo, tulikuwa hatuna vigezo vya kushusha umeme ule, lakini kwa sasa hivi kama alivyosema Mchungaji Lwakatare ni kweli, tulipokwenda Kihansi tumekuta kwamba maeneo yanayozunguka kwa miaka hii 15 – 20 yameendelea na yamebadilika sana na kuna umuhimu sasa wa kutoka pale, kuushusha umeme kutoka kwenye ile *high tension cable,* kuuleta kwenye *low tension* kwenda kwenye *sub-stations* na *transformer* zake ili wananchi wapatiwe umeme.

Mheshimiwa Spika, suala hilo tumewaambia *TANESCO* wafanye tathmini ya maeneo yale ambayo wanadhani kazi hiyo itafanyika, sio kazi ndogo, sio kuuona tu ule umeme ukasema utashuka, hapana! Sio kazi ndogo, lakini inawezekana na tumewasihi *TANESCO* wafanye kuangalia gharama zinazostahili ili wananchi hawa wapate huduma hiyo kwa sababu ya ujirani wao na mradi.

Mheshimiwa Spika, hili la pili. Sheria inayosimamia upatikanaji wa mrahaba kutokana na madini ni tofauti. Kwenye sheria ya umeme hatuna vigezo hivi. Lakini kusema kweli ninakubaliana na Mheshimiwa Lwakatare, kwamba pale ambapo maeneo yanayozunguka yanalinda vyanzo vya maji, maji yale yanachangia kwenye upatikanaji wa umeme. Labda tuangalie kama katika utaratibu huu wa ukusanyaji wa mapato yanayotokana na umeme, hawa wanaosimamia vyanzo hivi vya maji wanaweza kunufaika kidogo. Mimi nadhani nimelipokea, nitawapa wenzangu ili kwa pamoja tulifanyie kazi na tuone namna tutakavyolileta kwenye Bunge lako.

Na. 183

**Ahadi ya Kivuko Cha Pili Wilayani Pangani**

**MHE. SALEH A. PAMBA** aliuliza:-

Wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010, Mheshimiwa Rais, aliahidi kuipatia Wilaya ya Pangani Kivuko cha pili cha mto Pangani:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo:-

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saleh Ahmed Pamba, Mbunge wa Pangani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais, aliyoitoa wakati wa Kampeni ya Uchaguzi Mkuu 2010, Wizara ya Ujenzi imekamilisha kazi ya ununuzi wa kivuko kipya cha Pangani chenye uwezo wa kubeba tani 50, yaani magari madogo 8 na abiria 130. Kazi ya ujenzi wa kivuko hiki kipya cha *MV Pangani,* imefanywa na *Johs Gram Hanssen AS* ya Denmark kwa gharama ya *Euro 1,055,000* sawa na shilingi bilioni 2 za kittanzania. Fedha hizi ni za mkopo kutoka Benki ya Dunia na kivuko hiki kimeanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, aidha katika mwaka wa fedha 2011/2012 Wizara imetenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa kivuko cha *MV Pangani I,* ili wananchi wa Pangani waendelee kuwa na huduma ya vivuko viwili wakati wote.

**MHE. SALEH A. PAMBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina masali mawili ya nyongeza.

(i)Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *MV Pangani I* kimeegeshwa kwa muda wa miezi 8 bila kufanyiwa ukarabati. Je, Mheshimiwa Waziri, atawaeleza nini wananchi wa Pangani kwamba ukarabati wa *MV Pangani I* utaanza lini?

(ii) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ada za kivuko kwa *MV Pangani II* ziko juu ukilinganisha na gharama za vivuko vingine hapa nchini. Kwa mfano, magari madogo ni 5,000/= wakati *MV Kigamboni* ni 1,000/=. Mtu mzima ni 200/= wakati *MV Kigamboni* ni 100/=.

Je, Mheshimiwa Waziri, atakubaliana na mimi kwamba ipo haja ya kuziangalia gharama hizi ili kuwasaidia wananchi wenye kipato kidogo wa Jimbo la Pangani? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Saleh Ahmed Pamba, Mbunge wa Pangani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwamba Wizara ya Ujenzi imeshaandaa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya ukarabati wa *MV Pangani I.* Kwa hiyo, katika Mwaka wa Fedha 2011/2012 kazi hiyo tutaifanya.

Mheshimiwa Spika, lakini pili kuhusu ada ya kivuko kuwa ni kubwa, naweza kuelewa Mheshimiwa Mbunge, *concern* yake kuwajali wapiga kura wake. Lakini ningemuomba

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Kwa kuwa, ahadi ya kivuko cha mto Pangani inafanana na ahadi ya kupewa kivuko cha kutoka Mtwara kwenda Msanga Mkuu.

Je, ni lini pia ahadi hii itatekelezwa?

**SPIKA:** Hebu rudia, Mtwara kwenda wapi?

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Mheshimiwa Spika, Msanga Mkuu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hasnain, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sio tu kivuko cha Msanga Mkuu, lakini vile vile tuna kivuko cha Rusumo, kivuko cha Kilambo, vyote hivi mikataba ya kuleta vivuko hivyo tulisaini mwezi Juni, mwaka 2010 na ujenzi umeendelea vizuri na unakamilika wakati wowote katika kipindi cha mwaka huu na miradi hii yote iko kwenye Ilani ya Uchaguzi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge ajjue kwamba tunaijali sana. *(Makofi)*

Na. 184

**Serikali Kuunda wakala wa Barabara Vijijini**

**MHE. DKT. BINILITH S. MAHENGE** aliuliza:-

Barabara za Vijijini ndio injini ya uchumi wa nchi, na mtandao mkubwa wa barabara za vijijini unaosimamiwa na Halmashauri za Wilaya ambapo mafanikio yake ni kidogo sana kutokana na uchache wa wataalam:-

Je, ni kwa nini Serikali isiunde wakala wa Barabara Vijijini (*Rural Roads Agency)* kama iliyo kwenye sekta ya umeme na barabara za mikoa ili kuleta ufanisi zaiid?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI - (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Binilith Satano Mahenge, Mbunge wa Makete kama ifuatavyo,

Ni kweli kwamba mtandao wa barabara za vijijini wenye urefu wa zaidi ya kilometa 46 unaosimamiwa na Halmashauri za Wilaya, na miji ni mtando muhimu sana kwa vile ndiyo unaohudumia wananchi walio wengi nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikilifanyia kazi suala la kuanzisha chombo mahususi cha kusimamia barabara vijijini kwa kipindi kirefu sasa ikiwa ni pamoja na kutafuta vyanzo vya mapato kwa barabara hizo ili chombo hicho kikianza kifanye kazi kwa ufanisi. Tayari wataalam kutoka Wizara yangu na TAMISEMI wameshaanza kukutana na kuliangalia suala hili kwa kina.

**MHE. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, namhsukuru Waziri kwa majibu yake...

**SPIKA:** Hama microphone yako haisemi vizuri, naomba wataalam munagalie ule mstari kila wakati unaleta matatizo.

**MHE. BINILITH S. MAHENGE:** Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na ninalo swali moja la nyongeza, kwa kuwa Serikali imekiri umuhimu wa kuanzisha wakala wa barabara vijijini, na Serikali pia inakiri kwamba suala hili limechukua muda mrefu ikiwa ni pamoja na kutafuta fedha za kusimamia chombo hiki.

Je, Serikali haioni busara kuanzisha chombo hiki haraka iwezekanavyo ili kisimamie fedha zinazokwenda kwenye Halmashauri sasa hivi ambazo ni nyingi mathalani katika kipindi cha miaka mitano iliyopita TAMISEMI wamepeleka zaidi ya bilioni mia tatu, ambapo chombo hiki kingeanzishwa kingeweza kusimamia hizi barabara vizuri zaidi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE)**: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Binilith Mahenge, Mbunge wa Makete kama ifuatavyo, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi Serikali sasa hivi kazi yake kubwa ni kutafuta vyanzo vya mapato vya uhakika vya taasisi hiyo, wasiwasi wetu tukikurupuka kuanzisha hii taasisi sasa hivi tutapata shida namna ya kukiendesha. Naomba tu Mheshimiwa Mbunge avumilie na sisi wenyewe tumeona umuhimu wa kuwa na chombo hicho aiache Serikali iwe na uhakika kabisa wa chanzo cha pesa cha uhakika kwa ajili ya kuendesha chombo hicho.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, asante kwa kuniona, Serikali imefikia wapi mpango wa kujenga barabara ya lami, kuelekea hifadhi ya taifa iliyopo Ruaha Iringa ambayo ni ya pili kwa ukubwa nchini?

**SPIKA:** Hilo swali ni jipya kabisa, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI - (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu suala la ujenzi wa barabara kutoka Iringa kwenda mbuga au hifadhi ya taifa ya Ruaha, ni suala ambalo tumeliangalia kwa kina kama Wizara ningemuomba Mheshimiwa Mbunge alilete kama suala mahususi ili tuweze kumjibu kinaganaga na wananchi waweze kufaidika kwa majibu yetu.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha na maswali yamekwisha, sasa maswali ya nyongeza mkiyauliza mapya kabisa mjue majibu hamtapa kwa sababu hawakujiandaa kwa mtindo huo. Kwa mfano swali hili la mwisho, huyu anauliza sera ya kuanzisha agency ya barabara vijijini, sasa huyu anauliza barabara specific haya ni maswali mawili tofauti, kwa hiyo ni vizuri tukajifunza namna hiyo.

Waheshimiwa Wabunge tunao wageni wanafunzi wtu, tunaona wanafunzi 70 na walimu 8 kutoka shule ya msingi ya Engosejui Arusha, sijui nimetamka sawasawa hapo, naomba wasimame walimu na wanafunzi wa shule hiyo kutoka Arusha, asante sana karibu sana na msome vizuri, mkae. Tunao wanafunzi wengine 70 na walimu 5 wa shule ya msingi mazoezi Chang’ombe Dar es Salaam, asante sana karibuni sana na nyie mkazane kusoma.

Tuna wanafunzi 13 kutoka Chuo Kikuu cha Sauti Mtwara, na walimu wao, asante sana kwa kutoka Mtwara mpaka kuweza kuona shughuli zetu sisi. Tuna wanafunzi 15 wa mwaka wa kwanza kutoka Chuo cha Biashara CBE, Dodoma hao wenyeji wetu hao tena majirani wenyewe wako huku nyuma, asante sana msome kwa bidii mmalize mkafanye yanayokusudiwa.

Tuna wanafunzi wengine 31 wa Chuo Kikuu cha Tumaini, hao 31 kutoka chuo cha Tumaini wako wapi, asante sana, karibuni sana, sasa sijui Sebastain Koroa, na

Lushoto Tanga ni nani sasa peke yake, aah! Basi asante sana karibuni sana na mfanye bidii kusoma watu wanawategemea kuwa responsible leaders wa kesho kutwa asante sana.

Ninayo matangazo machache ya kazi, Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Abdulkarim Shaha, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo kutakuwa na kikao saa saba mchana katika ukumbi Na. 231. Na

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Faustine Ndugulile, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba mchana watakuwa na kikao chumba 219, kwa hiyo hizo ndiyo shughuli za leo tumetangaza. Katibu tunaendelea.

## KAULI ZA MAWAZIRI

### KUHUSU KUENDELEA KUTUMIA MIZANI YA RULA (*STEEL YARD)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, toleo la mwaka 2007 Kanuni namba 49, naomba kutoa kauli ya Serikali kuhusu suala la kuendelea kutumika kwa mizani ya rula, ijulikanayo kama steel yard kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, jana tarehe 4 Julai, 2011, Mheshimiwa Alphaxard Kangi Ndege Lugola, Mbunge wa Mwibara, akiomba muongozo wa Spika alieleza masikitiko yake kuhusu matumizi ya mizani ya rula ijulikayo kama steel yard katika kupimia mazao ya wakulima hasa zao la pamba katika msimu huu wa 2011/2012, kwani mizani hiyo inatumiwa na wafanyabiashara wasio waaminifu kuwaibia wakulima. Aidha, aliomba ufafanuzi wa juu ya kauli iliyotolewa na Serikali wakati wa kuhitimisha hotuba ya Waziri Mkuu juu ya kuanza kutumika kwa mizani ya aina digitali.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakubaliana na Mheshimiwa Lugola pamoja na Waheshimiwa Wabunge wanaotoka maeneo yanayolima pamba nchini, Waheshimiwa Wabunge hawa kwa nyakati tofauti wamesisitiza kuachana na matumizi ya mizani ya steel yard na kuanza mapema iwezekanavyo kutumia mizani ya digitali ili kunusuru wakulima dhidi ya wafanyabiashara wezi na wahujumu.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara inatoa ufafanuzi wa suala hilo kama ifuatavyo.

(i) Tarehe 11 Juni, 2011 Wizara ya Viwanda na Biashara iliridhia tamko la Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, Mbunge la kuamua mizani ya rula iitwayo steel yard itumike tena kwa mwaka mmoja zaidi katika ununuzi wa pamba wa msimu huu;

(ii) Tamko hilo lilitolewa kufuatia ukweli kwamba pamoja na kuwa sekta ya pamba ilishafanya maamuzi ya kutumia mizani ya digitali maandalizi ya upatikanaji wake hayakukamilika kwa wakati;

(iii) Licha ya kuwa bodi ya pamba mapema ilishatoa taarifa ya uamuzi matumizi ya mizani ya digitali. Kwa kuwa utafiti uliofanywa katika nchi Zambia, nchi ya Malawi na Zimbabwe imeonyesha kuwa mizani hiyo inafaa kwa sekta ya pamba, lakini changamoto ya mizani hiyo kuhitaji umeme haikuzingatiwa na maeneo mengi ya vijijini kwa sasa hayana umeme jambo ambalo linakwamisha kabisa matumizi ya mizani ya digitali kwa msimu huu;

(iv) Aidha, suala la upatikanaji wa mizani hiyo digitali ni changamoto nyingine ambayo ilijitokeza ambapo sampuli za mizani hiyo zilianza kuwasilishwa wakala wa vipimo kwa ajili ya uhakiki kuanzia mwezi Aprili mwaka huu. Sampuli 11 zilizowasilishwa hakikukidhi kabisa vigezo na hivyo zikakataliwa;

(v) Kwa upande wa Wizara ya Viwanda na Biashara, taratibu za kisheria za kuondoa mizani za rula kwenye matumizi ya biashara zilishafanyika, zilishafikia hatua ya mwisho kwani tamko la aliyekuwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dkt. Mary M. Nagu, Mbunge la kuruhusu matumizi ya steel yard kwa mmoja zaidi alilolitoa Bungeni tarehe 24 Juni, 2010 lilikuwa linaisha tarehe 28 Juni, 2011;

(vi) Hata hivyo, hatua ya ziada iliyochukuliwa na Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia wakala wa vipimo kuhakikisha kuwa wakulima wa pamba hawataibiwa kwa kupitia mizani hiyo ya rula ni kufanya uhakiki wa mara kwa mara. Mameneja wa mikoa chini ya wakala wa vipimo wamepewa maagizo ya kuhakikisha kuwa wanafanya kaguzi za kushitukiza ili wafanyabiashara watakaobainika kuwapunja wakulima, wakulima hao kwa kutumia hii steel yard watuchuliwa hatua za kisheria na kwa kauli hii nawaagiza mawakala wa vipimo nchini kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola kuwakamata wafanyabiashara wezi kuwanyang'anya leseni kuwafikisha mahakamani ili iwe fundisho kwa yoyote atakayethubutu kuwanyonya wakulima wa Tanzania;

(vii) Baada ya msimu huu wa ununuzi wa pamba 2011/2012 kwisha, Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Ushirika na Chakula, watasimamia mamlaka na taasisi zote zinazohusika na upatikanaji, uhakiki, usambazji na usambazaji wa mizani ili wakamilishe mapema utathimini wa mizani utakaotumika kwa msimu ujao wa ununuzi wa pamba. Hatua hii itasaidia kuthibiti udanganyifu katika ununuzi wa pamba na mazao mengine katika msimu ujao.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (Makofi)

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**SPIKA**: Asante, ahsante sana, Katibu.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma), (Utawala Bora), na Ofisi ya Rais (Uhusiano na Uratibu) kwa mwaka wa Fedha 2011/2012

*(Majadiliano yanaendelea)*

### HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa maelezo ya hoja ya kutengua kanuni za Bunge chini ya kanuni 150(1) za kanuni zetu toleo la 2007. Kwa kuwa wakati wa mjadala wa Kamati ya Matumizi, Mbunge yeyote anaweza kuomba ufafanuzi au maelezo zaidi katika kifungu chochote cha fungu linalohusika kufuata na masharti ya kanuni ya 101. Na kwa kuwa uzoefu wa Bunge hili unaonyesha kuwa idadi kubwa ya Wabunge wanajitokeza kuomba ufafanuzi wakati wa Kamati ya Matumizi kiasi kwamba muda uliotengwa hautoshi na hivyo kusababisha mafungu yaliyosalia baada ya muda kwisha kupitishwa kwa mkupuo. Na kwa kuwa chini ya kanuni ya 101(5) muda wa kusema wakati wa Kamati ya Matumizi kwa ajili ya kutoa ufafanuzi ni dakika isiyozidi 5. Aidha, kanuni ya 103(4) inaelezea kuwa muda wa kuzungumza wakati wa hoja ya kuondoa shilingi ni dakika zisizozidi 5 na pia kanuni ya 103(5) inatoa fursa kwa Wabunge wasiozidi watatu kuchangia hoja ya kuondoa shilingi kwa kutumia muda usiozidi dakika 3 kila mmoja na kwa kuwa ili kuleta uwiano sawa wa michango na kupata idadi kubwa ya wachangiaji na hivyo kuepuka kuingia kwenye utaratibu wa *guillotine* kwa kupitisha mafungu yanayobaki kwa mkupuo inalazimu kutengua kanuni zinazohusu muda wa kuongea wakati wa mjadala wa Kamati ya Matumizi. Hivyo basi ili kuongeza muda wa mjadala wakati wa Kamati ya Matumizi na hivyo kuwezesha Bunge kupitia mafungu yote ya Bajeti husika, Bunge linaadhimia kwamba,

(i) Kanuni ya 101(5) kitenguliwe na kwamba muda wa Mbunge kuomba ufafanuzi na Mawaziri kujibu hoja wakati mjadala wa Kamati ya Matumizi usizidi dakika 3 badala ya 5, hapa ni kwa Waziri na kwa Waheshimiwa Wabunge;

(ii) Kanuni ya 103(4) kitenguliwe na kwamba muda wa kuongea wakati wa hoja ya kuondoa shilingi usizidi dakika 3 badala ya dakika 5;

(iii) Kanuni ya 103(5) itenguliwe na kwamba muda wa kuchangia na kujibu hoja wakati wa hoja ya kuondoa shilingi usizidi dakika 2 badala ya dakika tatu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja hii imeungwa mkono, Waheshimiwa Wabunge tulipokuwa tunajadili hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, mliona kabisa sehemu kubwa ambayo tulibidi tupitishe kifungu kwa kifungu hasa miradi ya maendeleo hatukuweza kufikia. Kwenye suala zima la mafungu ya mikoa hatukuweza kufikia pamoja na kuongeza saa moja tuliyoongeza. Kwa hiyo tumejiona kwamba kwa sababu ya mwamko mzuri wa Waheshimiwa Wabunge kutaka ufafanuzi katika dakika za mwisho.

Tukiendelea na mtindo wa sasa wa dakika 5 Mbunge anauliza, anajibiwa kwa saa zisizojulikana kwa upande wa Mawaziri, anarudia tena Mbunge dakika tatu, anajibiwa na Mawaziri kwa muda usiojulikana, utakuta suala hilo moja tu linaweza likatumia dakika, tulifanya hesabu juzi kuna mahali Mawaziri walijibu mpaka dakika 20, kwa hiyo unafika mahali unakuta kama siku hiyo tungeendelea mngeuliza Wabunge 10 tu, tukaongeza saa nzima lakini hata hivyo mkatosha mliosimama tu.

Kwa hiyo, tumefikiria tutengeneze utaratibu kidogo ambao unakuwa unaruhusu kila atakayesimama aweze kupata nafasi, lakini wakati huo tuweze kufika kwenye mafungu kwa kuyapitia fungu moja hadi lingine kuliko kupita jumla tu kwa *guillotine* kwa hiyo ndiyo sababu ya kuhoji.

Kwa hiyo nawahoji kwanza kwamba tukubali Mbunge tukifika wakati wa Kamati ya Matumizi badala ya kutumia dakika 5 sasa atumie dakika 2, hivyo hivyo tutakapofika kwenye mtu atakayetaka kutoa shilingi, na tulisema anayetoa shilingi lazima liwe jambo mahususi, badala ya kutumia dakika 5 yeye peke yake, yeye atumie 3, halafu na wale watakaomuunga mkono watatumia dakika 2 nao watakuwa watatu. Sasa wanaofikiri mabadiliko haya tuyafanye waseme ndiyo.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Bunge liliafiki Kutengua Kanuni za Bunge zilizotajwa)*

**SPIKA:** Nadhani waliosema ndiyo wameshinda, kwa hiyo kuanzia leo jioni utaratibu huo utaanza kufanya kazi. Waheshimiwa Wabunge tunao wachangiaji na naomba msiombe tena.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, naomba muongozo wako Mheshimiwa Spika kuhususiana na uamuzi huu wa kupunguza muda wa mjadala katika kupitisha hotuba ya makadirio. Ni wajibu wa kikatiba wa Bunge hili kujadili na kupitisha bajeti za Serikali ibara ya 63(3) inaweka wazi kwamba moja ya kazi za Bunge hili ni kujadili Miswada, Mapendekezo, na hoja zinazoletwa na Serikali.

Sasa madhara ya kupunguza muda wa Bunge kujadili miswada ya Serikali maana yake ni kwamba hili Bunge litakuwa linapitisha, litakuwa lina rubber stamp vitu ambavyo vinaletwa hapa badala ya kuvijadili na tukielekea huko hili Bunge tutaliua kama chombo cha kufanyia maamuzi na kupitisha sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninapendekeza, kama suala ni muda hautoshi, basi muda wa Bunge kukaa na kupitia kila kitu kinacholetwa Bungeni uongezwe ili Wabunge wajadili mambo makubwa ya Kitaifa, huku kutupunguzia muda ni kuligeuza hili Bunge kuwa *rubber stamp* na kwa kweli tutakuwa hatutendi haki kwa nchi yetu na kwa Wananchi waliotutuma. Tuongezewe muda wa kujadili hizi hoja za Serikali.

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu, tuna utaratibu wa kupitia maamuzi yote haya, tunayokwambia sasa tumepita kwenye Kamati ya Uongozi baada ya kuzingatia kwamba, hatujitendei haki sisi wenyewe. Wewe fikiria juzi vifungu vyote tumevipitisha kwa *guillotine* tu kwa dakika moja na tuliongeza muda wa saa moja. Sasa tunasema mfumo mzima wa Bunge letu kwa ongezeko la Wabunge itabidi uangaliwe kwa upana zaidi siyo kwa leo hii, kwani kwa leo hii haitawezekana. Kuna haja siku za baadaye, maana yake tumejifunza kwamba, uwingi wetu una matatizo, hatufikii mahali tukajadili kitu inavyostahili.

Sasa huwezi kubadilisha kwa Mwongozo wa Spika, hilo ni suala la mfumo mzima. tumesema pia bajeti yetu tunavyowasilisha hapa hata Waziri Mkuu alisema wakati ule, nayo pia tuiangalie namna gani tunaweza kuingiza zaidi kwenye bajeti kuliko tunavyofanya sasa. Kwa faida ya hivi sasa, leo tunaijadili Wizara hii, utaratibu tuliopitisha sasa ndiyo utafuatwa, hayo mengine tutaangalia baadaye kwa mfumo mzima wa ongezeko la Wabunge na umuhimu wa kujadili Serikali. Hiyo tutaifanya lakini si kwa hivi sasa.

Kwa hiyo, tunaendelea tusipoteze muda mwingi kwa sababu hii Wizara ni kubwa kweli na sasa ninaomba nimwite Mheshimiwa …

## TAARIFA

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, kwanza, alichokisema Mheshimiwa Tundu Lissu, sicho ambacho mimi nilikitolea taarifa. Hatukupunguza muda wa kujadili, muda wa kujadili hotuba umebaki uleule ambao tumekubaliana kwenye Kanuni, dakika 15 na hizi dakika tatu huwa hazitumiki kwa ajili ya kujadili, ni kuulizia na kupata ufafanuzi wa jambo mahususi kwenye Kamati.

Meshimiwa Spika, nilitaka tu kumpa hiyo taarifa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninakubali hicho ndicho tulichokifanya kwa sababu mtu anapewa dakika tano nzima na ninyi wenyewe hata kwenye semina mnakuwa

na dakika tatu na zinawezekana. Tunaruhusu Wabunge wengi, tukienda na dakika hizi watakuwa labda ni Wabunge watano basi tunamaliza kazi na *guillotine*. Mimi binafsi *guillotine* siipendi hata kidogo, kwa sababu tunakuwa hatufikii azma yetu ya kupitia kifungu hadi kifungu. Kwa hiyo, kwa utaratibu tunaamini kwamba, tunaweza kufanya yale, lakini muundo mzima wa namna tunavyofanya tutauangalia siku zinazofuata.

Kwa hiyo, sasa ninawaita Mheshimiwa Rev. Peter Msigwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Rose Kamil Sukum na Mheshimiwa Michael Laizer na Mheshimiwa John Mnyika wajiandae.

Mheshimiwa Mchungaji.

**MHE. REV. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hotuba ambayo ameitoa Mheshimiwa Waziri.

Kwanza kabisa, ninataka nijikite katika maeneo matatu, lakini kuna mtu mmoja aliwahi kusema na ninaomba nimnukuu: *"A society fail if the Government are inefficient, poor performance, ineffective and corruption in public sector."*

Katika nchi yetu nilitegemea kwamba, suala linalohusiana na utumishi wa umma ni jambo nyeti, ni jambo la msingi, ambalo kama Wabunge ili kuboresha uchumi wa nchi yetu, tungelijadili kwa mapana ili tuweze kuleta mabadiliko katika nchi yetu.

Nikisoma historia mabadiliko haya au ku-*reform* utendaji wa watumishi wa umma katika Serikali, yameanza toka mwaka 1991 katika nchi nyingi za Kiafrika na Tanzania ikiwa ni mojawapo. Kwa bahati mbaya, nchi nyingi za Kiafrika ilikuwa ni mashinikizo kutoka *World Bank, IMF* na nchi zenye viwanda ambazo ili ziweze kutoa misaada, zilishinikiza haya mambo yafanyike ili tuweze kupata misaada kutoka kwa *donors*. Kwa bahati mbaya, halikuwa chimbuko la sisi wenyewe, matokeo yake hatujafanya kwa undani ili haya mabadiliko yaweze kuleta tija katika nchi yetu. Mabadiliko haya yaliwahi kufanyika Uingereza wakati wa Utawala wa Margaret Thatcher. Vilevile yalifanyika Marekani hata New Zealand, wao walifanya walipokuwa wana *review* utendaji kazi wa Watumishi wa Serikali na walikuwa wana pesa zao, walifanya ndani ya Serikali zao ili kupima kiwango cha utendaji kazi katika Serikali zao. Kwa kuwa sisi tulipata mashinikizo, mambo haya hayajatiliwa maanani, matokeo yake utendaji kwa Watumishi wa Umma umekuwa mbovu sana.

Kama nilivyosema, ukienda kwenye Ofisi nyingi za Serikali, kuna watu hawawajali Wananchi wetu wanapokwenda katika Ofisi za Umma. Ukienda katika Ofisi nyingi, kuna *negligence*, hakuna *attention*, Wananchi wanapokwenda kupata huduma, Watumishi wanaendelea kuangalia *television* kwenye Ofisi, wengine wapo kwenye *face book*, kwenye *tweeter*, wengine wana-*chart* kwenye simu zao, wengine wanaongea na simu, basi Wananchi hawapati huduma zinazotakiwa katika Ofisi za Serikali.

Haya ni mambo ya msingi ambayo ni lazima yatiliwe maanani na hili tatizo ambalo limekuwa kubwa zaidi limefanya vilevile kuwa na *poor customer service.* Mwananchi wa Tanzania anapoingia kwenye Ofisi ya Umma ni kama vile anaomba msaada, ni kama vile amekwenda kwenye *Private Sector. Private Service* sasa hivi nyingi zime-*improve*, hawajaliwi wala kuhudumiwa vizuri. Kwa mfano, kwenye Ofisi za Umma ukipiga simu hakuna majibu wakati mwingine simu zinaita muda mrefu wala hakuna anayejali. Nilitegemea Mheshimiwa Hawa Ghasia, anakuja na mpango kamili; ni namna gani tuta-*improve customer service* kwenye Ofisi zetu za Umma.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, ni Mheshimiwa Waziri wa Nchi na siyo Hawa Ghasia.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, samahani; Waziri wa Nchi, nilitegemea angekuja na majibu kwamba, tuna mpango huu ku-*improve customer service* ambayo iko *very poor* na inapokuwa *poor customer service* kwenye Sekta za Umma, maana yake utakuta hata kwenye Sekta Binafsi kuna utendaji mbovu.

Kwa mfano, ukienda kwenye Benki unaweza uka-*queue* kwa saa tatu hakuna mtu anayejali, kwa sababu ameona katika Sekta za Serikali hakuna hatua zinazochukuliwa kushughulikia tatizo hili ambalo linatuletea shida. Kwa hiyo, ninamwuliza Waziri anakuja na mpango gani kuboresha? Nenda hospitali, nenda kwenye Idara mbalimbali ambazo unaweza kuingia kwenye ofisi ya mtu unakuta koti lipo lakini muhusika yupo kwenye miradi yake; ni namna gani tuta-*improve* maeneo haya?

Jambo la pili ambalo ninataka kulizungumzia ni kuhusiana na rushwa. Jambo la rushwa ambalo tumepata *report* na *data* nyingi hapa zinazohusiana na rushwa jinsi ambavyo TAKUKURU wamejitahidi kufanya yale ambayo yanaonekana yamefanyika, mimi ninaweza kusema ni suala la kisiasa tu. Ninasema ni suala la kisiasa japokuwa watu wengine wamesifu sana kwamba, wasingekuwepo ndani ya nyumba hii kama siyo TAKUKURU wamefanya kazi yao, lakini kwa watu wengine ambao na sisi tuliathirika wakati wa uchaguzi, hatukuona jinsi ambavyo TAKUKURU wamefanya kazi. Mimi mwenyewe ni mwathirika, nilijaribu kupiga simu, nikatoa taarifa lakini hakuna kilichofanyika. Kwa hiyo, inawezekana wale waliokuja hapa ambao TAKUKURU iliwasaidia kwa namna fulani, lakini wengi tumeathirika na TAKUKURU ilikuwa ni kama haifanyi kazi.

Pia ninakumbuka tulipokuwa Ubungo, Mheshimiwa Hosea, alijaribu kuzungumzia matatizo ambayo yeye kama Mkuu wa Kitengo anayapata. Nilitegemea Mheshimiwa Waziri angekuja hapa, moja ya matatizo ambayo Mheshimiwa Hosea aliyazungumza alitoa mifano kwamba, chombo hiki kinashindwa kufanya kazi, alitoa mfano wa *Scorpion South Africa*, Mkuu wa Kitengo kile alivyojaribu kuwakamata wakubwa, aliadabishwa na kitengo kile kikafutwa. Nilitegemea Waziri anapokuja hapa atasema baada ya kusikia maoni ya TAKUKURU, tumeboresha na tumempa meno zaidi kwamba, amkamate yeyote bila kujali na bila kumwogopa; lakini sijayapata hapa, maana yake *business as usual.*

Kuna mtu mmoja aliwahi kusema kwamba, *make a difference tomorrow by becoming a better leader today*. Tumepewa dhamana ya kuwa Viongozi leo, *you have a weak father, a weak family, a weak leader, a weak society*. Kama Mheshimiwa Hosea alikiri kwamba, anaweza mwenyewe kutofanya kazi kwa sababu anapojaribu kuwashughulikia, akatoa na mfano wa Uganda kwamba, yule *Boss* wa Kitengo cha Rushwa alipojaribu kuwashughulikia wakubwa walimwadabisha na yeye ndiye amepewa dhamana. Nilitegemea Mheshimiwa Waziri atakuja na majibu kwamba, Wabunge mlisikia matatizo ni haya na sasa Mkuu wa Kitengo amesema hivi, tunatoka majibu haya ili Tanzania yetu tuepukane na rushwa.

Mheshimiwa Spika, lakini ujumbe ambao ninaweza kumpa Mheshimiwa Hosea kama Mkuu wa Kitengo hiki ambaye tunamtegemea na amepewa dhamana; mtu mmoja pia aliwahi kusema; *the question that must be always answered before accepting a new job*, hili jibu alitakiwa alijibu*; what is required of me. In other words what do I have to do that no one but me can do.* Jawabu kubwa ambalo Hosea anatakiwa atupe, yeye alipopokea kazi hii anatakiwa atuambie asipoifanya yeye nani anaweza kuifanya? Wananchi wa Tanzania, wana dhamana kubwa, wanamwamini kwamba, yeye ndiye anayesimamia rushwa. Anapotoa takwimu na majawabu ya kwamba, wakati mwingine anakamatwa basi angewarudishia waliompa kazi kwa sababu hapa ni kufuja pesa za Serikali, ni kuweka Taasisi ambayo ni kiini macho kwa Wananchi kwamba, kuna Wananchi wanaoshughulika na rushwa kwa sababu tuna Wananchi wengi Tanzania wanateseka.

Rushwa na ubabaishaji kuanzia kwa Mwenyekiti wa Mtaa mpaka juu. Mwenyekiti wa Mtaa kwenye eneo lake naye anauza kiwanja kilichoko upenuni kwa ujanjaujanja. Ukienda kwa Mtendaji naye hivyo hivyo, ukienda kwa Diwani naye hivyo hivyo. Tanzania ni ma-*deal* tu na kama kitengo hiki hakifanyi kazi, inakuwa ni ngumu. Sasa hivi hata tunapogombea Waheshimiwa Wabunge, utasikia mimi ninagombea nimeambiwa na Mgombea Urais nitakuwa Waziri, watu wanakimbilia Uwaziri kwa sababu ni *deal*, hawakimbilii kwa sababu wanataka kuwatumikia Wananchi. Sasa huu ni wito kwa Mheshimiwa Hosea kwamba, kama majukumu aliyopewa hawezi kuyafanya yeye ayafanye nani? Wananchi wa Tanzania tuna dhamana naye; vinginevyo, a-*step down* aseme hii kazi siwezi kuifanya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba Waziri atupe majibu ni namna gani hiki kitengo kinaweza kikaboreshwa ili tuweze kukomesha tatizo sugu la rushwa. *The only place in this country where corruption does not exist* ni kweli kale kakibao kanakosema: "Hurusiwi kutoa rushwa." Kila Ofisi kuna hako kakibao lakini rushwa *is everywhere.* Sote tunalifahamu, Watanzania wanajua na Dunia inajua kwamba, kuna rushwa *everywhere*.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, kwa sababu muda wangu umekwisha, ninataka nizungumzie suala la Usalama wa Taifa. Mkuu wa Kitengo hiki alikuja Ubungo Plaza akatuambia na sisi kama Wabunge, tulizungumza *concern* zetu. Kiuhalisia, mimi binafsi ninaamini Usalama wa Taifa hawafanyi kazi kama wanavyopaswa wafanye. Usalama wa Taifa badala ya kuwa ni chombo cha kutetea maslahi na mali za umma,

wamekuwa ni watu wa kudhibiti Vyama vya Upinzani kama CHADEMA, CUF na NCCR. *(Makofi)*

Hatutegemei nchi ambayo ina Mfumo wa Vyama Vingi, mali, magari ya Usalama wa Taifa, Wafanyakazi wa Usalama wa Taifa badala ya kushughulika na maslahi ya nchi hii, wanashughulika eti namna gani wawadhibiti Wapinzani. Jana wakati tunatoa maoni yetu, Kambi ya Upinzani imeshauri kwamba, na ninaomba ninukuu, katika ukurasa wa 15: "Kutokana na ukweli wa Sheria zilizounda Usalama wa Taifa hazitoi fursa kwa chombo hiki kufanya ujasusi wa kiuchumi, Kambi ya Upinzani tunasema, chombo hiki kifanye ujasusi wa kiuchumi badala ya kung'ang'ana kuwadhibiti Kambi ya Upinzani, waende nchi za nje, watafute mbinu za kiuchumi kuja katika hii nchi badala ya kuwadhibiti Wapinzani."

Hatutoki Rwanda wala Burundi, tunatoka katika nchi hii; *is just a deterrent way of seeing things,* sote tunataka maendeleo hapa. Hii ni *paradigm shift,* namna ya kuangalia maendeleo yaje vipi badala ya kutudhibiti sisi, kimekuwa ni chombo cha usalama wa CCM na siyo chombo cha Usalama wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, kama kingekuwa Chombo cha Usalama wa Taifa ni aibu kwa Taifa hili eti Ndege ya Kijeshi itoke nchi nyingine ibebe Twiga katika nchi hii iwasafirishe, wanyama 126 ndani ya nchi hii wanatoka nje; Usalama wa Taifa uko wapi? Kama kingekuwa ni Chombo cha Usalama wa Taifa, madini na mikataba mibovu ya nchi hii inafanywa halafu hakuna kinachotokea; ni usalama gani wa Taifa huo? Misitu ya nchi hii inaondoka; ni usalama gani wa Taifa huo? Hiki ni kiini macho ambacho tunataka ifanyike *reformation* katika Chombo hiki ili tulinde mali zetu. Wengine wanapenda kumnukuu Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere, *in the wrong reason,* wanaficha makosa yao, yaani *they reduce the nice word of Mwalimu Nyerere*.

*Mwalimu Nyerere was not corrupted;* alikuwa anapenda watu, alilijali Taifa hili. Kila mtu akisimama hapa anasema Mwalimu Nyerere alisema, lakini kuna rushwa ndani yake; Mwalimu Nyerere alisema, lakini kuna uonevu ndani yake; Mwalimu Nyerere tunampenda kwa sababu *he never talk the talk only but he work to the talk*. Tunataka tutendewe yale tunayoyasema. Usalama wa Taifa tunaomba isimamie rushwa na ifanye kazi kwa mujibu wa Sheria ili tulilinde Taifa hili, tuliokoe Taifa letu, Taifa ambalo linaonekana halina *direction* kama nilivyosema juzi. *(Makofi)*

Ninashauri waende nchi za nje wakatafute, wakaibe, wakafanye ujajusi wa kutafuta namna gani uchumi wa nchi yetu unaweza kubadilika badala ya kudhibiti Wapinzani. Hiyo ndiyo rai yangu. Tutakaa tutaongea hapa, tutapiga kelele na tunazungumza hapa, kama Usalama wa Taifa upo, mabomu mara mbili yanaua watu hakuna mtu anaye-*step down*, umeme sasa hivi ni shida, uchumi ume-*frees* katika nchi hii, hakuna mtu wa ku-*step down.* Tunazungumza hapa, hata Waziri wa Maliasili na Utalii, Twiga wanaibiwa katika nchi yake anakuja hapa hakuna anayefikiri ku-*step down*, utaratibu wa kuadabishana katika hii nchi utaishia wapi? Nimesema *you have a weak leader, you have a weak society*. Mawaziri kama wangeanza kuonesha mfano mzuri kwamba, akifanya makosa *off you go,* hawa watu wa chini nao wangetusikiliza. Kuna

*tendency,* mambo yanakwenda *business as usual,* Waziri anaweza aka-*mess up* na akafanya lolote mambo yanaendelea kama vile hakuna kilichotokea. Dunia inajua, Tanzania inajua na Watanzania wanajua kwamba, *business as usual.*

**MBUNGE FULANI:** Tumechoka!

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Tumechoka sasa! Ninaomba Bunge la Kumi hebu liwe Bunge la kihistoria, liwe Bunge ambalo tunaleta historia kama nilivyosema; *change tomorrow by making a difference today*. Hebu tuibadilishe kesho kwa kuleta tofauti leo. *Don't count today's harvest, rather count the amount of seed sowed and nurtured. (Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** *Thank you!*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Tumekuwa tunakula tu hatuangalii kesho itakuwaje, hebu kwa pamoja, watoto wanaokuja nyuma yetu waje waone kwamba, katika Bunge la Kumi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuna watu ambao walikuwa wanafikiri na kuangalia mbali ili tulete mabadiliko katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Msigwa, ulisahau ukadhani tuko kanisani. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa utaratibu ulio sahihi na wa haki, Hosea ni Mkurugenzi wa TAKUKURU, tukimwita Mkurugenzi ninadhani itakuwa na sura nzuri zaidi kuliko kumwita Hosea, kwa sababu sidhani kama yeye peke yake anaweza kufanya kazi. Tumwite Mkurugenzi wa TAKUKURU kwa watakaochangia baadaye.

Sasa ninamwita Mheshimiwa Rose Kamil Sukum.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii na mimi walau niwe mmojawapo wa wachangiaji wa Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, leo ninaomba niwe mwakilishi wa watumishi. Ninataka nisimamie suala la watumishi tu kwa sababu ni watu pekee ambao wameshindwa kusaidiwa hasa waliopo chini.

Mheshimiwa Spika, Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Utumishi wa Umma, katika ukurasa wa 66, ilizungumzia habari ya kurekebisha mishahara ya Watumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, lakini suala la mishahara limekuwa kwenye giza hakuna mishahara elekezi kwa kima cha chini kwa Sekta Binafsi na Sekta ya Umma. Sasa

tunapitisha hiyo bajeti iliyoletwa kwa ujumla kwamba, tupitishe shilingi trilioni 3.2 kwa ajili ya kulipa mishahara, kwa ajili ya kulipa malimbikizo na kwa ajili ya kulipa madeni na madai mbalimbali; nina uhakika kabisa kwamba, Wananchi wote ambao ni Watumishi wa Umma na wa Sekta Binafsi, wapo kwenye TV wakitaka kujua Wabunge wanasema nini kuhusu mishahara na ni kiasi gani, kwani wamedai kwa muda wote lakini cha kushangaza Serikali inaficha kwa kudai kuwa eti wanasubiri kasi ya mfumko wa bei; mfumko wa bei upi wakati sasa hivi upo na unajulikana? Hiyo bajeti inayosubiriwa ni ipi na vikao hivyo vya kwenda kukaa na hiyo Kamati iliyoundwa ni ipi? Ninadhani wakati bajeti inaandaliwa hivyo vitu tayari vilishakamilika na kilichotakiwa ni kuambiwa kwamba, Watumishi sasa wanapata kima cha chini kiasi fulani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi ninaomba niendelee kwa kusema kwamba, Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma, kazi yake ni kusimamia matumizi na maslahi ya rasilimali watu. Sasa kwa kuwa kazi yao ndiyo hiyo na watumishi hawa wanatakiwa wasaidiwe, mimi nitaeleza kwa kutoa mifano hai kutoka Wilaya ya Hanang, kwa sababu ndiko nilikotoka na bahati nzuri nilikuwa Diwani wa muda mrefu sana kwa miaka 16; kilio cha watumishi kilikuwepo muda wote wakidai madai yao, lakini ofisi yetu haitusaidii wala haiwasaidii hao watumishi. Tufahamu kabisa kwamba, aliye juu atashuka chini, pia anasubiriwa huko chini, hiyo ifahamike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, ninaomba ninukuu kumbukumbu Na. CAB157/539/0134, Waraka Mkuu wa Utumishi wa Umma Na. 1 wa Mwaka 2009 wa tarehe 1 Me, 2009, kuhusu udhibiti wa ongezeko la madeni ya Serikali kwa Watumishi wa Umma. Waraka huo unawataka Wakurugenzi kutokuzalisha madeni na endapo watazalisha madeni hayo, watawajibika kwa vyeo vyao na wakishindwa kulipa madeni waweza kuwasilisha ofisini kwa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo ya Utumishi wa Umma ili watumishi hao waandikiwe kwamba, wamelipwa nini na wanadai kiasi gani na kiasi hicho wanachokidai kwa ajili ya malipo yao kipelekwe katika ofisi hiyo husika.

Mheshimiwa Spika, mpaka leo hakuna Mkurugenzi aliyepeleka hilo, sijui ni kutokana na uwoga gani na walikuwa wanaogopa nini? Je, Ofisi yetu ya Utumishi wa Umma imefanya nini na imechukua hatua zipi kwa Wakurugenzi hao wakati Watumishi wanadai malimbikizo ya mishahara, posho ya kufundishia, posho ya mazingira magumu, uhamisho, matibabu, likizo na ajira mpya? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi ninadhani ifike mahali sasa Waziri atuambie wazi hii hela tunayopitisha shilingi trilioni tatu ni ya kulipa haya malimbikizo, maana ni mengi mno. Halmashauri ya Hanang watu 200 tu wanadai shilingi milioni 143,000 na wakati wapo zaidi ya 2,000 bado hawajapeleka hata hayo madai yao. Je, Tanzania nzima watakuwa wanadai mamilioni mangapi? Tunawalipaje na kwa nini kuna malimbikizo hayo ya watumishi mpaka leo? Tunaomba kwa heshima na taadhima, sasa Wizara ielekeze nguvu kwa Watumishi hao wenye matatizo makubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, inasemekana pia kuna Waraka wa Utumishi wa Umma, uliotolewa kwa ajili ya Watumishi wanaoishi na VVU. Hawa watumishi mpaka leo hawalipwi; kwa nini wanyanyaswe kuna tatizo gani? Hizo hela nani anayekula? Kama

imeelekezwa kwa wahusika hao kwa nini isipelekwe kwa wale wanaohusika? Hayo yote yanahusu Wizara hiyo hiyo, ina maana imenyamaza ikiangalia kwamba, wale hawahusiki na wala siyo watumishi wao, ndiyo maana nimesema aliye juu anasubiriwa chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, upandishwaji wa madaraja ni historia kwenye Halmashauri, labda uwe na mahusiano na Mkurugenzi ndiyo unapandishwa daraja, kama huna mahusiano na Afisa Utumishi na Mkurugenzi, kupandishwa daraja hakupo na sisi wanawake ndiyo tatizo kabisa, maana kama ni wa kiume hadithi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunataka Wizara iliangalie hilo, stahili za watumishi ziwepo kwa hali halisi inayotakiwa. Mtumishi akifika ofisini kwa Mkurugenzi anaambiwa nenda kwa Afisa Utumishi, akifika kwa Afisa Utumishi anaambiwa ondoka usinisumbue, hivi nani amtetee huyu mtumishi; hizo haki ziko wapi? Utawala Bora haupo huko Wilayani kwetu, siyo Hanang tu, ninazungumzia na nina uhakika kwamba, Wilaya zote hawana hizo haki; tunaomba haki hizo ziangaliwe. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala la ukandamizaji au unyanyasaji kwa wale wanaokwenda kusoma. Wakishapata hizo *degrees* cha kushangaza ni kwamba, wanaporudi kwenye vituo vyao vya kazi, wanarudishwa kwenye daraja la chini badala ya kupelekwa kwenye daraja linalostahili. Sasa alikwenda kusoma kwa ajili ya nini kama unamrudisha kwenye daraja la chini? Hii ni wazi kabisa, Watendaji walioko Wilayani wanaogopa kunyang’anywa madaraka kwa sababu wao hawakusoma, maana mtu akienda na *degree* na wewe huna *degree,* maana yake usogee mwenzako akalie pale. Unyanyasaji ni mkubwa, stahili hizo hazitolewi na watumishi wanakata tamaa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie suala la nyumba za watumishi. Inasikitisha sana, kwa kweli inafahamika wazi kabisa kwamba, Waraka ulitolewa mwaka 2008 wa kuuza nyumba za Watumishi. Wilaya ya Hanang ina upungufu wa nyumba za watumishi, lakini cha kushangaza ni kwamba, ule Waraka wa Mwaka 2008 ulikuja kuuza nyumba za Watumishi wa Kilimo na Mifugo; hivi kweli unapouza hizo nyumba na leo una watumishi zaidi ya 45 tunafanya nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunahangaika sasa kujenga nyumba nyingine kwa gharama za Wananchi kwa kuwataka wachangie kiasi fulani halafu na hela za Serikali zijenge; kwa nini nyumba zile ziliuzwa? Kuna nyumba mbili zilizouzwa Wilaya ya Hanang kutokana na ule Waraka uliotolewa, sasa hivi Watumishi wa Kilimo na Mifugo hawana nyumba za kuishi na hizo nyumba bahati mbaya zipo kwenye *Block No. 16*, jirani kabisa na ofisi, yaani ofisi ipo hapa na hizo nyumba zimepangana hapo pembeni, ina maana hata hiyo ofisi siku moja itauzwa na hakutakuwa na ofisi.

Mheshimiwa Spika, hilo lazima liangaliwe kwa sababu ni stahili zinazotakiwa kwa watumishi wetu, kwa ajili ya huo upungufu unaotakiwa wa watumishi kuishi kwenye nyumba kwa raha zao ili waweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie suala la *TASAF*. *TASAF* tunasema inafanya kazi vizuri ni kweli, lakini hamkuangalia suala la fedha za *TASAF* zimetumikaje (*value for money*). Wilaya ya Hanang *TASAF* imekwenda, ilikuwepo *TASAF I, TASAF II* kidogo, *TASAF III* sisi hatupo hata siioni kwenye bajeti. Utakuta Mradi wa jamii unaotengenezwa na *TASAF*, hela zingine zinakatika; zinakatika kwenda wapi? Tunaomba iundwe timu ya kwenda kuhakiki vizuri hizo fedha za *TASAF* zimetumikaje (*value for money*), hilo ni jambo ambalo linatakiwa liangaliwe kwa undani kabisa. Mfano, maji Gehandu yalichangiwa na *TASAF* Mradi wa Jamii, wametengeneza vioski vinane lakini Halmashauri pia fedha za *Quick Win* na fedha za Mradi wa Maji zimekwenda kutengeneza vioski hivyo hivyo vinane; pale kunakuwa na utata mkubwa. Tunaomba *value for money* ifanyike, *CAG* peke yake hataweza, lazima kuunda na timu nyingine ambayo itasimamia Miradi hiyo ya Jamii ili hela ziangaliwe kama zinafika kwa usalama kabisa, maana sehemu kubwa wanasema ufuatiliaji, kumbe ufuatiliaji ni sehemu ya kutaka kula hizo fedha.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuzungumzia suala la Utawala Bora na nianzie kwenye Ofisi ya Utumishi wa Umma. Watumishi hawasikilizwi, hata wakilalamika hawasaidiwi, watu wana madai ya tangu mwaka 1999, wengine wana madai yao ya uhujumu uchumi, hakuna anayewasikiliza. Kwa kweli hii hali sasa siyo nzuri na tunaomba Utawala Bora wa kweli ufanyike ili kusaidia jamii iliyoko hapa kwetu.

Ndugu zangu, mimi nina uhakika kabisa kwamba, kuna Watumishi mwaka 1999 wanadai madai yao, kuna Wazee ambao wanadai madai yao, lakini bado tunadharau pamoja na kuwapiga mabomu na nini, hiyo haisaidii na mbele za Mungu mnatenda dhambi. Lazima tuangalie kwamba, sasa Wananchi wanatakiwa wahudumiwe vile wanavyotaka stahili zao.

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la Utawala Bora, suala la uhamisho limekuwa sugu, Mkurugenzi akiletwa muda mfupi tu amehamishwa, halafu tunasema hatuna hela. Wilaya ya Hanang, Mkurugenzi aliletwa akakaa wiki moja, wiki ya pili, ameletwa mwingine; kwa ni? Ina maana uhamisho unafanyika wa *kindugunization* na hili lazima liangaliwe. Huo uhamisho pia umegusa jamii ya Wana-Hanang kwa watumishi walioko chini, mtumishi anahamishwa mara kumi mwingine hajahamishwa hata mara moja na bado hujamlipa hata stahili zake. Ninaomba hilo liangaliwe sana na Idara hii ambayo ina dhamana ya kuangalia suala la Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, Watumishi wa Hanang wananyanyasika sana, ninaomba nilizungumzie kwa upande wa Hanang kwa sababu mimi ni mdau wa pale na ni Diwani wa pale. Ninaomba nilielezee wazi kabisa, Mwalimu anahamishwa kwa makusudi eti kwa sababu ni ndugu wa fulani, anapelekwa kwingine. Wakati wa uchaguzi Walimu na Watendaji walihamishwa ovyo; nani anayelipa zile fedha za uhamisho wakati ule wa uchaguzi? Tunataka pia tuelezwe na Serikali hii kwamba; nani sasa ni mkuu wa ulipaji huo kwa sababu lazima stahili za waliohamishwa zipatikane?

Mheshimiwa Spika, upandishaji wa vyeo pia na kwenda masomoni ni kwa kuangalia undugu. Mkurugenzi anampeleka mtu yule anayemnyenyekea kwenda kusoma,

mwingine amepata nafasi ya shule anaambiwa huendi kusoma kwa sababu hatuna watumishi wa kutosha, lakini yule wa kwake amempeleka. Tunataka hilo pia liangaliwe kwa Wilaya ya Hanang.

Mheshimiwa Spika, lingine ni ajira; ajira kwa Watumishi wa chini imekuwa pia ni ya kindugu, hili nalo pia liangaliwe na watafute utaratibu mwingine wa ajira ili kila mtu aweze kupata ajira.

Watumishi wanaolipiwa na Wilaya ya Hanang; Halmashauri ya Hanang inawalipia wengine asilimia mia moja na wengine wanajilipia; kwa nini hayo yanafanyika? Ninaomba yafanyiwe kazi. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Bajeti hii ya Utumishi. Ningependa kukupongeza kwa kuongoza Bunge letu vizuri, ninaona sasa linaanza kutulia tofauti na tulipoanza, kwa hiyo, ninakupongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningependa kuipongeza Serikali hasa Rais wetu, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kutupa wafugaji mifugo. Wafugaji wengi wamepoteza mifugo, lakini kwa sasa Mheshimiwa Rais, amerudisha imani ya wafugaji ambao walikuwa wamekata tamaa baada ya ng'ombe kufa. Katika maeneo yetu ng'ombe ni kama Korosho kule Mtwara, ni kama Pamba katika maeneo mengine, kwa hiyo, tunaishukuru sana Serikali kwa kutusaidia kutupa mifugo kwa wale Wananchi wetu ambao hawana mifugo. Haijawahi kutokea, ni mara ya kwanza Serikali kununua mifugo na kuwapa watu ambao hawana mifugo; tunawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya kazi kubwa kuwapa Wananchi shilingi bilioni nane na kwa niaba ya Wafugaji wote wa Halmashauri ya Longido, Monduli na Ngorongoro, tunashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningependa kuzungumzia suala la ajira. Katika bajeti zote mimi huwa sichangii Wizara hii, lakini nimeamua leo kuchangia Wizara hii kwa sababu ya kazi ambayo imeshindikana kule vijijini. Ukishagawa maeneo ya utawala ni lazima utawapa watu ajira, kule vijijini hatuna tena Watendaji wa Vijiji, tunachosubiri ni Sekretarieti ya Ajira iliyoko Dar es Salaam ndiyo iwachague Watendaji wa Vijiji vyote Tanzania; huo ni usimamishaji wa maendeleo. Ninaomba kusema kwamba, Serikali itusikilize kwa jambo hili kwa sababu hili ni bomu ambalo linazuia maendeleo. (*Makofi*)

Vijijini tunategemea kwamba, kuna Serikali ya Vijiji, Serikali inarudisha fedha kwenye Halmashauri na Vijijini kule hakuna Serikali za Vijiji zinazokaa kwa sababu hakuna Watendaji. Hakuna *Ward C* inayokaa kwa sababu Madiwani wanategemea wale Watendaji ndiyo Wajumbe wa *Ward C*. Kwa hiyo, tangu wachaguliwe hawajawahi kuitisha vikao. Katika Jimbo langu, vijiji 15 havina Watendaji wa Vijiji, Kata kumi hazina Maafisa Watendaji wa Kata, sasa mnategemea tutafanya kazi namna gani?

Mheshimiwa Spika, ajira zimerundikana kule Utumishi na Serikali imesimamisha ajira; unasimamisha ajira nani afanye hiyo kazi? Mnakuwa wachoyo wa ajira, wasomi wamejaa nchi hii hamuwapi ajira na nafasi zipo! Ninaomba Serikali ilifanyie kazi jambo hili kwa sababu ni jambo ambalo limezuia maendeleo katika nchi hii. Ukiangalia katika Halmashauri yetu, hatuna Mkurugenzi, ninahangaika kila siku; Mkurugenzi, Mkurugenzi na wasomi wapo nchi hii. Tangu tuanze Halmashauri mpaka leo hatuna *DT;* hivi Halmashauri ambayo haina Mkurugenzi na DT utategemea ifanye nini? Halafu mnakwenda kuikagua mkitarajia itapata Hati Safi, Hati Safi itapatikana wapi? Watendaji walioko pale wote ni kaimu, kaimu, mimi ninashangaa nchi hii ina wasomi wengi, ina nafasi nyingi, lakini watu wamekalia tu nafasi hizo. Ninaomba hili lifanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mambo mengine ambayo tunaishauri Serikali, lakini hawataki kutusikiliza. Hata hili la nyumba lisingekuwa kero sasa kwa sababu tulisema nyumba zisiuzwe lakini zikauzwa. Unajua Baba hawezi akaomba radhi kwa mtoto wake na Serikali inashindwa kuomba radhi katika maeneo mengine, kwa sababu nao wangetakiwa waombe radhi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia, kwanza, hiyo Sekretarieti ya Ajira ni kitu ambacho hakiingii akilini kwamba, Watumishi wote wa Tanzania mpaka majina yaende Dar es Salaam, sijui hata kama wanaitwa Dar es Salaam; ninaomba Sekretarieti za Mikoa zifanye kazi hiyo. Kila Mkoa wajadili na waajiri Watendaji wanaokwenda katika Halmashauri zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni TAKUKURU. Leo nimepata afueni kidogo, kwa sababu mwenzangu Mchungaji pale alisimama akasema kwamba, TAKUKURU ni wa Chama cha Mapinduzi. Leo ndiyo nimegundua kwamba, TAKUKURU hawana chama, kwa sababu na sisi tunasema hawa TAKUKURU ni wa CHADEMA. Kumbe ninyi mnalia kwamba ni wa Chama cha Mapinduzi na sisi tunasema wametumwa na CHADEMA, ni Wana-CHADEMA hawa, lakini sasa leo ndiyo nimegundua kwamba, hawana chama. *(Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ningependa kusema hivi; ndugu zangu TAKUKURU haikuundwa kwa ajili ya wanasiasa. Suala la TAKUKURU unalisikia sana sana wakati wa uchaguzi, wakati ambapo hatuna uchaguzi mbona hatusikii wanakwenda wapi? Katika Halmashauri zetu ambazo fedha zinaliwa, ningeomba TAKUKURU wamefanya kazi huko, lakini hatuwaoni, wanatufuatafuata wanasiasa tu na ndiyo wanaandikwa andikwa kwenye magazeti; kwa nini katika fedha za Halmashauri hawafanyi hivyo? TAKUKURU huwaoni kwenye ununuzi na Miradi hafifu ambayo imepoteza fedha nyingi katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, ningependa kusema kuwa, kama hicho Chombo kimeundwa kwa ajili ya kuangalia maslahi ya Wananchi, ninategemea katika Halmashauri zote TAKUKURU ingefanya kazi. Ninajua TAKUKURU ni chombo muhimu sana kiwepo, kwa sababu rushwa imekithiri na rushwa inanyima haki na hasa haki kwa wanyonge na

inabadilisha haki ya mnyonge na maneno ya mnyonge maelezo yake hayatakuwa na kazi. Ninaomba sana hiki Chombo kimeundwa kwa ajili ya manufaa ya Wananchi.

Ninapendekeza iwepo, lakini iwepo kwa kufanya kazi hii, TAKUKURU wakianza wao kupokea rushwa hakuna namna ya kuzuia rushwa. Ndiyo maana ndugu yangu Mheshimiwa Selasini jana alisema tuna njaa na mahindi yanakwenda sana kupitia Rombo na Longido, lakini huoni hata siku moja magari yamekamatwa na yanakwenda kila siku. Kwa hiyo, unaangalia yanakwenda kwa ajili ya nini; ni rushwa ndiyo inayotumika pale na mahindi yanakwenda. Ninaomba sana hiyo Taasisi ya Kuzuia Rushwa ifanye kazi yake.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni la *TASAF*. Kwanza, kwenye majedwali imeandikwa Miradi ya *TASAF*, lakini Longido haipo, sijui hizo fedha za Longido zimetoka wapi. Nilitegemea fedha za *TASAF* zilizokwenda Longido zingekuwa kwenye majedwali yaliyoandikwa, Halmashauri zingine zimeandikwa lakini Longido haipo! Sasa ningependa kujua hizo fedha za Longido zimetoka wapi?

Ningependa kusema kwamba, katika *TASAF* Awamu ya Pili, waangalie kwa sababu hizo fedha zimetumika vibaya na wala utaratibu wa Miradi haueleweki. Ninaomba uwekwe utaratibu mzuri kwa sasa ili hizo fedha zisaidie, kwa sababu ni fedha ambazo tunategemea zingewasaidia Wananchi.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni mishahara. Mishahara ya wafanyakazi kila siku pesa zetu zinapungua thamani na bidhaa zinapanda kila wakati, lakini ni vigumu sana mishahara kupanda. Jamani tuangalie ni kilio cha wafanyakazi kwamba, mishahara ni midogo, hailingani na hali halisi ya sasa na ndiyo maana hata rushwa wakati mwingine inakuwa kubwa kwa ajili ya mishahara midogo. Hebu mfanye *evaluation* ya maisha ya watu, mishahara ilingane na hali halisi ya maisha yalivyokuwa magumu.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nimwite …

## TAARIFA

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA**: Taarifa.

Mheshimiwa Spika, ahsante. Ili tuweke vizuri kumbukumbu katika *Hansard;* mchangiaji alisema kwamba, nimesema TAKUKURU ni Chombo cha CCM. Sikusema TAKUKURU nimesema Usalama wa Taifa.

**MBUNGE FULANI:** Kanuni ipi?

**SPIKA:** Basi ninadhani imesikika tunaendelea. Ninamwita Mheshimiwa Mnyika, atafuatiwa na Mheshimiwa Pauline Gekul.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Ninaomba Mwenyezi Mungu aniongoze na kunilinda, nitakapotoa mchango huu kwa siku ya leo. La kwanza, niseme kwamba, siungi mkono hoja iliyoko mbele yetu. Jana Hotuba iliposomwa wakati wa mapumziko nilipigiwa simu na baadhi ya Wananchi kutoka kwenye Jimbo langu; wazee, akina mama na vijana, wakanieleza kwamba, nisiunge mkono hoja hii iliyoko mbele yetu. Kwa sababu moja; Watumishi wa Umma wamepewa ahadi hewa, tafsiri inayojaribu kujengwa ni kama vile mishahara itaongezeka kwa asilimia 40, kitu ambacho sicho.

Mheshimiwa Spika, fungu lililozungumzwa la takriban shilingi trilioni 1.2 na kadhalika, limehusisha vitu vingi sana; wafanyakazi wapya, uhamisho wa wafanyakazi na mambo mengi sana kwa ajili ya mishahara peke yake. Kwa hiyo; ni vizuri kwanza wakati wa kuhitimisha hoja, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma), awaeleze Watanzania hali halisi ilivyo. Pamoja na majadiliano yanayoendelea, uzoefu wa nchi mbalimbali umeonesha kuwa, kima cha chini cha mshahara na kima cha juu cha mshahara siyo siri. Kwa hiyo, isemwe wazi kabisa ili pengo lijulikane na hali halisi ijulikane.

La pili, Bajeti hii inahusu ofisi nyeti kuliko zote katika nchi yetu, Ofisi ya Rais. Ofisi ya Rais kwa mujibu wa Katiba pamoja na kasoro zake, ibara ya 33 mpaka ibara ya 50, imeeleza ukuu wa Taasisi ya Rais, mamlaka makubwa aliyonayo Rais kama Amiri Jeshi Mkuu, kama Mkuu wa Shughuli zote za Kiongozi Mkuu wa Serikali, kama Mwajiri na Mwajiriwa Mkuu; ni mamlaka makubwa sana. Kwa hiyo, utumishi wote wa umma; iwe Watumishi wa Kawaida, Mawaziri au Mawaziri Wakuu, wote wanafanya kazi tu kwa niaba ya kumsaidia Rais; tafsiri yake ni nini?

Upungufu wowote ule tunaoweza kuuzungumza wa utekelezaji wa bajeti iliyopita, wa kuwajibika kwanza kabisa ni Ofisi ya Rais. Iwe ni upungufu wa TAKUKURU, mgao wa umeme na kadhalika, ndiyo Ofisi Kuu. Siungi mkono kwa sababu taarifa ya utekelezaji wa miezi sita ya mwaka mzima, lakini ni miezi sita toka Serikali iingie madarakani, haileti matumaini ya Ofisi hii kusimama ipasavyo kushughulikia kero za msingi za Wananchi.

Mheshimiwa Spika, sababu ya tatu, halafu nitajielekeza kwenye vifungu vya bajeti iliyoko mbele yetu; nimepitia Hotuba ya Waziri, ukurasa 61, linazungumzwa jambo linalogusa Wananchi wa Jimbo ambalo wamenituma kuwawakilisha. Kifungu cha (4) pale kinasema: “Mpango wa Urasimishaji katika miji imetajwa vilevile eneo la Kimara Baruti, Dar es Salaam, kwenye Mradi wa MKURABITA.

Sasa kama Chombo cha Serikali kinaweza kuzungumza kwa mwaka mzima wa bajeti kufanya urasimishaji kwenye mtaa mmoja tu, Dar es Salaam, Kimara Baruti, mtaa tu siyo Kata wala siyo Jimbo; tupo kwenye hali mbaya kama Taifa na tupo kwenye hali hii kwa sababu ya kukosa vipaumbele.

Mheshimiwa Spika, ukiingia kwenye Kitabu cha Bajeti ya Maendeleo, Fungu 30, ukurasa wa 33, MKURABITA imetengewa shilingi bilioni tatu peke yake mwaka huu wa

fedha wakati mwaka uliopita wa fedha ilitengewa shilingi bilioni sita. Tafsiri yake ni kwamba, tunarudi nyuma kwa ari zaidi, nguvu zaidi na kasi zaidi. Sasa ningependa kupata ufafanuzi kuhusu hili suala la MKURABITA, urasimishaji eneo la Kimara Baruti. Kwa sababu nina ushahidi wa barua ambayo ipo Ofisi ya Rais (Ikulu), ya Kampuni inayoitwa *Twiga Chemical Industry Limited,* ikisema kwamba, Wananchi wa Kimara Baruti, eneo la ekari nane waondolewe.

Sasa hili jambo kwa sababu tunajadili kuhusu TAKUKURU na Usalama wa Taifa, hapa ndiyo nafasi yao sasa. Hili jambo ni ufisadi mkubwa, Kampuni hii imelipwa shilingi bilioni tatu au milioni 3,000 fedha za umma kama fidia kwenye mazingira yasiyoeleweka kuhusiana na ardhi hii hii kinyume na agizo la Kamati ya Deni la Taifa katika kikao chake cha mwaka 2006 na inakusudiwa kulipa pesa nyingine shilingi bilioni 4.5. Sasa kama tuna pesa nyingi za namna hii za kulipa; kwa nini hatuzipeleki MKURABITA wakafanya urasimishaji wa Jiji zima la Dar es Salaam?

Ningeomba TAKUKURU na Usalama wa Taifa wachunguze mazingira ya malipo kwa Kampuni hii ya Twiga na tuelezwe ni kigogo gani ndani ya Serikali yuko nyuma ya Kampuni hii ya *Twiga Chemical Industry. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaomba sasa nijielekeze kwenye vifungu vya bajeti hii, ambayo tunayo hapa na tunaipitia. Nimezungumza kuhusiana na Fungu la 30 - Ofisi ya Rais. Sasa ukilinganisha Kitabu cha Maendeleo na Kitabu cha Matumizi ya Kawaida, Ofisi ya Rais kwenye Matumizi ya Kawaida, imetengewa pesa nyingi kweli kweli, yatakuja kwenye takwimu kuliko matumizi ya maendeleo. Sasa kitu ambacho kinanifanya nisiunge mkono Bajeti hii mpaka nipewe maelezo ya kina sana ni kasma mojawapo, kasma ndogo inayoitwa Matumizi ya Kitaifa.

Kwanza, ninaomba wakati Waziri atakapohitimisha hoja, alieleze Bunge kwa nini baada ya kuwasilisha Randama ya Wizara yake, hatujapewa nakala, kwa sababu tungepewa nakala, tungeingia ndani ya vifungu? Mimi ninafahamu kwenye kasma hii, shilingi bilioni 135 hazina mchanganuo, zinaitwa tu Matumizi ya Kitaifa. Halafu Bunge tunatakiwa tupitishe Matumizi ya Kitaifa Ikulu, shilingi bilioni 135.

Mheshimiwa Spika, ninataka atueleze fedha za bajeti iliyopita zilitumikaje kwa sababu tunaelewa fungu hili ndilo ambalo linatumika ukisikia safari nyingi sana za Rais nje ya nchi? Msafara mmoja wa Rais kwenda nje unagharimu kidogo sana ni shilingi milioni 50 na wakati mwingine msafara unakwenda mpaka shilingi milioni 200 na safari ni nyingi kweli kweli.

Hatukatai Rais kusafiri; Mwalimu Nyerere, alikuwa anasafiri, wazee wangu walioko hapa wanajua kwamba, Mwalimu alikuwa anakwenda Marekani kipindi chote cha Urais wake, alikuwa akienda Marekani basi anakwenda kwenye Kikao cha Umoja wa Mataifa *(UN).* Kama amekwenda kwa shughuli za kawaida, *State Visit* Marekani, Mwalimu Nyerere alikwenda Marekani mara mbili au tatu kipindi chote. Safari nyingine ni za kwenda Umoja Mataifa.

Mheshimiwa Spika, tungekuwa na muda tungeingia ndani zaidi Zambia, nina kabrasha hapa la Bajeti ya Zambia.

*(Hapa Mheshimiwa Mbunge alionesha kabrasha la Bajeti ya Zambia)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Zambia, Bajeti inaonesha kwa kina mpaka Rais anakwenda safari ngapi? Ninachosema, kupanga ni kuchagua, tupunguze kwenye fungu la shilingi bilioni 135 tuongeze pesa kwenye MKURABITA, tuwasaidie Watanzania waweze kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, wenzangu wamezungumza kuhusu Idara ya Usalama wa Taifa na TAKUKURU. Ningeomba pamoja na kukimbizana na mambo mengine haya, Idara ya Usalama wa Taifa na Idara ya TAKUKURU, watusaidie maeneo ambayo yana kero zaidi kwa Wananchi.

Kule ninapotoka, Jimbo la Ubungo, kero kubwa ni maji; sasa mtu atashangaa Usalama wa Taifa na TAKUKURU wanahusika vipi na maji?

Kule kuna kero ya maji, kwa sababu kuna rushwa kwenye mtandao mzima wa maji na Mradi wa Maji uliopo pale wa mabomba ya Wachina, uliwekwa ovyo ovyo; rushwa; wizi.

Mimi ninatarajia kwamba, Vyombo vya Dola, kazi za kawaida za Mawaziri, TAKUKURU ikachunguze mambo haya ya maji. Kule tunakerwa kweli na migogoro ya ardhi, wengine wanasema sasa TAKUKURU inahusika na Usalama wa Taifa wanahusika vipi na ardhi?

Mheshimiwa Spika, Usalama wa Taifa ulikuwa na mwakilishi ndani ya Kamati iliyoundwa ya Kuchunguza Migogoro ya Ardhi Mkoa wa Dar es Salaam. Kulikuwa na Mjumbe wa Usalama wa Taifa. Ninataka kujua, baada ya hapo, pamoja na kwamba Ripoti imekuwa ni ya siri na inapaswa kuwa wazi; mapendekezo yaliyokuwa mle ndani ya Ripoti ni pamoja na hatua ambazo Usalama wa Taifa na TAKUKURU wanapaswa kuzichukua.

Ninataka kujua kwenye mwaka wa fedha uliopita, Idara hizi zimefanya nini kushughulikia kero hizi za Wananchi wa kawaida sana.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba; ninaamini kwamba, ili tuendelee, pamoja na yale aliyoyazungumza Mwalimu, tunahitaji misingi mikubwa miwili, kwa maana ya kuwa na maono *(Vision)* na kuwa na maadili *(Values*). Sasa hii inatutaka tutoke kama Taifa kuwa na utamaduni wa haya mazoea ya ufisadi na tuanze kuwa na utamaduni wa uwajibikaji.

Binafsi, nilisema na nirudie kusema hapo kwamba; kwa hali iliyofikia ya mgao wa umeme hivi sasa; ni wazi kwamba, Waziri wa Nishati na Naibu wake kimsingi nilisema mwezi Februari na ninarudia tena leo, wanapaswa kujiuzulu.

Kujiuzulu kwao hakutatoa tija zaidi ya tija ya uwajibikaji kwa Taifa kama Ofisi ya Rais, haitafanya maamuzi magumu. Tarehe 15 Februari, 2011, Baraza la Mawaziri lilikaa likapitisha maamuzi wakati ule, mimi nikatahadharisha kwamba, haya maamuzi yasiposimamiwa vizuri, tutakuwa na mgao. Rais, tarehe 1 Aprili 2011; na ndiyo maana nimesema Rais aanze kwanza kusafisha Ikulu; kuna watu wanamshauri Rais vibaya, alitoa Hotuba kwa Taifa kwamba, Julai, megawati 260 zitafanya kazi.

Hii ni Julai; kuna mgao na kuna mgao mkubwa zaidi unakuja kwa sababu ya ufisadi kwenye Sekta ya Umeme na kwenye sekta ya gesi. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninasema hapa panahitaji uwajibikaji wa pamoja, siyo Wizara ya Nishati tu. Nimesoma kauli ya leo ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Pinda na nilitarajia kauli ile ingetolewa Bungeni; Waziri Mkuu, hajatoa kauli Bungeni kuhusu mgao wa umeme.

Kauli aliyoitoa Dar es Salaam kwenye matembezi ya Maonesho Saba Saba siyo ya Wizara ya Nishati, siyo TANESCO, inalipotosha Taifa vilevile.

Katika hatua tuliyofikia hivi sasa, ninahitaji kwenye majumuisho hayo ya Hotuba ya Rais, tupate kauli kutoka Ofisi ya Rais, kuhusu mgao wa umeme.

**SPIKA:** Ahsante umefunga vizuri. Mheshimiwa Pauline Gekul, atafuatiwa na Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah.

**MHE. PAULINA P. GEKUL**: Mheshimiwa Spika, nami nashukuru kwa kupata nafasi hii niweze kuchangia hotuba ya Waziri wa Utumishi. Nianze sehemu ya mishahara. Katika hotuba hii ya Waziri wa Nchi, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, wasemaji waliotangulia wamesema kwamba bado hatujaona dalili za mishahara ya watumishi wa umma kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kima cha chini kabisa katika mishahara ya watumishi wa umma Tanzania ni Sh. 135,000/=. Ni fedha kidogo sana. Watumishi hawa ndiyo wanaofanya kazi, hawa wanaolipwa kima cha chini, ma-*secretary* na madereva, lakini Maafisa mbalimbali kima cha chini hiki tulitegemea katika mwaka huu wa fedha kingeongezeka ili watumishi hawa waweze kupata ari ya kufanya kazi. Lakini ukisoma hotuba ya Waziri, naomba kunukuu, alisema kwamba: *“ Serikali itarekebisha mishahara ya watumishi kwa kuzingatia kasi ya mfumko wa bei na uwezo wa bajeti.”* Katika Bajeti ya Mwaka huu, haya ambayo Mheshimiwa Waziri ameyazungumza kwamba yatazingatiwa ili mishahara hii iboreshwe mimi sijaona. Hakuna kilichozingatiwa. Siyo mfumko wa bei, siyo suala zima la bajeti na wasemaji waliotangulia wamesema kwamba watumishi wamedanganywa, hakuna ongezeko kama hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini ukiangalia, hawa wanaopata kima cha chini kabisa hata wangeongezewa hicho ambacho wanaongezewa kwa hali halisi ya mfumko wa bei hawataona nyongeza hizo za mishahara. Mimi niseme kwamba Kambi ya Upinzani kwa muda mrefu tunaishauri Serikali kwamba waweze ku-*adopt* kima cha chini cha Sh. 315,000/= ili kiwasaidie watumishi wa umma. Mimi nafikiri sasa ni muda muafaka waangalie ni jinsi gani ambavyo watumishi hawa watalipwa kiasi cha Sh. 135,000/=. Ni fedha kidogo sana. Watumishi hawa ndio ambao ukienda sasa hivi maeneo ya vijijini na mijini ni wale ambao hata wanatamani wapewe mahindi ya misaada kwa sababu kiasi wanacholipwa cha Sh. 135,000/= ikikatwa mapato, anapokea 80,000/= halafu ni mtumishi wa Serikali. Miaka 50 ya Uhuru, mtumishi huyu anaanza na kima cha chini kidogo kiasi hicho! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ukiangalia katika ukurasa wa 13 wa hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, ameeleza jinsi gani ambavyo Serikali inapoteza fedha nyingi sana. Ameeleza mwaka jana fedha ambazo zimepotea katika Sekta ya Utumishi wa Umma. Ukiangalia katika ukurasa huo amenukuu pale kwamba mwaka 2009/2010 Serikali ilipoteza fedha takribani ya trilioni moja na bilioni 842 kwa watumishi wa Serikali kuu ambao wao wameachishwa kazi, wengine ni watoro na wengine wamekufa, fedha zimepotea.

Wakati huo huo ukienda katika Serikali za Mitaa, takribani shilingi bilioni 583,211 zimepotea tena kwa watumishi ambao ni watoro, wameachishwa kazi na wengine wamestaafu, hizo fedha zimepotea. Wakati huo huo mwaka wa fedha uliopita 2009/2010 kuna takriban ya shilingi bilioni 1.1 zimepotea kwa mishahara hewa. Halafu Serikali ukiibana, wanasema bajeti ndogo, hawawezi kuongeza fedha, hawawezi kuongeza kima cha chini ambacho Kambi ya Upinzani tuna-*propose* kiwe Sh. 315,000/= wakisema kwamba kasungura kenyewe kadogo, hatuwezi tukaongeza fedha hizo au kiasi hicho cha mishahara.

Mheshimiwa Spika, imefika wakati Waziri husika wa Idara hii aangalie kwamba watumishi hawa kulipwa kima cha chini, ni janga la kitaifa. Watumishi hawa ukiangalia mwisho wa mwezi wana madeni mengi, fedha hazitoshelezi, wakati huo huo zile ambazo zinatengwa katika Bajeti ya mwaka inavyotengewa fedha nyingi zinapotea. Mwaka jana kwa mahesabu hayo ambayo nimeweza kuyasema, takriban trilioni 2.5 zimepotea na Mkaguzi Mkuu wa Serikali amezungumza haya. Kwa hiyo, wimbo katika masikio ya watumishi wa umma kwamba fedha hazitoshi, huu wimbo sasa upitwe na wakati. Kima cha chini kiongezwe, kama Sh. 315,000/= haitoshi, basi ifike hata Sh. 400,000/= hawa watumishi waweze kuishi. Kwa sababu mfumko wa bei ukiangalia thamani ya dola ya Marekeni sasa hivi imefika 1600 halafu unasema kwamba umeongeza asilimia takribani 40 inapotea hewani. Huyu mtumishi mwisho wa siku hapati hiyo fedha.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kwamba hakuna sababu ya kuziba masikio, watumishi ambao wanalipwa kima cha chini cha laki moja na *point* haitoshi na kwa sababu ikizingatia kwamba imeshindwa kudhibiti mianya ya fedha hizo zinazopotea ambazo naweza nikaita ni *constructive corruption,* kwa sababu haiwezekani fedha ikapangiwa bajeti kwa mwaka halafu hizo fedha nusu nzima zinapotea.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu tumepangiwa *almost* trilioni tatu kama mishahara ya watumishi ya umma. Lakini ukiangalia mwaka jana fedha ambazo zimepotea ni zaidi ya trilioni 2.5. Kwa hiyo, nitoe ushauri kwa Serikali kwamba Wizara iangalie hata kuanzisha *server* ambayo itaangalia watumishi kwa nchi nzima waandae kwa sababu tumeingia kwenye huu utaratibu wa *TEHAMA*, hii teknolojia itusaidie katika Sekta ya Utumishi wa Umma, Wizara iangalie watumishi ambao ni takriban laki nne, siyo wengi. Waangalie *data* zao, wako wapi wanafanya kazi wapi, wamestaafu wapi, ili kuhakikisha kwamba hizo fedha hazipotei.

Mheshimiwa Spika, kama mtu amestaafu, kuna sababu gani ya kutuma pesa kule? Kama mtu amefukuzwa kazi au amewajibishwa, kuna sababu gani ya kutuma kule halafu hazirudi Hazina? Kwa hiyo, naiomba Serikali, hatuna sababu ya kuimba kila mwaka kwamba kima cha chini ni kidogo, naomba hiki kima cha chini kifanyiwe *review* upya ili hawa watumishi waweze kuishi kutokana na hali ngumu ya maisha kwa sababu hawa watumishi wanakwenda soko moja na yule anayepokea mshahara wa milioni moja yeye anapokea Sh. 80,000/=, nyanya ni hizo hizo ananunua, sukari ni hiyo hiyo kilo shilingi 2,000/=, hawataweza kuishi kwa kima cha chini hicho.

Mheshimiwa Spika, nihamie katika suala zima la madai na malimbikizo ya walimu. Chama cha Walimu Tanzania kinaidai Serikali shilingi bilioni 13, inasikitisha. Yaani walimu katika nchi hii matatizo yao hayasikilizwi kabisa mpaka waandamane. Sasa hivi wanatangaza mgomo na tumesoma kwenye magazeti jana, lakini siku wakigoma watu hawachelewi kunyoosha vidole kwa CHADEMA kwamba nyie ndiyo mnachochea.

Naiomba Serikali kwamba hakuna sababu ya kujificha kwenye kichaka cha kudharau au cha kutokuangalia watumishi madai yao. Ikifikia wanafunzi wamegoma, CHADEMA wamechochea! Walimu wanataka kugoma, CHADEMA wamechochea! Huu wimbo unatuchosha! Serikali ifikie hatua kwamba Watanzania wanafahamu. Hakuna chama ambacho kinachochea maandamano. Watanzania wanafahamu kwamba maslahi yao yakicheleweshwa *last resort* imebaki ni migomo. Haitatupeleka mahali ambapo tunategemea kufika. Naiomba Serikali hizi shilingi bilioni 13, wenzangu wameshazungumzia, kuna likizo za walimu, kuna matibabu, kuna uhamisho, kuna masomo, lakini pia Wakaguzi wanadai fedha nyingi na sekta nzima ya elimu ni matatizo. Naiomba Serikali iangalie suala zima la mahitaji ya walimu, madai yao wasiwape nafasi ya kuanza kuwaza migomo wakati huo wanafunzi wetu wanafeli katika shule mbalimbali, walimu watulie madarasani, haki zao wapewe.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha unapoona kwamba mwalimu amestaafu anadai mpaka leo. Walimu wa Singida, Mheshimiwa Diana Chilolo alizungumzia juzi kwamba wanadai pesa nyingi sana, lakini Serikali haisikilizi. Ni walimu wangapi ambao wanahangaika katika nchi hii? Sekta ya elimu iboreshwe, walimu hawatagoma endapo stahili zao wamepelekewa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda wangu unakimbia, naomba nizungumzie suala zima la Mfuko wa Rais *(PTF)* na mifuko mbalimbali ambayo inaanzishwa. Hii mifuko tunaisikia wananchi walio wengi. Lakini pia tumesoma katika hotuba mbalimbali, ukiangalia hii mifuko ikianzishwa kuna mifuko ya wake za Marais. Kuna Mfuko wa Mama Salma Kikwete - Mfuko wa *WAMA* na Mfuko wa Mama Anna Mkapa wa *EOTF* (Fursa Sawa kwa Wote) lakini kuna mabilioni ya kikwete. Hii mifuko yote naiomba Serikali hizi ni fedha za wananchi wanatakiwa wapelekewe kwa usawa. Maana ukisoma katika hii mifuko inayoanzishwa ni kuwezesha na kutoa mikopo na vitu kama hivyo. Lakini utakuta hii mifuko ina-*base* kwenye maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nasoma kwenye hotuba mbalimbali utasikia Kisarawe, Kibaha, Kinondoni. Wanawake na vijana wa Mikoa mingine katika nchi hii na wenyewe wanataka kuona hizi fedha zinawafikia. Kama haiwezekani hizi fedha kuwafikia, basi hakuna sababu ya kuanzisha hiyo mifuko. Inaweza ikawa ni matumizi mabaya tu ya fedha za walipa kodi. Naomba hii mifuko iangaliwe upya na hii mifuko iwasaidie wananchi wengi kadri inavyowezekana, lakini pia *geographical location* izingatiwe, sio mifuko inaanzishwa Dar es Salaam, kina mama na vijana wa Manyara wao hawaoni. Ninaomba mifuko hii iangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba kodi katika mishahara ya watumishi wa umma, asilimia 30 ya *Pay as You Eearn* ni kiasi kikubwa sana. Kambi ya Upinzani imeshauri kwamba ipinguzwe angalafu ifike asilimia 27. Ukiangalia mtumishi anayechukua mshahara wa Sh. 719,000/= asilimia 30 hiyo ikienda kupunguzwa ni pesa nyingi. Hizi fedha zipelekwe kwa watumishi, zitazunguka katika soko, uchumi utakua. Lakini watumishi hao ndio wanalipa kodi kwa kiasi kikubwa sana. Kilio cha watumishi kiangaliwe upya, hizi kodi ziangaliwe. Kambi ya Upinzani tumetoa maoni mazuri kwamba asilimia 30 ni kubwa, ipunguzwe ifike hata asilimia 27 au 25 ili watumishi waweze kubakiwa na chochote mikononi waweze kumudu maisha magumu na mfumko wa bei ambao unaendelea hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nimalizie na TAKUKURU. Kwa kweli nashangaa kwamba baadhi ya vitu ambavyo wanajivunia ni kwamba wamejenga ofisi nzuri katika Mikoa mbalimbali hata Manyara. Lakini tumesikiliza Hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati hiyo akisema kwamba TAKUKURU wamepewa magari 120 ikiwa ni sehemu ya mafanikio. Mimi niseme kwamba TAKUKURU bado kazi na hatuna sababu ya kurushiana kwamba TAKUKURU ni ya CCM na CHADEMA. Niseme kwamba TAKUKURU wameshindwa kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, rushwa imetapakaa nchi nzima, popote pale. Sasa hivi zinatolewa leseni mpya hizi *electronic*. Zile leseni ukiangalia ni Sh. 40,000/= lakini vijana wetu wakienda kutafuta zile leseni wanadaiwa rushwa. Katika sekta zote, Waheshimiwa Wabunge tunapata simu nyingi sana, vijana wanatuambia wanachajiwa mpaka Sh. 400,000/=, wakati leseni ni Sh. 40,000/=. TAKUKURU wako wapi wasione hawa wanaochaji vijana laki nne, wanashindwa kupata leseni?

Mheshimiwa Spika, TAKUKURU wasifurahi kukaa katika majengo mazuri, ofisi nzuri wakati haki za wanyonge hazipatikani. Ninaomba TAKUKURU waweze kuangalia kipengele cha leseni lakini pia waangalie rushwa ambazo zimekithiri kwenye maeneo mbalimbali. Kama rushwa kubwa za *Richmond* za *Radar* wameshindwa kuzifanyia kazi, basi watelemke chini wafanye kazi na wananchi, waangalie zile rushwa ambazo zinawaumiza wananchi wa hali ya chini. Mahakamani, Polisi barabarani rushwa zimekithiri, lakini TAKUKURU wako maofisini. Naomba TAKUKURU wakae chini na waone kwamba wanahitajika na jamii ili wawasaidie, rushwa ipungue katika jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niishie hapo na nasema ahsante kwa kunipa muda huu. *(Makofi)*

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda nizipongeze Wizara zote zilizopo chini ya Ofisi ya Rais, lakini nichukue fursa hii pia kupongeza Baraza lote la Mawaziri, naelewa kwamba wana kazi ngumu lakini nawapongeza sana kwa kazi zao nzuri. Vilevile nipongeze hotuba nzuri zilizotolewa na Waheshimiwa Mawaziri katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, leo naomba nianze moja kwa moja kwenye suala zima la *Radar*. Naomba Serikali itueleze kinagaubaga kuhusu suala la *Radar*. Zipo tuhuma nyingi, yapo maneno mengi yanayoongelewa kuhusu *Radar* mpaka Watanzania hawaelewi. Kwa hiyo, naomba leo niliongelee hili suala na Mheshimiwa Waziri atupe majibu. Kuna tuhuma kwamba kwenye *Radar* kuna wizi, kuna tuhuma kwamba kwenye *Radar* kuna ukwapuaji, lakini taarifa nzima ya *PCCB* inasema kwenye *Radar* hakuna tatizo lolote. Nataka Serikali leo itoe tamko hapa iwaeleze Watanzania kinagaubaga kuhusu suala la *Radar*. Tumechoka na suala la *Radar*. Kama kuna mwizi, atamkwe leo na kama kuna mwizi, kwanini Serikali haijampeleka Mahakamani mpaka leo?

Mheshimiwa Spika, tunataka tujue suala la *Radar* likoje. Naiomba Serikali itoe tamko hapa Bungeni na leo hii nitakuwa radhi kabisa kukamata mshahara wa Waziri asipotoa tamko kuhusu *Radar.* Tumechoka na suala la *Radar*! Nchi hii ina mambo mengi, tunataka tujadili maendeleo ya Watanzania, tufanye kazi ya kuwaletea maendeleo Watanzania na siyo kila siku suala la *Radar*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuongelea *Radar*, nitaongelea sasa suala zima la utawala bora. Ninavyojua mimi utawala bora ni kuheshimiana kwa viongozi, kuvumiliana, kufanya kazi kwa pamoja kwa heshima na taadhima. Pamoja na uhuru wa kuongea, kumekuwa na baadhi ya viongozi wanapanda kwenye majukwaa wanamkashifu Kiongozi wa Nchi hii ambaye ni Mheshimiwa Rais. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri aniambie watu wote waliopanda majukwaani au walioongea kwenye sehemu tofauti wakamkashifu Mheshimiwa Rais au kiongozi wa nchi, Wizara yake ya Utawala bora imewachukulia hatua zipi za kinidhamu na ni wangapi? Naomba Mheshimiwa Waziri atueleze hapa leo. Hatuwezi kukaa kimya, hatuwezi kunyamaza tukiona watu wakiendelea kumkashifu, kumsema vibaya kiongozi wa nchi yetu. Huyu ni Rais, lazima apewe heshima yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niongelee suala zima la TAKUKURU. Kwanza kabisa nianze kuipongeza TAKUKURU kwa kazi zao nzuri, lakini kazi yao ni ngumu zinahitaji hekima, busara na uvumilivu. Nawapongeza kwa kufuatilia Mfuko wa Pembejeo kama walivyoongea kwenye hotuba yao ukurasa wa 59 *paragraph* ya pili. Kwa kweli pembejeo ni muhimu sana katika nchi yetu kwa sababu kilimo ni uti wa mgongo katika nchi hii. Nawapongeza sana. Nawapongeza pia kwa kusimamia Sheria ya Uchaguzi. Sheria hii imesaidia sana, lakini bado kuna upungufu wa hapa na pale na nina imani kabisa kwa sababu kitu ndiyo kwanza kimeanza, lazima kitakuwa na upungufu, lakini nitawaomba wakae pamoja na wadau wengine warekebishe ili sheria hii ikae vizuri angalau mwaka 2015 ifanye kazi kwa ubora zaidi kuliko ilivyofanya mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, napata shida kidogo baadhi ya watu wanapotoa taarifa za uzushi na wenyewe wanaziafiki taarifa za *Wiki leaks* ambazo zilisema kwenye vyombo vya habari kwamba *PCCB* inashindwa kukamata wala rushwa wakubwa kwa sababu inamwogopa Mheshimiwa Rais. Nasema taarifa hizi siyo za ukweli, ni za uongo, ni za uzushi na ni za uchonganishi mkubwa. Baada ya taarifa hizi kutoka TAKUKURU walikanusha, lakini Serikali ya Marekani haikukanusha. Naamini Serikali ile ni makini, inajua vyombo vikubwa vya usalama kama ingekuwa Mkurugenzi wake wa *PCCB* amesema uongo, lazima wale Marekani wangekanusha kwamba TAKUKURU ni waongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naamini kwamba *weakleaks* ni wachonganishi wakubwa, wanataka kutuvuruga na kuvuruga amani Tanzania. Ukitaka kujua kwamba *PCCB* wanafanya kazi vizuri sasa hivi wamepeleka Mahakamani kesi *grand corruption*, kesi 24 siyo kitu kidogo, ni kazi ngumu, inahitaji ujasiri. Kwa kweli inabidi tuwapongeze sana TAKUKURU.

Mheshimiwa Spika, *weakleaks* tusipoiangalia itatugombanisha na itatupunguzia maelewano yetu baina ya taasisi zetu na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Rais kwa hekima zake, busara baada ya kusikia suala hili la uzushi, nadhani alitumia vyombo vyake vya usalama vikamwambia hivi vitu siyo kweli na akaendelea kuwepo na Mkurungenzi wa *PCCB*. Naamini vitu hivi vingekuwa vimefanyika, Rais asingekubali leo Mkurugenzi wa *PCCB* Dokta Hoseah kuendelea kuwa Mkurugenzi. Kwa hiyo, nasema hiki kitu siyo kweli, *PCCB* wanafanya kazi na tunaiona.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa mfano mdogo wa nchi ya Uganda, Mbunge mmoja amesema kwamba kulikuwa na Mkuu wa *PCCB* anaitwa Justice Mubya yule Bwana alikuwa anafanya kazi vizuri sana, alikuwa anapambana na *corruption* lakini baadhi ya wanasiasa wakaingiza uchonganishi mpaka wananchi wakashindwa kumwelewa, yule Bwana akaamua kujiuzulu. Kwa hiyo, ninawaomba Watanzania tusifike huko.

Mheshimiwa Spika, *South Africa* kulikuwa na mtu anaitwa Leonard Macath, alichonganishwa na Rais wake, akachonganishwa na wanasiasa, akachonaganishwa na wananchi kwa sababu yeye alikuwa anafanya kazi kwa uadilifu mkubwa. Alifanya kazi ya kutetea maslahi ya wanyonge, alikuwa anafanya kazi kwa kulinda raslimali za *South Africa*, lakini leo hii huyu mtu akafukuzwa kazi na mpaka sasa hivi hayupo tena kwenye Taasisi na Wa-*South Africa* wanamkumbuka. Tumezoea sana mtu akifanya mambo mema hasemwi, lakini atakapokufa watasema yule mtu alikuwa anafaa sana.

Mheshimiwa Spika, hata leo tukiamua Mkurugenzi huyu wa *PCCB* tuliyenaye atoke, mimi nina imani tutamkumbuka sana. Mkurugenzi huyu anafanya kazi sana, ni lazima tukiri na tumpongeze. Ni lazima tumtie moyo, yasije yakatukuta mambo kama yaliyowakuta nchi nilizozitolea mifano.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa Watanzania wenzangu, tuachane kabisa na mambo ya mitandao ya kwenye kompyuta. Tuachane nayo, kwetu hayana tija. Tujikite kufanya kazi, tujikite kujenga Taifa letu na kuleta maendeleo kwenye nchi yetu change, tuilinde amani yetu tuliyonayo Watanzania, tuilinde demokrasia yetu, tuwe na uzalendo kama nchi nyingi huko nje zilivyo na uzalendo sana, tusikubali mtu anayetoka nje kuja kutuchonganisha na sisi tunamuunga mkono au tunafanyia kazi taarifa zake za uchonganishi.

Mheshimiwa Spika, naomba tuwaache *PCCB* wafanye kazi, wanaweza na wastahili sifa na pongezi kubwa. *Grand corruption* siyo kitu kidogo, ni kitu kikubwa sana. Wameweka historia katika nchi hii. Kukamata kesi 24 na kuzipeleka Mahakamani, hiyo ni *risk* kubwa wanayoifanya. Tunampongeza sana Mkurugenzi wa *PCCB*, tunamtia moyo na tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumpa ujasiri atufanyie kazi nzuri Watanzania, matatizo madogo anayafahamu, mmemwambia nadhani atayarekebisha.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri wa Utumishi. Suala zima la MKURABITA lipo Tanzania nzima, kama halipo, ni sehemu chache sana na kila sehemu imeguswa kidogo kidogo, haliwezi likaguza kila sehemu kwenye kila Wilaya, inagusa mtaa mmoja, vijiji vitatu vijiji viwili, lakini sasa hivi hakuna Mtanzania yeyote ukimwambia habari ya MKURABITA awe hajui. Wanajua, naipongeza sana Wizara husika.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie sasa la maadili. Sasa hivi ofisi zetu hazina siri, siri za Serikali zinakuwa zinatoka nje, kila kitu unakikuta kwenye kwenye magazeti kiko wazi, kwenye TV kinaongelewa, unabaki unashangaa maadili yameporomoka kweli kweli. Namwomba Waziri atueleze ameshawachukulia hatua watumishi wangapi waliotoa siri za Serikali hadharani na ni hatua zipi alizozichukua ili tukomeshe tabia hii ya kuvujisha siri za Serikali nje?

Mheshimiwa Spika, naomba nijikite kwenye ajira za Halmashauri za Miji. Halmashauri za Manispaa zilikuwa na nafasi ya kuajiri watu wa ngazi za chini hususani Madreva na wahudumu. Kitu cha kushangaza, sasa Serikali kuu imehodhi madaraka

hayo, inaajiri wao wahudumu na madereva kiasi kwamba inanyima haki kwa Watanzania. Kule kwetu Urambo Kapihula kwa Mheshimiwa Sitta, leo inatangazwa nafasi ya udereva, anapata wapi hizo taarifa mtu anayekaa Kata za Kijijini ambako hakuna TV na magazeti hayafiki kwa wakati? Kwa hiyo, Serikali hii inawanyima Watanzania wengine nafasi ya kufanya hizo *interview*. Lakini hata kama anapata taarifa, hiyo nauli ya kumtoa huko kijijini na kumpeleka Dar es Salaam kwa muda huo inatoka wapi? Huko Dar es Salaam anafikia kwa nani? Je, anapajua? Tunamwomba Waziri arudishe madaraka hayo kwenye Halmashauri za Manispaa. Kule kuna Bodi za Ajira, lakini cha kushangaza hata safari hii kumewekwa Bodi za Ajira wakati madaraka yote wamehodhi wao. Huo ni urasimu. *Central Government* iajiri mpaka mhudumu jamani! hiyo siyo sahihi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali Kuu iturudishie madaraka kwenye Halmashauri zetu za Wilaya tunaweza, tumeweza kuendesha Halmashauri, tumeweza kufanya maendeleo makubwa kwenye Halmashauri, tutashindwaje kumwajiri Dereva na Mhudumu? Matokeo yake ni kwamba wanaoajiriwa sasa ni watu wa Dar es Salaam, na watu wa Mikoani hawapati ajira. Hii itatuwekea uwiano mbaya wa Watumishi wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetusaidia imetuwekea Sekondari, *VETA*, watoto wetu wanaomaliza *Form Four* wanaweza wakapata hata kazi ya uhudumu kama watashindwa kuendelea na masomo. Mfano, katika Mkoa wa Tabora kuna Chuo cha *VETA* kikubwa sana Serikali imetujengea, tunazalisha madereva kila siku lakini unaponiambia waje wafanye *interview* Dar es Salaam: Je, wanazo nauli? Au unataka kuweka watu wa Dar es Salaam tu na watu wa Mikoani na Vijijini wakose hizo nafasi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM A. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii. Pili, naomba kuunga mkono hotuba zote mbili za Waheshimiwa Waziri wa Mahusiano na Uratibu pamoja na Waziri anayeshughulika na Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina michango mitatu kuhusiana na hotuba hizo mbili. Kwanza, naomba kuchangia kuhusu Tume ya Mipango. Katika uwasilishaji wake Waziri anayehusika na Mahusiano na Uratibu, moja ya rejea aliyotupa hapa Bungeni ni majukumu makubwa ya Tume ya Mipango, moja ikiwa ni kuibua na kufanya utafiti wa kina kuhusu uchumi na masuala ya kiuchumi kiujumla kwa ajili ya kuiendesha nchi hii, vile vile kuifanya Tume yetu ya Mipango kuwa *think tank* kwa ajili ya kusaidia kuongoza mwelekeo wa uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, hayo ukitazama yanatakiwa yajitafsiri katika takwimu. Upande wa takwimu suala la kuipa nafasi Tume ya Mipango kuwa kweli *think tank* yenye uwezo wa kuibua na kufanya tafiti za kina kwa ajili ya kusaidia uchumi huu ni lazima takwimu za utafiti *research budget* tuweze kuiona. Lakini kwa bahati mbaya ukiangalia takwimu zinaonekana hazithibitishi hilo. Pili, kuiwezesha Tume ya Mipango

kuwa *think tank* ni vizuri tukajua *required compentances* ambazo ni lazima ziwe pale ili kuhakikisha kwamba wao wamekaa kimtambuka kwa ajili ya kusaidia ku-*address all the issues* ambazo zinatukabili, wao kama *think tank* kwa niaba yetu, ingawae wote tutasaidiana pamoja nao lakini wao ni lazima waanze kama *think tank*.

Mheshimiwa Spika, hotuba inaeleza vizuri lakini wangetusaidia kuona kitaifa tunaposema wenzetu ni *think tank*, ni *collection* ya *compentances* ambazo ni lazima tuhakikishe sisi Tume ya Mipango kila wakati inazo. Kwa hiyo, nashauri viangaliwe ili kuwa na *think tank* ambayo ipo *all weather* na inaweza ika-*address* mambo yote muhimu ambayo yapo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ni mawazo yangu kwamba tunaposema kuwezesha wananchi wetu, basi tuchukue uamuzi ambao kweli utasaidia kuwezesha wananchi. Tunahitaji sasa ku-*create indegeneous industrialist*, nchi hii itambue kwamba tunahitaji kuwezesha matajiri katika viwanda wazalendo. Ninavyofahamu mimi, *if we can build this base* tutakuwa na *reliable industrial base* kwa ajili ya kuongoza uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, ninavyofahamu mimi, nchi zote hazikuweza kuendelea kwa kutegemea *direct investment* kutoka nchi za nje, ziliweza kuweka *a comprehensive package* ya kusaidia kujenga uwezo wa *local indegeneous* kuwa *strong industrialist* ambao walifanya nchi zao zika-*move from a low level* kwenda kwenye *middle economies*. Walifanya maamuzi ya makusudi kabisa kuwawezesha wananchi wa nchi zile kuwatajirisha na wale ndiyo walioweza kutengeneza *economic multiplicity* ya kuweza ku-*create more employment, more industries* na ku-*reinvest* kwa sababu tutakavyofanya hivyo, ndivyo tutajenga uchumi wa ndani.

Mheshimiwa Spika, uchumi wa ndani utatuwezesha sisi wenyewe ku-*invest* na ku-*reinvest* kwa sababu tumewawezesha wananchi wenyewe. Naomba Serikali itazame namna hiyo, hapo ndipo tutakapokuwa tumelenga kwenye uhakika wa kuiwezesha nchi hii i-*move* kwenda kwenye *industrial level*. Tukitegemea *direct investment* ya watu kuja ku-*invest* kesho wanapata *profit* wana-*repatriate* kwao, kwa hiyo, nchi inabaki na tatizo lile lile lililokuwepo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumza masuala ya vipaumbele na tuna mpango wa miaka mitano, kwamba vipaumbele vyetu vitano ambavyo tumekubaliana katika bajeti hii viendelee kuwa vigezo kwa ajili ya mpango wetu wa maendeleo wa miaka mitano na tukubaliane tuwe na vipaumbele ambavyo ni endelevu ambavyo havibadiliki mwaka kesho. Ikiwa kwa bahati mbaya mwaka kesho Wizara ya Fedha au Serikali kwa ujumla itakuja na mabadiliko ya vipaumbele tutakuwa tunaanza tena. Kwa hiyo, vipaumbele ambavyo tumevitambua kwamba ni vya muhimu kwa ajili ya nchi kuleta maendeleo, ni lazima tukubaliane viwe endelevu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, umeme ni lazima tuhakikishe hiki ni kipaumbele, mwaka huu mpaka *next five years* hapa tumemaliza, vivyo hivyo vipaumbele vyote

muhimu ambavyo tumekubaliana. Tusikubali kuwa na vipaumbele vinavyobadilika kila mwaka, hapo tutakuwa hatufanyi kazi ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni suala la mishahara hewa. Akili ya kawaida inashindwa kutathmini au kuelewa, inakuaje nchi ambayo tayari ina watu wanaomeneji *financial resources*, tunakuwa na mishahara hewa ya watu maelefu, hatupati lalamiko *from the collection point?* Hii mishahara, wale wanaopewa kwa ajili ya kuingiza kwenye akaunti za watu wengine, hata kama tunaweza tuka-*claim* kwamba *at the collection point* mishahara ile inaingia *direct* kwenye akaunti inakuwaje tumefika mahali hatuna *control*, na hatuna malalamiko kwa ajili ya kuleta *feedback* kwa *Paymaster General*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, suala la mishahara hewa likiendelea kufumbiwa macho, hata kama kuna *strategies* kiwizara, zimewekwa hapa, kwa upande wangu hazitoshelezi kwa sababu mishahara haiwezi kwenda kwa watu wanaoitwa hewa. Hakuna watu wanaoitwa hewa. Hakuna watu ambao wanaweza wakapata pesa bila kuingiziwa kwenye akaunti zao, au bila kulipwa kwa utaratibu wa kawaida. Haiwezekani ile *a spot check* ya siku moja ambayo tutashirikisha Wizara ya Fedha pamoja na wote *Government Ministries* walipwe siku moja dirishani ikawa ndiyo *solution*. *We must check ourselves what is major problems*. *Major problem* ni *integrity*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tujitazame, tuna tatizo la *integrity* na tusipofanya hivyo Serikali itaendelea kuwa na tatizo sana kwenye ku-*manage* fedha. Kwa hiyo, suala la mishahara hewa lisifumbiwe macho na Wizara zote kutoka ofisi ya Waziri Mkuu mpaka kwenye Halmashauri zetu. Ninaelewa kuna mahali ama jambo hili linafanyika kwa kusudi na kwa sababu kuna watu fulani wananufaika, lakini lisiwe suala ambalo litaichafua Serikali kwa sababu ninafahamu sehemu nyingine duniani vilevile yametokea matatizo ya mishahara hewa, lakini waliweza kuya-*manage*. Kwa hiyo, Serikali hii tu-*maintain intergrity* kwa kuhakikisha kwamba mishahara hewa inakuwa historia.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ni lazima kwa maamuzi ya msingi kabisa mishahara ambayo wananchi wamekuwa wakiingoja, *cost of living* imekuwa *very high*. Ni vizuri basi Serikali kama walivyosema wengine, tupate ufafanuzi ni kwa kiwango gani kama mishahara imepanda kwa kufikia mishahara gani ili wananchi wapate picha na waweze kuwa na uelewa wa kuambiwa siyo *speculation*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni wakati wa kuhakikisha kabisa mishahara imepanda ili wafanyakazi waweze kukidhi *cost of living* ambayo iko *very high*.

Mheshimiwa Spika, nimeona kwamba kwa dakika hii, haya ndiyo yawe sehemu ya mchango wangu. Nakushukuru sana kwa kupewa muda. *(Makofi)*

**MHE. SELEMANI SAID JAFO:** Mheshimiwa Spika, kwanza, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa sababu nilikuwa na shaka ya muda inawezekana nisipate muda wa kuchangia. Lakini nimepata fursa hii japo kuongea machache katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye ni mfanyakazi namba moja katika Jamhuri yetu ya Tanzania. Sisi sote tunaona na tunashuhudia tokea jana alikuwa kule Kigoma akiwahudumia Watanzania katika suala zima la miundombinu ya barabara. Kwa kweli hii haitii shaka kwamba Rais wetu ni Rais shapavu ambaye kwa kweli anajituma katika muda wote wa masaa yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ninasikitika sana, baadhi ya watu wanatumia vinywa vyao vibaya katika suala zima la kumtamka Rais. Hii mimi inanisikitisha sana. Wengine wanatumia vibaya vinywa vyao kuishawishi Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba Rais anasafiri sana nje, kana kwamba hawajawahi kusoma dini. Hata ukiangalia, Nabii Sulemani alikuwa na mnyama wake anaitwa huduhuda ambaye yeye kazi yake ni kufanya *research*. Wakati mmoja yule aliondoka katika nchi moja inaitwa Saba, sasa hivi ni nchi ya Yemen ndiyo *study tour* kwa ajili ya nchi yake na jeshi lake. *(Makofi)*

Kwa upande wa Waislam, wanajua kuna kisa cha Issa na Miraji, Mtume alisafiri kwa nchi za mbali mpaka Angani kwa ajili ya kupata *study tour* kwa ajili ya waja wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Kikwete anavyosafiri hafanyi jambo la ajabu, analifanya jambo kwa ajili ya mustakabali wa Tanzania yetu hii. Mangapi tunayaona ambayo ni bora, sisi Watanzania tunayashuhudia? Lakini ninasikitika, watu hatujivunii katika hilo. *(Makofi)*

Sasa naomba kuwazungumzia wale watu ambao Wabunge wao wamesema kwamba wao hawaungi mkono hoja. Mimi sasa nawaombea wafanyakazi, Wabunge wao wanasema hawaungi mkono hoja hii ya Serikali. Mimi nawapongeza sana wafanyakazi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa wanayoifanya kwa mustakabali wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini napenda kuwapongeza Mawaziri kwa hotuba zao. Waziri wa Utumishi, katika kitabu chake cha hotuba ukurasa wa 69 kinajiainisha kwamba kwa bajeti ya mwaka huu, bajeti imeongezeka kwa asilimia 40.2 sawa sawa na shilingi bilioni 938 ni asilimia kubwa sana imeongezeka. Jamani katika hili, lazima tushukuru kwamba Serikali imesikia kilio cha wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Wabunge tusiwe wapotoshaji wa kwanza. Serikali ikifanya vizuri, semeni Serikali katika hili imefanya vizuri. Tutumie sasa utaratibu wetu wa Katiba inavyotueleza kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) kwamba ongezeko hilo tunashauri vipi Serikali, jinsi gani litawagusa wafanyakazi wetu wa Tanzania, siyo kubeza tu, itakuwa haifai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nikijikita katika ukurasa huo, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, amebainisha wazi kwamba bajeti ya mwaka huu imeongezeka kwa asilimia 40.2. Lakini namshauri Waziri kwamba ongezeko hili naliomba sana liende

likawaguse wafanyakazi wenye kipato cha chini. Tuna Walimu wetu ambao hawajui posho yao, hawajui kwamba wana *per diem* wanafundisha wanakula chaki muda wote. Tuangalie jinsi gani hawa ndio wa kuweza kuwagusa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mabwana shamba ambao wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Kuna Askari Polisi, kuna makarani wa ofisini ambao kipato chao ni kidogo sana. Kuna manesi wetu wa hospitali ambao mshahara ni mdogo sana. Namshukuru Waziri kwa sababu hakuainisha kwamba ataongeza kwa asilimia 40, hapana, hilo ni ongezeko la jumla. Sasa sisi kwa nafasi yetu ya kuishauri Serikali, naomba kumshauri Mheshimiwa Waziri kwamba atumie fursa hii sasa kuangalia kwanza hii kada ya chini, tusiongeze *flat rate percentage*, tutakuwa tunawadhulumu hawa wafanyakazi wa kada ya chini. Kwa sababu ukiongeza kwa mfano kwa asilimia 10 kwa kila mfanyakazi, Mkurugenzi maana yake ataishi vizuri kuliko karani anayefanya kazi pale ofisini. Naomba tuangalie jinsi gani tutawalenga hawa wafanyakazi wa kada ya chini *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kushauri kwamba katika wafanyakazi tunaoajiri katika Idara yetu, watu ambao mara ya kwanza wanapata ajira ya kwanza inakuwa ni tatizo kuingizwa katika *payroll*. Watu hawa huwachukua zaidi mara nyingine hata miezi mitatu bado hawajaingia katika *payroll*. Watu hawa wanadhalilika sana. Kwa bahati mbaya, kama wafanyakazi, mfano, Walimu wa kike ambao wameajiriwa, wengine wanafadhiliwa inakuwa ni hatari jamani. Lazima wapate stahili zao mapema zaidi ili kuajiri waweze kukidhi maisha yao. Lakini hiyo haitoshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala zima la malimbikizo ya madeni ya Walimu na wafanyakazi mbalimbali. Kuna watu wengine kutoka mwaka 1998, wanadai mpaka hivi sasa. Hawa ndio watu wa kwanza kuwalipa madeni yao. Ndugu zangu hii ni kero! Kwa hiyo, nikimkumbusha Mheshimiwa Waziri, mwana mama shupavu kweli kweli, na kwa kweli namsifu kwa nguvu zote. Naona hili utaliangalia kwa umakini zaidi ili mradi wafanyakazi wa Tanzania watakuwa wanakukumbuka katika mustakabali wa maisha yao ya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuna tatizo lingine la ugonjwa. Bahati nzuri wenzangu wamelizungumza. Kuna wafanyakazi wanakwenda kujiendeleza, kwa mfano, kuna kada ya uhasibu, kuna watu wamekwenda kuchukua *CPA* lakini wakirudi Halmashauri wanawekwa katika vitengo ambavyo hawatambuliki kabisa. Hili ni tatizo. Namwomba Waziri mwenye dhamana apitie Halmashauri zote atakutana na watumishi ambao wamekwenda kuchukua *CPA* lakini wamekwa katika vitengo ambavyo hawajulikani kabisa. Tunazungumza matumizi mabaya ya fedha za Serikali, lazima hili tulisimamie vizuri ndugu zangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo linguine, kuna suala zima la watu wanaostaafu kazi, hili linatia uchungu. Mtu amefanya kazi miaka yote, siku anapostaafu anaambiwa alete barua yake ya ajira alipoajiriwa, mtu amefikia miaka 60, leo hii unamtaka barua yake ya kwamba siku alipoajiriwa, hii ni kumnyima haki mfanyakazi huyo aliyetumikia Taifa hili. Wengine mpaka wanakosa mafao yao. *(Makofi)*

Namwomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana alisimamie hili na aliangalie kwa kina sana kwamba tuna watu ambao kwa kweli wanakerekwa kwa kina sana kwamba tuna watu ambao kwa kweli wanakereka na wanahangaika sana na wengine imefikia mpaka sasa hivi hali yao ni duni kweli kweli, hata nauli ya kulipia kuhangaika katika hizo Halmashauri hawana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nijielekeze pia katika suala zima la ajira. Wenzangu wengi wamelizungumza, lakini na mimi lazima niongezee katika eneo hilo. Ndugu zangu, kuna ajira, kwa mfano watalaam tunaowahitaji katika Halmashauri zetu na kazi zetu mbalimbali hii naona ni wazi kwa kweli Sekretarieti ya ajira iweze kufanya kazi yake. Lakini hata dereva! Ukija kwangu kule Kisarawe nina madereva wamekaa wako kibao wanatafuta ajira. Leo unamwajiri dereva anakuja pale Kisarawe unamkabidhi gari la Mkuu wa Wilaya, hata kijijini kwenyewe hakujui, anakwenda wapi? Sasa inakuwa ni hatari kama Mkuu wa Wilaya ndio mgeni na dereva ni mgeni, wanaulizana, tunaanzia wapi, tunaishia wapi? Hii ni hatari.

Mheshimiwa Spika, kwa nini tusifanye hata hizi kada za chini madereva walioko katika maeneo yetu wakaweza kuajiriwa na kufanya kazi? Kwa nini wahudumu wa ofisi watolewe katika Mkoa mwingine wakati maeneo husika tuna kila sababu ya kuhakikisha kwamba watu wanapata ajira? Hili jambo hatuwezi kulifumbua macho. Mengine tutafumbia macho, lakini katika hili hatuwezi kulifumbia macho. Kama tunasema suala la *decentralization*, lazima tuhakikishe Halmashauri zina *power* na ziweze kufanya kazi yake kwa mujibu wa taratibu zinazotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumezungumza suala zima la mishahara hewa. Suala la mishahara hewa, hili jamani ni donda ndugu. Naomba kutahadharisha Wabunge wenzangu, naomba niwaeleze Wabunge wa CCM kwamba suala zima la mishahara hewa kuna watu wanatumia fursa hii kwa ajili ya kuhakikisha Serikali ya CCM haifanyi vizuri. Naomba sisi tuwe wa kwanza kuwakaba koo na watu hawa ndio wanauza nyaraka kwa watu ambao hawako sawasawa. Kwa mujibu wa ripoti ya Mkaguzi wa Serikali, nimeonyesha kwamba shilingi bilioni 1.1, hii imepelekwa Wilayani, halafu hazikurudi. Zaidi ya milioni 500 zimelipa watu ambao tukija kutoa katika mishahara ya wafanyakazi maana yake tungelipa zaidi hata hiyo asilimia 40, hawa watu wanaofanya hivi lazima tuwafanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri aweke rekodi kwa Tanzania, mwanamke wa kwanza kuisimamia Tanzania mpaka watu waliofanya ubadhirifu katika Serikali wachuliwe hatua za kutosha. Hili hatuwezi kulifumbia macho, watu hawa wanaosababisha mishahara hewa na watu hawa ndio wanaouza *document*. Leo hii mtu anasema *document* ya Ikulu ameipata, ameipatapataje? Hii inatisha! Katika hili hatuwezi kulivumilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, kwa sababu muda wenyewe mdogo na watu ni wengi, naona nimalize na wengine waje kuzungumza. Naomba tuhakikishe kwamba tutakaa miaka yote, lakini mwisho wa siku kama anavyosema ndugu yangu Sanya,

tutamkumbuka Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kazi kubwa aliyoifanya kwa suala zima la Utawala Bora. Kila mtu ana uhuru wake wa kuzungumza, midomo imekuwa mipana kila mtu ana haja ya kuzungumza alitakalo ni kwa ajili ya utawala bora. Tusingekuwa na utawala bora watu wasingethubutu kuinua vinywa vyao. Lakini utawala bora huo watu wengine wanaanza kukebehi kwamba siyo sawa sawa. Hii haiwezekani hata siku moja. Lazima tuthamini katika hili.

Mheshimiwa Spika, kikubwa kinachosumbua ni husda. Husda maana yake mtu hata akifanya vizuri, wewe roho inauma maana yake ndiyo husda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nasema Mheshimiwa Rais atakapomaliza muda wake sisi sote tutamkumbuka na tutasema ameacha historia kwa Tanzania. Historia hii itazidi kuendelea miaka yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Naunga mkono hoja kwa asilimia zote mia kwa mia. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru nami kwa kupata nafasi hii kuchangia. Tunachochangia ni hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Mahusiano na Uratibu, Sheria na Utawala. Kwanza niseme kwamba tunachangia Ofisi ya Rais ndiyo maana hawa watatu wameitwa Mawaziri wa Nchi, katika ofisi hii. Nataka nikumbushe kitu cha kwanza kama angalizo. Rais ambaye tunachangia hotuba yake alichaguliwa na wananchi wa Michenzani, Chokocho, Kisiwa Panza, Mtambwe na Bogoa. Hakuchaguliwa na wananchi wa Kyela na kule Iringa sehemu nyingine tu, kwa hiyo, ni Rais wa Watanzania wote. Hilo ni angalizo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, angalizo la pili, nataka kwanza ninukuu maneno ya Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU. Katika semina aliyowafanyia Wabunge, anasema hivi kazi ya Bunge ni kuona kwamba Serikali inawajali wananchi wake na kuhakikisha maslahi ya umma yanazingatiwa wakati wote. Serikali inapotoa maamuzi yanayoathiri haki za kila raia, msisitizo mkubwa katika kuhakikisha kuwa rushwa inadhibitiwa ni kwa Serikali kuwa wazi zaidi, kuwajibika katika maamuzi yake, kuhakikisha Watanzania kuwa maamuzi yake yanafikiwa yanazingatia maslahi ya nchi ya Watanzania na Bunge lina wajibu huu wa kikatiba kuona kuwa uwazi na uwajibikaji unazingatia wakati na kuwa ni sehemu ya utamaduni na utawala bora.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huu, nakusudia kwa utangulizi huu, kutakuwa na watu wa aina mbili. Ni kwamba Wabunge tunaposimama hapa tukailaumu, tukaikosoa Serikali au baadaye mtu mwingine akaingiza mambo ya kichama, huu siyo wajibu wetu wa Wabunge. Wajibu wa Wabunge, ni kuwatumikia wananchi na hapa ndani tusionyeshe kabisa maslahi ya kichama. Ikiwa inayolaumiwa ni Serikali ya CCM, wewe kama Mbunge, bado una haki ya kuwatetea wananchi, siyo kuilinda Serikali inayofanya matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, sasa nijikite kwenye tatizo la waombaji kazi kutoka Zanzibar. Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Zanzibar pia tumo. Lakini hii Idara ya Utumishi, kuna Serikali hapa imevaa koti la Jamhuri ya Muungano ambayo ni Serikali ya Tanganyika au kwa jina linalopendeza siku hizi Tanzania Bara ambayo imevaa koti la Muungano na hizi ajira watu wengi wa Zanzibar wanazikosa. Nataka nimweleze Mheshimiwa Waziri, atueleze hapa leo atafanya nini kufungua ofisi za ajira Zanzibar ili wale watumishi wa Sekta ya Muungano wasiwe na taabu ya kuhangaika kuja Dar es Salaam, kuhangaika sehemu nyingine wakati sisi ni sehemu na hii ni miaka 50 au miaka 47 ya Muungano.

Lakini jambo la pili, nataka Mheshimiwa Waziri wa Utumishi atufahamishe leo katika majumuisho kwamba hawa vijana wetu wanaomaliza *University* na sehemu nyingine ambao wakitaka ajira suala kubwa wanaambiwa uzoefu. Wakienda popote pale Serikali wawe na uzoefu, mashirika ya kigeni yaliyokuja kuwekeza yanataka uzoefu. Serikali yetu itake uzoefu. Wakishamaliza masomo hapa, waende wapi? Naomba suala hili Mheshimiwa Waziri ulifafanue kwa maslahi ya Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ninataka kulizungumzia ni chombo cha Usalama wa Taifa. Vilikuwa ni vyombo viwili tofauti kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Jamhuri ya Muungano. Lakini ilifika mahali kwenye miaka ya 1980 chombo hiki kikaunganisha. Kuanzia mwaka huu uliounganishwa, hatujaona maslahi ya chombo hiki kwa Makao Makuu kujenga hata jengo lolote lile Zanzibar zaidi ya ofisi ndogo ndogo zilizokarabatiwa Pemba. Sehemu zote zilizoko ni zile zilizoanzishwa na chombo kilichokuwepo Zanzibar kutoka awali. Kuna walinzi wa viongozi mpaka leo Zanzibar hawajajengewa nyumba hata moja na wanapata taabu. Lakini upande mwingine wa Jamhuri, tayari nyumba ziko za viongozi. Mheshimiwa Waziri atueleze Ofis yake inafanya nini kwa suala hili?

Mheshimiwa Spika, kuna wastaafu wa vyombo hivi vya Muungano, mpaka leo maslahi/stahiki zao ni taabu sana kuzipata mpaka wafuatilie huku na wana taabu sana ya usafiri wakati watu wanyonge hawana kitu tena. Mheshimiwa Waziri, masuala hayo leo tafadhali utueleze na hili siyo ombi, ni wajibu wetu wa Mbunge kutupa maelezo kamili.

Mheshimiwa Spika, tuje suala la utawala bora na haki za binadamu. Kabla ya kuja, ninukuu Azimio la Ulimwengu juu ya Haki za Binadamu ambapo kifungu cha 11 cha azimio hili kinasema kila mtu anayeshitakiwa kwa kosa la kuvunja sheria ana haki ya kuangaliwa kama siyo mkosefu mpaka ithibitishwe kisheria kwa hukumu hadharani kwamba ana hatia. Lakini kipengele cha 11(2): "Mtu yeyote asitiwe hatieni kwa tendo lolote au jambo lolote ambalo halikupinga Sheria ya Taifa au kati ya Mataifa wakati alipotenda, wala asipewe adhabu kali zaidi kuliko ile iliyokuwemo katika sheria wakati alipofanya makosa."

Mheshimiwa Spika, tunapozungumza haki za binadamu na utawala bora, siku hizi mara nyingi sana ukizungumzia utawala bora na haki za binadamu, watu walio wengi wanakwenda kwenye rushwa. Rushwa imetawala, lakini yako mambo mengi sana

makubwa zaidi ya utawala bora na haki za binadamu. Tusiende mbali, tuanze hapa Bungeni, lipo tatizo la Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako lina sheria ya *The National Assembly Administration Act* ya *Cap. 115*. Sheria hii, ibara ya 12(1) na (2) imeeleza wale Makamishina namna gani wawepo. Lakini sheria hii haikuzingatia upande wa Jamhuri ya Muungano. Hizo siku za nyuma alikuwa Kiongozi wa Upinzani kwa kuwa anatokea Zanzibar, ndio alikuwa anaingia kwa kupitia Kiongozi Mkuu wa Kambi ya Upinzani. Dunia inabadilika, leo hii Kiongozi ametokea CHADEMA, matokeo yake hakuna Mzanzibar anayewakilisha katika hili Bunge la Jamhuri ya Muungano. Utawala bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge lina wafanyakazi mbalimbali zaidi ya 200 au 300, kuna Wazanzibar watano, utawala bora na sisi tunaita Bunge la Jamhuri ya Muungano na tumo Wabunge takriban theluthi moja tunatokea Zanzibar. Lakini wafanyakazi wa Bunge wapo watano tu, utawala bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende katika ukiukwaji wa haki za binadamu. Jeshi la Polisi, Magereza, Mahakama, vinatajwa kwa nguvu kwamba wanakiuka haki za binadamu na hiyo imo katika utafiti uliofanywa na *Legally and Human Right Centre* pamoja na *Zanzibar Legally Service* imo katika ukurasa wa 234, 235 Wabunge wote mmegawiwa someni. Vyombo hivi vimetajwa na kwamba katika hii awamu ya nne vitendo vya uvunjwa wa haki za binadamu vimeongezeka, siyo kwamba vimepungua, imo katika ripoti hii. Sasa tunapovilaumu vyombo hivi vya dola ambavyo vimepewa mamlaka kisheria na kuna sheria nyingi ambazo baadhi ya sheria hizo vyombo hivi vya dola hasa Polisi wanakiuka sheria hizo ambazo wanazitumia vibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sheria ambazo zinakiukwa ambapo zipo katika Jeshi la Polisi ni pamoja na *Police Force and Aauxiliary Act* na *Criminal Procedure Act* ambayo hiyo *General Order and Public Service* zinavunjwa na wanazitumia vibaya. Uwezo wa kupeleleza, uwezo wa kuweka kizuizini vinatumika vibaya na Jeshi la Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jana mchana kumetokea unyanyasaji mkubwa Geita wa Jeshi la Polisi. Wanafikiria kule *GGM* tu ipo migodi mingine midogo midogo. Jana kuna watu wamechukua udongo ule wa dhahabu kwenye *Hiace* yao na matokeo yake *Hiace* imeharibika, wamekwenda gereji kutengeneza kidogo, Polisi wameingia, wanadai Sh. 150,000/= walipwe wawaachilie na wamekamatwa kilomita tano nje ya Mgodi *GGM*. Mgodi uko wa *GGM* tu? Geita kila *OCD* anayepelekwa hakai muda mrefu. Kuna askari sita, hao miungu watu ambao *OCD* akileta maneno, akiwapa amri wana haki ya kumwambia *OCD* wewe umekuja jana, sisi tuko hapa na utaondoka na kweli Ma-*OCD* wanaondoka. Watu sita hao majina tunayajua, wapo mpaka leo.

Mheshimiwa Spika, utawala bora pamoja na kwamba *IGP* asiwaweke askari wake kituo kimoja miaka 20. Leo Geita kuna udhalilishaji mkubwa sana kwa askari hao sita. Wanatoa kesi nyingi za kubambikiza, huo siyo utawala bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naona kengele imelia. Naomba pia niseme kwamba katika mambo ya utawala kuna hizi *NGO*. Kuna *NGO* ambayo inasaidia sana, huwa wanaleta mpaka hizi *unit diversity foundation*. Kuna *container* mbili bandarini zimeingia kutoka tarehe 1 Oktoba, 2010, *container* mbili hizi zina baiskeli za walemavu Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, tunaombwa tusitaje jina, lakini kama Wizara inanipa shida Mheshimiwa Maige na *DC* hawa wamepata kufaidika na baiskeli hizi. Kila mmoja alichukua *container* nzima, *DC* kachukua *container* nzima, Mheshimiwa huyu Waziri kachukua *container* nzima la baiskeli za walemavu. Leo kuna miezi nane makontena mawili yameshindikana kutolewa pale na gharama sasa wanatakiwa walipe shilingi milioni 58.5, utawala bora huo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baiskeli hizi ni *non profit organisation*, baiskeli hizi katika hali ya kawaida zinauzwa Sh. 50,000/= tu, leo inafikia mpaka shilingi milioni 40. utawala bora huo! *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, nakupongeza sana Mungu akubariki. Vile vile napenda kuwashukuru Mawaziri watatu, Mheshimiwa Mathias Chikawe, Mheshimiwa Hawa Ghasia na Mheshimiwa Stephen Wasira kwa kuleta bajeti nzuri yenye msimamo ambayo inafanana. Vile vile nawashukuru kwa kupokea simu za Wabunge. Ahsanteni sana. Mungu awabariki. *(Makofi)*

Vile vile napenda niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri kwa kazi nzuri mnazofanya, lakini mwangalie na sisi wakulima tulioingia Bungeni, shida zetu mzitatue kwa haraka iwezekanavyo. Vile vile napenda niwashukuru Wakurugenzi wafuatao: Nataka nimshukuru Mkurugenzi wa TAKUKURU kwa kazi nzuri anayoifanya. Nataka nimshukuru Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa - Ndugu Othman kwa kazi nzuri anayoifanya. Vile vile tusimsahau Mkurugenzi wa Maadili ya Umma - Mama Salome Kaganda. Mimi nashangaa mtu anaposema kwamba watu hawafanyi kazi vizuri! Mimi nawapongeza kabisa kwamba Wakurugenzi hawa wamefanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesema hivyo, kwanza nianze na TAKUKURU. Kama kweli TAKUKURU wangekuwa hawafanyi kazi, mimi Maji Marefu nisingefika hapa, wala Obama asingefika hapa. Kwa sababu kama kuna watu ambao wamepambana kabisa ni mimi mkulima. Kule kulikuwa kuna watu wenye fedha kuliko mimi. Lakini TAKUKURU walikwenda pale wakasimamia na hatimaye mimi mkulima leo nawawakilisha wakulima wenzangu. Lazima tuwapongeze. Unapoamua kumkosoa mtu lakini mwangalie na yale mazuri ambayo ameyafanya, tusiseme tu kumkosoa mtu uzuri wa mtu unajengeka siku nyingi. Lakini ubaya wa mtu unaharibika siku moja. Lakini napenda niwapongeze sana hawa Wakurugenzi watatu. *(Makofi)*

Lakini nataka niseme, ndugu yangu katika hawa Wakurugenzi, watatu mimi nimezunguka kwenye Ofisi zao, lakini kwenye Ofisi ya Salome Kagando inatisha, inashindana.

**SPIKA:** Yule anaitwa Jaji.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Ahsante sana. Jaji Salome Kagando, mimi nimefika mpaka ofisini kwake nikapeleka fomu. Naomba Serikali iangalie hii ofisi. Haiwezekani mtu anaangalia maadili ya wananchi, maadili ya wafanyakazi ofisi yake inalingana na mkulima Ngonyani, haiwezekani! Naomba Serikali itenge kiwango kikubwa cha fedha hii, ofisi yake ijengwe haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba TAKUKURU waongezwe mshahara mara moja. Watakapopewa mshahara mzuri na vifaa vya kisasa watafanya kazi vizuri. Leo hii TAKUKURU kila wanapofika mahali wakiona wamezidiwa, wanakimbilia Polisi, wapewe msaada na Polisi. Lakini kama mnawapa vifaa vya kisasa, Polisi watakimbilia kufuata nini? Watafanya kazi yao vizuri. Sasa leo hii TAKUKURU anamwambia akakutane na Polisi, leo hii TAKUKURU huyu anatakiwa akamkamate Polisi, hapo patafanyika kazi kweli? Kazi ambayo inamhusu TAKUKURU, Polisi hataifanya kwa sababu na yeye Polisi akikosea akienda kukamatwa na yule atakwenda kumkamata. Sasa inakuwa badala ya kusaidiana inakuwa ni vita. Naomba pia TAKUKURU wapewe vifaa vya kisasa na pia ikiwezekana waongezewe watendaji kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nashangaa mtu anaposema Tanzania haina usalama wa Taifa, huyo ni mpotoshaji. Mimi nimeishi nje ya nchi kwa miaka 14. Wenzetu wanasumbuka kweli kweli kule. Lakini Tanzania hii ina usalama wa hali ya juu. Hakuna mahali mwananchi unamkuta anateseka, kama anateseka ni wao wenyewe nyumbani, lakini siyo kwa ajili ya usalama wa nchi. Hebu kaangalie nchi jirani watu wanavyopata shida.

Mimi kuna siku nimelazwa saa sita za mchana kwa ajili ya usalama. Leo hii Tanzania, natoka hapa, nakwenda Kigoma bila tatizo la aina yoyote. Unaingia hapa Bungeni, unakuta Usalama wa Taifa wanafanya kazi vizuri kweli kweli. Ingekuwa nchi nyingine, watu wanapigana viti. Nchi jirani watu wanapigana viti, watu wanatoa mawe hujui yameingia wapi. Leo hii Usalama wa Taifa kwa nini msiwaongezee hela zao? Naomba Serikali safari hii Usalama wa Taifa waongezwe hela. Tunawashindisha hapa mpaka saa nne za usiku, ikifika mambo ya maslahi tunawaona hawafai. Usalama wa Taifa wapewe kiwango chao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nimetembea na Mheshimiwa Rais nje ya nchi, watu wanasema kwamba Rais anatembeatembea tu, hawa watu ni wa kuangalia, wanapotosha nchi. Anapokwenda Rais kuongea kule, haongelei masuala ya Kikwete, anaongelea masuala ya nchi kwamba nchi hii ya Tanzania ipatiwe misaada gani.

Mheshimiwa Spika, leo hii mtu anakuja anasema safari za Rais, safari za Rais. Safari za Rais maendeleo haya yameletwa na nani? Mbona hamtaki kumwona Mheshimiwa Rais anafanya kazi nzuri? Mimi nimezunguka naye na nimeona alichokifanya, haiendi kule kutaja familia yake, anataja nchi ya Tanzania. Leo hii watu tukikaa kwenye kikao tunatafuta umaarufu kwa kusema Rais anakwenda, anakwenda. Mbona ninyi wengine mkienda nje ya nchi hamsemi? Wengine wako Malaysia huko,

wengine wako Uingereza, wengine wako Ulaya, mkitolewa na Bunge mkienda kule mkirudi hapa mmenyamaza. Lakini Rais akitoka inakuwa ni nongwa jamani! Hebu acheni haya maneno ya mitaani, tufanye kazi zinazolingana na watu. Tufanye kazi za Tanzania kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumzie suala lingine ambalo ni utumishi. Nimezunguka kwenye Wizara nyingi, nasikia kila mahali unapokwenda mtu anakaimu. Huko kukaimu kunaletwa na nini? Mtu anashindwa kutekeleza majukumu yake mazito, eti nakaimu. Akifanya makosa, eti anakaimu, Wakurugenzi wanakaimu, jamani! Huku kukaimu kila wakati, mtu anakaimu kwa sababu gani? Kama kweli mtu umemwona amefanya kazi yake nzuri, mtu anakaimu miaka sita! Kwa nini asikaimu miezi sita, mmpeleke jina lake kwa Mheshimiwa anayetia saini kwamba huyu anastahili kuwa Mkurugenzi kamili? Tunakwenda maofisi mengi, kila ukienda mahali ukiomba msaada, anakaimu. Jamani, maamuzi hayafanyiki. Hapa naomba mwangalie hawa watu mnaosema wanakaimu hii kwa kweli hailingani kabisa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi hapa tunakaa Wabunge muda mwingi sana tuko Bungeni na wewe kwenye ofisi yako ya Bunge una watumishi na hawa watumishi kila siku tunasema maslahi ya Wabunge. Hawa watumishi wa Bunge nani anawasaidia na wao pia ni viongozi na wao pia wanafanya kazi? Kama tunaangalia maslahi yetu sisi Wabunge nao wapandishiwe mshahara, watumishi ya Ofisi ya Bunge. Tusijipendelee tu sisi wakati kuna wenzetu tunashindaa nao hapa mpaka usiku na wako mpaka Jumamosi na wanatufanyia kazi sisi na wanatoa makabrasha kwa ajili ya Wabunge hapa. Leo hii tunasema mshahara upande, mshahara upande, naomba ofisi yako nao Watumishi wa Bunge wapandishiwe mshahara mara moja. Wapandishiwe kuanzia hiyo tarehe 1 Julai, 2011. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, walimu nao tunaongea tu, walimu wanapata shida. Walimu wa kwenye Jimbo langu kule siku mbili wanazunguka barabarani kutafuta mishahara yao, lakini wakishapata mshahara huo unakuwa umeishia kwenye hoteli na chakula wanakokwenda kutafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Madiwani ndiyo hivyo hivyo, wafanyakazi wa hospitali kule Magunga ndiyo hivyo hivyo. Magunga leo hii mfanyakazi akienda kupata dawa anasema Daktari anaringa, daktari ananisema vibaya. Lakini ukiangalia mazingira anayofanyia kazi ni haki aseme vibaya. Mtu anakuja pale anakwambia nipe dawa kama aliziweka. Lakini ikifika mahali akimwambia ziko wapi dawa? Hakuna, nenda kanunue. Inakuwa nongwa na matokeo yake mtu huyu anafanya kazi katika mazingira magumu, anafanya kazi kama mganga wa kienyeji! Jamani anafanya kazi kama mganga wa tiba asilia kama mimi wakati mtu anastahili apewe mafao yake yote! Wako walimu katika Jimbo la Korogwe vijiji mpaka leo hii ninavyokwambia mishahara hawapati, ukiuliza sababu wanaambiwa itakuja. Leo kuna watu wanafanya kazi Mamlaka ya Mkonge, mpaka leo hii wamefanya kazi miaka zaidi ya 30 hata mafao yao hawajui. Sasa mnasema utawala bora, namna gani? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie utumishi. Mamlaka ya Mkonge kuna wafanyakazi wangu ambao wamefanya kazi muda mrefu sana na watu wale hawawaoni, wawaangalie jamani msiweke mazingira ya sisi kujifanya mnajua jamani, muda wa Mbunge ni miaka mitano. Unapokuwa hapa unatakiwa uwatetee waliokuchagua, siji hapa kuuza sura yangu. Nimekuja hapa kutetea walionichagua. Naomba sana Serikali, haya niliyoyasema kuanzia Wakurugenzi wa TAKUKURU, Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa, Mkurugenzi wa Tume ya Maadili naomba sana tuwaangalie jamani. Wafanyakazi wanapata shida sana. Wafanyakazi hapa wa Bunge tunawaona kila siku tunawakuta saa 12.00 wako hapa. Huko vijijini kwangu ndiyo msiseme, kama mnaangalia utumishi mwangalie na Korogwe Vijijini. Korogwe Mjini na Mkoa mzima wa Tanga kule wanakolala katika mazingira magumu kuna miinuko mikubwa. Katika Mkoa wenye miinuko mikubwa ni Mkoa wa Tanga. Wanapokwenda kudai haki zao wanapata shida, wanakaa siku nne kungoja maslahi yao.

Mimi sitaki kuchukua saa nyingi. Nasema naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Wewe ni kielelezo mojawapo cha utumishi uliotukuka. Wengi wako hapa wametoka mbali, Mheshimiwa Stephen Wasira ametoka mbali sana ambaye ni mtoa hoja na wengine. Sasa tunapokuwa tunataka mahusiano mazuri, ni lazima sisi kwanza tuonyeshe mfano humu ndani. Maana hapa ni *dialogue* na humu ndani tunajenga, hatubomoa. Kinachotoka humu ndani kinapaswa kuwa *cream,* watu waweze kuona mfano.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningeliomba jengo hili lilindwe, viongozi wetu wafanye kazi kwa uadilifu bila hofu. Lakini habari zinazotoka humu kwenye magazeti, picha zinazotoka, kwa kweli zinadhalilisha hili Bunge. Mimi niliona juzi picha moja wamemdhalilisha Kiongozi wetu – Mheshimiwa Mzee Stephen Wasira. Mheshimiwa Stephen Wasira ninamfahamu kutoka mwaka 1970, alikuwa Mbunge na Naibu Waziri Bunge la mwaka 1970 mpaka 1975, nilimwona mimi ni mtu aliyetoka mbali. Sasa mnapotoa picha za kudhalilisha viongozi, mnasema anatafakari, basi kwa nini msiseme anasali? Maana sisi Wakristo tunasali tumefumba macho. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilitolewa naambiwa kwamba nasikiliza kwa makini, mguu unatafakari? Mguu unasikiliza? Sasa ninavyosema ni kwamba tuwe na mahusiano mazuri. Niliisifu hotuba ya Mheshimiwa Akunaay jana. Naomba hiyo hotuba tafadhali iangaliwe ifanyiwe kazi na ile pengine hata hotuba ya akina Selasini, tulikuwa tunamtania asubuhi tunasema Mheshimiwa Selasini tena ni Arobaini kwa sababu ni *well balanced*. Lakini hizi hotuba zinatoka hazitusaidii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeomba sana hizi hotuba zinazotolewa hapa zisi-*inflame,* zijenge ziweze kutusaidia. Historia ya Utumishi wa Umma katika nchi hii ni historia ya utumishi uliotukuka. Tuna viongozi wetu wamepita, mimi ni mtumishi wa muda mpaka nilipoacha niko hapa ndani. Lakini nimeona wakati wa uhuru tulianza na Katibu Mkuu Kiongozi Dunstan Omar, Halafu akaja Joseph Namata, halafu akaja Dickson Nkembo, akaja Timothy Apio, akaja Mzee Rupia, akaja Lumbanga na sasa tunaye Luhanjo.

Mheshimiwa Mzee Ntukamazina nafikiri anajua yote haya. Lakini alikuwepo pia kwa upande wa utumishi Marehemu Mzee Bernard Mlokozi.

Mheshimiwa Spika, niliwahi kufanya kazi katika ofisi hiyo, Mzee Bernard Mlokozi alikuwa akikuangalia wewe kama ni mbabaishaji hata kalamu inadondoka. Kule kukuangalia tu! Maana ilikuwa ndiyo kielelezo na alikuwa ni *Custodian* wa *Standing Order*. Lakini sasa nimemsikia wakati wa wiki ya Utumishi Serikalini ana-*lament* kuhusu *mindset* ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, watumishi wamekuwa ma-*boss* na wala siyo watumishi wa kuweza kuwatumikia wananchi tena. Sasa na ndivyo alivyo na ni kweli. Lakini mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria nikiangalia kule juu, naona kama wamekaa vizuri, ila *top grass* na nini imekaa vizuri tu na wengi tunawafahamu, huwezi ukasema huyu anapokea rushwa, huyu anapokea nini, unawafahamu *they are good people.* Lakini bado kuna uvundo wa rushwa, bado kuna uvundo wa ukosefu wa utawala bora. Sasa ni wapi? Sasa labda tuseme kwanza, basi kule chini Wilayani na Vijijini.

Kwa hiyo, ndugu zangu, mimi nafikiri tutafute suala hilo. Mimi wakati naanza kazi nilikuwa napokea mshahara wa Sh. 1,200/= mwaka 1974 mshahara huo mwezi ule niliopokea uliniwezesha mimi kununua kitanda, nikanunua redio na nikanunua seti ya makochi mazuri tu ya kuweza kumkaribisha mgeni, *girlfriend* na nini.

Lakini nikabaki na shilingi 200 ambazo zilinisukuma mpaka mwisho wa mwezi. Hali hii ilikwenda mpaka wakati wa vita, shilingi yetu ilikuwa na thamani sana. Baada ya hapo sasa, baada ya vita, ndiyo likaingia tatizo la bidhaa adimu, madukani hakuna kitu, *inflation*, wafanyakazi wakaanza kujiingiza kwenye masuala ya biashara na sasa wafanyakazi wamejiingiza kwenye mambo ya siasa, kwa hiyo, ikawa vurugu.

Mheshimiwa Spika, sasa tuna- *rescue* vipi *situation* hii. Nadhani hilo ndiyo suala la kuweza kuji-*address.* Ni kweli hali ya uchumi na kipato chetu cha wafanyakazi hakilingani na hali ya uchumi ya sasa. Nadhani Serikali ingeliangalia hilo kwa undani ili tuweze kuona kama tunaweza kurekebisha. Kwa kuwa watu sasa wamezoea hata wangelipwa kiasi gani sasa hivi, bado itakuwa tatizo hilo linaendelea, kwa hiyo mimi nashauri kwamba viongozi wetu tuwe *serious*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tatizo moja mimi nililoliona, naona viongozi wengi tunapenda kupokea zawadi bila sababu, sasa hii inapunguza ile *relationship* kati ya viongozi na wafanyakazi wao. *Boss and subordinate relationship* pale inapungua. Nikitoka Itigi nimekuletea galoni moja ya mafuta ya kupikia, hiyo ni zawadi, uongo ndugu zangu lakini unampelekea mtu lori, unampelekea mtu mbuzi 10, *boss* unampelekea mahindi lori zima, tena gari lenyewe la Serikali, hivi kweli atakuchukulia hatua? Hiyo si imeshakuwa ni biashara, hiyo imekwishakuwa *deal.* Sisemi kwamba msipokee zawadi lakini kwa kazi gani? Hizi zawadi ni kwa kazi gani? Mtu anatoka Sumbawanga na lori anampelekea *boss* Dar es Salaam, kweli wewe utamdhibiti huyu, atakuwa anafanya anavyotaka yeye. Kwanza zamani tulikuwa tukipewa zawadi unatoka nje, inabidi una-*surrender*, uongo ay kweli Mzee Ntukamazina, samahani Mheshimiwa

Spika napaswa kuku-*address* wewe, huo ndiyo ukweli wenyewe lakini sasa hivi utakuta hamna kitu cha namna hiyo. Kwa hiyo iwe *questionab*le kwa nini kuna vitu vya namna hiyo ambavyo vinajaribu kuleta mkanganyiko na kuharibu mustakabali nzima wa utumishi. Naomba *State Institutions* ziachwe zifanye kazi, zisiingiliwe. Mimi nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mama Kaganda, huyu *boss* mpya wa hii Tume ya Maadili ya Viongozi.

**SPIKA:** Jaji

**MHE. JOHN P. LWANJI:** *Sorry, sorry* Mheshimiwa Jaji Kaganda. Kweli hilo Baraza la Madili ambalo liko chini ya Taasisi yake au Taasisi ya Serikali sasa hivi limeonyesha uwezo mkubwa wa kuweza kufanya kazi, inaaminika. Sisi katika Kamati yetu tulipiga sana kelele, ilikuwa ni kama haipo lakini sasa inafanya vizuri. Viongozi matumbo moto, unaitwa, unahojiwa, kuna *seriousness* ya kuweza kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo nina-*question* kuhusu hili Baraza la Vyama vya Siasa, kazi yake ni ipi hasa? Maana kuna vurugu tu, watu wanajizungumzia hovyo, viongozi wa vyama wanapanda chuki miongoni mwa watu, hivi kweli haliwezi kuwahoji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri Ofisi ya Waziri Mkuu au wanaohusika na Baraza hili basi watueleze waziwazi hili Baraza toka limeundwa sijui mwaka 2009 au 2010 kazi yake hasa kubwa ni nini? Kama Serikali inahangaika katika hali hii watu hawaoni mazuri, watu hawataki kuamini kwamba uchaguzi umekwisha, uchaguzi ulishakwisha muda mrefu lakini bado hawataki kuamini sasa hiyo siyo demokrasia hata kidogo. Hizo ni vurugu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue nafasi hii…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuchangia katika hotuba ya makadirio ya Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu. Kwa kuwa rushwa ni adui wa haki, naomba niende moja kwa moja katika tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, wote tunatambua kwamba rushwa imesababisha watu wengi kukosa haki zao. Awali ya yote, naomba nitoe mchanganuo kuhusu rushwa. Kuna makundi mawili ya rushwa. Kundi la kwanza linaitwa *petty corruption* na pili linaitwa *grand corruption.* Lile kundi la kwanza ni zile rushwa ndogondogo na kundi la pili maana yake ni zile rushwa kubwa kubwa. Nchi yetu imekuwa ikisumbuka sana na hizi rushwa ndogondogo wakiwemo TAKUKURU, wamekuwa wakitumia nguvu nyingi sana kujaribu kufuatilia rushwa ndogondogo.

Mheshimiwa Spika, unapoenda shuleni kwa mwanao kuomba matokeo ya mtoto, Mwalimu akakuambia kwamba hana karatasi ya kuandikia matokeo hayo, unapompatia shilingi 2,000, hiyo utaiita rushwa? Mimi nadhani hiyo siyo rushwa. Hiyo ni kumwezesha ili aweze kufanya kazi hiyo ambayo wewe mwenyewe unamhitaji akufanyie. Unapoenda kwa Daktari, unahitaji matibabu, ukamkuta Daktari yuko gizani kwa sababu hakuna umeme, hana pesa ya kununulia mafuta ya jenereta, ukiwa muungwana utampatia Daktari huyo shilingi 10,000 angalau anunue mafuta ya jenereta hatimaye akupatie hiyo huduma unayoitaka. Kwa maoni yangu, sidhani kama hiyo ni rushwa. Tumekuwa tunajichanganya sana, tunashindwa kutofautisha uwezeshaji na rushwa. Mara nyingi hii *petty corruption* inajitokeza kwa sababu watumishi wanashindwa kufanya kazi zao kwa sababu Serikali inashindwa kuwawezesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mambo haya yako kila sehemu, mambo haya yako maofisini, unaenda ofisini anakuambia hana karatasi wala kalamu ya kukupatia taarifa ambazo unafuatilia, sasa mara nyingi watumishi hawa huwa hawaombi awezeshwe lakini sisi wenyewe wateja huwa tunajitolea kuwawezesha. Tunawapa kama ni shilingi 2,000/= unampa ili mradi tu aweze kukufanyia kazi yako lakini tumekuwa na mawazo potofu na tunatuhumu watumishi hawa kwa kuchukua rushwa wakati kwa mtazamo wangu sidhani kama mfanyakazi anaposhindwa kufanya wajibu wake au kukupa huduma ambayo umeifuata siyo kwamba anasubiri umpe rushwa, anahitaji awezeshwe kuifanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie *grand corruption*, *corruption* kubwakubwa maana yake rushwa kubwa kubwa. Mimi nadhani wakati umefika Serikali yetu sasa ijikite zaidi kwenye hizi rushwa kubwakubwa. Rushwa hizi ndizo zinazolimaliza Taifa letu. Nikizungumzia rushwa kubwakubwa namaanisha rushwa zinazopatikana kupitia mikataba ya Serikali na kupitia *public procurement* yaani manunuzi ya umma. Naomba niwasaidie TAKUKURU kwamba kinachotakiwa hapa siyo kutumia muda mwingi kuelimisha watu madhara ya rushwa, mimi nadhani wafuatilie hizi rushwa kubwakubwa ambazo zinafanywa na wengi ambao wako katika nafasi za maamuzi. Endapo Serikali yetu itafuatilia kwa undani rushwa hizi kwa kutumia *mechanism* inayokubalika, kwa kutumia wataalam ambao wamebobea, nina imani kabisa rushwa zitapungua kwa asilimia kubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la ajira. Jimboni kwangu Kwimba, Jimbo ninalotoka, wafanyakazi waliopo katika Jimbo lile wana hali ngumu sana. Wengi hawana ajira na hata zile ajira ndogondogo kama Mhudumu, Dereva, cha kushangaza Halmashauri imekuwa ikileta *expatriates* Madereva. Nikisema *expatriates* maana yake ni Madereva kuletwa toka Mikoa mingine badala ya kuwapa nafasi wananchi wa Kwimba. Jambo hili ni la kusikitisha sana. Sidhani kama kuna haja ya kuleta Dereva kutoka Kigoma wakati kuna Wasukuma wengi tu ambao wanajua kuendesha magari, tena wamesoma angalau mpaka Kidato cha Nne lakini wewe unaamua kumleta Dereva kutoka Kigoma. Naomba Serikali iliangalie suala hili na kama ikiwezekana Sheria isiruhusu Wakurugenzi kuajiri watu nje ya Mkoa ambao Kurugenzi hiyo imo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitoe masikitiko yangu kuhusu Wahudumu. Tuna Wahudumu ma-*expatriates* Kwimba, pale Halmashauri ya Ngudu nadhani tunaongoza kwa kuajiri Wahudumu ma-*expatriate*s, hakuna Mhudumu mzawa wa pale, tunaagiza Wahudumu kutoka Mikoa mingine. Mimi nikiwa kama mkazi wa Kwimba na vilevile Mbunge wa Viti Maalum kutokea Kwimba, kwa kweli hili jambo halifurahishi na ni lazima lishughulikiwe ili lisiendelee.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie nyumba za watumishi. Watumishi wanaofanya kazi Jimboni kwangu Kwimba au Wilaya nzima wana matatizo ya makazi. Ni jambo la aibu! Kuna Walimu wanaletwa kufanya kazi lakini Serikali haiweki mpango wowote wa makazi ya Walimu hawa. Matokeo yake wanazunguka mitaani, wanatafuta sehemu za kuishi lakini hawapati, wengine wanapanga vijijini wanatembea kwa mguu kuja kufundisha Ngudu mjini, jambo hili linasikitisha, naomba Serikali, Wizara husika ilishughulikie hili, ihakikishe kwamba watumishi waangaliwe, wapewe hata kama siyo nyumba basi wasaidiwe kulipia pesa ya pango ili kuwarahisishia maisha.

Mheshimiwa Spika, si Walimu tu ambao wananyanyasika Wilayani Kwimba tuna watumishi wa Jeshi la Polisi, Askari hawana makazi ya kueleweka, nyumba zao zimechakaa, wengine hawana kabisa hata nyumba za kuishi. Tuna Madaktari ambao hawana nyumba za kuishi. Kama hatuwezi kuwaangalia hawa watu ambao tunawategemea kutupatia huduma je, tunatarajia kweli wataweza kutufanyia kazi inavyotakiwa? Je, tunawategemea kweli wasituhumiwe kwa hiyo rushwa kwa sababu mimi bado nawatetea wanapopewa hela ndogondogo za kuwawezesha halafu sisi tukaita ni rushwa ni kuwaonea na hatuwatendei haki kwa sababu sisi kama Serikali tumeshindwa kuwawezesha ili waweze kufanya kazi bila ya kutegemea msaada wa mtu mwingine yoyote.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba Ofisi ya Rais, Waziri husika alifanyie kazi suala hili hatimaye matatizo haya yaweze kuondoka.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. OMARI R. NUNDU**: Mheshimiwa Spika, kumejitokeza suala la Maafisa wa Ngazi za Juu katika Taasisi za Serikali kukaimu nafasi hizo kwa muda mrefu, zaidi ya mwaka mmoja na nusu na baadhi yao kukaimu hadi wanastaafu. Jambo hili ni upungufu na hasara kwa Taifa katika ufanisi wa taasisi hizi kwa kuwa:-

(i) Watendaji hao wanakuwa katika hali ya kutojiamini kwenye nafasi hizo hivyo kudumaza mchango wa utendaji kazi wao kwa Taifa;

(ii) Kutokutendewa haki watendaji hao;

(iii) Kuweka picha ya kukosekana maadili ya ajiri; na

(iv) Kuliweka shirika na taasisi kwenye hali ngumu ya kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kuwa mfumo na hatua za kuthibitisha watendaji hawa uboreshwe na uwekewe kiwango ambacho hakikiukwi katika kukaimu na kinapofika, Mtendaji aidha athibitishwe au atenguliwe kwenye ukaimu huo.

Mheshimiwa Spika, pia kabla Mtendaji hajakaimu, ithibitishwe kuwa ukaimu wake hautotiliwa mashaka baadaye kiasi cha kushindwa kuthibitishwa katika nafasi hiyo. Vilevile kabla ya kufika wakati wa kustaafu Mtendaji, hatua ziwe zimekwishachukuliwa kuandaa na kuwaweka tayari Maafisa wa kukaimu bila mashaka katika nafasi hizo hivyo kurahisisha kuthibitishwa kwao. Tusipofanya hivyo kuna athari ya kukaimu kwa muda mrefu kwenye nafasi za juu na hivyo kudumaza utendaji kazi katika taasisi husika ambazo ufanisi wake ni muhimu kwa maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, utendaji bora katika Mashirika na Taasisi za Serikali ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi na ufanisi wa Mashirika na Taasisi hizi. Matatizo mengi yanajitokeza ambayo yanaashiria utendaji usioridhisha kwenye Bodi na Menejimenti ya Mashirika na Taasisi hizo. Hata hivyo, ni adimu sana kuwajibishwa Bodi na Menejimenti hizo katika muda unaofaa kuyasitiri Mashirika na Bodi hizo zisiingie kwenye matatizo makubwa zaidi hadi kufa kwa vile hatua zinazoweza kuchukuliwa zinakuwa na mlolongo mrefu.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni:-

(i) Kuwe na mikakati ya ziada itakayochokonowa Watendaji na Wanabodi wazuri ili wapatikane kusimamia na kuendesha mashirika na taasisi hizo. Nafasi hizo zote zingetangazwa na zikagombaniwa ingesaidia.

(ii) Kungekuwa na mikataba ya kazi kati ya Menejimenti na Bodi pamoja na Wizara ambayo ingeonyesha waziwazi vigezo ambavyo vingetumika kuengua uteuzi wa Menejimenti ambazo zingeshindwa kufikia vigezo hivyo au ambazo zitayumba kimaadili. Bodi nazo zingewekewa vigezo vya utendaji kazi ambavyo vingetumiwa kuhakiki na kusimamia utendaji kazi wa Bodi hizo. Pamoja na hivyo, Bodi inapodhihirika kushindwa kusimamia matatizo makubwa yasiyozidi matano katika taasisi au shirika aidha kwa kutoyagundua au kwa kuyazembea au kwa kuyaanzisha au kuyapalilia basi Bodi hizo zivunjwe mara moja.

(iii) Bodi na Menejimenti zitakazothibitika kuziingiza taasisi na mashirika kwenye matatizo makubwa ya kiutendaji, kiubadhirifu, ziwajibishwe kwa mujibu wa sheria pamoja na kufikishwa Mahakamani.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF**: Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo ya Miaka Mitano kuanzia mwaka 2011/2012 mpaka 2015/2016 umeweka vipaumbele karibu vitano. Sina mashaka na vipaumbele hivyo uwe makini bado urasimu katika nchi yetu ni adui mkubwa wa maendeleo yetu. Ili nchi yetu iweze kupiga hatua ya maendeleo ni

lazima urasimu huo tuuondoe vinginevyo yote yanayotarajiwa katika miaka mitano hayatawezekana.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia ukurasa wa 9(v) wa hotuba ya Waziri, kuna nia ya kuendeleza Rasilimali watu kwa kuboresha elimu ya Sayansi na Ufundi. Ni sawa lakini ushauri wangu katika suala la ufundi tusisahau Shirika la Viwanda Vidogo Vidogo *(SIDO)* kushirikishwa katika mpango mzima wa kuendeleza ufundi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kila ifikapo wakati wa bajeti ni Wizara ya Fedha na Uchumi ndio inayotoa mwelekeo wa Serikali katika utendaji wa kijumla kutoka Wizara zote. Sasa kwa kuwepo Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ni taasisi ipi itastahili kutoa mwelekeo wa Wizara zote kwa mwaka husika. Je, itakuwa ni Wizara ya Fedha au Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Spika, inavyoonekana TAKUKURU bado haijajikita kwenye rushwa za ofisini. Wananchi hawapati huduma ipasavyo kwenye ofisi bila ya kutoa chochote, TAKUKURU ina kazi kubwa katika suala la rushwa.

Mheshimiwa Spika, katika kada ya utumishi iliyosambaa nchi nzima ni ya Ualimu. Walimu wana mazingira magumu ya kazi. Licha ya ugumu wa kazi zao, Walimu bado wana madai ya malimbikizo yanayofikia shilingi bilioni 13. Huu ni uonevu mkubwa kwa kada hii ya utumishi. Ipo haja kwa muda mfupi Walimu hao wapatiwe maslahi yao.

Mheshimiwa Spika, Serikali imehakiki tatizo la wafanyakazi hewa, matokeo yake kuna upotevu mkubwa wa fedha za Serikali. Suala hili ni la muda mrefu, je, Serikali imechukua hatua gani ili suala hili lisitokee tena?

Mheshimiwa Spika, kuna udhaifu mkubwa wa utendaji kazi maofisini. Wafanyakazi wanaingia na kutoka ofisini (kazini) kwa wakati wanaotaka. Kazi ya kuchukuwa siku moja inaweza ikichukua wiki mbili, huu si utumishi uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, nilitegemea baada ya hotuba ya Waziri nitapata ufahamu juu ya ongezeko la mshahara lakini mpaka nachangia sielewi ongezeko la mishahara liko vipi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli *TASAF* imefanya miradi mingi hapa nchini, lakini baadhi ya miradi ya *TASAF* iko chini ya viwango, baadhi ya miradi yao hailingani na thamani ya fedha inayotumika. Kwa hiyo, ipo haja miradi hiyo ikaguliwe. Ahsante.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI**: Mheshimiwa Spika, pamoja na kupongeza hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba wakati wa majumuisho anipe ufafanuzi kuhusu suala la likizo ya kustaafu. Nachojua ni kuwa sheria inaelekeza mfanyakazi anapokaribia kustaafu, anapewa likizo ya kujiandaa kustaafu mbali na likizo ya kawaida. Katika Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), wafanyakazi wananyimwa haki yao hiyo

ya likizo ya kustaafu kwa kuchanganya na likizo ya mwaka. Nitaomba ufafanuzi ili kuwatoa hofu wafanyakazi.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA**: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri kwa uwasilishaji wa hotuba yake ila nina yafuatayo ambayo napenda Serikali iyazingatie.

(i) Nidhamu, baadhi ya Watumishi wa Umma wamekuwa na ukiukwaji mkubwa wa nidhamu hasa kwa wananchi wanapokwenda kufuata huduma, kwa mfano, kuongea na simu na kula maofisini wakati wa kazi.

(ii) Utawala bora, Ili kuimarisha utawala bora, napenda kushauri Serikali iweze kutunga sheria zitakazokuwa zinawawajibisha Watumishi wa Umma pale wanapoenda kinyume ili iwe funzo kwa wengine.

(iii) Upendeleo katika ajira, kumekuwa na *unfair competition* katika soko la ajira. Watumishi wengi wanapata ajira aidha kwa kuwa na marefa, ndugu au jamaa wa karibu wa waajiri. Hali hii ni mbaya na itaweza jenga tabaka katika nchi yetu.

(iv) Watumishi kutoripoti mahali ambapo wanakuwa wamepangiwa. Tatizo hili limekuwa sugu hasa Mkoa wa Kigoma. Suluhisho, Serikali iweke adhabu kwa watumishi wanaobagua maeneo ya kufanyia kazi kwa sababu tu ya hulka zisizokuwa na msingi aidha wasipate ajira kwa miaka mingine mitatu ili kupunguza tatizo hili, nawasilisha.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA**: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vijana wengi wanamaliza Vyuo Vikuu na Vyuo vya Ufundi, tatizo kubwa kwa vijana hawa ni ajira, vijana wengi wapo mitaani hawana kazi, naishauri Serikali kuanzisha utaratibu wa Serikali kuwatafutia kazi vijana wote wanaomaliza Vyuo Vikuu ili kutatua tatizo la vijana wetu kukosa ajira.

Mheshimiwa Spika, hali ya Utumishi wa Umma, wafanyakazi wanatakiwa kujua majukumu yao katika kazi, pia kutumia muda mwingi katika kazi zao walizoajiriwa siyo kufanya kazi za binafsi wakati wa kazi.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la mishahara kwa watumishi, wafanyakazi wa Utumishi wa Umma wanalalamika sana kuhusiana na ongezeko dogo la mishahara yao, kwa mfano Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari, ongezeko lao la mishahara ni dogo sana kwa mwaka. Naishauri Serikali kuongeza ongezeko kubwa la mishahara yao, pia kulipa malimbikizo yao kwa wakati bila kuchelewesha.

Mheshimiwa Spika, mafao ya wafanyakazi wanaostaafu kazi, mfanyakazi anapofikia muda wa kustaafu ni vizuri Serikali kutoa malipo/mafao yao siku ileile wanapotoka kazini ili kuondoa usumbufu wa kufuatilia mafao yao.

Mheshimiwa Spika, upandishwaji wa madaraja katika kazi, mfanyakazi ana haki ya kupandishwa daraja kila mwaka hasa sekta ya Ualimu na Manesi kuna tatizo la upandishwaji madaraja yao. Naishauri Serikali kwa Wakurugenzi ambao hawapandishi madaraja wafanyakazi hao bila sababu maalum wachukuliwe hatua za kisheria.

Mheshimiwa Spika, mazingira ya kazi kwa Watumishi wa Umma, mazingira ya wafanyakazi wa Polisi ni magumu sana kwa mfano nyumba wanazoishi ni mbovu sana kwa mfano Kituo cha Polisi, kituo kidogo cha Kibao, Jimbo la Mufindi Kusini nyumba zao ni mbaya sana yaani kuta zimechakaa ni heri wangejengewa nyumba nyingine mpya. Pia hawana hata gari la kazi tukizingatia wanahudumia sehemu kubwa sana katika Jimbo la Mufindi Kusini. Wanahudumia sehemu ya viwanda vingi sana katika Jimbo. Naishauri na kuiomba Serikali kuwapa Polisi wa Kituo cha Kibao gari litakalowasaidia katika kazi yao.

Mheshimiwa Spika, ukosefu wa Madaktari na Manesi katika Jimbo la Mufindi Kusini, napenda kuishukuru Serikali kwa kujenga Zahanati kwa kila Kata na kujenga Vituo vya Afya kwa kila Tarafa. Tatizo kubwa watumishi hawatoshi katika vituo. Naomba Serikali kuongeza watumishi katika Zahanati na Vituo vya Afya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH**: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nianzie na suala la rushwa, mara nyingi Serikali imekuwa ikiainisha mikakati mbalimbali inayohusiana na kudhibiti mianya ya rushwa nchini. Wananchi huwa wanajenga matumaini mema ya kuondokana na rushwa iliyokithiri nchini na kuona kwamba sasa Serikali yao inawapatia mazingira mazuri ya maboresho kupitia sekta mbalimbali jinsi wanavyokerwa na vitendo vya rushwa nchini lakini kadri siku zinavyokwenda mbele vitendo vya rushwa ndivyo vinavyozidi kwenda mbele na kuwaachia malalamiko wananchi. Wanaotaka rushwa nchini hawajali mtu wala kikundi cha watu kuwa masikini, wala hali duni za kimaisha, wanapoamua kudai rushwa hufanya kama kitu hicho cha rushwa ni cha lazima.

Mheshimiwa Spika, maeneo yanayohusika na rushwa zaidi ni Madereva barabarani, Dereva anapotuhumiwa kufanya kosa na ukifuatilia kwa makini hakuna makosa yaliyofanyika ila udhalilishaji na uonevu ndio uliotawala katika masuala ya kudai rushwa. Mfano, gari kituoni imetakiwa kuanza safari ya kuelekea Dar es Salaam saa 3.00 kamili asubuhi, wakati abiria wameshajaa kwenye gari hadi saa 3.02 na basi linaondoka, anakuja Askari anasema kwa nini mmeondoka kabla ya wakati. Askari anawatishia twende kituoni, hamtaki hivyo toeni hela haraka muondoke. Askari huyo anaangalia kwenye gari kuna abiria wamejaa, wengine wanawahi msibani, wengine wanatakiwa kwenda hospitali na hili nimelishuhudia mimi mwenyewe hapa Dodoma, wananchi wanailalamikia Serikali na kuilaani Serikali, hii kweli ni haki!

Mheshimiwa Spika, tufahamu kwamba wananchi wanatusikiliza, wanatuona na matamko ya Serikali yanasikika, hivi wananchi wanapoona bado vitendo hivi vinaendelea na kuwakandamiza wananchi, wananchi hawa wataendelea kuiunga mkono Serikali kweli? Naiomba sana Serikali inapotamka na kuunda kitengo kama hiki cha kushughulikia masuala yanayoendelea kuwakera sana wananchi, itekeleze au kitengo chenyewe kifanye kazi kwa nguvu moja katika maeneo mbalimbali, wasambae sio kukaa ofisini tu na kuchukua mishahara ya mwezi, wakati kazi waliyotumwa haileti matunda na kuendelea kuwachosha wananchi.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine yanayohusika na rushwa ni Mahakamani, Bandari, Hospitali, Shule, maeneo yanayohusika na ajira, mikopo ya wananchi, *TANESCO* kuhusiana na uungwaji wa umeme, utaratibu wake umetawaliwa na rushwa, mafao ya Afrika Mashariki, watumishi. Serikali ifahamu kwamba maeneo mengi yaliyotawaliwa na rushwa yako karibu na wananchi wa kipato cha chini na huko ndiko waliko wanaoamua kupitia kura zao wenyewe, hivi haya ni maboresho au ni kuiangusha Serikali iliyoko madarakani? Naiomba Serikali kupitia Kitengo cha Kupambana na Rushwa, TAKUKURU pamoja na kazi zilizopangwa kutekelezwa pia iendelee kujaribu kupeleka nguvu zao zaidi katika maeneo niliyoyataja ili kuweza kuona vitendo vya rushwa vilivyotawala, huko wataweza kugundua mambo mengi na wananchi watakuwa na imani kubwa na Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, napongeza juhudi mbalimbali zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali tokea kuwepo Wizara hii hadi leo. Naiomba Serikali iongeze nguvu zaidi ili wananchi waweze kuwa na imani na Serikali yao inayowaongoza ili kipindi kingine cha miaka mitano wasirubuniwe na wachache.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo machache, naunga mkono hoja.

**MHE. SUBIRA K. MGALU**: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema moja kwa moja naunga mkono hoja. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri iliyozungumzia mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 50 ya Uhuru, mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa 2010/2011 na mwisho hotuba iligusia mapendekezo ya mpango wa utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajielekeza kwenye maeneo yafuatayo:-

Kwanza, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kwa kuwa Kifungu 27 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Na 11 ya mwaka 2008 imempa mamlaka *CAG* kuwasilisha taarifa zake za ukaguzi kwa TAKUKURU na *DCI* endapo katika ripoti hizo imebaini matukio mbalimbali yenye sura ya udanganyifu na rushwa. Naiomba TAKUKURU kila mwaka wa fedha iandae taarifa ya matokeo ya mapitio ya ripoti za *CAG* ili tuone hatua zilizochukuliwa. Hii itasaidia sana kupunguza kilio cha wadau kwamba ripoti za *CAG* hazifanyiwi kazi hasa mapendekezo anayotoa.

Pili, Mfuko wa maendeleo ya Jamii *TASAF*. Mfuko huu umefanya kazi kubwa na nzuri. Binafsi napongeza sana kazi iliyofanywa na Mfuko huu wa *TASAF* kwenye Mkoa

wetu wa Pwani. Hata hivyo, baadhi ya miradi haijakamilika kwa takribani miaka miwili sasa hasa miradi ya ujenzi wa madarasa, majengo ya utawala, masoko n.k. Sababu kubwa inayosababisha miradi kutomalizika ni kupanda kwa bei za vifaa vya ujenzi, usimamizi hafifu wa miradi hiyo na pia kukosekana kwa michango ya wananchi kutokana na kipato duni.

Mheshimiwa Spika, nashauri Mfuko wa *TASAF* uendelee kufanya ukaguzi na tathmini nchi nzima ili kubaini miradi ambayo haijakamilika na sababu zake ili kabla mfuko wa *TASAF* haujatoa pesa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mipya iliyoibuliwa na wananchi. Iandae mpango mkakati wa kutafuta fedha za kukamilisha miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa kwenye miradi inayotekelezwa na mfuko wa *TASAF* ni kukosekana kwa elimu/ujuzi wa kutunza hesabu na kumbukumbu zingine za miradi pamoja na Sheria za Manunuzi hasa kwa wajumbe wa Kamati za Miradi. Hivyo naiomba Serikali kupitia Mfuko huu wa *TASAF* kuharakisha mpango wa utoaji mafunzo kwa wajumbe wa Kamati za Miradi, wajumbe wa Kamati za Serikali za Vijiji/Mitaa na wataalam wa sekta zinazohusika. Mafunzo mengine yanayofaa kutolewa ni jinsi ya kuibua miradi yenye kuleta tija kwa haraka kutokana na mazingira. Kwenye ripoti ya *CAG* ya mwaka 2009/2010 inaonyesha kuna baadhi ya miradi imekamilika lakini haitumiki pamoja na kukamilika kwa huduma zote. Miradi hiyo ya thamani ya milioni 700,971,208 (Uk.148 *CAG* Ripoti).

Mheshimiwa Spika, tatu, Mfuko wa Rais wa Kujitegemea pamoja na taarifa ya kazi zilizotekelezwa katika mwaka 2010/2011 kuonyesha kuwa kuna baadhi ya vikundi toka Chalinze, Mkuranga, Kibaha umefaidika na mikopo iliyotolewa na Mfuko huu. Hata hivyo, kwa malalamiko makubwa sana ya wanachama mfano wa kutoka Kata za Chalinze, Mbwewe wanaolalamika kutapeliwa na Mfuko huu. Naiomba Serikali ifanye uchunguzi haraka iwezekanavyo na kuchukua hatua za kisheria kwa watakaobainika kuwatapeli wananchi hao.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa kusimamia vizuri matumizi sahihi ya Rasilimali Watu pamoja na kuratibu ajira katika Utumishi wa Umma. Naiomba Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma itoe taarifa ya hatua ilizochukua mpaka sasa juu ya mishahara hewa iliyolipwa kwa wastaafu, watumishi waliokufa na kuacha kazi. Jambo hili linaifedhehesha sana Serikali na pia kuongeza matumizi ya Serikali. Naiomba ofisi hii itoe takwimu halisi ni kiasi gani cha mishahara hewa iliyolipwa kwa kipindi cha miaka mitano. Serikali iwachukulie hatua kali Maafisa Masuuli, Maafisa Utumishi na Wahasibu wanaohusika na kadhia hii ya mishahara hewa.

Mheshimiwa Spika, ili kuzuia malipo zaidi ya mishahara hewa, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, ifanye haraka katika zoezi la kulipa mishahara ya Watumishi wa Umma katika vituo vyao vya malipo badala ya kupitia Benki. Siku hiyo maalum itengwe ndani ya mwanzo wa mwaka huu wa fedha (2011/2012). Mfumo mpya wa uingizaji wa kumbukumbu za watumishi wapya na

wa zamani *(Payroll Management)* usambazwe kwenye mamlaka za Utumishi wa Umma ili kuzuia malipo ya mishahara ya hewa.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu kwa hotuba nzuri iliyoainisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango kwa mwaka 2010/2011, taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2010 na mapendekezo ya mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mipango ina jukumu kubwa la kusimamia rasilimali ya taifa na kuishauri Serikali kuhusu matumizi bora ya rasilimali. Katika jukumu hili, naomba Tume ya Mipango, iwe makini katika kuishauri Serikali namna ya kugawa rasilimali ya nchi. Ugawaji wa rasilimali ya nchi kwa mwaka wa fedha 2011/2012 haukuzingatia ahadi ya Serikali ya kusaidia Mikoa ambayo iko nyuma kimaendeleo. Mikoa hiyo ni Lindi, Singida, Mtwara na Pwani. Mfano katika bajeti ya mwaka huu 2011/2012 kwenye pesa za maendeleo Mikoa mitatu ya mwisho ni Lindi (20,676,450,000), Pwani (22,380,749,000) na Singida (23,484,488,000). Mikoa inayoongoza ni Mwanza (63,640,682,000), Mbeya (52,625,045,000) na Shinyanga (49,600,896,000). Mfano Mkoa wa Pwani ni Mkoa ambao uko nyuma sana kimaendeleo katika sekta za afya, kilimo, uvuvi, viwanda n.k.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2011/2012 – 2015/16 umebainisha vipaumbele vitano ukianzia Miundombinu, Kilimo, Viwanda, Maji na Rasilimali Watu, hata hivyo, Tume ya Mipango imeshindwa kuishauri vizuri Serikali juu ya ugawaji wa rasilimali fedha ili kufanikisha vipaumbele vinavyotajwa katika mpango huo. Kwa kuwa Mkoa wa Pwani, katika sekta ya kilimo, bajeti ya mwaka huu tumetengewa kiasi cha shilingi bilioni 1.29 kulinganisha na bajeti ya mwaka 2010/2011 ambapo jumla ya shilingi bilioni 2.37 zilitengwa. Je, kwa upungufu na bajeti ya mwaka huu ya zaidi ya shilingi bilioni 1.08, kipaumbele namba mbili cha kilimo kitatekelezwa vipi Mkoa wa Pwani na ukizingatia Mkoa wetu upo nyuma sana, mabonde ya Rufiji, Mto Wami na Mto Ruvu hayajaendelezwa kwa kiasi kikubwa kupitia kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya maendeleo, katika Sekta ya Miradi ya Kilimo *(ASDP)*, Mkoa wa Pwani ni Mkoa wa mwisho kabisa kwa bajeti iliyotengwa ya kiasi cha shilingi bilioni 1.29 tu. Hivyo naiomba Tume ya Mipango ishauri vizuri Serikali juu ya ugawaji wa rasilimali fedha kwa kuzingatia uwiano wa kimaendeleo. Suala la ugawaji wa rasilimali fedha kutozingatia uwiano wa kimaendeleo yaliyofikiwa linaleta manung'uniko na kukata tamaa kwa wananchi wa maeneo hayo na hatujui vigezo vinavyotumika katika ugawaji wa keki ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, hata sekta ya afya, miradi kama ya *Basket Fund*, Mkoa wa Pwani ni wa mwisho kwa kiwango cha bajeti kilichotengwa ambacho ni kiasi cha shilingi bilioni 2.10 pamoja na changamoto ya uhaba wa vituo vya afya ambavyo ni vitano (5) tu kati ya Kata zaidi ya 100, zahanati zipo 235 kati ya mahitaji ya zaidi ya zahanati 600, kwa idadi ya vijiji hivyo inashangaza kuona ni kigezo gani kilichotumika kupanga

kiwango hicho cha bajeti katika mazingira ya changamoto hizo. Je, Tume ya Mipango inajipangaje kuona maeneo yenye changamoto nyingi inatengewa rasilimali fedha na watu za kutosha?

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, Utumishi wa Umma, ni nguzo kuu ya uchumi wa Taifa lolote lile kwani hapa ndipo rasilimali watu wanapopatikana. Tanzania kumekuwa na ufanisi mbovu kwa Watumishi wa Umma kutokana na utendaji ulio mbovu na watendaji kufanya kazi kwa mazoea bila kuendana na kasi ya TEHAMA na mambo yaendeleayo katika duni ya sasa. Ni vema basi Serikali ianze utaratibu wa kupima watendaji wake kwa wiki au mwezi ili wale wasiofikia malengo wapewe adhabu ama onyo na wakiendelea wasimamishwe kazi kwani tuna watu wengi hususani vijana ambao wanazurura ovyo mitaani.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni ukarabati wa Ikulu ya Rais. Kama nilivyochangia katika Ofisi ya Waziri Mkuu, napenda nipate maelezo ya kina ni kwa nini Ikulu inatengewa fedha nyingi hivyo kwa ajili ya ukarabati Tshs. bilioni 7.2 ya mwaka 2010/2011 na mwaka huu ombi la shilingi 10.2 bilioni linaacha maswali mengi sana. Nataka Waziri aeleze Bunge hili fedha hizi za mwaka jana zilikarabati nini na mwaka huu wanakarabati nini. Je, thamani ya fedha inazingatiwa? Je, Mkaguzi Mkuu anakagua matumizi haya makubwa?

Mheshimiwa Spika, utawala bora ni pamoja na Serikali kuwajibika kwa wananchi na si kinyume chake kama inavyojieleza katika Katiba yetu. Imekuwa ni jambo la kawaida kwa viongozi wa Serikali kujiona Mungu Watu na hivyo kuwafanya wananchi kuwanyenyekea. Tunataka viongozi wawajibike kwa wananchi na si vinginevyo. Hii italeta tija na heshima kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha kuona TAKUKURU kwa miaka takribani 15 ni asilimia moja tu ya kesi zote TAKUKURU imeshinda huku 99% ikishindwa. Pamoja na jitihada za kujenga Ofisi Mikoani na Wilayani kama hakuna Watendaji wa kutosha na walio *effective* bado tatizo la kupambana na rushwa halitapungua.

Mheshimiwa Spika, udini ni tatizo kubwa kuliko ukabila na Baba wa Taifa aliwahi kulikemea hili kwa nguvu zake zote. Katika siku za karibuni suala hili limeshika kasi na hakuna anayekemea hili. Tatizo hili limetokea kipindi cha Chaguzi Mkuu wa mwaka 2005 na 2010. Hivyo ni wazi suala la udini linatekelezwa au kuanzishwa na Wanasiasa. Itakumbukwa mwaka 2005, Mheshimiwa Jakaya Kikwete alipigiwa kampeni na Makanisa kuwa ni chaguo la Mungu kuwa Rais, Vyama vya Upinzani wala hawakusema lolote. Cha ajabu mwaka 2010, Dkt. Slaa kugombea ikawa taabu na Makanisa yaleyale yaliyosema JK ni chaguo la Mungu yakakemewa kuwa yana udini. Hili ni jambo baya kwani ilifikia hata Viongozi wa Kisiasa kuwaambia Maaskofu wavue majoho yao waende katika majukwaa ya siasa. Hii ni aibu na hakuna tija kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Usalama wa Taifa ndio Idara inayosimamia ujasusi na kujua nini kinachoendelea katika nchi. Ni jambo lisiloeleweka pale Usalama wa Taifa unapojiingiza katika siasa. Usalama wa Taifa wamekuwa mstari wa mbele kulinda na kutetea Chama Tawala. Tumeshuhudia mengi wakati wa Uchaguzi Mkuu jinsi ambavyo Watendaji wa Usalama wakidiriki kusimamia chaguzi na kufanya yale wanayotaka yafanyike.

**MHE. SALOME D. MWAMBU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja (100%).

Mheshimiwa Spika, Utumishi wa Umma unatakiwa uboreshe au uhakikishe unaboresha mazingira ya kazi na kusogeza huduma kwa jamii. Masuala yote yanayohusu wastaafu yasiishie Mikoani kwa *RAS*? Naomba hili nipatiwe jibu.

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa nini wastaafu wasilipwe *pension* zao kwa kipindi au wakati mmoja, mfano wastaafu wote waliostaafu mwaka 2004 na kurudi nyuma, pensheni yao ni ya kila baada ya miezi sita. Hii ilitokana na makubaliano ya wastaafu na Serikali lakini tukiangalia hali ya ugumu wa maisha na fedha kushuka thamani, miezi sita ni mingi sana. Je, kwa nini wasilipwe pensheni zao kwa miezi mitatu kama wale wastaafu waliostaafu mwaka 2005 na kwenda juu? Kwa nini wasilipwe tarehe moja na kwa miezi mitatu mitatu?

Mheshimiwa Spika, napenda nizungumzie kuhusu mishahara ya Watumishi wa Umma. Watumishi waongezewe mishahara yao bila kujali anatoka wapi kwani hata wale wanaokaa mijini, bado mazingira yao ni magumu kwani *ratio* ya watoto darasani ni wengi sana, mfano 1:90, 1:70 n.k. Maisha ya Watanzania yanahitaji kuboreshwa hata wakulima waboreshewe masoko.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE**: Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, upungufu wa watumishi katika Halmashauri za Wilaya, sababu zake ni:-

1. Ajira kutolewa Makao Makuu ya Wizara, Dar es Salaam.

2. Waombaji kutopenda kwenda katika Halmashauri zetu na hasa vijijini.

3. Mazingira ya vijijini yanatofautiana sana katika ugumu wa mazingira, mfano kutokuwapo umeme, barabara, nyumba za watumishi, ukosefu wa maji safi n.k.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, kwa kuwa ajira hizo zinapotolewa Dar es Salaam huwa haziangalii aina ya watumishi na mahali wanapopangiwa, mfano unampangia mtumishi anayeanza kazi, elimu yake yote ameipata akiwa mazingira ya

mjini, kwa namna yoyote hataweza kukubali kwenda Shule ya Msingi Ngwamuhungile – Kibakwe. Ni dhahiri shairi hatakubali kwenda lakini ungempangia mtumishi mpya aliyesoma Pwaga – Kibakwe angekubali kwenda.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa jumla:-

(a) Halmashauri zirudishiwe uwezo wa kuajiri kada za Walimu, Waganga wa Zahanati na Manesi, Maafisa Ugani na Watendaji wa Vijiji na Kata.

(b) Watumishi wanaoomba ajira za umma waseme wanataka kufanya kazi Halmashauri zipi ikibidi hata Kata wataje.

Mheshimiwa Spika, jimbo langu la Kibakwe lina upungufu mkubwa wa watumishi mfano tulipangiwa Walimu wa Sekondari zaidi ya 30 lakini 13 walipoenda kwenye shule hizo, kesho yake waliondoka na hawajarudi tena, huo ni mfano mmoja tu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. STEPHEN J. MASELE**: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya M. Kikwete kwa kuchaguliwa tena na Watanzania kuongoza Taifa letu. Pia napenda kuchukuwa nafasi hii kuwapongeza Mawaziri wote wa Ofisi ya Rais kwa kuanzia na Mheshimiwa Stephen Masato Wasira, Mheshimiwa Mathias Chikawe na Mheshimiwa Hawa A. Ghasia kwa hotuba zenu nzuri. Mchango wangu katika hotuba hizi nitajikita katika Utawala Bora na Sera na Mahusiano.

Mheshimiwa Spika, kwanza, Idara ya Usalama. Idara ya Usalama iongezewe uwezo wa kibajeti ili iweze kutimiza majukumu yake kikamilifu. Mara kadhaa Viongozi wa Juu hususani Mheshimiwa Rais, amekuwa akipotoshwa na taarifa ambazo zimekuwa na utata ama upungufu. Kwa mfano, uzinduzi wa Hotel kule Arusha, tukio la kukabidhi magari ya wagonjwa pale Ikulu na kadhalika. Hoja yangu ni kuimarisha utafiti wa taarifa mbalimbali ikiwemo za kiutendaji, kimaadili na kiutafiti.

Mheshimiwa Spika, pili, uvujaji wa nyaraka za siri za Serikali. Inasikitisha kuona watu binafsi wakiwemo Waheshimiwa Wabunge wakijitapa kuwa wana nyaraka za siri za Serikali. Naiomba Serikali idhibiti taarifa hizi muhimu za Serikali na endapo kuna watumishi wa Umma wachukuliwe hatua za kinidhamu.

Mheshimiwa Spika, tatu, mahusiano ya Serikali na Taasisi za Dini nchini. Naiomba Serikali iongeze juhudi kubwa kuimarisha mahusiano baina yake na Taasisi za Kidini kwani dini imekuwa mhimili na mdau mkubwa wa maendeleo na amani ya nchi hii. Kuwe na *control* kubwa ili kudhibiti mambo yanayolenga upotoshaji kwa umma unaoweza kufanywa na taasisi za dini. Mfano, uchaguzi wa mwaka 2010 dini imehusishwa kwa kiwango kikubwa na ushawishi ama uchochezi wa kisiasa, ni jambo la hatari sana kwa usalama na ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nne, watumishi hewa na stahili za watumishi. Serikali iunde kikosi maalumu cha kufuatilia utendaji na huduma zinazotolewa na Watumishi wa Umma ambao wamekuwa wakituhumiwa kutoa huduma mbovu, pia Serikali ihakikishe suala la watumishi hewa linatatuliwa mara moja. Watumishi wanaostahili nyongeza za mishahara walipwe kwa wakati. Kuna ongezeko kubwa la madeni ya watumishi mfano Walimu, Polisi na Idara zingine za umma.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata nafasi ya kuchangia, naiomba Serikali pia iongeze posho kwa watumishi wasioona ambao wana mchango mkubwa kwa Taifa hili. Serikali iangalie mpango wa *incentives* kwa walemavu wa ngozi na wasioona katika Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED**: Mheshimiwa Spika, mimi napenda nizungumzie kuhusu utawala bora, huu utawala bora kwa kweli katika nchi yetu ni ndoto tu. Hata mtu akienda ofisini na madai yake basi hasikilizwi. Matatizo ni mengi sana katika ofisi za Serikali, mtu anaweza kuhamishwa katika sehemu moja na kupelekwa nyingine kwa ajili ya chuki za kisiasa tu. Akienda kada wa Chama Tawala akimchukia mtu basi ataongea na Afisa wa Serikali basi itatafutwa sababu ya uongo na kweli atahamishwa tu.

Mheshimiwa Spika, pia nataka nizungumzie kuhusu rushwa, kwa kweli matatizo haya ni makubwa sana katika nchi yetu. Ushahidi wa rushwa ni tabu sana kupatikana. Kwenye maofisi ya Serikali jambo hili limetawala sana, mtu hawezi kuajiriwa kirahisi, mazingira yanaonesha wazi kuwa rushwa inatembea kiujanjaujanja. Mimi nashauri Serikali ifikirie upya namna ya kudhibiti rushwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda nipate maelezo kuhusu malipo ya waliokuwa watumishi wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wameshalipwa kiasi gani na wanadai kiasi gani na watamaliziwa lini madeni yao ya muda mrefu.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA**: Mheshimiwa Spika, nami napenda kuchangia bajeti iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuongelea utawala bora na utawala wa kisheria. Katika nchi yetu, dhana ya utawala bora na wa kisheria, unaathiriwa na Watendaji wasioitakia mema nchi yetu, kwani mtu anaweza kuthamanishiwa mali zake kwa uwazi na hesabu ikatolewa, mfano migomba 700, lakini mtu huyo wakati wa malipo analipwa migomba 120 na anapoteza migomba 580, huu ndio utendaji bora au ni unyonyaji wa wananchi. Huyu anaweza akawa mwanakijiji, ataenda kwa Katibu Kata atasema kadhulumiwa, ataenda kwa Mkuu wa Wilaya atasema kadhulumiwa, lakini mlipaji wa mwisho ni nani? Mtu huyo atamaliza miaka hata mitano au zaidi anahangaikia malipo yaliyopungua kwa muda mrefu hata kumaliza pesa zake kidogo ambazo anazo.

Hebu Serikali iangalie tatizo la Watendaji wake ambao ndicho chanzo cha kuchafua Serikali na wananchi kuichukia Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, katika Jiji la Mwanza maeneo mengi, wananchi hawapati haki zao za msingi. Mfano hivi Watumishi wa Umma hawaoni kuwa ukiwa Nesi unahitajika kuhudumia wagonjwa, baadhi ya kina mama hupoteza maisha wakati wa kujifungua, mara nyingi huwa ni uzembe wa Manesi kutowajibika katika kazi zao. Naiomba Wizara kuwafahamisha watumishi wake, ukiwa katika Zahanati au hospitali unachohitajika ni kuwa mtii katika kazi yako ambayo unatumika nayo, ukiwa Bwana au Bibi Afya unatakiwa kuwa karibu na kazi yako na si busara kukamata watu na kuwatoza pesa eti wamekiuka taratibu za afya.

Mheshimiwa Spika, rushwa ni adui wa haki na adui wa maendeleo, rushwa inatutafuna Watanzania, hasa rushwa kubwakubwa kama rushwa ya Rada. Ni rushwa mbaya sana na imelitia aibu Taifa letu. Nafahamu wazi Prof. Lipumba alipigia kelele sana suala la kununua rada hii na kusema ina harufu ya rushwa lakini Wanasiasa hawa wa Chama cha Mapinduzi baadhi yao walimwita Profesa Uchwara. Leo hii tunadai tumeibiwa pesa kwenye manunuzi ya rada, tukisema tumeibiwa ni uongo kwani TAKUKURU ilimuhoji Salesh na kumruhusu aondoke, baadae wakaanza kumtafuta, huu ni uongo mtupu. Nadhani TAKUKURU nao ni wadau wa kupoteza pesa hizo. Ni vema basi waliohusika wakamatwe na wafilisiwe ili iwe fundisho kwa wengine. Hata hao TAKUKURU nao ni bora mhusika ajiuzulu au achukuliwe hatua na uwe mfano bora kwa wengine, hapo Tanzania bila Rushwa Inawezekana. Ni lazima tuwe makini sana na hawa wanaopewa kazi ya kudhibiti rushwa, kwani badala yake wamekuwa wanakamata rushwa ndogondogo lakini wakina bwana visenti wako huru na tunao humu ndani.

Mheshimiwa Spika, katika utumishi wa umma kuna baadhi ya watumishi ni mzigo kwa Serikali maana hawafanyi kazi kwa uzalendo. Ni lazima sasa Watumishi wa Umma waambiwe kwa uwazi kuwa wanahitajika kuwa wazalendo zaidi ndani na nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, ni lazima wafanyakazi hao nao wapate mishahara ambayo inaweza kukidhi haja, kwani maisha kwa sasa yako juu sana na Serikali iangalie mishahara ambayo inaweza angalau kukidhi haja hata kidogo. Tuwajali watumishi wetu ili waepukane na rushwa, ahsante.

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULLA**: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa wema wake mwingi kutuwezesha sisi sote kuwa wazima wa afya.

Mheshimiwa Spika, napenda kupongeza sana hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi. Pia nimpongeze Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu, kwa kazi zao nzuri wanazozifanya pamoja na changamoto nyingi zinazojitokeza lakini naomba niwapongeze kwa ukomavu wao huo.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nijikite upande wa ajira kwa vijana wetu. Vijana wetu wamekuwa wakimaliza Vyuo na kukosa ajira kabisa, wakati huo wafanyakazi kada mbalimbali wanastaafu kazi, kwani zile nafasi zinaenda wapi? Kumekuwa na tabia mbaya ya kufahamiana au kujuana na hata kama nafasi zinapokuwepo watu hawatangaziwi au hazitangazwi na kama hata zikitangazwa inakuwa *formality* tu lakini zinakuwa zimeshajazwa tayari. Hii sio sawa, ni kuua demokrasia ya kweli, pale nafasi zinapojitokeza hatua za kujaza nafasi hizo ziwe wazi ili watu wanaostahili na wenye sifa waweze kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu watumishi kwa ujumla, kuna baadhi ya kada kama Madaktari na Manesi wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Unakuta Kituo cha Afya au *Dispensary* wana Daktari mmoja, huyohuyo azalishe akina mama, huyohuyo asafishe vidonda, huyohuyo atoe dawa dirishani na akienda kuchukua mshahara kituo kinafungwa. Huu ni unyanyasaji, ni kumnyanyasa Daktari huyu na pia kuwanyanyasa wananchi. Serikali sikivu ya CCM tunaiomba itoe ajira kwa vijana wetu na katika vituo hivyo waweze angalau kukaa watu watatu yaani Daktari mmoja na Manesi wawili.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya maeneo ya Tabora Vijijini, Geita, Iringa Vijijini na kwingineko kwingi kuna vituo ambavyo wafanyakazi wameshastaafu lakini kutokana na uhaba wa wafanyakazi wa kada ya Afya na utaalamu wao walionao wameomba kupewa mkataba ili waweze kuendelea kutoa huduma pale ikizingatiwa wataalam hao wachache lakini cha ajabu mikataba hiyo hawapewi na watu wanaendelea kuteseka. Tunaiomba Serikali iweze kuliona hilo ili wataalam hawa waweze kupewa mkataba ili waendelee kusaidia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kupandishwa vyeo, tunaiomba Serikali iweze kuliangalia vizuri suala hili kwani linakatisha tamaa kwa upande mwingine kwa mfano, Wahasibu hawapandishwi daraja mpaka aende kusoma au vinginevyo. Sasa unakuta Mhasibu huyu kafanya kazi muda wa miaka 20 na ni mzee tayari kwenda shule hawezi tena, watoto wanaajiriwa wanakwenda shule wanamzidi mshahara, sawa, lakini sasa unakuta wahudumu ambao wao sheria zao wanapanda kutokana na uzoefu na *increment* nao pia wanampita mshahara. Tunaomba Serikali iweze kuwafikiria watu kama hawa ili nao waweze kupandishwa kutokana na kufanya kazi kwa muda mrefu au kutokana na uaminifu wao kazini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la *overtime*, ni suala ambalo linampa ahueni kidogo ya maisha mfanyakazi huyu. Kwani kama tunavyojua mshahara si mkubwa, hautoshi lakini watu wakipewa kidogo hiyo *overtime* inamsaidia kwa kiasi fulani kupunguza ukali wa maisha. Naiomba Serikali iwape wafanyakazi wote muda wa ziada wa kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia 100%.

**MHE. AUGUSTINO L. MREMA:** Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri, ukurasa wa 35, imetajwa kazi ya kuhudumia Viongozi Wastaafu wa Kitaifa 12.

Naomba kuiambia Serikali kwamba mwaka 1993, Rais Ali Hassan Mwinyi, aliniteua kuwa Naibu Waziri Mkuu. Cheo hicho kiliwahi kushikiliwa na Dkt. Salim Ahmed Salim. Wakati nikiwa na cheo hicho, nilikuwa napata mafao *(privileges)* ya Waziri Mkuu ikiwa ni pamoja na ulinzi, *motor cade* na marupurupu yote. Baada ya hapo, Mheshimiwa Rais Ali Hassan Mwinyi alinibadilisha kazi na kuwa Waziri wa Kazi na Maendeleo ya Vijana. Pamoja na kutumikia cheo cha Unaibu Waziri Mkuu kwa uadilifu mkubwa, kinachosikitisha ni kwamba hadi leo hii sijawahi kulipwa stahili zangu kama Naibu Waziri Mkuu Mstaafu. Naomba Waziri anayeshughulikia masuala ya Utumishi wa Umma atoe maelezo ni lini ataanza kulipa stahiki hizi pamoja na malimbikizo yake.

Mheshimiwa Spika, hoja zinazotolewa kwamba cheo hiki hakipo kisheria, hazina mashiko kwani Rais aliyeniteua hakuwa na madaraka Kikatiba ya kuanzisha au kuendeleza ofisi hiyo? Kwa nini nilikuwa napata *privileges* zote za Waziri Mkuu, ikiwa ni pamoja na *motorcade?* Wako Mawaziri Wakuu waliojiuzulu, lakini wakachukuliwa kuwa walistaafu na kulipwa haki zao zote hadi leo, kwa nini mimi nabaguliwa?

Mheshimiwa Spika, aidha pia kuna aliyekuwa Waziri Kiongozi aliyewekwa hata kizuizini lakini sasa anapewa mafao yake yote na Serikali. Je, kwa nini iwe nongwa kwa mimi Augustino Lyatonga Mrema? Naomba Waziri aeleze huu ubaguzi atauendeleza au ataukomesha.

Mheshimiwa Spika, MKURABITA, malengo ya MKURABITA ni pamoja na kurasimisha biashara za wanyonge. Kwa kuwa jukumu hili linajumuisha kupima maeneo ya vijiji ili kuondoa mvutano unaoweza kujitokeza pindi wanapokuja wawekezaji, je, vijiji vingapi vya Jimbo la Vunjo vimekwishapimwa?

Pamoja na vijiji, MKURABITA wana jukumu la kupima viwanja vya Watanzania, je, viwanja vingapi vimepimwa na wahusika kupatiwa hati miliki za maeneo yao huko Vunjo? Hii itamsaidia Mtanzania kuweza kupata hati itakayomwezesha kupata mkopo Benki. Nitashukuru sana kama Wizara itaelekeza nguvu zake Vunjo.

Mheshimiwa Spika, utawala bora, napenda Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge ni hatua zipi zimekwishafikiwa katika uchunguzi wa:-

(a) Kesi za Uchaguzi wa Mwaka 2010;
(b) Kesi ya Kagoda;
(c) Kesi ya *Tangold*;
(d) Kesi ya *Deepgreen*; na
(e) Kesi ya Meremeta.

Mheshimiwa Spika, kesi hizi zimechukua muda mrefu sana, wananchi wanataka kujua ni lini zitakamilika na waliohusika kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri alijulishe Bunge ni wakati gani *PCCB* wanaamua kuanza kuchunguza kesi za rushwa zinazotajwa hata huku Bungeni, ni lini zitaanza kuchunguzwa na hatua kuchukuliwa?

**MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, naomba niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri sana inayokidhi mahitaji ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kuhusu mishahara midogo ya Walimu. Walimu ni taaluma ya muhimu sana nchini, lakini sababu ya maslahi madogo taaluma hii imeshuka hadhi. Wengi hawaiheshimu, imepoteza ladha sababu ya maslahi madogo. Walimu wana mishahara midogo sana, hawana nyumba za kuishi, hawana marupurupu ya aina yoyote. Naomba hilo liangaliwe kwa sababu Walimu wanafanya kazi kwa mazingira magumu sana, vitendea kazi hawana, wanasahihisha madaftari mengi bila posho, wanaishi vijijini, mishahara inachelewa lakini bado wanavumilia. Tujue kwamba walimu wakifurahi ndio watazalisha Madaktari, Wanasheria, Mainjinia na hata wasomi wazuri.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iwaangalie walimu kwa jicho la huruma, waongezewe mishahara wapewe nyumba za kuishi walipwe malimbikizo ya madai ya walimu ili watoto wetu wapate huduma nzuri ya hao walimu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia hoja iliyo mezani, naomba nitumie nafasi hii kuwapongeza Mawaziri wote waliopo katika Wizara hizi akiwemo Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mhesimiwa Stephen Masato Wasira na Mheshimiwa Mathias Chikawe.

Mheshimiwa Spika, nianze na uvujaji wa nyaraka za siri katika ofisi za Serikali. Jambo hili ni hatari sana, tumeshaona jinsi vyombo vya habari vikianika siri katika magazeti yetu, hii ni aibu sana kwa nchi. Huwa najiuliza ni kweli Serikali haijui wanaovujisha hizo nyaraka? Kama wanawajua wanawapatia adhabu gani ili iwe fundisho kwa wengine?

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ninalopenda pia kulichangia ni jinsi Idara nyingi za Serikali zinazokaimisha vyeo kwa muda mrefu. Ni kwa nini usiwepo utaratibu wa kisheria ambao kama mfanyakazi anakaimu labda uwekwe muda ili muda huo ukifika huyo aliyekaimu apande *automatical*.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu ucheleweshaji wa mafao mara mfanyakazi anapostaafu. Tumeshaona jinsi wazee wastaafu wanavyopatishwa tabu ya nenda, rudi Wizara ya fedha wanapopata tabu. Ushauri wangu sasa hivi kuna Teknolojia mpya kwa nini mafao yasiandaliwe kabisa mwaka mmoja kabla ya kumaliza. Nadhani hili linawezekana sababu tunajua idadi ya wafanyakazi wanaostaafu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu rushwa kwa baadhi ya ofisi za Serikali na hasa Askari Polisi, *Traffic Police*, Mahakama zetu, katika Hospitali. Maeneo yote haya yanaigusa jamii moja kwa moja. Ningeshauri Serikali iweke mkakati madhubuti ya kuhakikisha

kuwa kero hizo katika idara hizo inadhibitiwa ipasavyo. Maana ni aibu sana kwa Taifa letu na fedheha kwa wananchi tunaowaongoza.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitoe mchango wangu kwa Ofisi ya TAKUKURU. Nimpongeze Waziri mwenye dhamana hiyo Mathias Chikawe na watendaji wote wa Wizara yake. Niwapongeze kwa kazi yao ya kuzuia rushwa nchini. Lakini kuna baadhi ya watendaji si wazuri sana, wamekuwa wakiwalinda wala rushwa mpaka kupatiwa majina ya TAKUKURA. Hivyo, naiomba Serikali ichunguze tatizo hilo ili watendaji hawa watambuliwe na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Spika, pia nichukue nafasi hii ya kumpongeza sana Mkurugenzi wa *TASAF*, Mary I. Likwelile, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kusaidia uibuaji wa miradi katika Halmashauri zetu na hasa katika ngazi ya Mtaa. Ningeomba sana uwepo mkakati wa kazi hii nzuri kuwafikia wananchi waliopo katika ngazi ya vijiji wapatiwe elimu ya jinsi ya kuibua miradi katika vijiji vyao ili waweze kufaidi kama ilivyo katika Halmashauri zilizopo mijini.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nawaomba *TASAF* itupatie mkakati wa elimu kwa wananchi ili sisi Wabunge tuweze kuisemea tunapokwenda kukutana na wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI**: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kusema kwamba naunga mkono hoja hii. Hata hivyo ninayo maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ajira ya Maafisa Watendaji wa Vijiji *($VEO_S$)*. Kigezo cha elimu ya kidato cha nne katika ajira ya *$VEO_S$* ni kizuri, lakini kwa sasa acheni kuweka kigezo cha nyongeza kwamba wawe na *Certificate* ya ujuzi! Nashauri tuwapate vijana wa *form four* na tuwaajiri, baada ya hapo ndipo Halmashauri husika ziwapeleke kwa mafunzo ya *certificate* na hasa Chuo cha Hombolo ili kuimarisha utendaji katika Serikali za Vijiji ambako hivi sasa utendaji ni mbovu sana. Fedha nyingi za miradi zinapelekwa vijijini lakini uwezo wa kuzisimamia haujajengwa, hivyo Serikali ianze kuzijengea uwezo Serikali za Vijiji kwa kuajiri vijana wenye elimu ya *form four* na kuwasomesha katika Chuo cha Serikali za Mitaa cha Hombolo.

Mheshimiwa Spika, niongelee kuhusu Wilaya ya Manyoni kutokuwa na *DAS*. Kwa takriban miaka minne Wilaya ya Manyoni imekuwa na Makaimu Makatibu Tawala *(Acting DAS)* bila ya kuwa na *DAS* kamili, aliyepo hivi sasa anakaimu nafasi hiyo kwa miaka mitatu. Kwa nini hali hii inaendelea kwa muda mrefu?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, kumekuwepo malalamiko toka kwa wananchi juu ya ajira na hususan taratibu iliyoanzishwa ya kuwa na Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, kwa matarajio ingeweza kuleta ufanisi na kupunguza kero, matokeo yake yamekuwa tofauti na kuwa kero badala ya ufanisi na faraja.

Mheshimiwa Spika, hofu yangu hayakufanyika maandalizi ya kutosha na kuiwezesha Sekretarieti hiyo kwa rasilimali fedha na watu kwa kuzingatia ukubwa wa nchi hii na mahitaji yake ya ajira pia uamuzi huo unakinzana na mpango wa kugatua madaraka  na kuipunguzia mzigo Serikali Kuu ya maamuzi na kuwepo kwa Sekretarieti ya Ajira ni kinyume chake.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza kero na malalamiko ipo haja Wizara kuangalia upya uwepo wa Sekretarieti hii na kama ni lazima basi wawezeshwe vya kutosha kukabili changamoto zilizopo na kupunguza malalamiko mengi.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Ghasia, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanazozifanya za ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kuhusu Sekretarieti ya Ajira lengo la kuundwa kwa Sekretarieti ya Ajira la kuendesha mchakato wa ajira wa watumishi wa umma kwa niaba ya waajiri nchini, ni mzuri kama kusingekuwa na urasimu mkubwa uliopo sasa wa mchakato wa ajira kuchukua muda mrefu, Halmashauri zinapotuma maombi kwenye Sekretarieti.  Kwa sababu ya urasimu uliopo ndio maana baadhi ya Halmashauri hudhani kuwa, kuna upendeleo wa huduma za ajira kwa baadhi ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, hakuna sababu ya kupeleka madaraka makubwa kwa wananchi *(D & D)*, fedha nyingi kwenye Halmashauri lakini hawaruhusiwi kuajiri japo mhudumu, dereva na kadhalika kwa maana ya kada za chini.  Nashauri Sekretarieti ya Ajira aidha ianzishe Ofisi zao katika Wilaya zote au ikasimu madaraka ya ajira za kada za chini kwa Halmashauri ili utendaji wa ajira za kada hizo ufanyike kwa ufanisi mzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, maadili katika utumishi wa umma yameporomoka sana. Kwa sasa kupata nyaraka za siri za Serikali au kusoma nyaraka za siri za Serikali ni jambo la kawaida kabisa, baadhi ya watu na hata Waheshimiwa Wabunge hujua kilichozungumzwa kwenye kikao cha Baraza la Mawaziri na pia kikao cha Makatibu Wakuu.  Maadili ya watumishi wa umma yako wapi? Mbona Tume ya Maadili hushughulika kujua mali za viongozi lakini hawashughuliki na viongozi au watumishi wanaovujisha siri za Serikali?

Mheshimiwa Spika, siyo ajabu kuingia ofisi ya Serikali na kumkuta Afisa au Katibu Muhtasi akicheza karata kwenye Kompyuta.  Sio ajabu pia kumkuta mtumishi wa umma mitaani saa za kazi na kuchelewa kufika ofisini.  Ofisi za umma pia zimefanywa maduka ya kuuza nguo, viatu na bidhaa mbalimbali.  Hii inaonesha jinsi morali ya kazi ilivyoshuka kwa watumishi wa umma, inaonesha pia kuwa hakuna usimamizi au watumishi wamekata tamaa.  Nashauri watumishi wa umma wafuate sheria na kanuni za kazi na utaratibu wa *OPRAS* utiliwe mkazo.

Mheshimiwa Spika, TAKUKURU wanafanya kazi nzuri. Nawapongeza viongozi tuwape ushirikiano wa karibu ili waweze kufikia malengo yao. Kwa kuwa Watanzania walio wengi ni maskini, wanarubunika na wenye uwezo mkubwa, hivyo, kushindwa kutoa ushirikiano wa karibu kwa TAKUKURU hasa kipindi cha uchaguzi. Hata hivyo, kipindi cha chaguzi za 2010, TAKUKURU walijitahidi sana. Nawasihi TAKUKURU wasiwaogope Polisi. Polisi wanakula rushwa sana kuwaonea wananchi waaminifu wasiotoa rushwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha hoja zangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, ni mmonyoko wa maadili kwa vijana wetu. Hivi sasa nchi yetu ina tatizo la mmomonyoko wa maadili, vijana wetu wanazungumza jambo bila ya kuangalia anazungumza nini, anazungumza wapi na anazungumza na nani, au anayezungumza naye yupo katika rika gani.

Mheshimiwa Spika, hii inatokana na vijana wetu baada ya kumaliza kusoma kukosa elimu ya ziada, anapotoka Sekondari au Chuoni anaajiriwa au anakimbilia katika siasa. Naiomba Serikali kurejesha ule utaratibu wa vijana wetu baada ya kumaliza vyuo kwenda JKT ili kupata elimu ya ukakamavu yenye maadili ya Watanzania na kufundishwa pia kuogopa rushwa.

Mheshimiwa Spika, pili, Jiji la Dar es Salaam ni kero; umeme, miundombinu na ongezeko kubwa la watu. Pia kuna kero ya msongamano wa magari, vipi kuhusu ujenzi wa njia za kupita mabasi yaendayo kwa kasi? Kuhusu ujenzi huu naona bado Serikali kuipa uzito. Ingawa hatua ya awali imeanza Agosti, 2010 na hatua ya pili na ya tatu zimo katika maandalizi ya usanifu. Je, tatizo ni nini kwa wananchi wanaotaka kuona utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nichangie kuhusu Mfuko wa *TASAF*. Pamoja na uamuzi mzuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti wa kuomba kuendeleza ujenzi wa miradi mbalimbali (viporo) ambayo ilianzishwa kipindi cha miaka iliyopita. Ujumbe kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti ukiandamana na Mbunge wa Jimbo la Serengeti ulikwenda Ofisi ya Rais kuwasilisha hoja hii ya msingi na muhimu ya kupewa fedha ya kumalizia viporo ambavyo vilikuwa viishe mwaka 2009/2010. Hadi leo hii fedha hizo hazijatolewa tangu ujumbe huo ulipokwenda Ofisi ya Rais, Januari 2011. Kwa kuwa viporo hivyo vya miradi vikiwemo Zahanati, madarasa na barabara za vijiji. Ilikuwa ni matarajio ya Wilaya, baada ya kumaliza kazi hiyo ya viporo ndipo kuanza kazi ya miradi mipya, hivyo Wilaya imekwama kufanya kazi za maendeleo kutoka *TASAF*. Naomba mazingira haya ichukuliwe ni dharura ili kuokoa hali hii iliyopo. Pia tunaomba fedha ya *retention* iliyoko Halmashauri itumike Wilayani.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa MKURABITA ulipoanza nchini mwaka 2004 ulipokelewa kwa hamasa kubwa sana na Watanzania wengi. Lakini kutokana na utekelezaji wa pole pole sana mfano Wilaya ya Serengeti iliingia katika utekelezaji wa MKURABITA mwaka 2009 ambapo vijiji vitano (Ikoma Robanda, *Park* Nyigoti, Makundusi, Nyigoti na Kyambahi) viliteuliwa kuingia katika mpango huu wa MKURABITA. Lengo ilikuwa baada ya vijiji hivyo vitano kukamilika kupimwa kungekuwa na mwendelezo kwa kupima Vijiji vingine 77 kwa masikitiko makubwa hadi leo hii kasi ya upimaji imesimama, hali hii kama itaendelea itachukua kama miaka 22 ili kukamilisha upimaji wa maeneo katika Wilaya ya Serengeti. Ni vizuri hali hii ya ucheleweshaji itazamwe upya na hii itasaidia kuwapa wananchi haki yao na kuondoa au kupunguza migogoro mikubwa iliyopo ya kugombea ardhi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu TAKUKURU. Chombo hiki wakati kinaanzishwa, ilionekana ni faraja kwa Watanzania kwa sababu rushwa ni adui wa haki lakini umekuwa ni usemi bila vitendo thabiti kudhibiti rushwa. Rushwa imekuwa Kansa, haitibiki machoni kwa Watanzania. Haiwezekani hadi leo hii kesi zilizo TAKUKURU, ni asilimia moja ndizo imeshinda, huu ni udhaifu mkubwa sana. Hii ilidhihirika wakati wa uchaguzi mkuu na kura za maoni, 2010 waliotumia fedha na rushwa hawakufuatwa na TAKUKURU bali wagombea ambao hawakuwa na fedha ndio waliofuatwa fuatwa na kusumbuliwa na kusababisha usumbufu mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa *OPRAS (Open Performance Review Appraisal System)*, kwa dhana ni nzuri sana lakini ufuatiliaji na usimamizi wake ni hafifu. Tangu uanzishwe nchini mwaka 2000 utekelezaji wake haueleweki sehemu za kazi hata kwa viongozi wasimamizi. Hivyo, lengo la kuondoa ujazaji wa taarifa za siri za mtumishi imeshindikana kwa sababu utaratibu wa zamani haufanyiki na huu mpya (*OPRAS*) haufanyiki na kujikuta hadi leo, hii nchi haina utaratibu mahiri wa kufuatilia utendaji wa kazi na tathmini kwa watumishi. Hakuna tija inayoonekana dhahiri kutokana na mishahara wanayolipwa watumishi na kazi wanazofanya. Utaratibu huu wa *OPRAS* ulianza na dhana iliyosababisha ufifie wa *SASE (Selective Appraisal for Salary Enhancement)*, hivyo ilijengeka kuwa kujaza fomu za *OPRAS* ni kwa ajili ya kupata posho ya ziada, utaratibu huu wa *SASE* ulipofeli kutekelezwa hivyo mwelekeo wa ujazaji wa fomu na kutekeleza *OPRAS* ukafifia. Pia maeneo mengi nchini hayana mipango mikakati *(Strategic plans)*, *Annual plans* (mpango wa mwaka), hivyo sio rahisi mtumishi kujaza malengo ya kazi zake kama hakuna mpango anaoweza kuutafasiri au msimamizi wake kuelewa atampima vipi mtumishi wake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi kazini. Upo usimamizi usioridhisha katika sehemu ya kazi ambao unasababisha kushusha ufanisi wa kazi. Watumishi wengine kuzurura jirani na maeneo ya kazi hata kutoroka kwa visingizio vya kwenda kunywa chai, posta, benki ama matibabu na hivyo kutotoa huduma inayotakiwa kwa wakati huo. Utaratibu wa kusimamia watumishi kazini uangaliwe upya ili kuongeza uwajibikaji kwa wasimamizi na watumishi kwa jumla. Je, mbona wanavyodai mishahara iongezwe watumishi hao hao hawaelezi upungufu huo. Haki na wajibu ni vitu viwili haviachani kwa utaratibu. Lakini pia Vyama Huru vya Wafanyakazi vinachangia kutosimamia vema

watumishi kwa vile hawatoi mafunzo ya kina ya haki na wajibu kwa watumishi wanaowaongoza na mara nyingine wanachochea migomo makazini.

Mheshimiwa Spika, Utaratibu wa *e-Governance* uanzishwe sehemu zote za kazi ili isaidie kufuatilia na kusimamia watumishi ili kuongeza tija pia *e-governance* itasaidia kudhibiti hata ulipaji wa kodi kulingana na biashara ya mtu.

Mheshimiwa Spika, uhusiano wa kimapenzi kazini na rushwa ya ngono litafutiwe ufumbuzi nalo ni suala linalosababisha usimamizi wa kazi kuwa duni. *Induction course* kwa watumishi wapya ifanyike maeneo yote ya kazi na pia watumishi wote wafundishwe jinsi mtumishi anapaswa ku-*behave*.

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Spika, madai mbalimbali ya watumishi yameendelea kushughulikiwa na Serikali, lakini madai ambayo yamepewa kipaumbele ni madai ya walimu. Licha ya kuwa watumishi wa kada nyingine nao wana madai mengi. Zipo kada mbalimbali kama Afya, Kilimo, Maendeleo ya Jamii, Ujenzi, Mifugo na kadhalika, watumishi wake wanaidai Serikali fedha nyingi. Ni vizuri tujue pia haya madai ya watumishi wa kada nyingine yanashughulikiwaje na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri nyingi nchini zimeshindwa kulipa madai ya mafao mbalimbali kwa watumishi iliowaajiri ambao ama sasa wamestaafu au wamepunguzwa. Nashauri ofisi yako itoe maelekezo ya Halmashauri zote za Wilaya zifanye uhakiki wa madai hayo yote kwa kila Halmashauri ili kila Halmashauri ijue kiasi cha madai ya wastaafu au walioachishwa kazi ili kwa ujumla Wizara yako ijue ukubwa wa tatizo, lakini zaidi kuziagiza Halmashauri hizo kuandaa mpango wa kulipa madeni hayo ili watumishi wanaoendelea kutaabika waweze kulipwa kabla hawajafa.

Mheshimiwa Spika, watumishi wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi, baada ya Wilaya hiyo kuanzishwa mwaka 2007 sasa wamehamia katika Makao Makuu ya Wilaya hiyo wakitokea Dodoma Mjini lakini watumishi hao bado hawajalipwa fedha zao za uhamisho hadi sasa. Ni matumaini yangu kwamba, jambo hili Mheshimiwa Waziri atalitolea maelezo ili nijue watumishi hao wapatao zaidi ya 200, ni lini hasa Serikali itaandaa malipo hayo?

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na napenda kuwapongeza Mawaziri wafuatao: Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mheshimiwa Stephen Wasira, na Mheshimiwa Chikawe, bajeti yao ni safi na napenda kuwapongeza Wakurugenzi wafuatao: Ndugu Othman, Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa; Ndugu Dokta Hosea, Mkurugenzi wa TAKUKURU; Ndugu Jaji Solome Kaganda, Mkurugenzi wa Tume ya Maadili ya Viongozi. Nawapongeza sana hawa Wakurugenzi wamefanya kazi nzuri hadi leo Tanzania inasifika.

Mheshimiwa Spika, Usalama wa Taifa wanatakiwa wapewe msaada mkubwa na bajeti yao iongezwe ili waweze kufanya kazi yao vizuri.

Mheshimiwa Spika, TAKUKURU wamefanya makubwa kama sio wao hadi leo hii mimi nisingefika hapa. Wagombea wengi walizuiwa na kukamatwa wakati wa kampeni hadi mimi mkulima nimeingia Bungeni, wanatakiwa wapongezwe sana na wapewe vifaa vya kisasa, vitendea kazi na mishahara ipandishwe ili wafanye kazi yao vizuri.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie Tume ya Maadili Viongozi. Uongozi wa Jaji Solome Kaganda tumeona anavyofuatilia maadili ya viongozi lakini cha kushangaza Ofisi yao haiendani na jinsi ilivyo, wajengewe ofisi mara moja ya kisasa, iendane na utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, wafanyakazi wa Ofisi ya Bunge na wao wana haki ya kupewa posho na marupurupu mengine kama Wabunge kwani na wao ni sehemu ya Bunge na wana haki zote kama Wabunge, kwa hiyo, wapandishiwe mshahara mara moja.

**MHE. MWIGULU L.N. MADELU:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dokta Jakaya M. Kikwete kwa nia yake ya dhati na jitihada zake katika kutekeleza majukumu kwa uongozi thabiti unaojali sheria na uliojaa ujasiri, hekima, busara na utawala bora kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, mafanikio makubwa yamejitokeza katika nyanja tofauti tofauti ikiwemo katika mapambano dhidi ya rushwa. Hii ina vielelezo vingi sana ikiwepo kupungua kwa vitendo vya rushwa wakati wa uchaguzi. Vijana wengi nami nikiwa wa mfano nimeshinda uchaguzi kwa kuwa TAKUKURU imefanya vizuri kazi yake. Hivyo hivyo, ni dhahiri kwamba katika Bunge, Wabunge 140 ni vijana tusio na pesa hata kama wananchi wangetaka watuchague bila utawala bora tusingeweza kuchaguliwa. Pia katika Bunge, 57% ya Wabunge ni wapya, hii nayo inadhihirisha jinsi uchaguzi ulikuwa ni wa haki.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze TAKUKURU kipekee kwa kusogeza huduma karibu na wananchi kwa kujenga ofisi zao Wilayani ikiwemo Wilaya ya Iramba. Hii imesaidia kufanya kazi au huduma iwafikie wananchi kwa wakati na watumishi wa TAKUKURU kufika katika maeneo husika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, sehemu pekee inayohitaji kuangaliwa ni kuhusu kucheleweshwa kwa kesi zinapofikishwa kwa *DPP*. Hii imekuwa ni kero, hivyo ingefaa TAKUKURU wapewe mamlaka ya kupeleka kesi Mahakamani. Pia ushahidi wa kimazingira nao uwe na nafasi ya kutumia kwa ajili ya maamuzi na hukumu kwenye kesi za matumizi mabaya ya fedha za umma ushahidi wa kimazingira huonesha fedha zimeibwa ila nyaraka zinapokosekana mtu huonekana hana hatia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ASHA MSHIMBA JECHA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Gharama za Uchaguzi ni muda mfupi tokea kupitishwa mwaka 2010, hivyo ni dhahiri haijazoeleka hasa kwa wananchi. Ni vema kuendelea kuelimisha wananchi juu ya sheria hii ili kuepuka rushwa hasa wakati wa uchaguzi. Pia ni vema kuiangalia sheria kwa baadhi ya vipengele kwani kumekuwa na utata mkubwa katika utekelezaji wake mfano, sheria hii kwa wagombea wa makundi maalum kama wanawake, vijana, walemavu, *NGO's* na vyuo vikuu.

Mheshimiwa Spika, aidha, sheria hii inazungumzia nini kwa wanaotangaza nia ya kugombea, kiongozi ambaye kwa sasa yuko madarakani na hata Taasisi ambayo inawawakilisha baadhi ya wagombea. Ni lini hasa sheria hii itamdhibiti mtu, mgombea, taasisi, kiongozi ambaye yuko madarakani na mwisho wake ni wakati gani?

Mheshimiwa Spika, Sheria hii ya gharama za uchaguzi kwa kiasi fulani nayo imechangia watu wasiende kupiga kura kwa sababu wagombea wengi wakati wa uchaguzi hutoa huduma mbalimbali kuwawezesha kwenda kupiga kura kama usafiri, chakula, posho na kadhalika, jambo ambalo kwa mara hii halikuwezekana. Hivyo, taaluma zaidi inatakiwa kutolewa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kumpongeza Mheshimiwa Stephen Masato Wasira, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu) kwa kuandaa bajeti nzuri sana yenye lengo la kuboresha Wizara yake kwa sekta zote kwa maslahi ya Watanzania. Vile vile nampongeza sana Mheshimiwa Wasira Waziri kwa uwezo wake wa juu katika kutekeleza majukumu yake pamoja na uwezo mkubwa wa kujieleza, ni wazi kwamba, anayafahamu majukumu yake vyema.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia hoja hii napenda kuunga mkono hoja hii mia kwa mia, nawaombea kwa Mwenyezi Mungu wote walioshiriki kuandaa hotuba hii wakiwemo Katibu Mkuu na watendaji wote, kwa kweli bajeti ni nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Tume za Haki za Binadamu. Napongeza kazi nzuri zinazofanywa na Tume hii katika kutoa elimu kwa Watanzania pamoja na kufuatilia kero mbalimbali zenye kuwanyima wananchi haki zao za msingi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kuiongezea Tume hii bajeti ili iweze kufanya kazi hadi Vijijini, Wilayani na Mikoani. Ni matumaini yangu kuwa, Tume hii itasaidia sana wananchi kuelewa haki zao pamoja na kudai haki zao.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie Mfuko wa Mama Salma Kikwete (*WAMA*) Mfuko Wa Wanawake na Maendeleo pamoja na Mfuko wa Mama Anna Mkapa (*EOTF*), Fursa Sawa Kwa Wote. Napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza kwa dhati ya moyo wangu mama yetu mpendwa Mama Salma Kikwete kwa kuanzisha Mfuko wa kusaidia wanawake na watoto wa kike. Mfuko ambao umekuwa ukombozi

sana kwa wanawake kuondokana na utegemezi kwa waume zao pia kuwasaidia wasichana wanaokosa wazazi au walezi na kuwasababishia kushindwa kuendelea na masomo.

Mheshimiwa Spika, vile vile nampongeza Mama Anna Mkapa kwa Mfuko wake ambao naye aliwalenga wanawake hasa wajasiriamali ambao walikuwa tayari kuondokana na umaskini. Nawashangaa wanaowabeza wake wa viongozi wetu ambao waliombwa kwa nia njema kuwa karibu na jamii kwa kuisaidia. Hivi wake wa Marais wetu wakikaa tu bila kazi tutakuwa tumewatendea haki? Sio sahihi, nawaomba wasonge mbele, Taifa hususan sisi wanawake tupo nao mia kwa mia, kelele za mlango zisiwanyime usingizi.

Mheshimiwa Spika, pia nizungumzie haki na wajibu. Napenda kuishauri Serikali kuwa wapo watumishi waliofukuzwa kazi lakini watendaji wamewasaidia kwa kusema uwongo ili warudi kazini na walipwe mishahara yote ambayo hawakuifanyia kazi. Hii sio haki tena ni kuiibia Serikali mfano ninao, naomba Waziri anione nimpe taarifa ya Mwalimu mmoja aliyetoroka miaka mingi amerudishwa kazini na sasa anaandaliwa madai ya mishahara ambayo hakuifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu rushwa. Nampongeza Ndugu yetu Hosea pamoja na timu yake kwa kazi nzuri ingawa bado wanayo kazi kubwa kwani rushwa bado ipo kwenye maeneo ya kazi hasa Mahakama za Mwanzo, hospitali na kadhalika, wananchi wanakosa haki zao za msingi kwa watu kutumia fedha.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kwa njia ya maandishi kumpongeza Mheshimiwa Hawa Ghasia - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri ambayo imeonyesha sura ya kutekeleza majukumu yote yaliyomo ndani ya Wizara hii. Nawaombea Mungu afya njema, maisha marefu na mshikamano ili waweze kutekeleza malengo yao ya barabara.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kutoa mchango wangu, napenda kutamka rasmi kuwa ninaunga mkono bajeti hii asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Serikali pale inapoona mtumishi mstaafu bado anazo nguvu za kufanya kazi, huajiriwa kwa mkataba ili kuondoa upungufu wa watumishi hasa waalimu na madaktari. Hivyo naishauri Serikali kuweka mikataba wazi ili kuondokana na adha ya waajiriwa wa mkataba, kupata tatizo la kukosa mshahara kwa muda mrefu jambo ambalo linaleta fedheha kwa Serikali ukizingatia Waziri Mheshimiwa Hawa Ghasia yuko makini, bali Watendaji wachache wanamwangusha. Mfano, ni walimu waliofanya kazi kwa mkataba wa Singida Mjini kwa kufundisha Sekondari za Kata hadi leo wanadai mishahara ya miezi 16.

Mheshimiwa Spika, lipo pia tatizo la watumishi hewa kwa kada mbalimbali mfano walimu, wauguzi na kadhalika. Hili nalo siyo zuri, ni vyema kumbukumbu zikawekwa vizuri na pale wanapostaafu, basi waondolewe kwenye orodha ya malipo. Ni fedha nyingi sana zinahujumiwa hasa kwenye Halmashauri za Manispaa, Miji, Wilaya na

kadhalika, fedha ambazo zinaweza kufanya kazi nyingine za maendeleo. Naiomba Serikali kufuatilia na kubaini mambo haya.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuweka utaratibu mzuri wa kupandisha watumishi vyeo pale wanapokuwa na sifa. Napenda kuikumbusha Serikali kuwa bado wapo watumishi ambao husahaulika kupandishwa vyeo. Naomba Serikali ihakiki watumishi ambao wamesahaulika, basi wapandishwe vyeo na pia utaratibu wa kulipwa nyongeza za mishahara yao na kurekebishiwa iwe inafanywa mapema, kwani tatizo bado lipo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Serikali kwa kuongeza mishahara ya watumishi karibu kila mwaka wa fedha suala ambalo huwatia moyo wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ongezeko la mishahara la kila mwaka, bado haijakidhi haja kwa watumishi kulingana na hali halisi ya maisha. Naishauri Serikali kuandaa mabadiliko ya mishahara, kushirikisha vyama vya wafanyakazi kutoa hoja zao ili kuondokana na migomo au malumbamo yasiyo na tija kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kuwa wafanyakazi ambao wanafanya kazi vijijini ambako hakuna miundombinu kama barabara, nyumba, zahanati na kadhalika ni walimu, ukizingatia hata wanafunzi wanakuwa wengi kupita kiwango, vitabu vya kiada na ziada hakuna na upungufu mwingine mwingi.

Mheshimiwa Spika, kipindi walimu walipokuwa wanalipwa asilimia 50, zilikuwa zinawatia moyo sana. Naiomba Serikali kusikia kilio cha walimu kuwarudishia asilimia 50 ili waweze kuwa na kipato cha kukabiliana na hali ngumu ya maisha huko vijijini na mijini msongamano wa magari na mwalimu kupanda magari hata matatu kwenda kazini na kurudi kila siku huku akiwa amebeba daftari na vitabu vya kwenda kuandaa masomo ya kesho yake.

Mheshimiwa Spika, bado kuna adha ya watumishi wapya kuchelewa kuingizwa kwenye orodha ya malipo. Hili nalo linavunja moyo wafanyakazi wapya na kusababisha utoro au kuacha kazi. Naiomba Serikali kuwa makini sana ili tusiwapoteze watumishi.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa rai kwa Serikali kuwa makini kutunza vielelezo vya wastaafu pamoja na vielelezo vya wasimamizi wa mirathi. Hii ni kero kubwa sana kwa wastaafu wengi ambao hufariki bila kupata malipo yao. Vile vile wasimamizi wa mirathi hupata taabu sana kufuatilia mirathi pale wanapofariki ndugu zao, mume au mke aliyekuwa mtumishi.

Mheshimiwa Spika, vile vile bado kuna tatizo la vibali vya kuajiri kuchelewa kutolewa na kusababisha Idara mbalimbali kuendelea kuwa na Makaimu. Ninaomba vibali viwe vinatolewa mapema.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumalizia kwa kurudia tena, naunga mkono asilimia mia nikiwa na mategemeo kuwa ushauri wangu utachukuliwa na wafanyakazi watasikia wakati Mheshimiwa Hawa Ghasia Waziri mwenye dhamana akijibu hoja.

Mheshimiwa Spika, mwisho, narudia tena kuunga mkono hoja.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais na Taasisi zake zote zimekaa vizuri kwa maana ya utekelezaji wa majukumu yake. Naipongeza sana Ofisi hii. Aidha, nalipongeza Baraza la maadili ya viongozi kwa kazi nzuri ya kuwabana viongozi kuwaonyesha mali zao, naishauri iende mbali zaidi iwashughulikie viongozi wasio waaminifu kwa kupendekeza kwa Mamlaka husika iwafukuze kazi na kuwapeleka Mahakamani, iwafilisi mali walizopata isivyo halali, ili kupunguza manung'uniko ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, hatua kama hizi zitaimarisha imani ya wananchi kwa Serikali yao na kupunguza dukuduku ya yale yanayotokea Kaskazini mwa Afrika na *Asia Minor*. Chimbuko la matatizo huku ni viongozi wachache kujilimbikizia mali na madaraka na kuwasahau wananchi wakati nchi hizo zina rasilimali nyingi hususan mafuta na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali ilihimiza pia Baraza la Vyama vya Siasa lifanye kazi kama Baraza la Maadili. Baraza la Vyama vya Siasa chini ya Msajili wa Vyama vya Siasa, Ofisi ya Waziri Mkuu bado halijaonesha uwezo wake tangu liundwe 2010. Linatakiwa liwabane viongozi wa siasa wanaochochea vurugu na kuhatarisha amani na utulivu wetu badala ya kazi hiyo kuachiwa Serikali peke yake. Ofisi ya Rais iigize Ofisi ya Waziri Mkuu ilibane Baraza hili lifanye kazi yake na kuangalia upya muundo wake hususan viongozi wanaosimamia chombo hicho.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Sekretarieti ya Ajira kwa kazi nzuri japokuwa ina muda mfupi. Viongozi walioteuliwa ni waadilifu, ni watu waliolitumikia Taifa katika nyadhifa mbalimbali kwa Utumishi uliotukuka. Hawa ni *Corruption Free Zone*. Nashauri kuwe na *extension* ya mchakato wa usaili kwa kiasi fulani yafanywe na Sekretarieti hii kwa Majeshi yetu lakini maadili na kanuni za kijeshi yasimamiwe na wanajeshi wenyewe. Hili litasaidia sana kuepusha manung'uniko mengi dhidi ya ajira majeshini kwamba yanapendelea zaidi watoto au ndugu za wanajeshi wenyewe na kuhatarisha dhana ya Jeshi la Umoja wa Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, asilimia 82 ya malalamiko yaliyowafikia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa mwaka 2009/2010 ni kuhusu ukiukwaji wa misingi ya Utawala Bora. Maana yake ni kwamba watawala katika maeneo fulani hawatendi haki. Nadhani maeneo hayo ni Wilayani na Vijijini ambako watendaji ni wahusika. Serikali ichukue hatua kumaliza matatizo haya.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri kwa kazi nzuri kudumisha Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, maoni yangu, hali ya wafanyakazi ni mbaya na mishahara haitoshi. Nashauri nyongeza ya kila mwaka itasaidia kupunguza makali ya maisha. Walimu wana maisha magumu sana. Naomba kazi yao iwekwe kwenye kundi la *Rare Profession* kama Madaktari na wengine.

Mheshimiwa Spika, hali ya posho ya wanajeshi ni mbaya. Naomba posho zao za kujikimu ziongezwe maradufu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. ENG. CHRISTOPHER CHIZA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Wizara na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote kwa kazi nzuri na Hotuba nzuri. Napenda kuchangia maeneo mawili yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mkataba wa Huduma kwa Mteja. Inaelekea Wizara nyingi pamoja na kuandaa Mikataba ya Huduma kwa Mteja, lakini haitumiki. Hata baadhi ya viongozi wapya wenye nyadhifa za juu hawaitumii. Iko haja kurejea mikataba hiyo na kuifanya sehemu ya utendaji wa Watumishi ili kutoa taswira na picha nzuri ya Serikali kwa watu wanaotumia huduma za Serikali. Karibu kila Wizara ina nafasi au inahusika kuwapa taarifa muhimu wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Ni muhimu watoe majibu ya maswali ya wateja wao katika muda waliojiwekea katika mikataba ya huduma kwa mteja.

Mheshimiwa Spika, nichangie kuhusu Hati Miliki za Kimila. Dhana ya kurasimisha Rasilimali na Biashara za wanyonge Tanzania (MKURABITA) ni nzuri sana, hata hivyo wanyonge wengi (asilimia 80) ni wakulima. Kuna changamoto kubwa zilizojitokeza katika utekelezaji wa MKURABITA:-

(i) Gharama za upimaji wa mashamba ni kubwa zikilinganishwa na uwezo wa wakulima ambao wanatakiwa kuzilipa.

(ii) Bado wakulima wengi hawajawa na mwamko wa kukubali kuchukua *risk* ya kuweka dhamana mashamba yao. Inahitajika elimu ya kutosha katika eneo hili.

(iii) Taasisi za fedha kutokubali hati miliki za kimila na kutoa masharti magumu ya mikopo. Baadhi ya Taasisi za Fedha zinatoa masharti magumu kwa wakulima yakiwemo muda mfupi (kama miaka 3) ya kurejesha mikopo. Kwa mkulima mdogo miaka mitatu ni muda mfupi sana ukizingatia kwamba hali ya hewa huathiri uzalishaji wa mazao mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba, MKURABITA washirikiane na Taasisi za Fedha na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ili mashamba yenye miundombinu ya umwagiliaji yapewe kipaumbele katika upimaji. Mashamba yenye umwagiliaji yana nafasi kubwa ya kupunguza *risk* ya uzalishaji. Naipongeza Benki ya *CRDB* imeanza kuliona jambo hili (kilimo) na sisi tutashirikiana nao ili tuwasaidie wakulima kupata mikopo kwa kutumia Hatimiliki za Kimila za mashamba yao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kima cha chini cha mshahata wa Sh. 135,000/= kwa mwezi bado ni kidogo sana. Natambua jitihada za Serikali za kuongeza mshahara kwa Watumishi wa Umma. Hata hivyo, ongezeko ambalo linatolewa na Serikali ni dogo sana ambalo halikidhi mahitaji. Najua Vyama vya Wafanyakazi kupitia *TUCTA* vilishapendekeza kwamba kima cha chini cha mshahara kiwe Sh. 315,000/= ili angalau watumishi hawa waweze kuishi kwa kiwango kizuri. Ni lini sasa Serikali itakubaliana na mapendekezo hayo?

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Pension* kwa Watumishi wa Umma. Bado kima cha chini cha *Pension* kinacholipwa kwa watumishi ni Sh. 51,000/=, ni kidogo sana, kwa kuzingatia hali halisi ya maisha. Je, Serikali haioni kwamba ni busara kuongeza au kupandisha kiwango hicho angalau kufikia Sh. 100,000/= kwa mwezi?

Mheshimiwa Spika, kiwango hicho ambacho hulipwa kila baada ya miezi sita kinawafanya wastaafu hao wakae kipindi kirefu sana bila kupata malipo yao. Nashauri Serikali iangalie upya kipindi hicho ili kipunguzwe na kuwa miezi mitatu na haya ni maoni pia ya wastaafu.

Mheshimiwa Spika, bado Mashirika ya *Pension* yanalipa viwango tofauti kwa wastaafu wa Serikali jambo ambalo kwa maoni yangu siyo sahihi sana. Napenda kujua suala la kuhuisha viwango hivyo limefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, nichangie kuhusu suala la ucheleweshaji wa vibali vya ajira. Bado kuna ucheleweshaji mkubwa kwa ajira mpya, kwa maombi yanayofanywa na Taasisi mbalimbali za Serikali zikiwemo Halmashauri za Wilaya. Kwa kufanya hivyo, shughuli nyingi huathirika sana. Nashauri Serikali kupitia Wizara hii irekebishe hali hii mara moja ili kazi zisikwame.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*). Naipongeza Serikali kwa kuendelea kutekeleza mipango mbalimbali ya maendeleo kupitia *TASAF*. Pamoja na pongezi hizo bado naishauri Serikali kupitia *TASAF* ihakikishe kwamba miradi iliyoanza kutekelezwa kupitia *TASAF* II inakamilishwa. Nasema hivyo kwa sababu ipo miradi, hasa ya Zahanati, vyumba vya madarasa, miradi ya maji na kadhalika ambayo haijakamilika. Nashauri wakati *TASAF* III inaanza, basi Serikali ihakikishe pesa zinazotengwa kwa kila mradi zinatosheleza.

Mheshimiwa Spika, nashauri pia waratibu wote nchini wa miradi ya *TASAF* kwenye Halmashauri zote nchini wajengewe uwezo ili waweze kuratibu vizuri miradi yote. Aidha, nashauri muda wa utekelezaji miradi ufupishwe kwani miradi mingine huchukua muda mrefu bila sababu za msingi. Nashauri pia pesa za miradi chini ya

*TASAF* zitolewe mapema. Hali halisi ya sasa, bado inaonyesha kwamba mchakato wa miradi ya *TASAF* huchukua muda mrefu sana na wakati mwingine hukatisha tamaa.

Mheshimiwa Spika, nichangie kuhusu Sekretariati ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Kwanza, napenda niipongeze sana Sekretarieti hii kwa kazi nzuri inayopendelea kuifanya. Hata hivyo, bado kuna upungufu kidogo hasa katika ufuatiliaji wa taarifa zinazojazwa kwenye fomu za kutaja mali. Viongozi wengi huandika taarifa za uongo kwa kutotaja mali zao zote walizonazo. Hudanganya kwa njia zisizo halali. Naomba Sekretarieti ifanye kazi zake kwa nguvu zaidi.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mipango ni chombo muhimu sana katika maendeleo ya Taifa lolote lile duniani. Tume ya Mipango ya Tanzania imeanza kufanya kazi vizuri sana, nami naipongeza sana. Hata hivyo, kwa kuwa na Tume ya Mipango ni jambo moja na kuifanya Tume ifanye kazi vizuri ni jambo lingine. Sasa Tume ipo, imeanza vizuri, naomba iwezeshwe kwa kuwa na Watumishi wenye weledi (*professional*) nchini wa kutosha katika fani zote. Nimemsikiliza Waziri Mheshimiwa Wasira akisema Tume ina upungufu wa Watumishi katika baadhi ya maeneo. Naomba tusianze vibaya. Aidha, naishauri Serikali ihakikishe Tume inapewa pesa za kutosha ili iweze kutekeleza kazi zake vizuri. Mwisho na muhimu zaidi, ushauri wa Tume upewe kipaumbele na Serikali, vinginevyo kazi na kuwepo kwa Tume hakutakuwa na maana.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuwapongeza Mawaziri wahusika kwa kutoa Hotuba nzuri na zenye malengo bayana kwa maendeleo yetu na hususan rasilimali watu. Napongeza Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma kwa kazi nzuri inayofanya katika kudhibiti ajira ili kupunguza tatizo la ajira au Watumishi hewa ambapo Serikali imekuwa ikipoteza fedha nyingi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ajira katika Mamlaka za Serikali za Mitaa yafaa zitazamwe upya hasa katika nafasi za chini kuliko kuhusisha Sekretarieti ya Ajira moja kwa moja. Hii inaondoa dhana ya *D by D* na utaratibu huu unaweza kuongeza urasimu na gharama.

Mheshimiwa Spika, ni kweli tunahitaji kuwa na wataalam wetu wa kutosha na hasa katika sekta za kiuchumi, hivyo basi, ni muhimu kufanya utafiti ili kubaini *skills gaps* (*competences*) ili kusudi katika kujenga rasilimali watu, nguvu zaidi za mafunzo zielekezwe huko. Sasa hivi hatuna vipaumbele vya mafunzo kwa wataalam wetu.

**MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, ni Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma sura 398. Napendekeza kwamba siku zijazo Waziri atoe ufafanuzi wa namna viongozi wa

Umma walivyotekeleza au kukiuka maadili yaliyowekwa na changamoto ambazo Tume inakabiliana nazo viwe wazi.

Mheshimiwa Spika, pili, nichangie kuhusu *TASAF* na MKURABITA kama nyenzo za kutekeleza *vision* 2025. Vyombo hivi vielezwe namna gani kwa mwaka husika kazi zao zilikidhi au kushindwa kutekeleza malengo yao ndani ya mpango wa 2025 *vision*. Wabunge waelezwe nini changamoto na mikakati ya kukabiliana nazo ili kuboresha majukumu ya vyombo hivi.

Mheshimiwa Spika, tatu, niongelee Watumishi hewa. Mpaka sasa hayajatolewa maelezo ya ndani kuhusu tatizo la Serikali kuwa na Watumishi hewa kwa maelfu. Hoja zifuatazo ni muhimu:-

(a) Je, nani huwa anachukua fedha hizo?

(b) Kwa nini wale walipaji ngazi za chini (*collection point*) hawajawahi kulalamika kwamba mishahara inalipwa kwa watu wasiomo kwenye *list* ya walioajiriwa?

(c) Je suluhisho la kutenga siku maalum moja tu kushirikiana na Wizara ya Fedha kulipa *Cash* inaweza kuondoa hoja namba (1 na 2) hapo juu?

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, baada ya kuisoma Hotuba hii kwa makini nimeona kuna haja kubwa ya kutoa mapendekezo ili kufanya Hotuba hii kuwa kamili. Naona mambo yafuatayo lazima yazingatiwe:-

(1) Nidhamu ya kazi;

(2) Maslahi ya wafanyakazi; na

(3) Huduma za wafanyakazi

Mheshimiwa Spika, sasa nianze kwanza kuongelee nidhamu ya kazi. Nidhamu ni jambo muhimu sana kulizingatia kwani bila ya nidhamu hakuna ufanisi wa kazi. Nidhamu ndio inayosababisha kutokujali mali ya Taifa na hatimaye kuleta hujuma dhidi ya wananchi wa Taifa hili. Ili kudumisha nidhamu lazima kuwe na *work evaluation report* kwa kila mfanyakazi ili kuweza kujua ni kwa kiwango gani kunakuwepo na ufanisi wa kazi.

Mheshimiwa Spika, pia nizungumzie suala la maslahi ya wafanyakazi. Wafanyakazi wamekabiliwa na hali ngumu ya maisha kwa kutolipwa mshahara wenye kulingana na maisha kwa wakati ule. Kutokuwalipa mshahara wafanyakazi unaolingana na hali ya kiuchumi, kunaleta athari kubwa na hii inaleta kutokuwa na imani na mwajiri wao na hivyo kutokea Ufisadi ndani ya sehemu ya kazi.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Wizara izingatie katika malipo hayo mambo yafuatayo:-

(a) Matumizi ya kawaida (chakula);
(b) Matumizi ya matibabu;
(c) Matumizi ya kodi ya nyumba; na
(d) Matumizi ya usafiri.

Mheshimiwa Spika, kama watumishi watalipwa kwa kuzingatia mahitaji hayo, basi nidhamu na ubora wa kazi utapatikana na hivyo kunyanyua uchumi wetu Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, mwisho nimalizie na suala la huduma za wafanyakazi. Mfanyakazi mara nyingi anakuwa na mahitaji yake ili aweze kufanya kazi nzuri. Kwa mfano, kupata bima ya afya, kupatiwa mikopo nafuu kutatua matatizo yao na kupata usafiri ili kurahisisha ufikaji kazini mapema.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzingatia haya, wafanyakazi wapewe elimu juu ya kazi zao ili kuleta ufanisi wa kazi zao na kwa tija kwa Serikali.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kuwasilisha kwako mchango wangu katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2011/12, kama ilivyowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ninaanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Hawa Abdul-rahman Ghasia, Waziri, kwa uwasilishaji wake mzuri na wenye weledi wa hali ya juu kabisa. Pili, ninampongeza kwa imani, uvumilivu na moyo wa kujitolea sana kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, kama sote tunavyofahamu, Wizara hii ni roho ya ajira zote Serikalini na kwa Taasisi zote za Umma. Hivyo, majukumu yake ni mazito na yanahitaji umakini mkubwa sana katika utekelezaji. Ni kheri tuwaunge mkono na kusaidiana nao katika kuboresha na kuondoa upungufu unaojitokeza kila siku, maana sidhani kuwa ni busara kukosoa tu bila kutoa suluhisho.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hotuba hii kujumuisha mengi, ambayo ninaomba nichangie machache kufuatana na hali halisi ya Jimbo la Kilwa Kaskazini na nchi kwa ujumla. Lipo tatizo kubwa sana katika ajira za Watumishi Sekta ya Elimu, hasa katika upandishaji madaraja, mafunzo kazini na semina. Upandishwaji madaraja kwa walimu unachukua muda mrefu, kiasi kupelekea kukosa hamasa ya kufanya kazi, lakini pia pale wanapopandishwa, huchukua muda mrefu sana mishahara yao kulipwa kufuatana na madaraja yao. Hii inapelekea kuwa na malimbikizo makubwa sana na ucheleweshwaji wa kulipwa malimbikizo husika.

Mafunzo kazini ni kikwazo kikubwa sana maana toka siku anaajiriwa hadi anahamishwa au vinginevyo, anakuwa hajawahi kuhudhuria mafunzo hata ya siku mbili,

ambapo ni kinyume cha Sheria za Kazi lakini pia tunahuisha ujuzi na kuwafanya wasiwe na ujuzi endani na wakati.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine linahusu mfumo uliopo sasa katika ajira zetu, mamlaka yote tumeweka mahala pamoja katika Tume ya Utumishi, lakini yapo maeneo ambayo ni vyema tukaangalia namna bora katika kurekebisha ili watu waajiriwe kufuatana na maeneo yao, hasa ukizingatia hata ajira ndogo ndogo kama madereva, wauguzi na hata watumishi wa maofisi, wengi wao hutoka maeneo husika ilhali wapo watu katika maeneo yetu wanaweza kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa ajira pia mpaka sasa bado unatoa masharti ya , kwa maana unatajwa uzoefu kama ni kigezo wakati wapo vijana ambao wana vigezo na uwezo mkubwa wa kufanya kazi bila uzoefu, kwani walipokuwa masomoni wamekuwa wanafanya *field* na pia wamefaulu masomo yao na kutunukiwa vyeti.

Mheshimiwa Spika, pengo lililopo sasa katika utoaji huduma kutokana na upungufu wa wataalam ni vyema tukaangalia uwezekano wa kubadili sheria zetu ili tuweze kuleta wataalam kutoka katika nchi nyingine kama India, Pakstan na Bangladesh hasa katika Sekta ya Afya na Elimu kwa walimu wa masomo ya Hisabati, Kiingereza na Sayansi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, asirudi nyuma katika jitihada zake za kuhakikisha tatizo la watumishi hewa ambalo linagharimu sana nchi, lakini pia linaharibu taswira nzuri ya utendaji wa Serikali yetu linakwisha.

Ahsante.  Ninaunga mkono hoja.

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mungu kwa kuniwezesha kushika kalamu na kuwasilisha mchango wangu kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa yapo malalamiko ya Wafanyakazi wengi wa Utumishi wa Umma, kunyanyaswa, kunyimwa stahili zao, kupunjwa stahili zao, kupandishwa madaraja bila kuongezewa mishahara na kutopandishwa daraja kwa wakati.  Kwa mfano:  Yapo malalamiko ya Walimu kutoka Mikoa na Wilaya kadhaa ikiwemo Wilaya ya Kilombero; wapo Walimu walioajiriwa mwaka 2004 walipandishwa daraja 2010, lakini hadi leo mishahara haijapanda; wapo Walimu walioanza kazi 2008, TSD wamepata mwaka 2011, wakati walioanza kazi 2009 na 2010 wamepewa TSD kwa wakati.  Hivyo, baadhi ya Maafisa Utumishi wana urasimu.  Pia wapo baadhi ya Walimu walioanza kazi mwaka 2008 hadi sasa hawajapandishwa daraja; ninaomba majibu. ninaomba majibu.

Mheshimiwa Spika, wapo Walimu ambao wanastahili kwenda likizo, lakini hawalipwi stahili zao mfano; anastahili kulipwa elfu hamsini, hupewa elfu ishirini eti kwa huruma ya mlipaji au kama msaada; ninaomba majibu.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuzungumzia utendaji wa TAKUKURU katika eneo la migogoro ya ardhi na rushwa kwa baadhi ya Watumishi wa Umma, kushirikiana na Wawekezaji, kutaka kupora ardhi za Wananchi.

Mheshimiwa Spika, haya matatizo yametokea na kuendelea hadi leo katika Kata mbalimbali na Vijiji Wilayani Kilombero, ambapo baadhi ya Viongozi ambao ni Watumishi wa Umma ngazi ya Wilaya, Kata na Vijiji, wakishirikiana na watu wasio waaminifu kutaka kupora ardhi na kumpa Mwekezaji wa Kilimo cha Miwa bila kushirikisha Wananchi . Hivyo, dhana ya Utawala Bora haipo na wanaojitokeza kutetea na kuhoji uporaji huo, hadi leo wamefunguliwa kesi na kuandikiwa barua za kusimamishwa uongozi. Mfano; Mwenyekiti wa Kijiji cha Namwawala, aliandikiwa barua na Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, kuondolewa madarakani na kumfungulia kesi ingawa waliomchagua hawako radhi kumpoteza Kiongozi wao waliyemchagua. Pamoja na uwakilishi wa Wananchi hao kufuatilia kwa Mkuu wa Mkoa, kwa Waziri Mkuu na Ofisi ya Rais, lakini hadi leo migogoro hiyo haijatatuliwa na Wananchi wanazidi kuhangaika na hawajui hatima ya ardhi yao na kushindwa kufanya shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ninahitaji Mheshimiwa Waziri afafanue kuhusu stahili za Walimu walioajiriwa Januari 2011, ambao walipata Waraka toka Ofisi ya Utumishi kuhusu stahili watakazolipwa kwa mizigo kuwa ni tani tano na baadaye ofisi yako ilipeleka kwa Wakurugenzi Waraka mwingine baada ya miezi mitatu kuwa Walimu wanastahili kulipwa mizigo tani moja; na pia hadi leo hawajalipwa gharama za wategemezi. Bado wanazungushwa; hivyo, Walimu baada ya kufundisha darasani huishia barabarani kufuatilia stahili zao; hili ni tatizo na litasababisha ufaulu mdogo wa Kidato cha Nne.

Mheshimiwa Spika, maadili yameporomoka katika Utumishi wa Umma, kutokana na ukosefu wa ufuatiliaji, maslahi kwa watumishi, vitendea kazi, kukaa muda mrefu kwenye kituo kimoja cha kazi, kutopandishwa madaraja na mishahara kwa wakati, pia muda uliowekwa kwa wataalam kuthibitishwa kuwa Mkurugenzi/Mkuu wa Idara kwa miaka saba ni mrefu mno; hivyo, urekebishwe hadi miaka miwili. Ahsante.

**MHE. ABIA M. NYABAKARI**: Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ni chombo chenye jukumu la kujenga imani ya Wananchi kuhusu uadilifu wa Viongozi wa Umma. Jicho kubwa lipo kwa wanaojihangaikia siyo kwa wanaoihujumu nchi hii.

Mheshimiwa Spika, Serikali isiendelee kuwaamsha waliolala, ipo siku tunaweza kuchomwa moto kwa uongozi huu unaojifanya hausikii shida za watu, ni pale wanapojua mbinu za ulaji wa hawa Viongozi wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, mwanzo wa mvua ni mawingu na mawingu hayo tayari yameshaanza kutanda, msifikiri Wananchi wetu hawaelewi kinachoendelea, unaweza kunya umeinamisha uso ukadhani hawakuoni kumbe waliosimama wanakuona, mimi ninadhani Serikali ijisahihishe.

Mheshimiwa Spika, bandari zetu zilitakiwa ziwe zimetuletea maendeleo makubwa kuliko kitu chochote. Rais Kagame wa Rwanda alisema, kama Mungu angempa Bandari Dar es Salaam, Rwanda ingekuwa ya mfano. Kwa nini tusiwe nchi ya mfano? Mna gamba gani Wananchi wasilolijua? Kwa nini Viongozi wanajiona kama wako salama? Siyo kweli, tendeni Haki.

Mheshimiwa Spika, pamoja na yote hayo, watu wamepiga kelele kuhusu ajira zitolewe na Halmashauri, cha ajabu mtakaa kimya! Watu wanayo dhiki hata kupata nauli ya kuwaleta Dar es Salaam kufuatila maswala ya ajira hawana, watu wamekosa haki zao za msingi katika nchi yao. Huu ni utandawazi wa hatari!

Mheshimiwa Spika, wenye haki wamenyimwa haki waovu wanazidi kunawiri, hii ni nchi ya ajabu! Halafu usemi unafuata kuwa ni nchi ya amani na utulivu; tendeni haki, imani kwa matendo, watu wamepoteza imani kwa Serikali yao hasa Wizara zinazosimamia fedha za maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS**: Mheshimiwa Spika, kwanza, ninampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kazi nzuri anayofanya katika Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, utendaji mzuri wa Serikali unategemea kwa kiwango kikubwa, umakini wa Wizara hii katika kupanga na kutekeleza majukumu yake ya kila siku. Inavyoonekana, hivi sasa sheria nyingi za utumishi pamoja na kwamba zipo, lakini hazitekelezwi ipasavyo kwa mfano: Mahudhurio kazini, uwajibikaji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, TAKUKURU inaonekana katika mtazamo wa wengi kuwa haina meno katika kuwashughulikia wala rushwa wakubwa. Huu ni udhaifu mkubwa. Kwa kuwa taarifa za ndani na nje zinaripoti kuwa, wahisani wamepunguza michango yao kutoka shilingi trilioni moja hadi bilioni 430 kutokana na Tanzania kukithiri kwa rushwa kubwa kubwa; ninaomba Serikali iwatake TAKUKURU wafanye kazi zao bila kujali cheo au itikadi ya mtu.

Mheshimiwa Spika, *TASAF* ni Mfuko unaolenga kuwasaidia Watanzania wanyonge kupitia Miradi midogo midogo. Moja ya upungufu wa Mfuko wa *TASAF* ni jinsi Serikali ilivyopanga matumizi ya fedha za *TASAF*. Ikiwa 75% ya pesa za Mradi wa *TASAF* ni kwa ajili ya wafanyakazi *(labour)* na asilimia 25 tu ndiyo kwa ajili ya vifaa, basi haiwezekani kuwa na Mradi wa maana hasa ikiwa ceiling ya Mradi ni milioni arobaini tu. Ninaomba kama hivyo ndivyo, basi mgao huu uachiwe upangwe na Wadau husika. Vinginevyo, hatutakuwa na Miradi endelevu na yenye maana.

Mheshimiwa Spika, ajira limekuwa tatizo kubwa hapa nchini. Vijana wanaomaliza Shule za Sekondari au Vyuo Vikuu, wanahangaika kutafuta ajira lakini hawapati. Ninapendekeza Serikali ijenge viwanda vingi vikiwemo vile vya kusindika mazao ya kilimo. Pia ni muhimu elimu yetu ilenge kuwa na vijana wengi wanaoweza kujitegemea baada ya kumaliza masomo yao.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Mifuko ya Rais ya Kujitegemea itolewe kwa haki na usawa. Baadhi waliopewa pesa hizo, hawana sifa zinazokubalika na ndiyo maana hawakuweza kurudisha pesa hizo baada ya kukopeshwa.

**MHE. ALIKO N. KIBONA**: Mheshimiwa Spika, malalamiko ni mengi sana kuhusiana na uamuzi wa Serikali kufanya ajira zote za Serikali mahali pamoja, yaani Tume ya Utumishi. Ninashauri kuwa, ajira zote ziwe *decentralized.*

Mheshimiwa Spika, Maafisa Elimu wote wa Mikoa siyo Wakuu wa Idara; hata hivyo, Maafisa Elimu wote wa Wilaya ni Wakuu wa Idara na wana madaraka na wanawazidi Wakuu wao wa Elimu Mkoa kwa ziadi ya Sh. 800,000; huu siyo Utawala Bora.

Ninashauri marekebisho yafanyike na hii itakuwa sehemu ya kupandisha morali ya kazi.

Mheshimiwa Spika, wakati wa uhamisho wa Watumishi walio katika ndoa ni vizuri wote wapate uhamisho kwa mara moja, kwa sababu akihamishwa mmoja ina maana wameachana na kila mmoja anakwenda kwenye kituo kipya cha kazi, huku akisononeka na kuwa *frustrated* kwa sababu ya kuachana na familia yake.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo kubwa la Ugonjwa wa UKIMWI. Tatizo hili kwa takwimu zilizopo ni pamoja na kutoka Idara ya Elimu na hasa Walimu. Zipo taarifa kwamba, baadhi ya wanandoa wanashindwa kuungana kwa sababu maelezo yanayotolewa ni kwamba ili mtumishi ahame kumfuata mume au mke kutoka mathalani Kigoma kwenda Rukwa au Rukwa kwenda Mbeya, kwa ajili ya kuungana na mwezi wake ni lazima apate mtu wa kubadilishana naye.

Ninashauri kwamba, ni vizuri sana tuepushe vifo vya Walimu kwa kuwaruhusu waungane katika ndoa zao. Huo utakuwa Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, tatizo lililopo katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ni tofauti: Yapo katika mfumo wake wa ulipaji wa mafao; Watumishi wenye elimu sawa, kwa mfano, daktari aliyekuwa akifanya kazi Serikalini, anapostaafu analipwa na Mfuko wa *PSPF* kati ya shilingi milioni 60 kama mkupuo kabla ya pension. Daktari aliyekuwa anachangia *NSSF*, anapostaafu anapata mkupuo kati ya shilngi milioni mbili mpaka tatu au nne.

Ninashauri kuwa, *Commission* ya Kusimamia na Kuendesha Mifuko ya Jamii ianze sasa.

**MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI**: Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchukua fursa hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa Hotuba nzuri, pamoja na maoni na mapendekezo yangu kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba, Ofisi hii ni kiungo kikuu katika ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Watumishi wa Umma. Kwa kweli ni vyema, Ofisi ya Rais, ikaangalia kwa kina maslahi ya Watumishi wa Umma. Maslahi ya sasa ni madogo sana na yanawavunja moyo watumishi. Fedha inayotolewa haitoshi hata kumgharimia mtumishi ambaye hana familia. Hivyo; ni vyema, maslahi yapangwe kulingana uhalisia. Aidha, ninapenda pia kutoa kilio kwa niaba ya Walimu kuhusiana na malimbikizo yao ya madeni yanayokadiriwa kufikia shilingi bilioni 13. Imani yangu ni kwamba, madeni haya yatalipwa kwa wakati, kwani yamekuwa ya muda mrefu mno na ni stahili na haki ya msingi ya walimu hawa ambayo wameitolea jasho.

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kugusia Waraka wa Utumishi wa Walimu wanaokwenda kujiendeleza na ngazi ya ajira ambayo watarudi kuifanyia kazi. Waraka huu ni wa unyonyaji na unawaumiza walimu. Ninashauri Waraka huu upitiwe upya na endapo itafaa basi ni vyema marekebisho yakafanyika.

Suala lingile ni uandaaji wa Nyaraka za Utumishi Serikalini. Ni muhimu sana, watumishi wakawakilishwa ili kuridhia yaliyomo katika nyaraka hizo.

Baada ya kusema hayo, ninaomba kuchukua fursa hii, kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**MHE. LUCY F. MAYENGA**: Mheshimiwa Spika, ninampongeza kwa dhati, Mheshimiwa Waziri wa Utawala Bora, kwa Hotuba nzuri na kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akiifanya katika kujenga Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ushauri ninaotaka kuutoa leo ni kuhusu Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Nchini (TAKUKURU). Taasisi hii imekuwa ikifanya kazi nzuri katika kuzuia na kupambana na tatizo ambalo limekuwa ni sugu la rushwa hapa nchini. Ushauri wangu ni kuwa, Jamii ya Watanzania ielezwe nini kazi ya TAKUKURU, kwani katika jamii yetu ikiwemo Wananchi na Viongozi hata Wabunge, wameonesha kutofahamu vizuri majukumu ya Taasisi hii. Mfano; Taasisi hii haiwezi kufanya kazi ya kudhibiti bei ya bidhaa. Kadhalika, TAKUKURU katika kufanya kazi yake, ninaomba iwe makini kushughulikia matukio ya rushwa wakati maalumu. Mfano; Taasisi hii inakabiliwa na matatizo ya kutokuwa na idadi ya kutosha ya Wafanyakazi hasa pale inapotaka kufanya kazi katika matukio makubwa kama nyakati za uchaguzi. Hata hivyo, TAKUKURU iwe angalifu sana kwa aina ya watu inaowatumia katika matukio hayo. Iepuke sana kutumia vijana ambao wanatoka moja kwa moja vyuoni, kwani wamekuwa

na tabia ambayo imekuwa inaleta malalamiko kwa watuhumiwa na hata kuleta chuki. Mfano, wamekuwa na tabia ya kutumia nguvu kubwa, kauli zisizo na heshima na ubabe. Ninaona hii inatokana na vijana, tabia za ujana zinajulikana huwa wanakuwa na jazba na utendaji wa lengo la kuonekana na kupata sifa au hata kuogopwa. Matokeo baada ya hapo huwa ni chuki kwa Taasisi hiyo.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**MHE. JOHN J. MNYIKA**: Mheshimiwa Spika, ninaomba maelezo ni kwa nini nakala ya randama hazijatolewa kwa Wabunge wote baada ya kuwasilishwa Mezani kama Kanuni ya 99(4) inavyohitaji.

Mheshimiwa Spika, ninaomba maelezo ni kwa nini Ikulu imetengewa kiasi kikubwa cha posho, takriban bilioni moja kwenye Fungu 20, Kifungu 1001, Kasma 210300 na Kasma 210500.

Mheshimiwa Spika, ninaomba maelezo ni kwa nini kiwango cha posho kwenye Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma - Fungu 33, ambapo zimepanda kwa zaidi ya asilimia mia moja; mfano: *Personal allowances* - Kasma 210300, 210300 na 21030 kwa vifungu 1003, 1004 na 1006.

Mheshimiwa Spika, Mawaziri watoe maelezo ni kwa nini hotuba zako zimekwenda kinyume na maelekezo ya *instrument* iliyotolewa na Rais tarehe 17 Desemba, 2010 iliyochapwa kwenye *Supplement Number 49.* Hii ni kwa sababu Hotuba ya Waziri, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu, imejikita katika mpango pekee wakati ambapo majukumu yake yamejikita katika siasa, masuala ya dini, mashirika yasiyo ya kiserikali na kadhalika. Wakati huo huo, Hotuba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, imezungumzia masuala ya MKURABITA, *TASAF* na kadhalika, ambayo yalipangwa kuwa kwenye Mahusiano na Uratibu.

Mheshimiwa Spika ninaomba maelezo ya kina ikiwemo kupatiwa mchanganuo/mnyumbulisho wa Kasma 229900 iliyopo kwenye Kifungu cha 1001. Ninataka ufafanuzi hususan kuhusu kasma ndogo 229915 ya gharama za kitaifa. Kifungu hiki kimekuwa kikitumika kuruhusu mianya ya anasa na ubadhirifu. Kiwango cha fedha cha kasma ndiyo hiki cha takriban shilingi bilioni 135; ni kikubwa sana. Waziri asipotoa maelezo kuhusu kifungu hiki wakati wa Kamati ya Matumizi, itabidi nishike shilingi. Aidha, ninaomba Waziri afanye utaratibu wa kupunguza fedha katika kasma ndogo hiyo na kuongezea kwenye bajeti ya maendeleo kwa fungu hilo hilo la 30, kifungu cha 1003, kasma ya 4921 ili kuongeza kiasi cha fedha katika bajeti ya MKURABITA.

Serikali izingatie kuwa, kwenye Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Serikali ilitenga shlingi bilioni sita kwa ajili ya MKURABITA, lakini mwaka huu wa fedha zimetengwa shilingi bilioni tatu pekee. Ukurasa wa 61 wa Hotuba ya Waziri wa Nchi, Utumishi, umetaja urasimishaji umepangwa kwa eneo la Kimara Baruti kwa upande wa Jimbo la Ubungo. Kiwango cha fedha kikiongezwa vitaanza kufanywa kwa eneo kubwa zaidi la Kata ya Kimara na Saranga. Aidha, Serikali itoe kauli kuhusu barua ambayo Ofisi ya

Rais inayo nakala yake ya tarehe 4 Machi, 2011 toka *Twiga Chemical Industries* inayotaka kupora eneo la ekari nane la Wananchi wa Kimara Baruti. Pia, ishughulikie ufisadi uliofanywa wa kuilipa Kampuni hiyo shilingi bilioni tatu, kinyume na maagizo ya Kamati ya Deni la Taifa. Aidha, isitishe malipo ya shilingi bilioni 4.5 zingine ambazo zinakusudiwa kulipwa kama fidia kwa kampuni hiyo.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE**: Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchukua nafasi hii, kuwapongeza Mawaziri; Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu); Mheshimiwa Hawa Abdul-rahman Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma); pamoja na Mheshimiwa Mathias Meinard Chikawe, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utawala Bora); kwa juhudi zao za kuwasilisha Hotuba nzuri Bungeni. Pia ninawapongeza kwa kulitumikia Taifa letu kwa juhudi na maarifa.

Katika kuijadili hoja hii, nitajikita katika vipengele vifuatavyo: Tume ya Mipango; ajira kwa Watumishi wa Umma hususan vijana; rushwa na suala la TAKUKURU; suala la udini katika nchi yetu; kutokuwajibika kwa wafanyakazi na suala la mishahara hewa; mgawanyo wa rasilimali za taifa letu; uhamisho wa watumishi; na suala la maadili kwa Viongozi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, lengo zuri la Tume ya Mipango ni katika kuhakikisha kuwa, inatatua vipaumbele vitano vya Taifa letu katika miaka mitano ijayo. Ninasema kuwa, inatatua vipaumbele kwani vipaumbele vilivyooneshwa na kubainishwa ni vikwazo na changamoto za maendeleo katika nchi yetu. Vipaumbele hivyo ni miundombinu, kilimo, viwanda, maji na rasilimali watu; ni ukweli usiopingika kuwa Tume ya Mipango kama kweli itatekeleza yote yaliyoainishwa katika Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu), nchi yetu itaendelea kwa kasi ya ajabu.

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa ya Tume hii ya Mipango ihakikishe kuwa, inasimamia rasilimali za taifa letu kwa umakini wa hali ya juu ili kuleta maendeleo katika nchi yetu. Tume inatakiwa kutoa miongozo mbalimbali juu ya mwelekeo wa uchumi wa Taifa letu. Tume isimamie maendeleo ya watu wa vijijini kwa umakini ili kuondoa ama kupunguza tatizo la umaskini unaowakabili mamilioni ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, tumeona dhahiri kuwa, Tume ya Mipango inayo kazi nyingi pamoja na majukumu mengi ya msingi ambayo yamelenga kuikomboa nchi yetu katika fani za maendeleo ya kiuchumi, kijamii, kisiasa na hata kiutamaduni. Tatizo kubwa ninaloliona hapa ni kuwa, Tume inaweza ifikie malengo yake kwani fedha za bajeti zilizotengwa katika Wizara hii ni ndogo sana. Hali hii itasabaisha utekelezaji wa majukumu ya Tume ishindwe kufikia malengo. Jambo hili litakuwa ni aibu kwa Taifa na hii itadhihirika wazi kuwa, sisi Watanzania ni mabingwa wa kupanga mipango, lakini utekelezaji wake ni *zero*. Hii inaashiria wazi kuwa, sisi Watanzania tumeegemea kwenye nadharia za kufikirika, lakini tunaogopa sana vitendo. Binafsi, ninaungana na Waheshimiwa Wabunge, walioliona tatizo hili la ufinyu wa fedha za Tume ya Mipango kuwa, hazitoshi ili Serikali ione namna itakavyoiongezea fedha Tume hii ya Mipango.

Ushauri kwa Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana katika Tume ya Mipango pamoja na Watumishi/Wafanyakazi ni kuwa, wafanye tafiti za kutoka katika Mikoa yote ya Tanzania na kuhakikisha kuwa, tafiti hizo zinawafikia raia wote wa mijini na vijijini kuhusu mpango wa maendeleo kwa eneo husika. Tafiti hizo zichapishwe kwa Lugha ya Kiswahili ili kuwawezesha raia wengi kuzisoma. Tafiti hizo zielekezwe vijijini zaidi na si mijini.

Ninasisitiza Tume ya Mipango ifanye tafiti katika Wilaya ya Tarime ili iweze kusaidia kutatua matatizo ya umaskini wa kipato kwa Wananchi wa Tarime. Tume itatue tatizo la miundombinu, kilimo, ajira, viwanda, maji, nishati ya umeme, pamoja na tatizo la miundombinu, kilimo, ajira, viwanda, maji, nishati ya umeme pamoja na tatizo la uporaji wa rasilimali ya dhahabu katika Wilaya ya Tarime. Msisitizo uwekwe kwenye kutatua matatizo kwa kutoa mapendekezo yakinifu yanayotekelezeka. Tatifi hizo zisiwekwe kwenye makabati kama ilivyozoeleka katika nchi yetu kuwa tafiti nyingi huliwa na mchwa badala ya kuzifanyia kazi. Tufikiri zaidi.

Mheshimiwa Spika, ninapendekeza kwa dhati kuwa, Vijana wa Tanzania waajiriwe katika Taasisi na Mashirika mengine ya Umma mara tu wanapohitimu kiwango fulani cha elimu. Uzoefu unaonesha kuwa, watumishi wengi katika Taasisi nyeti na Masharika mengi ya Umma ni wazee waliokaribia kustaafu au wamestaafu sasa wanafanya kazi kwa mikataba. Hali hii inasababisha Vijana wengi wa Kitanzania waliosoma na kupata elimu nzuri, kukosa ajira kwa kisingizio cha kukosa uzoefu. Kijana akienda kuomba ajira, anaambiwa uzoefu wa miaka mitano hadi kumi; huu ni unafiki uzoefu atapata wapi kijana aliyeanza shule ya msingi, sekondari, vyuo na hata kupata shahada. Aajiriwe ndipo apate uzoefu. Tatizo hili kwa kiasi fulani linasababishwa na ubinafsi, tamaa, fikra finyu na hata usaliti kwa Viongozi wa Umma, ambao wana uchu wa madaraka. Viongozi hawa hawataki mabadiliko hata kidogo; matokeo ya uchu wa kung'ang'ania katika vyeo husababisha ufanisi wa kazi kuwa dhaifu.

Ninashauri Wizara ifanye utafiti ili kubaini ni Watumishi wangapi wa Umma wamestaafu na bado wanaendelea kufanya kazi kwa mikataba. Pia iangalie namna ya kuwaingiza vijana katika nyadhifa mbalimbali ili wapate uzoefu. Tutafakari zaidi!

Mheshimiwa Spika, suala la rushwa katika nchi yetu bado ni tatizo na kikwazo cha maendeleo katika nchi hii. Rushwa husababisha kukosekana kwa haki katika nchi hii. Pamoja na pongezi nyingi wanazopewa TAKUKURU; binafsi sikubaliani na ushabiki wa pongezi hizo! Sababu iko wazi kuwa, rushwa kubwa kubwa bado hazijatafutiwa ufumbuzi, suala la mikataba mibovu kama vile ununuzi wa rada, suala la Kagoda, suala la Meremeta, Suala la *IPTL*, suala la Richmond hatimaye *DOWANS*, suala la mikataba ya madini na mengineyo mengi, bado hudhihirisha wazi kuwa, TAKUKURU haina meno ila ni mchezo wa kuigiza.

Kama hiyo haitoshi, ninauliza Taasisi hii vipi suala la asilimia kumi katika Halmashauri zetu, Taasisi zetu za Umma na hata katika tenda (zabuni) katika Masharika ya Umma? Vipi suala la *traffic* na polisi? Suala la rushwa katika nchi yetu ni kubwa na mtu maskini ndiye anayedhalilishwa, anayenyonywa, anayeonewa, anayenyanyaswa,

anayepuuzwa na anayesalitiwa! Jambo la muhimu la kuzingatia hapa ni kwamba, mzigo wowote mzito unaomwelemea Mwananchi maskini kama vile uporaji wa rasilimali za nchi yetu, hutokana na rushwa toka kwa Viongozi na Watumishi wabinafsi na wenye tamaa ya kujilimbikizia mali. Rushwa inayotolewa au inayopokelewa iwe ndogo au kubwa, ifahamike wazi kuwa mwisho wa yote anayeumia ni mtu maskini wa Tanzania.

Hii niaibu sana kwa Viongozi wetu tena Waheshimiwa Wabunge kutoa sifa kwa TAKUKURU bila kutafakari ukweli wa mambo. Kiza kinene bado kimetanda, hatuoni tuelekeako! Macho yamepofuka, hatuoni giza! Ninaishauri Serikali ihakikishe kuwa, rushwa inapigwa vita kwa hali na mali na sheria kali itungwe juu ya wala rushwa hata ikibidi wanyongwe hadharani. TAKUKURU ifahamu wajibu wake na katu isipokee sifa ambazo ni za kinafiki. Fikra zaidi zahitajika kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Spika, suala la udini katika nchi yetu limekua kwa kiasi kikubwa. Suala hili si la kupuuza hata kidogo. Kwanza, dini nyingi hapa nchini katika kipindi hiki, badala ya kuhubiri neno la Mungu la kuwaokoa kondoo wa Mungu ili wajiwekee hazina mbinguni, dini hizi zinatumika kuwanyonya, kuwadhulumu, kuwabagua na kuwasaliti Wananchi wa Tanzania. Dini hizi zinahubiri mahubiri yenye uchochezi, chuki, fitina, ubaguzi, utengano na hata wizi. Siasa zimeingia misikitini na makanisani. Viongozi wa Vyama vya Siasa wanajivunia udini na Viongozi wa dini nao wanajivunia siasa kwa waumini wao! Hali hii imesababisha matabaka yaliyogawanyika wazi. Waislamu na Wakristo wameamua kufuata kauli za Viongozi wao wa Kisiasa wanaotokana na madhehebu/misikiti yao. Hali hii wakati inaendelea, Serikali yetu inayaona haya. Ingawa Viongozi wetu wanajaribu kukemea, lakini hakuna hatua madhubuti zinazochukuliwa; inasikitisha!

Ni vyema ieleweke wazi kuwa, Baba wa Taifa letu, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alijenga misingi imara isiyo na udini katika Taifa letu. Alipiga vita kwa nguvu zote suala hili la udini kwa nia njema ya kujenga amani, umoja na mshikamano katika nchi yetu. Ninawashauri Viongozi wetu waige mfano wake. Wachukue hatua kali za kueneza suala la udini katika nchi yetu. Wasimwonee haya mtu yeyote; awe kiongozi wa dini au kiongozi wa siasa anayeeneza itikadi za dini katika nchi yetu.

Ninapenda kuishauri Serikali kuwa, izingatie haya kuwa imani za dini ni hatari na mbaya sana kuliko imani za kisiasa. Hivyo; ni bora semina za mara kwa mara zifanyike ili kuwaunganisha Viongozi wa Dini (Ukristo Vs Uislamu). Pia hata ikiwezekana Serikali ichukue hatua za makusudi za kudhibiti mahubiri yanayotolewa misikitini na makanisani. Itawezekana kama tutaamua na Serikali iwajibike kupitia vyombo vyake vya usalama, kuhakikisha kuwa, inasimamia kuzuia suala la udini kuenea katika nchi yetu. Ninaamimi Mungu ni mmoja ila mashetani ndiyo wengi! Tuzidi kutafakari zaidi!

Mheshimiwa Spika, suala la mishahara hewa linatokana na uzembe pamoja na suala la kutokuwajibika ipasavyo kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, ifahamike wazi kuwa, Viongozi/Watumishi wa Serikali, hawawajibiki ipasavyo. Muda mwingi Watumishi wanautumia kupiga

soga/mazungumzo, kufanya siasa, kusikiliza redio, kuangalia televisheni na hata wakati fulani kuanzisha vikao vya semina ambazo hazina kichwa wala miguu. Hali hii husabisha Watumishi wetu kutowajibika na kufanya kazi kwa bidii. Kinachosikitisha zaidi ni Watumishi wa Serikali kutokuwa wazalendo hususan wanapofanya kazi katika Taasisi au Mashirika ya Umma. Watumishi hao hao wakiwa katika kazi za umma, hufanya kazi kizembe lakini wakiwa katika shughuli zao binafsi au katika Sekta zisizo za Serikali, huwajibika na kuonesha ujuzi wa hali ya juu sana. Huu ni unafiki; tubadilike.

Mheshimiwa Spika, haingii akilini kwa Serikali makini kama ya Tanzania, Idara na Taasisi za Serikali, zinalipa mishahara hewa. Huu ni utani. Ninashauri hatua kali zichukuliwe dhidi ya wahusika wote wanaohusika katika kashfa hii. Huu ni uhaini, usaliti na ubinafishaji usioweza kuvumiliwa katika nchi yetu. Waziri anayehusika, hana budi kuchukua hatua kali kwa wale wote waliohusika kuiba mamilioni ya Watu wa Tanzania. Huu ni wizi wa kodi za walalahoi wa Tanzania. Kulipa mishahara hewa ni sawa na kuteka nyara za Serikali; hivyo ni uhaini.

Mheshimiwa Spika, ninaomba suala la ugawaji wa rasilimali za Taifa liangaliwe kwa makini. Keki ya Taifa letu isipogawanywa kwa usawa na haki, ni ukweli uliodhahiri kuwa, kutatokea ulalamishi, manung'uniko na hata uhasama. Kuna baadhi ya Mikoa katika nchi hii imeendelea sana. Mikoa hii imeendelea si kwa sababu ya upendeleo ambao unatokana na ubinafsi na roho mbaya ya baadhi ya watumishi wetu katika Taasisi za Umma. Uroho, tamaa na ubinafsi, umepelekea baadhi ya watumishi wetu kuangalia zaidi maeneo wanayotoka na kusahau maeneo mengine.

Ninawashauri watumishi wetu waipende nchi yetu kwa dhati bila kuweka mbele maslahi binafsi. Hali hii itasaidia sana Wilaya kama Tarime ikumbukwe na kuletewa maendeleo yanayotokana na keki ya Taifa hili. Tarime nayo ni sehemu ya Tanzania; hivyo, ninaiomba Serikali ifanye kila linalowezekana ili kuisaidia ipate maendeleo. Tarime, Tarime, daima nitakupigania! Tanzania! Tanzania! Daima nitakulilia!

Uhamisho wa Watumishi katika nchi yetu hauko makini. Kwanza, watumishi wengi wamejaa mijini, hawataki kukaa vijijini au mawilayani. Watumishi wengi wanahama toka Wilayani na kukimbilia Makao Makuu ya Mikoa au Dar es Salaam. Hali hii imesababisha hata ajira itolewe kwa rushwa. Vijana wengi wanatoa rushwa ili wasiajiriwe vijijini/wilayani. Vimemo vingi vinatumwa kwa mabosi ili kuwalinda watoto wa vigogo wapate ajira mijini au wapate uhamisho toka vijijini na kwenda mijini. Hili litawezekana tukiamua kwa moyo wa dhati kulirekebisha.

Jambo lingine ni juu ya Watumishi wanaotenda makosa katika Taasisi, Idara, Mashirika na hata Halmashauri zetu, wanapewa uhamisho haraka haraka bila kuwahukumu kutokana na makosa yao. Binafsi, ninaishauri Serikali iangalie utaratibu huu wa kiuwendawazimu kwani ni utani kwa Wananchi wetu. Mtumishi akifanya kosa katika Taasisi husika awajibishwe. Mtumishi yeyote akifanya kosa katika shirika husika awajibishwe. Mtumishi yeyote akifanya kosa katika Halmashauri husika awajibishwe. Hali hii itasaidia kutoa hukumu na kuondoa manung'uniko kwa Wananchi na hata

Watumishi wengine wa ngazi ya chini. Mtumishi akifanya kosa, apate haki yake kabla hajahamishiwa sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, Viongozi au Watumishi wa Umma kwa kiasi kikubwa siyo waadilifu; hawana maadili. Hali hii inatokana na ukweli kuwa, Watumishi wengi hawana uzalendo katika nchi hii. Kutokana na kukosekana kwa maadili ya Viongozi wa Umma ndiyo maana hata nyaraka nyeti za Serikali zinavuja na kupewa watu wasioitakia mema nchi hii. Hili suala ni la hatari sana katika nchi yetu. Nyaraka toka Baraza la Mawaziri zinavuja; Nyaraka za Wizara zinavuja; Nyaraka za Taasisi zinavuja; na Nyaraka za Mashirika zinavuja! Matokeo ya kukosekana kwa maadili kwa Viongozi wa Umma, husababisha kukosekana kwa uadilifu kwa Viongozi wa Umma.

Viongozi hawa wanakosa maadili ndiyo maana wanakula rushwa. Viongozi hawa wanakosa maadili ndio maana wanalipa mishahara hewa. Viongozi hawa wanakosa maadili ndiyo maana hawana uzalendo. Viongozi hawa wanakosa maadili ndiyo maana siyo wakweli. Viongozi hawa wanakosa maadili ndiyo maana ni wabinafsi.

Ninashauri kianzishwe Chuo Kikuu cha Watumishi wa Umma ili Viongozi wa Wananchi wapate kufundishwa maadili.

Mheshimiwa Spika, niliyoyatoa yafanyiwe kazi. Ninaunga mkono hoja.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba na mimi nichangie kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Lipo tatizo juu ya utendaji bora kwa Watumishi wa Umma. Watumishi wengi wamejijengea tabia ya kuweka mahusiano na Viongozi ili wanapofanya maovu wasiweze kuchukuliwa hatua za kinidhamu. Watumishi wa namna hiyo ni wepesi wa kutoa zawadi (mbuzi, ng’ombe, gari, zana za kilimo na michango mikubwa ya harusi pale inapoonekana kiongozi huyo ana sherehe za harusi). Mfano, baadhi ya Watendaji Kata kwa Mkurugenzi, Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa, Wakurugenzi, kutoa misaada mbalimbali kwa Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa na kadhalika. Matokeo yake, unatengenezwa mfumo wa kulindana. Inapofikia hatua hiyo, maovu mengi hufanywa na wahusika, lakini mamlaka husika haziwezi kuchukua hatua. Wafanyabiashara wakubwa, halikadhalika, nao wamekuwa na mtindo huo huo kwa Viongozi wetu Wakuu. Nini kifanyike? Inafahamika pafanyike uchunguzi na Tume Maalum kupitia Wananchi, taarifa za Watumishi wasiofaa hata Watumishi wanawafahamu kama ambavyo imezungumzwa na wachangiaji wengine, Watumishi wa namna hiyo huhamishwa pale inapoonekana wamefanya hujuma.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali iikomeshe tabia hii ambayo haina tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, mifumo mbalimbali imewekwa kwa ajili ya kudumisha Utawala Bora na Utawala Bora ni ule unaoishirikisha jamii na unaozingatia misingi ya

sheria. Lipo tatizo kwa baadhi ya Wizara kutozingatia, mfano, Wizara ya Maliasili na Utalii, imekuwa ikijichukulia ardhi kutoka kwa Wananchi bila kufuata taratibu za kisheria zilizowekwa na Sheria ya Ardhi na Mamlaka ya Mheshimiwa Rais; ni vyema Serikali ikaangalia vizuri sheria ambazo zimewekwa kwa maslahi ya umma. Ahsante.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri husika pamoja na Watendaji wote, kwa Hotuba nzuri na ninapenda kuelekeza ushauri/maombi katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, Utawala Bora: Matatizo makubwa yanatokana na kupishana kwa kauli na matendo kati ya Viongozi Wakuu wa Serikali kama vile Mheshimiwa Waziri Mkuu au Mawaziri na Watendaji kama vile Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na hata Viongozi wa Vyuo. Hali hii imechangia kuchochea maandamano na lawama kwa Viongozi. Tuepuke kupishana kwa kauli na vitendo kwa kuwa na vikao vya pamoja na kuheshimu makubaliano ili yafanane na utekelezaji.

Pili, utekelezaji Miradi ya *TASAF:* Wilaya ya Muheza ilifanya vizuri sana katika *TASAF I*. Utendaji katika *TASAF II* umekuwa mbaya na uliambatana na Wilaya kugawanywa kuwa Muheza na Mkinga, lakini usimamizi wa Miradi kuachwa katika Wilaya ya Muheza. Baada ya Wilaya kugawanyika, ulikuwepo utaratibu wa kugawana mapato na madeni yaliyokuwepo ila hili halikutokea kwa *TASAF*. Taarifa za Ukaguzi wa *TASAF II* na Ukaguzi wa Kamati ya Bunge ya Mahesabu ya Serikali za Mitaa, imeona udhaifu mkubwa katika Miradi ya Huduma za Jamii katika maeneo ya Muheza na Mkinga. Agizo limetolewa Wilaya ya Muheza kutakiwa kulipa sehemu ya hasara inayotokana na upungufu katika Miradi. Hasara hiyo imeelekezwa Wilaya ya Muheza wakati utekelezaji wa Miradi hiyo ulikuwa kabla ya Wilaya kugawanywa. Tunashauri mgao huu uhusu Wilaya zote mbili. Ninaomba nipate ushauri wa *TASAF*.

(a) Miradi ya Makundi Maalum: Jedwali Na. 2 linaonesha Muheza imefanya vizuri sana katika Miradi 123 ya Makundi Maalum kwa jumla ya thamani ya Sh. 2,040,756,958.90 kwa *TASAF II*. Je, Wilaya itasaidiwa vipi katika kupewa mafunzo katika maeneo ya usimamizi wa Miradi na uwekaji wa kumbukumbu za fedha na mali wanazomiliki?

(b) Mfuko wa Rais wa Kujitegemea: Taarifa za Hotuba zimeonesha kwamba, mikopo imetolewa kiasi cha Sh. 38,140,000 kwenye *SACCOS* 22 katika Wilaya tatu za Mkuranga, Rufiji na Morogoro. Wilaya ya Muheza ina *SACCOS* kubwa, kwa mfano, *TCCIA, Muheza SACCOS, Amani SACCOS, CWT SACCOS* (Chama cha Walimu), VICOBA na kadhalika. Je, ni lini na kwa utaratibu gani Mfuko huo utajielekeza katika *SACCOS* katika Wilaya ya Muheza? Tunaomba ushauri na maelekezo.

Tatu, udhaifu wa ushirikishwaji kwa Watendaji katika usimamizi wa Miradi ya *TASAF*. Mfumo wa utendaji wa kuwa na Kiongozi ndani ya Halmashauri ya Wilaya, umetoa mwanya mbaya wa kiutendaji kwa Viongozi hao kujiona wao ni Watendaji wa *TASAF* na kuwajibika kwa *TASAF* badala ya Halmashauri yao na hivyo, kwenda katika usimamizi wa Miradi ya Jamii; kwa mfano, bila kumshirikisha kwa makusudi Mhandisi

wa Ujenzi katika Miradi ya Ujenzi wa Madarasa au Zahanati na Barabara au Mhandisi wa Maji katika Miradi ya Maji (visima) na kadhalika. Inahitajika elimu ya ushirikishwaji ili kuondoa udhaifu huu unaochangia sana kudhoofisha utekelezaji wa Miradi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. YUSUPH A. NASSIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kupata fursa hii kuchangia hoja hii ya matumizi Ofisi ya Rais Utumishi. Aidha, napenda kuipongeza Ofisi ya Rais, Utumishi kwa yale machache yanayoonekana kuongeza tija katika ufanisi wa kazi na kuongeza ubora wa maslahi ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuzungumzia Idara ya Utumishi, kwa kujitahidi kuongeza uwezo wa watumishi wa umma na kupanga mfumo mpya wa ajira.

Mheshimiwa Spika, suala la mishahara midogo ni kilio cha walio wengi katika Sekta hizi, hivyo natoa Rai kuwaomba viongozi tuongeze maslahi kwa watumishi.

Mheshimiwa Spika, madeni ya walimu, watumishi wa Serikali kuu, na stahili zao mbalimbali ni lazima zipatiwe ufumbuzi sasa. Serikali ijivue gamba la Madeni haya.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuishauri Serikali kuwa mfumo uliopo sasa una upungufu sana katika uajiri wa watumishi wa Sekta nyeti za kimaendeleo kama Nishati.

Mheshimiwa Spika, kufuatia kuwepo uwekezaji mkubwa katika Sekta hii, kuna upungufu mkubwa wa wataalam na hata warithi wa wale waliopo kwenye nafasi mbalimbali sasa hawana warithi wa kazi zao, kwani wengi wao hawana zaidi ya miaka miwili kustaafu.

Mheshimiwa Spika, hii ni hatari sana kwa Taifa letu, lenye raslimali nyingi, na uwezo mdogo wa kitaalam. Tunahitaji kuajiri kuboresha na kuridhia maombi ya taasisi mfano, Shirika la Maendeleo ya Petroli *(TIPDC)* na kuwaruhusu kuajiri vijana 100 wenye taaluma mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu raslimali gesi asili na mafuta imekuwa, lakini tujiulize, ni Watanzania wangapi wameajiriwa mle ndani? Tuone kuwa Serikali imetoa leseni za utafutaji wa uchimbaji wa gesi na mafuta zaidi ya 20. Hivyo ni vyema tukafunza na kusomesha vijana wa jinsia zote wa kitanzania ilikuwa na jeshi imara lenye taaluma maalum kwenye uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, “Mtumaini cha ndugu au rafiki, hufa hali maskini.” Tanzania ya sasa kutegemea watu wa nje Ma-TX na Makampuni ya nje na magenge ya watumishi waliokuja nao, kutatufikisha pabaya na siku wakiondoka hatutakuwa na pa kuanzia.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu sasa ina miaka 50 tangu iwe Jamhuri. Sasa mabadiliko na mageuzi ya nguvu na ya dhati ya kimaendeleo ni lazima. Sasa, tuajiri,

tusomeshe na kuweka sheria kupitia Idara zote, Utumishi, TAKUKURU na utawala bora/usalama wa kuwafunda kimaadili ili wakasimamie vyema shughuli hizi kwenye Sekta nyeti.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Mipango chini ya Ofisi ya Rais, Uratibu na Mahusiano, inahitaji kuajiri wafanyakazi 47. Je, Wizara inapanga hadidu za rejea? Kwa nini? Je, umuhimu wa mpango wa mwaka 2011 – 2015 utafanikiwa? Waziri atupe majibu.

Mheshimiwa Spika, nawapongwza TAKUKURU kwa kazi nzuri sana kama siyo wao, Wabunge wengi wapya tusingekuwepo. Rushwa ya kura za maoni na tuhuma za wazi na ushahidi wa wazi umeibua mengi. Naishukuru *PCCB* kwa kutusaidia sana tuwahimize wawapeleke wahusika Mahakamani, kwani wengi wanajisifu kuwa Mkurugenzi wanamjua.

Mheshimiwa Spika, kama ni hivyo, hii ni aibu. Nawasilisha.

**MHE. SULEIMAN NASSIB OMAR:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Waziri kwa kuwasilisha hotuba yake vizuri.

Mheshimiwa Spika, fedha nyingi sana zinapotea katika wizi unaofanyika katika kuwalipa wafanyakazi hewa. Suala hili limekuwa likiongezeka mwaka hadi mwaka badala ya kupungua. Serikali lazima ichukue hatua za dharura zilizokuwa thabiti katika kudhibiti suala hili. Maofisa watakaobainika kuchukua mishahara hewa, wapewe adhabu kali, pamoja na kuilipa mishahara yote waliyoiba.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kutoa mikopo mbalimbali kwa wajasiriamali wadogo wadogo. Kwa bahati mbaya, mikopo hii haiwafikiii wananchi wengi vijijini, hasa vijiji vya Zanzibar. Masharti ya mikopo ni magumu, hivyo wananchi vijijini hawawezi kupata mikopo hiyo. Ni vyema masharti ya mikopo yakaangaliwa upya kwa azma ya kulegeza masharti ili wananchi wengi waweze kufaidika.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ambalo linapatikana katika kila Wizara ni Maafisa wengi kukaimu katika Idara na Masharika ya Serikali. Unakuta katika Wizara na Mashirika yake, zaidi ya Maafisa kumi wanaikaimu kwa muda mrefu. Naomba waraka utolewe kwa mashirika na Wizara zote ili kubidhibiti suala hili.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina idadi kubwa ya watumishi waliostaafu. Wastaafu hawa waliotumikia Taifa letu kwa utiifu na uaminifu mkubwa wanataabika sana baada ya kustaafu. Kiwango cha fedha kinachotolewa kama posho ya wastaafu ni ndogo sana na haipatikani kwa wakati.

Kuna Tume iliyoundwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu mwaka 2009 chini ya Katibu Mkuu Kiongozi iliyoangalia suala la wastaafu pamoja na mambo mengine, na baadhi ya mapendekezo yake yalikuwa ongezeko la pensheni liendane na ongezeko la kima cha chini na pia Tanzania itekeleze Azimio la Shirika la kazi Duniani *(ILO)* ambalo

nchi hii imeridhia kwamba kiwango cha pensheni kiwe asilimia 80. Je, utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati hii yamefikia wapi?

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono hoja. Nianze kuchangia hoja hii kwa kuzungumzia kero kubwa inayowakabili watumishi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, suala la mishahara midogo kwa watumishi wa Serikali kwa sasa ni kero. Watumishi wengi wa ngazi za mishahara hasa kima cha chini, maisha yao ni duni sana. Kima hiki cha chini cha mshahara hakimwezeshi Mtanzania huyu kuweza kuishi vizuri yeye pamoja na familia yake. Ni vizuri kwa sasa kuangalia kwa makini upandishwaji wa mishahara hasa kima cha chini kwa kuzingatia hali halisi ya mahitaji ya mtumishi huyu ili aweze kuishi na kuendeleza familia yake. Mishahara ya sasa kwa kiasi kikubwa haina uwezo wa kumwezesha mtumishi kukabiliana na changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Spika, ipo azma ya Serikali kuwapatia posho maalum watumishi wote wanaoishi na kufanya kazi katika maeneo ya mazingira magumu. Azma hii tangu ilipotangazwa na Serikali hadi leo bado ni kitendawili. Nchi hii ina maeneo mengi yenye mazingira magumu kama vile watumishi wanaofanya kazi katika maeneo ya Delta ya Mto Rufiji ambako wanatumia mitumbwi kuweza kuwafikisha katika mtumbwi kwa zaidi ya masaa 12 ili wafike kwenye vituo vyao vya kazi. Ni vizuri sasa kwa Serikali kuanzisha posho hii kwa watumishi hao wanaoishi na kufanya kazi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, malimbikizo ya madeni ya watumishi wa umma ni kero kubwa. Watumishi wengi hasa walimu, hadi sasa wanadai kiasi kikubwa cha fedha. Aidha, katika Wilaya ya Rufiji kuna watumishi ambao ni Watendaji wa vijiji wanadai mishahara yao zaidi ya mitatu. Watumishi hawa walishajaza fomu za madai, lakini mpaka leo bado watumishi hao hawajapa mishahara hiyo ingawa aliyekuwa Waziri wa TAMISEMI - Mheshimiwa Celina Kombani alilithibitishia Bunge hili kuwa Watendaji hao watalipwa. Ni vizuri sana kwa Serikali kuweza kulipa madeni ya watumishi hawa kwani kero hii ni kubwa na inawafanya watumishi hawa kutokuwa na imani na Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la MKURABITA ambalo limekuwa likisemwa kwa muda mrefu bila utekelezaji nalo ni tatizo. Wilaya ya Rufiji ni miongoni mwa Wilaya chache za Tanzania ambazo zinatekeleza MKURABITA. Azma ya Serikali ni nzuri, lakini utekelezaji wake ni mdogo mno. Vijiji ambavyo MKURABITA umeingia hadi sasa, hakuna chochote kinachoendelea. Ni vizuri kama Serikali haina fedha, wasianzishe miradi hii, kwani inawapa matumaini wananchi ambayo baada ya muda mfupi yanatoweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *TASAF* kwa kiasi kikubwa imechangia kuinua kipato na maisha ya Watanzania, miradi mingi ya maendeleo imefanywa na *TASAF*. Ombi langu kwa Serikali ni kuendeleza miradi ambayo imeanzishwa na *TASAF*. Miradi hii ni kama vile barabara zilizoanzishwa na *TASAF*. Vijiji vingi vimeibua miradi ya

barabara, lakini tangu watengeneze barabara hizo hadi sasa barabara hizo zinakufa kwa kuwa hazina matengenezo ya kila mwaka *(routine Maintanaice)* kama *TASAF* itaendelea vizuri ikaiangalia sana miradi hii ili iwe endelevu. Siyo vizuri kuainisha miradi mipya wakati iliyoanzishwa inakufa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ilenge nyongeza ya bajeti ya mwaka huu, iwalenge Watendaji wa chini. Watendaji wa chini hawana posho za *per diem*, maisha yao ni magumu sana.

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti ya Ajira irudishe chini madaraka kwa kazi za kada za chini kama vile madereva, wahudumu wa ofisi, Watendaji wa Kata, naomba irudishe kwa ngazi ya Wilaya au Mkoa.

Mheshimiwa Spika, nashauri mishahara hewa isimamie kuondoa tatizo hili. Serikali inapoteza fedha nyingi sana kutokana na watumishi wasio waaminifu.

Mheshimiwa Spika, pia naomba Wafanyakazi waingizwe haraka katika *pay roll* mara baada ya kuajiriwa na wastaafu walipwe mafao yao wanapomaliza kutoa huduma katika Sekta ya utumishi wa umma.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Spika, nitachangia katika maeneo ya
maadili ya utumishi wa umma na maslahi ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, kanuni za maadili ya utumishi wa umma ni nzuri, na kama zingefuatwa kungekuwa na ufanisi katika utumishi wa umma. Katika historia ya utumishi hapa nchini, dalili za kuporomoka kwa maadili ya utumishi zilianza kuonekana miaka ya 1980 (katikati) kuanzia wakati huo, dalili za uzembe kazini, rushwa/ubadhirifu, kutojali muda, upendeleo katika ajira, ukosefu wa uzalendo, zilianza kuonekana. Matatizo haya yameongezeka kulingana na jinsi hali ya maisha ilivyozidi kuwa ngumu.

Mheshimiwa Spika, ingawa matatizo hayo yanahusiana, lakini kwa maoni yangu tatizo kubwa kuliko yote ni ufisadi ambao ni kielelezo cha utovu wa uwajibikaji na uzalendo na ubinafsi. Ufisadi katika utumishi wa umma ndiyo ulikuwa kiini cha kusambaratika kwa mashirika ya umma yaliyoanzishwa katika awamu ya kwanza. Hivi karibuni ufisadi umejitokeza katika kashfa mbalimbali, mfano, *EPA, RADA, IPTL,* Kagoda, *Deep green*, Meremeta, Mikataba mibovu ya Madini, ubadhirifu wa mabilioni katika Halmashauri na mashirika ya umma, hata Idara mbalimbali za Serikali, na kadhalika. Vitendo hivi vya ufisadi siyo kwamba tu vinatoa picha mbaya katika utumishi, bali vimepoteza mabilioni ya fedha ambayo kama zingetumika katika shughuli za maendeleo, zingeleta tija ya wazi.

Mheshimiwa Spika, iwapo Serikali inataka kuonyesha udhati wa nia wa kusafisha safu zote za utumishi ifanye yafuatayo:-

(1) Kuwawajibisha wote waliohusika na kashfa ya *EPA*, na kadhalika. Hatua hii itawapa moyo watumishi wote na kuwaonyesha kuwa badiliko la msingi katika mtazamo na utendaji kazi wa Serikali;

(2) Kuhakikisha fedha yote iliyoibwa, inarudi na kutumika katika miradi ya huduma za kijamii kama afya, elimu na kadhalika;

(3) Pamoja na hayo, Serikali iwawajibishe wote ambao wanahusika na upotevu wa mabilioni katika Wizara, Idara za Serikali Kuu na za Mitaa kwa mujibu wa ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu; na

(4) Kuwapa watumishi (waliopo na wastaafu) madai yao.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi zitarejesha imani miongoni mwa wananchi kwa Serikali yao. Bila kuchukua hatua hizi kikamilifu, hakuna mabadiliko yoyote ya msingi kuhusiana na maadili ya utumishi yatakayotokea.

Mheshimiwa Spika, sababu mojawapo kwanini wananchi wanapoteza imani kwa Serikali yao ni ukweli kwamba watumishi wengi katika Serikali Kuu na Serikali za Mitaa wana maslahi duni ambayo hayatoshelezi mahitaji ya familia. Maslahi duni hayahusu mishahara midogo tu, bali yanahusu pia mafao duni ya uzeeni.

Mheshimiwa Spika, mengi yameshasemwa katika hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani. Hapa nitasisitiza mambo yafuatayo:-

(1) Madai/malimbikizo ya watumishi wote yalipwe. Hatua hii itawatia moyo walimu na watumishi wengine na kuanza kurejesha imani yao kwa Serikali.

(2) Wastaafu wote walipwe stahili zao.

(a) Wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki walipwe. Serikali inapaswa kuwajibika kwa kubeba jukumu hili.

(b) Wahadhiri/maprofesa wastaafu (Chuo Kikuu cha DSM, Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine); Waraka wa Serikali uliotolewa mwaka huu ulielekeza kuwa wahadhiri/maprofesa waliochini ya *SSSS* watakaostaafu baada ya Machi, 2011 ndio watakaoingizwa katika *PPF*. Waliostaafu kabla ya hapo (1993 – Feb, 2011) hawajui hatima yao. Hawa ni wale waliolipwa malipo ya mkupuo mmoja tu, bila pensheni ya kila mwezi. Hawa wamedhulumiwa stahili hii ambayo wenzao katika utumishi wa umma wanaipata. Serikali itende haki kwa kuwalipa hawa wahadhiri/maprofesa wastaafu. Hivi sasa wanahangaika sana, huku wenzao wanaishi maisha mazuri.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika suala zima la watumishi wa umma, yaani *public employee*. *Induction rate* ya watumishi

hawa ni ndogo sana, yaani uki-*compare* na nchi jirani za Kenya na hata na *private sector employee* utakuta ni katika *ratio* ya 5:1, yaani watu watano wanaofanya kazi katika Sekta ya Umma ya Tanzania ni sawa na uzalishaji wa mtu mmoja katika nchi ya Kenya na kwa *private sector*. Hii ni fedheha sana na ni *factor* nyingi sana zinazopelekea haya yote kutokea. Kikubwa zaidi ya yote ni *luck of seriousness*, yaani mtu kukosa utayari wa kufanya kile anachotakiwa kufanya ndani ya masaa halali ya kazi ambapo hii inapelekea utoaji duni wa huduma kwa wateja. Kwanza *priority* ya wafanyakazi hawa kuwa ni kusogoa, kupigiana simu, kuangalia *facebook*, kusoma magazeti, na kutojali mteja *(no customer care)* hawajui kwamba mteja ni mfalme na kufanya hivyo ni kuwajibika ili kuongeza pato la Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupunguza hili, naishauri Serikali kuweka katika kila Ofisi ya Umma *discipline* kwa maana ya kuwa na *job description* ambayo itaonyesha *in details responsibilities* za kila mfanyakazi kuanzia ngazi ya chini hadi ya juu. Pia iwepo *system* ya *either daily report and weekly report* ya kile ambacho mfanyakazi amefanya kwa siku au masaa husika aliyokuwa kazini. Maana wengine wanakuja ofisini kama picha au pambo, anasaini *attendance register* lakini akili yake yote haipo pale, na hawafanyi kazi, bali kusubiria muda ufike aondoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo lingine ni kwamba tuondoe zana ya kuwa ukishaajiriwa, basi hufukuzwi kazi kirahisi, labda uwepo ubadhirifu mkubwa. La hasha! Inabidi iwepo adhabu ya kumfukuza au kum-*demote* mfanyakazi yeyote ambaye hafanyi kazi kwa ufanisi na uadilifu. Vile vile kuwepo na motisha katika Idara husika kuwa kila mfanyakazi ambaye anafanya kazi kwa uadilifu na ufanisi zaidi. Hii itaongeza bidii kwa wale ambao hawafanyi kazi kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kuwepo na *suggestion box* ambazo zitakuwa zikitumika kama *feedback from the customer in a respective office if the customer care is being offered as expected* au mteja anakuwa *treated, increasing the production* na maoni yote yazingatiwe na kufanyiwa kazi. Hii itasaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ni kuhusu suala zima la rushwa. Inawezekana kabisa baada ya kuwepo kwa TAKUKURU, rushwa imepungua, lakini pia inawezekana kuwepo kwa TAKUKURU bado hatujasaidia kupunguza rushwa katika taasisi ambao zinatoa huduma za jamii. Kwani huko tumeona rushwa imekithiri sana hasa mahospitalini, barabarani, yaani *(traffic police)*, Vituo vya Polisi kwa Watendaji wa ngazi za Wilaya, Kata, Tarafa, Vijiji hadi Vitongoji huku ndiyo kuna rushwa ambayo inaathiri wananchi wetu ambao hawana vipato vya kutosha na ambazo zinapelekea wananchi kukosa huduma muhimu na stahili kwa sababu ya wimbi hilo la rushwa. Hivyo, nashauri kitengo cha rushwa ambacho kimeenea Wilayani kifikie huko nilipotanabaisha na kuhakikisha urasimu huu unaondolewa. Hii itasaidia sana kulijenga Taifa lenye watu imara na kufanya kazi kwa bidii.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie Taasisi ya TAKUKURU.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mlundikano wa kesi nyingi za rushwa Mahakamani, nashauri TAKUKURU ijengewe uwezo, ipewe mamlaka Serikali ianzishe Mahakama ya Rushwa kama ilivyo kwenye Mahakama ya Ardhi na Mahakama ya Biashara. Naamini kuwepo na Mahakama ya Rushwa itasaidia kesi ya rushwa kushughulikiwa haraka na haki zilizopotea kupatikana kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na mlundikano wa majalada ya rushwa wa *DPP*, hotuba inaonyesha zaidi ya majalada 200 yanayohusu rushwa yamekwama kwa *DPP*. Hii inaonyesha *DPP* ana majukumu mengi, hivyo nashauri TAKUKURU wapewe mamlaka ya ku-*proscute* kesi za rushwa Mahakamani, ili raslimali zilizochukuliwa na watu wachache na kujinufaisha nazo zirejeshwe kwa wananchi kwa muda muafaka.

Mheshimiwa Spika, nashauri hivyo kwa sababu kesi za rushwa uchunguzi wake ni mgumu sana sababu mtoaji na mpokeaji rushwa wanakubaliana kufanya hiyo. Rushwa za mikataba mibovu ya nchi na kwenye Taasisi za umma pande zote mbili wanakubaliana, hivyo Serikali inapokuwa na mifumo inayochelewesha kupatikana kwa ushahidi, kufikishwa kesi Mahakamani hatimaye kutolewa hukumu na haki za wananchi kupatikana. Hivyo nashauri TAKUKURU wapewe mamlaka ya kushitaki na kusimamia kesi Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yake yote kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara. Nitachangia maeneo machache.

Mheshimiwa Spika, mipango yote mizuri ya Serikali ikiwemo utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa miaka Mitano (2011 – 2012), isipotekelezwa ipasavyo ni kazi bure. Naiomba Serikali ibuni utaratibu wa ziada wa kuwawajibisha watumishi wa umma ili kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Utaratibu wa sasa umefeli maana miradi mingi haiendi vizuri kwa kutowajibisha watekelezaji ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, elimu haitaboreka, waalimu wasipotekeleza majukumu ipasavyo, afya haitaboreka kama wahudumu wa afya hawatawajibika, na kama hawana utaalam unaotakiwa; vifo vya akina mana vitaendelea; biashara hazitaboreka kama wafanyakazi wataiba sementi na kadhalika na majengo ya Serikali yatabaki na nyufa kama ubora unaotakiwa hautazingatiwa. Hivyo naiomba Serikali ibuni utaratibu mzuri wa kuwawajibisha wafanyakazi, kwanza kutekeleza majukumu yao, lakini pili wawajibishwe hadharani wanapogundulika na mapungufu hayo ili wasirudie.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana TAKUKURU kwa kazi nzuri wanayofanya. Naomba Watanzania waelewe kuwa Watanzania tumeongezeka sana na uhalifu umeongezeka sana. Naishauri Serikali iwe inatoa kauli kuhusu ongezeko la watu na utekelezaji majukumu (magumu) chombo chake cha TAKUKURU. TAKUKURU inafanya kazi kubwa na wote tunajua, lakini upana wa eneo la kushughulikia umekuwa mkubwa sana. Uhalifu umekuwa mkubwa na zaidi sana wapinzaji wanajenga kazi

kubwa ya fitina na matokeo yake TAKUKURU inaonekana haifanyi kazi, na Serikali haiwajibiki. Hii siyo sahihi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali na Wizara ya Utumishi iwe inatoa tamko rasmi kuhusu maneno ya uzushi au tuhuma dhidi ya Watumishi wa Serikali pindi wanapotuhumiwa. Hii siyo tu italeta amani na utulivu kwa watuhumiwa, bali pia itarudisha imani ya Watanzania kwa Serikali. Pia Wizara isisite kutoa uamuzi wa tuhuma mbalimbali ili watumishi watekeleze majukumu yao kwa ufanisi, wasiishie kujiona wakosafi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. MUSSA Z. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, watumishi wengi Serikalini hawana tija kwenye utumishi wao kutokana na ajira ya kudumu. Ni bora kukawa na utaratibu wa mikataba, pale mtumishi atakaposhindwa kutekeleza majukumu yake hapewi mkataba mwingine. Zoezi hili pia litaongeza ajira kwa kupeana zamu za mkataba.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Spika, kimsingi, naunga mkono hoja ya Mheshimiwwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, hotuba imezingatia mambo mengi ya msingi yanayohusiana na shughuli zote zinazohusiana na Menejimenti ya Utumishi wa Umma na namna nzuri ya kuboresha utumishi nchini. Mheshimiwa Waziri kwa umakini mkubwa amezielezea taasisi zilizomo ndani ya Wizara yake kwa mfano Sekretarieti ya Maadili TAKUKURU, Ofisi ya Rais/Ikulu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, mipango yote ambayo imo ndani ya hotuba hii kama kweli itatekelezwa kwa kuimarisha elimu kupitia vyuo mbalimbali vya utumishi wa umma vilivyopo hapa nchini na nje ya nchi yetu na kupitia mitandao, utumishi wa umma unatarajiwa kuwa ndilo chimbuko rasmi la mabadiliko hata kwa jamii ya wananchi wa kawaida katika kupata mawazo mapya kwao.

Mheshimiwa Spika, watumishi wa umma wamefundishwa njia mbalimbali na ujuzi katika fani mbalimbali za elimu, afya – miundombinu, Kilimo, maji, umeme na mategemeo ya walio wengi ni kwamba ukombozi wa nchi hii utatokana na aina ya watumishi tunaokuwa nao.

Mheshimiwa Spika, wakati umefika kwa Wizara hii ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma kuangalia kwa makini uwezekano pia wa suala la urasimu unaotawala katika ofisi za umma ambapo watumishi wanakuwa hawajali wateja wao. Ipo mifano mingi inayoonyesha kuwepo kwa madhaifu katika ofisi za umma ambapo wahudumu kwenye ofisi au Makarani katika Masijala wanakuwa wasumbufu bila sababu, wakati mwingine

wanahusika kuficha majalada mfano Mahakamani, Idara ya Ardhi na Hazina. Kwa wanaofuatilia mafao ya kustaafu au mirathi, Masijala katika Halmashauri, watumishi wanalazimishwa wakati mwingine kutoa rushwa ili kutafutiwa majalada yao ili yashughulikiwe kwa lengo la kupatiwa huduma zao. Kisheria inabidi waanze kuinunua haki katika mazingira yasiyokubalika. Kwa watu kunyanyaswa na watu wadogo kama makarani na wahudumu kujaribu kuonekana ni watu muhimu kwa kusababisha usumbufu usiokuwa wa lazima wakati kuna viongozi waandamizi kwenye Ofisi za Serikali, lakini mambo haya yanafanyika na wao wapo.

Mheshimiwa Spika, inakuwaje huduma wakati mwingine zinatolewa pengine kwanza mtu ajulikane ama kwa cheo? Je, kwa wale wasiokuwa na vyeo huduma kwao itakuwaje?

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inazingatia utawala wa sheria, basi na ijulikane hivyo kwa watu wote aliyekuwa na cheo au asiyekuwa na cheo. Utumishi wa umma ukibadilika tutapiga hatua kwa kasi zaidi iwapo uwajibikaji utakuwa wa hali ya juu na kuondokana na urasimu unaoliyumbisha Taifa na wakati mwingine unaowafanya hata wawekezaji toka nchi za nje kulazimika kukimbilia nchi nyingine kuepuka urasimu katika kushughulikia taratibu za uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, mambo mengine yamesemwa kuhusiana na urasimu unavyoifanya bandari yetu ya Dar es Salaam kukimbiwa na wafanyabiashara toka nchi za maziwa makuu zisizokuwa na malango bahari. Nchi kama Uganda, Burundi, Rwanda hata Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo hulazimika kutumia bandari ya Mombasa. Urasimu vile vile umeua mashirika ya umma. Naomba ifike mahali mbinu iliyotumika kuunda *TRA* itumike kuyaunda upya Mashirika ya Reli, Shirika la Ndege, Shirika la Bima na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kama Watanzania wameweza kufanya vizuri katika *TRA* na Benki ya *CRDB*, kwa nini Watanzania, watumishi katika maeneo haya wasifanikiwe? Basi tuige uzoefu wa Sekta zinazofanya vizuri ili tupige hatua.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Spika, nchi yetu inaongozwa kwa sheria, kanuni na taratibu. Kwa kweli huu ndio msingi wa utawala bora. Ajira na kustaafu kazi katika utumishi wa umma umewekewa utaratibu maalum ndani ya Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma na kadhalika. Mfano, umri wa kustaafu kwa hiari ni miaka 55 na kustaafu kwa lazima ni miaka 60. Lakini wako watumishi wa umma hususan wale walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kushika nyadhifa mbalimbali Serikalini au katika Mashirika ya umma, wanaomba kuongezewa muda na kukubaliwa hata pale ambapo kazi hiyo siyo *rare profession.* Wahitimu wa Vyuo Vikuu wamejaa Mitaani bila kazi: Je, hali hii siyo kupendeleana? Je, kufanya hivyo si kuvunja misingi ya utawala bora katika utumishi wa umma?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi za uwasilishaji mzuri wa hotuba ya bajeti, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara husika pamoja na Watendaji wao.

Mheshimiwa Spika, maadili ya utunzaji wa nyaraka nyeti za Ofisi ya Serikali yameshuka sana na hatimaye kuifanya Serikali isiwe na maana katika neno "siri". Ni tatizo kubwa! Naomba Serikali inipatie majibu na kunieleza ni mkakati gani umewekwa ili kuzuia uvujaji wa taarifa nyeti za Serikali.

Mheshimiwa Spika, suala la ajira kuwa Serikali kuu ni urasimu usio na tija na pia kuzuia nafasi za ajira kwa wananchi ambao wanaishi kwenye Halmashauri zetu. Ni magazeti mangapi ambayo yanafika kwa wakati kwenye Wilaya zetu ili wananchi waweze kusoma matangazo ya kazi na kuanza kuomba hiyo ajira au msafiri hadi Dar kwa ajili ya mahojiano?

Mheshimiwa Spika, ni vema waziri atoe taarifa/ufafanuzi ni vipi wataondoa kadhia hii na kuruhusu fursa hizo za utangazaji wa ajira kwenye Halmashauri/Wilaya zetu. Naomba nipate mkakati uliopangwa katika hili. Pia, nini mkakati wa kupunguza sifa za ajira ya Mtendaji wa Kijiji? Vijiji vingi havina Watendaji, kwani sifa ni *Form IV* na kozi ya miaka miwili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza kazi kubwa ambayo Wizara hii imekuwa ikifanya kuhakikisha kuwa watumishi wa umma wanaondolewa kero mbalimbali ili kuongeza ufanisi katika kazi ili kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika Wizara hii nianze kuchangia suala la wazee wastaafu na wazee wa kawaida. Katika nchi yetu wapo wazee ambao walikuwa watumishi na hivi sasa wamestaafu, lakini wapo wazee ambao walijiajiri wenyewe katika kazi mbalimbali kama kilimo, biashara na kadhalika na kusaidia kuchangia pato la Taifa na hivi sasa hawana uwezo tena wa kufanya kazi hivyo kuishi katika mazingira magumu sana.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu kwa kuwa imekumbwa na janga kubwa la UKIMWI, wazee hawa ndio wenye mzigo mkubwa sana wa kulea wajukuu na watoto yatima hivyo kupelekea kuwa maskini zaidi na kushindwa kuwasomesha watoto hao, kuwapatia huduma za afya, hata makazi yao kuwa duni mno. Nchi yetu tuna sera nzuri sana kuhusu wazee, lakini utekelezaji wake umekuwa mgumu, hata MKUKUTA namba moja ulilenga sana kuwasaidia wazee lakini wazee hawakunufaika kabisa.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonyesha kuwa kwa hivi sasa tuna asilimia nne ya wazee wastaafu wapo mjini na asilimia 96 ni wazee walioko vijijini ni wale wazee ambao katika ujana wao walikuwa wamejiajiri wenyewe. Lakini hadi sasa Serikali inawatambua wale wazee ambao walikuwa wameajiriwa tu kwa kuwapatia penseni, lile

kundi kubwa ambalo ni wazee waliokuwa wamejiajiri wenyewe tumewaacha kabisa na hawapati chochote na huwa ndio waliofikisha Taifa hili hapa tulipo. Je, Serikali haioni kuwa ipo haja ya wazee hawa kufikiriwa kupata posho kila mwezi kama nchi za wenzetu wanavyofanya? Suala hili katika sherehe za siku ya wazee duniani waliomba Serikali iweze kuwafikiria wazee hawa kupata posho na Waziri Mkuu aliahidi kulifikiria jambo hili, je, hadi sasa limefikia hatua gani?

Mheshimiwa Spika, wazee hawa Serikali iliwaondolea gharama za matibabu ili waweze kutibiwa bure lakini maeneo mengi katika hospitali zetu watumishi tulionao hawazingatii hilo hivyo kukosa kupata haki yao ya matibabu bure. Nchi yetu tuna utaratibu wa kuwa na madaktari wa watoto, madaktari wa akinamama, lakini tunasahau kabisa kuwa wazee ni kundi maalum ambalo linahitaji kupata huduma nzuri za matibabu.

Mheshimiwa Spika, kwa makundi yanayopata pensheni wamekuwa wakiomba sana kiwango wanacholipwa waongezewe, kwani gharama za maisha zimepanda sana, lakini vile vile pensheni hizi zimekuwa hazina uwiano kati ya wale wanaostaafu hivi sasa na wale waliostaafu miaka kumi iliyopita kutokana na viwango vya mishahara waliyostaafia. Naomba nichukue nafasi kutoa ombi maalum kwa Serikali kama ifuatavyo:-

Kwanza, Serikali iwe na kiwango maalum cha malipo kwa wastaafu chenye uwiano kulingana na hali halisi ya maisha, pili, wazee ambao walikuwa wanajiajiri wenyewe wawekewe utaratibu wa kupata posho kila mwezi angalau shilingi 20,000 kwa mwezi ili ziwasaidie kujikimu katika mambo madogo madogo, tatu, sera ya wazee ibadilike iwe sheria, nne, Serikali isimamie sera ya matibabu bure kwa wazee itekelezeke kwa vitendo na tano, Serikali iweke utaratibu wa kuwa na madaktari wanaoshughulikia matatizo ya afya za wazee.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja hii kwa kuanza na ajira za mahakimu wa mahakama ya mwanzo. Serikali itoe ajira ya mahakimu kwa vijana wetu ambao tayari wamesomea, wana vyeti na wengine wana stashahada za sheria kuliko kuendelea kuwarudisha mahakimu waliostaafu. Kama Serikali inadai kuwa inatoa ajira ya uhakimu kwa watu wenye shahada tu, kwa nini wanarudia kuwarudisha mahakimu waliyostaafu na wakiwa na elimu ya vyeti vya elimu ya sheria.

Mheshimiwa Spika, ajira za *WEOs* na *VEOs* zije na watumishi wengine wa chini kama watumishi wa afya, kilimo na kadhalika waajiriwe na Serikali za mitaa ili kuondokana na upungufu wa watumishi wa kada hizo kulikoni watumishi hao kuajiriwa na Serikali Kuu. Hali hiyo ni kuipokonya Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, rushwa, tafiti zinazofanyika nchini zinaonyesha polisi na mahakama, ni idara ambazo zinaendelea kutesa wasio nacho kwa kuwagandamiza na

kutoa haki isiyo haki kwa walionacho. Serikali iwe inachukua hatua kali na kwa muda mfupi kwa watumishi wanaobainika na kosa hilo.

Mheshimiwa Spika, TAKUKURU inafanya kazi kwa shinikizo, ni idara isiyo na msaada wowote kwa mwananchi wa chini, ukiona TAKUKURU inachukua hatua ujue kuna rushwa ya shinikizo toka kwa mtu mkubwa kwa maslahi ya mtu fulani.

Mheshimiwa Spika, tunapofikiria kutoa mishahara kwa madiwani na Wenyeviti wa Halmashauri za Vijiji tunajaribu kufikisha na Wenyeviti wa Vitongoji na kutoa posho kwa wajumbe wa Halmashauri za Vijiji.

Mheshimiwa Spika, kugawa Majimbo na Wilaya. Lengo la Serikali katika jambo hili ni zuri lakini jinsi inavyofanyika baadhi ya maeneo yanapewa upendeleo na maeneo mengine kusahauliwa mfano halisi ni Jimbo la Kwela katika Ukanda wa Ziwa Rukwa kutokana na jiografia ilivyokaa inatakiwa kuwa na Wilaya au Jimbo pekee ili kuharakisha maendeleo ya eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Spika, naipongeza sana TAKUKURU kwa kazi nzuri sana wakati wa mchakato wa uchaguzi. Walifanya kazi nzuri kwenye kuta ya maoni na hata kwenye Uchaguzi Mkuu, lakini hapo hapo nina masikitiko makubwa sana kwa kuwa TAKUKURU hawajafika Zanzibar kuanzia mchakato wa kura ya maoni hadi mwisho kwa hivyo ninaomba katika uchaguzi wa mwaka 2015 wafike Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi ya Umma, hiki ni chombo chenye majukumu ya kujenga imani ya wananchi. Nakipongeza sana kwa kazi yao nzuri wanayofanya, lakini kwa nini haitoi ripoti ya changamoto ambazo Sekretarieti ya Maadili ya Umma inazipata ili Wabunge wasaidie kuzijadili.

Mheshimiwa Spika, suala la Mfuko wa Maendeleo wa *TASAF*, maandalizi ya mpango wa awamu ya tatu *TASAF* tumeelezwa kwa urefu na miradi yote lakini mbona changamoto zinazoikabili *TASAF* haijaandikwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho mishahara ya wafanyakazi hewa. Hili tatizo ni la muda mrefu sana ingawa linapungua lakini bado lipo suala langu ni mikakati gani itafanyika ili tatizo hili limalizike. Je, hawa *Pay Master* ambao unaamini wanaelewa wanawalipa wafanyakazi hewa wamechukuliwa hatua gani? Lazima iwe mkakati maalum kumaliza hili suala.

Mheshimiwa Spika, nitagusia kidogo kuhusu wafanyakazi ambao hawawajibiki ipasavyo, watu wanaingia wakati wanaotaka na wanarejea wakati wanapotaka, natoa rai moja ambayo itaweza kufanyika kila Idara na Wizara kila siku dakika 20 kabla ya kuanza kazi Mkuu wa Idara akae azungumze na watu wote wa Idara yake kuhusu wajibu wao na

hii itasaidia kuwakumbusha wajibu wao nani bado. Kila mfanyakazi amuandikie ripoti yake kwa kila mwezi na hii itapatikana kujua maendeleo yake na akiwa hawajibiki ipasavyo hatua kali ichukuliwe.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, hongera kwa hotuba nzuri. Hotuba imegusa wananchi, safi sana.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Makatibu na Wenyeviti wa Serikali za Vijiji walipwe angalau shilingi 5,000/= kwa mwezi. Ni kazi kubwa wanafanya kusimamia maendeleo nchini. Tunaomba Makatibu Tarafa wawajibike pia kwa Halmshauri ya Jiji, *Council* na Halmashauri ya Wilaya ili kuendeleza Utawala Bora. Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa isibaki muda mrefu bila Mkuu husika *(RC/DC)* na kuwa maofisa wengine wanakaimu kwa muda mrefu sababu wanaokaimu watakuwa hawana maamuzi ya mwisho, hivyo kukwaza shughuli za Mkoa na Wilaya. Tunaomba Makaimu wa Ofisi za *RC/DC* zisiwepo. Awepo msaidizi wake na *DAS*, lakini Kaimu *RC/DC* haipendezi. Ofisi ya *RC* Lindi ni muda mrefu sasa kuna Kaimu Mkuu wa Mkoa mnalionaje hilo?

Mheshimiwa Spika, shughuli za ma-*DED* na Wenyeviti wa *Council* hukutana *ALAT* kila mwezi ni gharama na muda mwingi unapotea bila kufanya kazi. Iangaliwe suala la mikutano, haipendezi muda mwingi unapotea kuzunguka mikoani kwa mikutano. Litazameni hilo.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuipongeza hotuba ya Waziri kwa kuwa na mambo mazuri yaliyopangwa kutekelezwa katika mwaka 2011/2012. Nikianza na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* ambao umepanga kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa zote kubuni na kuongeza kipato katika miradi 1,200 itakayobuniwa na wanachi. Hili ni wazo zuri sana la kimaendeleo endapo mpango huu utatekelezwa mpaka ngazi ya vijiji, nina uhakika tutainua kipato cha wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa kwa miradi ya *TASAF* ni fedha kutopelekwa kwa wakati kiasi kwamba inaathiri utekelezaji wa miradi. Niiombe Wizara/Serikali ifanye utaratibu maalum kwa mwaka mpya wa fedha yaani 2011/2012 kwamba miradi inapoibuliwa na kupitishwa na fedha ipelekwe kwa wakati ili kuwezesha utekelezaji wa miradi iliyopangwa.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni huu mpango wa kurasimisha rasilimali na biashara za wanyonge Tanzania (MKURABITA). Utaratibu huu ni mzuri sana kwa kuwa wananchi wa kawaida wanapata nafasi ya kumiliki ardhi yao waliyonayo. Kupitia MKURABITA wananchi hata waliopo vijijini watakuwa na uwezo wa kupata hatimiliki. Kwa kuwa na hatimiliki wananchi hawa wataweza kukopesheka katika vyombo mbalimbali vya fedha. Ninaomba Serikali kuwa mpango huu wa MKURABITA upelekwe kote kabisa na utekelezaji wake vijijini uanze mara moja.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa watumishi wa umma wanapostaafu wanapata matatizo makubwa sana hasa wanapofuatilia mafao yao. Wengi wanasafiri kutoka vijijini kuja Dar es Salaam kufuatilia mafao yao. Mara nyingi kutafuta faili tu inachukua muda mrefu. Matokeo yake wengi wamefuatilia kwa miaka mitano hadi kumi bila mafanikio. Sambamba na hili ni wale wanaofuatilia mirathi baada ya mtumishi kufariki. Ninazo kesi za watu wengine wamekaa miaka 20 bila kufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, hii ni changamoto kubwa sana katika utumishi wangu kwa mwaka mmoja na sasa ikiwa ni mwaka wa pili nimeona kuwa ni kero kubwa sana kwa wananchi hasa walio wanyonge watokao vijijini. Inawezekana kabisa ninyi katika ngazi za juu hamuwezi kulima lakini nasema kuwa hili ni tatizo kubwa na ninaomba hatua za makusudi zifanyike ili kutatua kero hii.

Mheshimiwa Spika, katika mambo haya matatu suala la *TASAF* kupeleka fedha kwenye miradi kwa wakati suala la MKURABITA kuanzishwa kote mpaka vijijini na suala na pensheni za wastaafu na mirathi ni muhimu yakaangaliwa na kuboreshwa kama nilivyoshauri. Naunga mkono hoja.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kuhusu suala la kupambana na rushwa. Kwa kuwa chimbuko la rushwa ni pamoja na mishahara midogo, watumishi kukosa vitendea kazi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ukienda hospitali ukamkuta daktari yuko gizani kwa kukosa umeme wala mafuta ya kuwashia jenereta, ni dhahiri kwamba kama wewe ni muungwana utampa daktari shilingi 10,000/= ili angalau aweze kupata mafuta ya jenereta na hatimaye aweze kutoa huduma kwa wagonjwa. Je, hii itaitwa rushwa au uwezeshaji?

Mheshimiwa Spika, ukienda shuleni kwa mwanao kuomba matokeo ya mitihani ya mtoto, ukaambiwa kuwa hakuna karatasi ya kuandikiwa hayo matokeo, kama ni muungwana utatoa shilingi 2,000/= ili huyo mwalimu aweze kununua karatasi hatimaye aandike matokeo ya mwanafunzi. Je, hii shilingi 2,000/= ni rushwa au ni uwezeshaji? Ukienda Mahakamani hali ni ile ile, hawana vitendea kazi. Je, raia anaposaidia kumwezesha karani ili atoe taarifa ya mhusika akampa pesa ya kununua kalamu na karatasi bado tutamtuhumu kwa kupokea rushwa?

Mheshimiwa Spika, ili TAKUKURU iweze kufanya kazi kwa ufanisi na kwa kutoa haki, lazima Serikali iwawezeshe watumishi kufanya kazi zao bila kuwa na kipingamizi cha kukosa vitendea kazi. Endapo tutajikita kuwawezesha watumishi, tatizo la rushwa litapungua kwa asilimia kubwa. Ni ukweli usiopingika kwamba wakati mwingine watumishi wanapokea pesa za kuwawezesha kufanya kazi kama nilivyoeleza hapo juu, lakini pesa hizi hupewa tafsiri ya rushwa. Ni matumaini yangu kuwa Serikali itazingatia maoni haya ili tuweze kupunguza na hatimaye kutokomeza kabisa rushwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Waziri kwa kazi yake kubwa ya kuwasilisha hotuba ambayo ni muhimu sana katika Taifa letu. Naomba nizungumzie udahili wa wanafunzi uliongezeka kote kwenye shule za msingi, shule za sekondari na elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, ni jambo jema kuona kuwa tunakuwa na wanafunzi wengi na ongezeko hili linatia moyo. Lakini mimi nadhani Serikali yetu ingezingatia zaidi ubora wa elimu. Nadhani Serikali ifanye juhudi za kuboresha shule zilizopo sasa ili yawe na ubora. Endapo shule na vyuo vyetu vitakuwa na ubora, hakika tutakuwa na kila sababu ya kujivunia mafanikio ya wananchi katika sekta ya elimu.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali yetu izingatie kuboresha shule tulizo nazo badala ya kuendelea kuongeza shule nyingi ambazo hazikidhi soko la ajira. Juzi nilishiriki kwenye kongamano la Bunge la Afrika Mashariki huko arusha na moja ya changamoto za kushirikiana kisiasa yaani *political federation* ilikuwa ni ushindani mkubwa kwenye ajira.

Mheshimiwa Spika, ili Watanzania tuondokane na uoga wa ushindani kwenye soko la ajira ni lazima tuzingatie ubora wa elimu yetu badala ya kuongeza idadi ya shule ambazo ndizo zinazosababisha ongezeko la udahili.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, nami nashukuru kwa nafasi ya kuchangia. Kwanza, niwapongeze Mawaziri wote wa Wizara husika, pamoja na watendaji wote. Mimi mchango wangu utakuwa wa maswali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini Serikali inashindwa kudhibiti nyaraka za siri za Serikali? Mimi naogopa sana kwani humu ndani Bungeni tumeshuhudia tangu Bunge la Tisa na Bunge hili wapinzani wanaingia na nyaraka za siri ama kutaja mambo yaliyopo kwenye nyaraka hizo. Naogopa! Nchi inaweza kuuzwa!

Mheshimiwa Spika, kwa nini TAKUKURU wanakuwa wanalaumiwa kwa kazi ambayo ameshaifanya na iliyobaki ni jambo la mahakama. Kwa nini Serikali haijibu tuhuma hizo? Kwa wapinzani kung’ang’ania hoja za Meremeta, *Richmond* na kadhalika na Serikali imekaa kimya? Wajibuni!

Mheshimiwa Spika, Benki ya Rasilimali ndio mkombozi wa mkulima wa Tanzania na inaonekana kuwa na utaratibu mzuri sana. Je, ni kwa nini wasiwezeshwe zaidi ili wafungue matawi mengi angalau kila Wilaya au Mkoa? Au waweke kila Benki ya *NBC* dirisha la kupatia mkopo kule.

Mheshimiwa Spika, kuna manung’uniko ya unyanayasaji wa kijinsia kwa wanawake maofisini, kwanza kama mwanamke akitongozwa na bosi wake na akakataa ni lazima atawekewa mikwara na mikingamo mbalimbali ili aonekane hawezi kazi na hivyo ama kutokupandishwa cheo au safari hapati za kikazi ama kozi mbalimbali na kadhalika na mara nyingine kuhamishwa bila utaratibu maalum na kupelekwa mahali pengine kama adhabu. Je, hilo Serikali mnasemaje?

Mheshimiwa Spika, ni kitu gani hupelekea nafasi moja kukaimiwa kwa muda mrefu? Kama anayekaimu anaonekana anaweza kukaimu, kwa nini asipewe moja kwa moja?

Mheshimiwa Spika, suala la pensheni kwa wazee wote. Suala hili ni zito sana, naishauri Serikali isiharakishe kutoa majibu, ilichunguze na kuleta hapa Bungeni ili tulipitishe. Nasema hivyo kwa sababu linahitaji pesa nyingi sana. Wazee ni wengi mno inabidi iundwe Wizara inayojitegemea, vinginevyo tutakwama. Pia ni vema umri ukazingatiwa, uwe ni wa juu sana ili kupunguza idadi. Pia nimeona kuna mfuko wa jamii ambao unajumuisha watu wote, hasa wakulima, wafanyabishara wadogo, wa kati, wakubwa na kadhalika. Kweli nimeipongeza sana, nimeiona kwenye *TV TCB1* leo wakati wakiwa kwenye Maonyesho ya Sabasaba.

Mheshimiwa Spika, mfuko huo mimi naunga mkono asilimia mia, kwani ndio utakuwa mkombozi wa kitendawili hiki cha pensheni kwa wazee. Nashauri elimu itolewe kote, pia endapo Serikali itakamilisha mchakato wa kuanza kuwalipa wazee, ni vema ikawalipia chochote kwenye mfuko huo wa jamii ili waingie kule na kuanza kulipwa kule.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nimalizie kwa kuiomba Serikali itafute namna ya kufundisha raia juu ya maadili kwa semina ama vyovyote, kwani nashangaa wale walio mstari wa mbele kwenye kuleta vurugu kwa kutumia wafanyakazi na ndio maana nyaraka zinatoka kirahisi hasa zilizo za siri. Wameanza eti kulaumu kuwa amani inavunjwa. Serikali tuwe wakali kidogo kwa wachochezi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kwa machache katika Wizara hii juu ya suala la rushwa. Rushwa katika nchi hii imekuwa ni tatizo sugu. Sehemu nyingi kama ukitaka kuchunguza katika Wizara/Idara mbalimbali utakumbana nazo. Tatizo hili haliwezi kuondoka kwa vile hata wale waliokabidhiwa dhamana ya kupambana nayo nao wamo humo humo, hivyo wanashindwa kutekeleza. Vilevile rushwa ipo kwa wakubwa ambao TAKUKURU inashindwa kukabiliana nao.

Mheshimiwa Spika, vilevile nizungumzie juu ya udini. Suala la udini kule nyuma Chama cha Wananchi *(CUF)* kilikuwa kimepakazwa kuwa ni chama cha udini kwa kutaka kukichafulia ili kisipate kuungwa mkono. Lakini hivi karibuni tumeshuhudia wakati wa kampeni ilifanyika makanisani. Kampeni makanisani ilikuwa ikiendeshwa bila kificho ya kuwa achaguliwe fulani ambaye ni mkiristo mwenzetu. Mimi ni mkiristo na nimeshuhudia mapadri wakitangaza hivyo na sio kwa kusikia kwa kinywa cha pili au cha tatu. Matangazo hayo yaliyotangazwa katika makanisa mengi na baadhi ya vyama vingine walikuwa wanalalamika. Lakini hakuna mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mimi kuwa mgombea mkiristo, haikujalisha kuwa wananipiga vita mwenzao, ila kwa kuwa niligombea chama tofauti na lengo lao. Bila kusita mchungaji wangu aliwaambia waumini ya kuwa kura zetu tumpe fulani bila

kificho na kwamba tusiwape waislamu kwani tukiwapa hao wataleta uislamu nchini pia wataleta Mahakama ya Kadhi. Mimi binafsi nilisema ya kuwa udini uliokaririwa kwa *CUF*, leo udini si wanauona? Hivyo hawa ndugu wanaolalama kukanusha ni kwa kuwa imebainika na sasa wanaona haya.

Mheshimiwa Spika, pia nizungumzie juu ya mipango shirikishi. Mipango mingi katika nchi hii haifanikiwi kwa sababu haifuati utaratibu mzuri jambo fulani kama linatakiwa utekelezaji ufanyike toka mwanzo. Isiwe linaamuliwa tu na watu wachache na kisha kuwapelekea watekelezaji kama amri. Matokeo yake huwa kinyume cha matarajio. Kwa mfano, shughuli za maendeleo, viongozi Serikalini wanabuni jambo zuri bila kuwaelemisha/elekeza huenda tu kuwaambia wananchi wafanye. Wao kwa vile wana utashi, hujikuta wamedharauliwa. Hatima ya yote mpango ule huwa batili.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika vipengele vifuatavyo; Ikulu, TAKUKURU, MKURABITA na *TASAF*.

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi kabisa nampongeza Rais wa awamu ya nne kwa uamuzi wake wa kuanzisha Sheria ya Gharama za Uchaguzi, hii imeleta maana halisi ya kuwa Tanzania ni nchi ambayo haijengwi kwa matabaka. Sheria ya Gharama za Uchaguzi imewezesha watu maskini kushiriki kwa usawa katika zoezi la kidemokrasia yaani uchaguzi. Naomba jitihada ziongezeke, nchi hii kabla ya sheria hii ilikuwa imebaki ya wenye pesa (mafisadi). Hakika Mheshimiwa Kikwete ametuokoa, nampongeza sana na mimi ni tunda la jitihada zake wala nisingethubutu hata kuchuka fomu.

Mheshimiwa Spika, TAKUKURU inafanya vizuri sana, iongezewe nguvu isiogope wakubwa kwenye suala la kusimamia pembejeo. Viongozi wakubwa wanatusaliti hasa ma-*DC* wanawakingia vifua watumishi wanaochakachua vocha bila shaka kwa manufaa binafsi, hili liangaliwe kwani linarudisha nyuma jitihada za Serikali ya Mheshimiwa Kikwete kuinua wakulima.

Nashauri kuwa TAKUKURU ipewe meno yaani isimwachie *DPP* kupeleleza kesi zake. Kesi zinazoibuliwa na TAKUKURU zimalizwe na kupelelezwa na TAKUKURU vinginevyo kazi nzuri ya TAKUKURU inahujumiwa na *DPP* na ndugu zangu wana TAKUKURU wanakufa moyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu MKURABITA jitihada zinasuasua mno, dhamira ni nzuri lakini kule kijijini vijiji vyote vya Nkasi Kusini hakuna hata dalili za kumwezesha mwananchi ajue nini MKURABITA. Naomba dhamira nzuri za MKURABITA upewe mkazo na utafsiriwe kwa utekelezaji kwa maskini walioko kule vijijini.

Mheshimiwa Spika, awamu ya kwanza ya *TASAF* ilifanya vizuri, ilisimamiwa vizuri kwa sasa inanufaisha watumishi wanaosimamia, mfano kule Nkasi Kusini watumishi wa *TASAF* wanasimamia ujenzi wa barabara, madaraja, ukarabati na ujenzi wa madarasa na zahanati. Badala yake wamekuwa wakiwarubuni wananchi waliopo kwenye kamati ya usimamizi kwa kuwapa visenti kidogo na kushindwa kusimamia kazi. Maafisa hawa wanasimamia kazi ambazo hawajazisomea na kuwaacha ma-*engineer* bila

kuwashirikisha, kilichotokea miradi karibu yote hasa Nkasi Kusini haina thamani inayolingana na fedha iliyotumika, ni aibu. Naomba maelekezo na usimamizi wa karibu kwa viongozi hawa na ikiwezakana wafilisiwe mali ambazo wamelimbikiza kwa kuhujumu miradi ya *TASAF*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba, nawapongeza wataalamu wako kwa kazi nzuri wanayofanya kumsaidia Mheshimiwa Waziri. Ofisi ya Raisi Ikulu, nashukuru mandhari ya eneo la Ikulu inapendeza kwa upandwaji maua na kuzuia uegeshaji wa magari katika maeneo ya Ikulu kwa ajili ya usalama lakini ni pamoja na ile heshima ya eneo la Ikulu.

Mheshimiwa Spika, katika siku za nyuma gari alilotumia Mheshimiwa Rais lilipata hitilafu akiwa njiani ikiwemo ni pamoja na kuchakachuliwa kwa gari lake kwa kuwekewa mafuta yaliyochanganywa na mafuta mengine, nashauri magari ya viongozi (Serikali) yatumie/yachukue mafuta kutoka Bohari kama ulivyo utaratibu. Usalama wa Rais wetu ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Ofisi ya TAKUKURU chini ya *CEO* Dkt. Edward Hosea kwa kazi nzuri sana inayofanya. Nikuombe ufanye utaratibu wa kuwahamisha Maofisa wa Mikoa na Wilaya waliokaa muda mrefu sehemu moja, wengine wamekaa kwa zaidi ya miaka kumi kwa kukaa muda mrefu sehemu moja hujenga mazoea ya kujuana na kumfanya mtendaji huyo asifanye kazi yake kwa mujibu wa kazi yake.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nikuombe uangalie uwezekano wa kuwapelekea vitendea kazi hasa Wilaya ya Kwimba. Kwimba ina Majimbo mawili Sumve na Kwimba, kutoka Mwemushimba kwenda kijiji cha Nyanhonge ni zaidi ya kilomita 200, hivyo Ofisi ya TAKUKURU kuwa na gari moja. Utendaji kazi wa kwenda kufuatilia matukio huwawia vigumu. Najua ufinyu wa Bajeti wa ofisi yako, naomba angalau wanunuliwe pikipiki zinazoweza kumudu maeneo ya Kwimba.

Mheshimiwa Spika, wizi wa mali za umma. Naiomba TAKUKURU, Tume ya Maadili na *CAG* wafuatilie nyendo za viongozi wanaotumia nafasi zao kuliibia Taifa kwa kujinufaisha, kujitajirisha na kulifanya Taifa kutosonga mbele katika maendeleo. Tunawajua, TAKUKURU inawajua Tume ya Maadili inawajua, Ofisi ya *CAG* inawajua kwa majina lakini kuna kigugumizi cha kuwachukuliwa hatua, viongozi inafikia hatua ya kushindwa kujaza fomu za maadili zilizoko kwenye Katiba ya nchi na hatua zimetajwa lakini kigugumizi kimewakamata miguuni na midomoni, mnashindwa kuchukua hatua dhidi yao. Lakini kama hilo halitoshi maafisa hao wamejilimbikizia mali wanaporomosha majengo, wananunua magari yenye fahari kubwa, mbaya zaidi hawalipi kodi inayotakiwa, wanakula/wanaiba fedha yetu ya walipa kodi, basi walipe kodi kwa biashara zao. Naomba Waziri wakati anahitimisha hotuba yake aniambie ni Wabunge wangapi hadi sasa hawajajaza fomu za maadili na ni akina nani, na wamechukuliwa hatua gani?

Mheshimiwa Spika, inasikitisha vyombo vyetu vikubwa vinaona yanayofanywa ya kuliibia Taifa mali zake lakini nyie mmekaa kimya tu hata baada ya kupata taarifa za maandishi au kuona kwa macho yenu, fanyeni kazi zenu mliokoe Taifa hili linalozidi kuibiwa. Fedha tunazopitisha hapa Bungeni zingeelekezwa kwenye miradi ya maendeleo tungekuwa mbali mno kimaendeleo, fanyeni maamuzi. Hivi kweli twiga anaweza kupakizwa kwenye ndege bila taarifa? Wakubwa nyie, ni kweli hamjui anayehusika na mpango huo wa utoroshaji?

Mheshimiwa Spika, nidhamu kwenye Ofisi za Serikali imepungua sana hasa upande wa Makatibu Muhtasi tofauti na ilivyokuwa zamani katika utunzaji siri za ofisi. Pamoja na utandawazi kwenye dunia hii lakini kwetu imezidi kwani siri za Serikali zimekuwa zikizagaa hovyo kwenye vyombo vya habari na hata humu Bungeni. Baadhi ya Wabunge kujidai kupata barua/waraka wa siri toka hata ndani ya Baraza la Mawaziri ambalo mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Rais. Hii ni mbaya sana. Je, Serikali imeshawachukulia hatua gani watu wa aina hiyo baada ya kubainika? Naomba nijibiwe na Waziri kwani ikiendelea kuachiwa itapelekea kusambazwa kwa taarifa za kiusalama/Jeshini. Naiomba Serikali ili kuondoa usumbufu kwa wananchi kama alivyosema Mheshimiwa Rais hivi unashindwa nini kumjibu mtu aliyekuandikia barua kuhusu kitu alichoomba hata kwa mistari miwili? Tuondoe urasimu, tujibu barua hata kama haitampendezesha mhusika.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendelo ya Jamii *TASAF*. Tunaishukuru sana Serikali kwa awamu zote mbili yaani *TASAF I* na *TASAF II* ambapo nasikia kutakuwa na *TASAF III*. *TASAF* imesaidia sana kuboresha majengo ya shule, zahanati, barabara na kuimarisha vikundi mbalimbali. *TASAF One* ilipoanza ilionyesha mafanikio makubwa sana hasa katika jimbo langu la Sumve, semina zilieleweka sana kuanzia ngazi ya wilaya hadi waibuaji wenyewe. Usimamizi wa miradi ulikuwa mzuri utumiaji wa fedha ulikuwa wa uhakika tofauti na sasa hali iliyopelekea baadhi ya miradi kutokamilika kutokana na fedha kuchelewa hali iliyosababisha gharama kuongezeka.

Nashauri ni bora kuwe na miradi hiyo ikamilike kwa wakati, miradi inapokaa miaka mitatu bila kukamilika haileti maana. Lakini siyo vibaya tathmini ya kweli ikafanyika kabla ya kuanza *TASAF III* kwani mazingira ya *TASAF I*, *TASAF II* na baadaye *TASAF III* yanatofautina. Naomba nimpongeze ndugu Swai msimamizi wa miradi ya *TASAF* Wilaya ya Kwimba kwa kazi nzuri sana anayofanya.

Mheshimiwa Spika, mishahara hewa na wafanyakazi hewa. Nimesema kuwa nchi yetu kutokuwa na mapato yake kama yangeelezwa pale palipolengwa basi, tungekuwa tumepiga hatua kubwa mno. Mheshimiwa Hawa Ghasia, suala la wafanyakazi hewa ni Wizara/Idara gani inaongoza kwa kuwa na wafanyakazi hewa na wanalipwa mishahara. Je, ni hatua gani zimechukuliwa dhidi yao? Takribani miaka mitano iliyopita ni mishahara ya watu hewa shilingi ngapi zililipwa? Hapo naomba nijibiwe, la sivyo nitasimama kwenye vifungu nisipojibiwa, pesa zilizokwapuliwa na wajanja kulipa mishahara zingeweza kwa njia moja au nyingine kulipa au kuongeza mishahara kwa watu wa chini au kuongeza ajira na kuondoa upungufu wa watumishi katika kada fulani.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri naunga mkono hoja na nikutakie kila la kheri na Wizara yako kwa pamoja na wanaokusaidia, lakini nasema nchi ni yetu sote tukiamua tutaijenga vilevile tukiamua vibaya tutaibomoa, hatutaki wabomoaji wanaojulikana wasiotaka kufuata Utawala Bora, Utawala wa Sheria, Sheria na taratibu zichukue mkondo wake, tusioneane aibu wametosha kujilimbikizia mali.

**MHE. JADDY SIMAI JADDY:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza kwa dhati Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia kwa hotuba yake nzuri aliyoiwasilisha leo hii. Pia napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza wapigakura wangu wa Jimbo la Mkwajuni kwa uamuzi wao wa busara wa kunichagua mimi ili nije niwawakilishe katika chombo hiki. Nami nawaahidi kwamba nitatumia muda wangu wote wa kipindi cha uhai wa Bunge hili kwa kuwatumikia ipasavyo na hivyo nawaambia kwamba sitowaangusha.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nichangie katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejiment ya Utumishi wa Umma katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mpango wa kurasimisha rasilimali na biashara za wanyonge Tanzania. Serikali kufikiria suala hili kwa kweli kuwa ni hatua mojawapo ya uwezeshaji wananchi kiuchumi pia kufanya kuwa ni mkakati maalum wa kuongeza fursa za ukusanyaji wa mapato ya nchi yetu. Wasiwasi nilionao katika mpango wa MKURABITA ni kwamba mpango huu wananchi na hasa wale wa vijijini. Kwa mfano upande wa Zanzibar watakaokuwa wanauelewa kwa undani mpango huu basi watakuwa ni watu wachache sana hasa hasa wale waliobahatika kuingia moja kwa moja ndani ya Taasisi inayoshughulikia mpango wenyewe, lakini kwa wananchi wengi mpango huu haufahamiki. Hivyo ni vyema mpango huu ili uweze kufanikiwa basi ni lazima kuanzishwe utaratibu maalum wa kuenda moja kwa moja kwa wananchi na kuelezea dhana nzima ya mpango huu kwa kuwa naamini kufanya hivyo ndivyo kutakavyowezesha kufikia malengo halisi yaliyokusudiwa na mpango huu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)*, Mfuko huu umeonyesha dalili nzuri za kuwakomboa wananchi kiuchumi isipokuwa unaonekana kuzidiwa sana na maombi yanayowasilishwa mbele yake. *TASAF* ni Taasisi muhimu sana katika Taifa letu, lakini inasikitisha kuona kwamba Taasisi hii bado mpaka hivi sasa haijawekwa kisheria na hivyo kufanya baadhi ya wakati Ofisi hii kuendesha shughuli kwa mtindo wa kinyemela kwa kuogopa kubanwa na baadhi ya sheria za nchi. Hivyo ili kuifanya Taasisi hii ifanye kazi zake ipasanvyo ni lazima kwanza iwepo kisheria na kisha Serikali nayo ielekeze nguvu zake katika mfuko huu kwa kuwa ni mmojawapo wa mifuko ambayo majimbo yetu yanautegemea hasa katika suala la kusukumwa mbele miradi mingi ya maendeleo yanayoanzishwa katika majimbo husika. Hivyo naiomba Serikali kupitia Wizara inayohusika na mfuko huu, kutoa kipaumbele zaidi kwenye mfuko huu na hivyo kuweza kusaidia kwa asilimia kubwa utekelezaji wa ahadi za maendeleo zinazotolewa na viongozi wetu mbele ya jamii inayohusika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kwa maandishi. Nianze kwa kuwashukuru Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, kwa hotuba nzuri zilizowasilishwa kwa umakini mkubwa. Ninatamka kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naipongeza TAKUKURU kwa kazi nzuri inayofanya katika mazingira magumu. Kazi zinazotekelezwa na chombo hiki zinaonekana wazi wazi. Nashauri Serikali iendelee kukiimarisha chombo hiki kwa kukitengea fedha za kutosha ili kazi zake ziendelee kushamiri. TAKUKURU iendelee kuajiri vijana wasomi katika fani mbalimbali na wapewe mafunzo ya kutosha na waendelee kunolewa na hasa kwenye eneo muhimu la uchunguzi. Uchunguzi makini ndio utakaowezesha kesi za rushwa zinazofikishwa mbele ya vyombo vya sheria kufanikiwa na watuhumiwa kutiwa hatiani. Uchunguzi ulio makini ni sawa na kukubali kushindwa kesi hata kabla kesi haijaanza.

Mheshimiwa Spika, pale ambapo TAKUKURU inafanya uchunguzi na uchunguzi umekamilika bila ya kuwa na ushahidi wowote dhidi ya mtuhumiwa ajulishwe kuhusu matokea ya uchunguzi na umma ufahamishwe kuwa jalada limefungwa kwa kukosa ushahidi hata kama hatua hiyo haitawafurahisha wengi.

Mheshimiwa Spika, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma katika hotuba yake (ukurasa wa 11 aya ya mwisho inayoendelea hadi ukurasa wa 12) ametoa madai ambayo yanakinzana na ukweli uliotolewa tarehe 8 Novemba, 2010 kupitia vyombo vya habari kwamba uchunguzi wa pamoja uliofanywa na TAKUKURU kwa kushirikiana na *SFO* hakupata ushahidi wowote unaomuhisisha aliyekuwa Mwanasheia Mkuu wa Serikali wa wakati huo na tuhuma ya rushwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua ukweli huo, naiomba Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Utawala Bora, ilieleza Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla kuhusu matokeao ya uchunguzi huo ili kukata mizizi ya fitina. Iwapo Kambi ya Upinzani ina ushahidi mpya unaonyesha kuwapo kwa rushwa katika mchakato mzima wa ununuzi wa rada basi nawashauri wawe wepesi katika kuukabidhi ushahidi huo TAKUKURU badala ya kuja kulalamika Bungeni. Sisi kama viongozi wa wananchi lazima tuwe mstari wa mbele katika kulinda na kutetea Utawala wa Sheria *(rule of law)* ambao ni *component/ingredient* muhimu wa Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kama nilivyoanza kwa kusema naunga mkono hoja hii.

**MHE. DKT. SEIF S. RASHID:** Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali katika kuwasilisha Bajeti na hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu. Kwanza nianze kwa kuchangia eneo la mgawanyo wa rasilimali watu baina ya maeneo katika wilaya moja na katika kata kwa mtazamo usiofichuka kuwa pamoja na idadi ndogo/isiyotosha ya

watumishi lakini kwenye maeneo ya miji imepangiwa watumishi wengi kuliko mahitaji yao na kufanya maeneo ya vijiji kukumbwa na upungufu mkubwa wa watumishi. Maeneo hayo ya kazi ni pamoja na shule za misingi na sekondari, zahanati na vituo vya afya na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, mishahara hewa ni changamoto ya kila mwaka kuwa inatokea na Serikali imekuwa ikijaribu mifumo mbalimbali ya kudhibiti hili hii bila ya mafanikio. Inasikitisha kuona katika karne ya 21 ya ulimwengu wa *TEHAMA* kushindwa kudhibiti hili. Naishauri Serikali kuharakisha zoezi la utoaji wa vitambulisho vya uraia na mfumo wake ili uweze kutumika katika kudhibiti hilo na mengine mengi kwa kufanya mfumo wa vitambulisho uwe wa sifa zifuatazo:-

Kwanza uunganishwe na mifumo mbalimba ya takwimu na taarifa za maeneo ya ajira au vituo vya kazi, mifumo ya kodi, leseni, umiliki wa rasilimali mbalimbali; na mifumo ya usajili wa vizazi na vifo bila ya kuvuja kwa takwimu hizo kwenye mikono hatari. Usalama wa mfumo ndio cha msingi zaidi.

Pili, kuunda chombo kitakachokuwa na uwezo wa kuhakikisha kasoro/makosa ya kielektroniki na ulipaji wa mishahara hewa kwa kutumiwa mfumo unavyounganisha mifumo mbalimbali na kutoa taarifa kwa madhumuni ya udhibiti wa makosa mbalimbali ikiwa ya ulipaji wa mishahara hewa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na naunga mkono hoja.

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Mheshimiwa Spika, naomba na mimi nichangie kwa maandishi katika hotuba hii kama nilivyoanisha hapo juu. Naomba nichangie katika suala la kutoa huduma bora. Baadhi ya wafanyakazi wanakuwa wanasubiri mishahara tu lakini hawatoi huduma bora kwa wanaoenda katika eneo la kazi, mfano kumekuwa na wakati mgumu sana kwa wananchi wanaohitaji kuwaona viongozi wa juu ambao wanaona wangeweza kuwaeleza matatizo yao lakini kunakua na uzito/ugumu wa hali ya juu katika kufanikisha hilo na hivyo wananchi wanabaki na matatizo yao mioyoni na kusababisha hata wengine wachukue hatua ambao hawakuzitegemea kuzifanya. Napendekeza wafanyakazi husika wawasikilize wananchi na kuwasaidia inavyopaswa na sio wao wenyewe kujiamulia wanavyotaka.

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kuongelea suala la uhamisho kwa watumishi. Kumekuwa na tabia ya kuhamisha wafanyakazi toka sehemu moja ya kazi kwenda nyingine aidha, kwa nia njema au mbaya. Nasema hivi kwa sababu kuna baadhi ya viongozi wamekuwa wakifanya hii kwa ajili tu ya kumkomoa mhusika kutokana na sababu anazozijua yeye. Hii inasababisha maambukizi ya Virusi vya UKIMWI kuongezeka kwani kwa wanandoa wanapata mianya ya kuwa na wenza wapya na pia Serikali haisaidii kujenga familia bora bali bora familia kwa kuwatenganisha baba na mama pamoja. Nashauri Serikali iwasikilize wale wenye ndoa pindi wanapoomba hivyo kwani itaongeza hata ufanisi wa kazi kwa kuwapunguzia mawazo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, lipo tatizo kubwa la ajira kwa watumishi wa kada za chini katika Halmashauri zetu. Baadhi ya vijiji na kata hazina watendaji. Hoja ambayo inatolewa katika Halmashauri ni kwamba hawajapata kibali kutoka Idara Kuu ya Utumishi.

Mheshimiwa Spika, watendaji hawa ndio wasimamizi wakubwa wa miradi na shughuli zote za maendeleo kwa wananchi. Naishauri Serikali kwamba ni vema kazi ya kuajiri watumishi kama *WEOs, VEOs* wahudumu na madereva iachwe au ifanywe katika Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni watendaji wengi ambao wanakaimu nafasi zao na wale ambao wana mashauri. Kitendo cha watumishi kukaimu kwa muda mrefu kinawafanya watumishi kutowajibika na kuongeza uwezekano wa ubadhilifu wa mali za umma. Nashauri kwamba muda wa kukaimu upunguzwe na nafasi ambazo watendaji wake wamedhihirika kufanya vema wathibitishwe kazini.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo mashtaka na kesi za watuhumiwa ambao ni watumishi zinachukua muda mrefu sana. Hali hii inalifanya Taifa kupoteza fedha nyingi kutokana na watuhumiwa kulipwa wakiwa wanasubiri uamuzi wa kesi zao. Vilevile nashauri baadhi ya watumishi wastaafishwe kwa manufaa ya umma badala ya kuwashtaki na kuendelea kuwalipa.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kuzungumzia maslahi, posho pamoja na kupandishwa vyeo walimu wetu. Katika Jimbo la Rombo wapo walimu ambao tangu mwaka 2005 bado hawajapandishwa madaraja na au kuthibitishwa kazini. Naiomba Serikali kumaliza tatizo hili. Sambasamba na hilo matatizo ya walimu vilevile yanawakumba walimu wapya ambao Halmasharui bado haijawalipa baadhi ya walimu fedha zao za kusafirisha mizigo kutokana na sababu mbalimbali. Namuomba Waziri wakati wa majumuisho kutoa kauli kuhusu jambo hili.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia suala la ubaguzi katika jamii ambalo linaanza kujitokeza litolewe kauli. Hivi sasa baadhi ya viongozi wanawaorodhesha wananchi ili kuwapatia chakula cha njaa au pembejeo za kilimo kwa kuwataka kuonyesha kadi zao za vyama au zile za kupigia kura. Naomba Serikali iseme kama huu ni utaratibu au ni uvunjifu wa sheria, jambo hili linaendelea sasa katika Jimbo la Rombo.

Mheshimiwa Spika, mwisho ningependa kuchangia kuhusu wataalamu wetu ambao wanatoka nchini kwenda kufanya kazi nje ya nchi hasa katika nchi za *SADC* kama Zimbabwe, Lesotho,Afrika Kusini na kadhalika. Watumishi wanaohama kwa wingi ni walimu, madaktari pamoja na manesi na mainjinia.

Mheshimiwa Spika, kwa vyovyote wanaondoka wanakwenda kutafuta maslahi na wala sio kukosa uzalendo. Naishauri Serikali kwanza ifanye tathmini ya Watanzania wangapi ambao wanafanya kazi nje. Ichunguze pia mafao ambayo wanapata huko na lishe, kutengeneza *insetive scheme* ambayo itawavutia kurudi nyumbani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nashukuru na naomba kuwasilisha.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, chombo cha dola (Polisi) hakitendi haki kwa wanyonge, mimi mwenyewe nimeshuhudia kabisa kitengo cha Polisi Dar es Salaam wakati wa tatizo la kesi ya Ndugu Chenge ya *traffic police* walimkamata mmiliki wa bajaji aitwaye Majid na kumwekwa ndani lakini aliyesababisha ajali hakuwekwa ndani hata siku moja, mimi nilijitahidi kumwekea dhamana Majid bila mafanikio yoyote ile hata baada ya kutoa *photocopy* ya *driving lisence* ya dereva wa bajaj aliyekimbia baada ya ajali ambayo ilitoke saa 10 za asubuhi. Wakati mmiliki huyo alikuwa nyumbani kwake amelala, mimi katika jitihada za kutaka kumwekea dhamana nilishangaa sana polisi wananijibu hilo ni suala la kisiasa sasa kesi ya *traffic* inakuwa kesi ya kisiasa, nilijitahidi mpaka kufika kwa Kamanda wa Kanda Maalum alinikatalia katu katu kabisa sasa huo ni Utawala Bora au Bora Utawala?

Mheshimiwa Spika, wakati huo mimi sikuwa Mbunge na hayo ndiyo wanaofanyiwa watu wengi hasa vijijini, kama Dar es Salaam ni hivyo mwenye cheo au mwenye pesa anathaminiwa hata kama anahatia kama hiyo hapo hayo niliyoeleza ni kweli tupu, hata jina langu lipo polisi Oysterbay kushughulika kwa huyo kijana alvyoonewa na mpaka sasa hawajalipwa hiyo bajaj yake. Ilihali mhusika ameahidi kumlipa huku anamzungusha na hana kilichomsaidia kwa maisha na hana hatia yoyote ile. Je, huo ndio utendaji wa Jeshi la Polisi na Utawala Bora?

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Mchango wangu kwa muhtasari naomba kuchangia na kushauri hoja zifuatazo:-

Kwanza ni kuhusu Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ajira isifanyike Dar es Salaam tu, nafasi za kazi za ngazi ya chini zifanyike katika ngazi za Wilaya na Halmashauri au Mkoani. Pia ufanyike utafiti wa nchi yetu hasa katika utumishi wa umma kufanyakazi kwa utaratibu wa mkataba. Badala ya utaratibu wa sasa wa kudumu ambao unafanya uwajibikaji usiwe mkubwa. Watumishi wasihamishwe, wawajibike katika maeneo ya ajira zao yaani Halmashauri, Wilaya, Mkoa na Wizarani kuhamisha watumishi, kumedumaza utendaji na kushamiri kwa rushwa. Pia mishahara iangaliwe kwa kina cha ndani kutafuta ulipwaji mishahara kutegemea uzalishaji wenye tija.

Mheshimiwa Spika, suala la utawala bora. Mfumo wa TAKUKURU uangaliwe kwa kina. Mamlaka ya viongozi wake wa juu na utaratibu wa kuwahoji na kuwadhibiti urekebishwe. Kwa sasa kufanya kazi kama miungu watu. Upo ubadhilifu na matumizi mabaya ya madaraka katika TAKUKURU. Pia TAKUKURU iimarishwe usimamizi wa kesi Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Maadili iimarishe Ofisi zao Mikoani/Wilayani kuepuka usimamizi hafifu na ufuatiliaji usio na tija kama inavyotokea sasa katika migogoro ya ujazaji fomu za matamko ya mali za viongozi.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mipango, *TASAF* na kadhalika, usimamizi wa mpango wa maendeleo ya miaka mitano uliopitishwa na Bunge hivi karibuni ni budi ufanyike kwa umakini mkubwa sana. Iundwe Benki ya Maendeleo ambayo itasimamia fedha zote zitakazopatikana kwa kutekeleza mpango kikamilifu. Riba katika taasisi ya mfuko wa Rais iangaliwe na *TASAF* iimarishwe na iratibiwe utendaji wake mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri katika Ofisi ya Rais kwa kuandaa hotuba nzuri na kazi kubwa waliyoifanya ya kuandaa hotuba hiyo na Kamati husika bila kusahau wadau wote walishiriki katika maandalizi ya Bajeti hiyo, hongereni sana na naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na suala zima la elimu yaani ajira ya walimu. Walimu wa sasa ni hodari kwa kujitafutia nyongeza za elimu. Nawapongeza walimu, Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi imetekeleza ilani kwa kuanzisha shule nyingi za sekondari. Hayo ni maendeleo makubwa kwa Taifa letu. Lakini panapo mazuri hapakosi kuwa na mabaya zipo changamoto nyingi ambazo zinawakabili walimu ikiwemo zifuatazo:-

Kwanza, walimu wanapojiendeleza kurekebisha mishahara yao inachukua muda mrefu na maana nyingine wengine hawarekebishiwi kabisa.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kweli walimu wanaotaka kujiendeleza ni wengi lakini hawawezi kwenda wote. Inabidi waende kwa awamu. Tatizo linalojitokeza hata pale wanapopata fursa bado hawapatiwi fedha za ada ya chuo. Matokeo yake ni kujaza malimbikizo ya madai. Je, Serikali itafanya mkakati gani kuepuka balaa la malimbikizo ya madeni kwa walimu?

Mheshimiwa Spika, tatu, suala lingine linahusu *course* zinazochukuliwa na watumishi. Watumishi wanaambiwa wachukue kozi zinazoendana na ajira zao. Mfano, walimu wa daraja B, A na *Diploma*, *Masters of Education*, *Adult Education* na *Special Education*.

Mheshimiwa Spika, naomba nishauri Serikali yetu iliangalie Taifa kwa mtazamo mwingine kwani kuna mabadiliko makubwa katika dunia na hasa katika mfumo mzima wa elimu. Kuna kozi mpya nyingi ambazo zinamfaa mwalimu na zikaleta manufaa makubwa kwa Taifa. Mfano, *computer science, guidance and conselling, cultural heritage* ambayo ime-*specialized* katika historia ya Tanzania. Kozi zote hizo na nyingine nyingi zinaweza kufanywa kwa mwalimu. Hivyo basi ni vyema Serikali yetu ikaenda na wakati si kung’ang’ania mambo ya zamani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Spika, hakuna Serikali isiyokuwa na utumishi wa umma na binafsi pia. Ningependa katika Wizara hii kuishauri Serikali katika suala la ajira iliangalie upya. Serikali yetu inaongozwa kwa sheria, kanuni na taratibu hivyo tuzifuate. Kuwepo na utaratibu mzuri wa kuajiri, kuwepo na mikataba maalum ili pia kuwawezesha vijana waliomaliza vyuo vikuu na wamefaulu vizuri waweze nao kuajiriwa pasipo kuwawekea masharti magumu sana kama vile *experience* ya muda mrefu. Huyu kijana kamaliza tu Chuo Kikuu, *experience* ya muda mrefu ataitoa wapi? Watabaki tu wazee makazini na ufanisi wa kazi kushuka kwani watakuwa wanafanya kazi tu kwa mazoea bila kuwa na nidhamu/maadili kazini. Muda wa *experience* upunguzwe.

Mheshimiwa Spika, mtumishi akifanya makosa, utaratibu wa kumpa adhabu kama onyo la mdomo, maandishi, kusimamishwa ama kuachishwa kazi. Uhamisho sio tija ni kulea ubovu kwani huko atakapohamishwa ataendeleza huo ugonjwa. Katika kustaafu kazi muda ukifika, wastaafu wasiongezewe muda wa mikataba kwani haileti mantiki hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, katika Ofisi ya Rais, Utawala Bora; TAKUKURU wapewe meno ya kuendesha kazi zao kwa ufanisi zaidi bila shinikizo lolote, viongozi mbalimbali waipe meno taasisi hii ili ifanye kazi zake *independently* ili iweze kuzaa matunda bora. Ikifanya kazi *indepently and professionally* itatakiwa waonyeshe *results* (matokeo), wasipofanya hivyo inakuwa ni rahisi kuwafanya wawe *accountable*, hii itawapa ari na nguvu zaidi ya kufanya kazi kwa maadili zaidi. Matatizo mengi tuyaonayo leo kama vile ununuzi wa rada, *Richmond, EPA* na kadhalika yasingefika hapa yalipo na kuwa ni ajenda ya wananchi endapo taasisi hii ingefanya majukumu yale *professionally and ethically from the beginning.*

Mheshimiwa Spika, suala hili la rada ningeshauri lijadiliwe Bungeni kwa uwazi kama wawakilishi wa wananchi ili kujenga taswira nzuri kwa wananchi tunaowawakilisha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ABUU HAMOUD JUMAA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mungu, mwingi wa rehema, kwa kuniwezesha kupata nafasi ya kuchangia hoja ya Bajeti ya Ofisi ya Rais (Menejiment ya Utumishi wa Umma). Bajeti hii inawapa matumaini makubwa watumishi wa umma kwa kuwa ustawi wao umepewa kipaumbele ili nao waweze kutekeleza majukumu yao si kwa kufata misingi ya sheria na taratibu za kazi tu, bali kwa moyo wenye ari, weledi na maadili mema utakaopelekea utendaji kazi wao katika kutoa huduma kwa wananchi, kuleta tija na mafanikio makubwa katika maendeleo ya nchi yetu. Kama Bajeti hii itatekelezwa kama ilivyo basi wananchi na wadau mbalimbali tutegemee utumishi uliotukuka na huduma bora zenye tija kwa wakati kuafaka.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma) kwa Bajeti nzuri iliyoandaliwa kwa kujali maslahi

ya wafanyakazi wa kada zote. Kwa mfano, huu utaona kwamba kodi ya pango na usafiri kwenda na kurudi kazini ni zaidi ya mshahara wa mfanyakazi huyu na bado mahitaji mengine ya lazima kwa maisha ya binadamu ya kila siku hayawezi kutekelezwa kwa mshahara huu. Sasa kweli mfanyakazi huyu mwenye shida na kipato duni, ataweza kufanya kazi yenye tija? Je, ataweza kutoa huduma kwa umakini na amani? Je, mfanyakazi huyu hawezi akashawishiwa kuvunja maadili au kufanya vibarua na mambo mengine nje ya ajira yake? Je, mfanyakazi huyu akishawishiwa hawezi kuanguka kwenye mtego wa kuomba rushwa ili apate fedha zaidi za kumuwezesha kujikimu na mahitaji ya familia yake?

Mheshimiwa Spika, kutokana na maslahi duni, nchi yetu imekuwa inapoteza wataalamu wengi katika fani ya Udaktari, Uhandisi, Maprofesa na kadhalika, wanaondoka kwenda kufanya kazi katika nchi za nje kutafuta maslahi bora katika mishahara mizuri, maisha bora na huduma bora. Wataalamu hawa wanapoondoka wanaacha pengo kubwa linaloathiri sekta ya huduma.

Mheshimiwa Spika, suala la kupandisha wafanyakazi vyeo lifanyike kwa haki na kwa wakati unaostahili. Ninaamini ukifanya sensa kwa watumishi wa umma utakuta kuna baadhi wamechoka na wanafanya kazi ili mradi kwani wamekaa muda mrefu au hata kupelekwa katika mafunzo ya kuwaendeleza taaluma za pale walipo. Kwa kuwa tatizo hili ni sugu zaidi kwa wafanyakazi wa vijijjini, hii imepelekea hata waajiriwa wa ajira ya kwanza wanapopangwa kwenda kufanya kazi vijijini, hawaendi kwa kuogopa kudumaa katika taaluma zao, na kuendelea kuishi katika maisha duni. Katika Bajeti ya mwaka huu, nahimiza ilenge katika kutoa kipaumbele kwa wafanyakazi walioko vijijini. Wafanyakazi hawa wapewe mafunzo na pia wale wanaostahili au waliokaa muda mrefu bila kupandishwa vyeo, wapandishwe vyeo ili wawe na moyo wa kujituma katika huduma na kuwa kichocheo na kuwapa matumaini Watumishi watakaoajiriwa na kupangwa kufanya kazi maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli maisha ya vijijini ni magumu. Napendekeza kuwe na mipango ya kuwapongeza na kuwapa tuzo watumishi hasa wale wa vijijini ambao maeneo yao ya huduma yatakuwa yanafanya vizuri katika huduma. Kwa mfano, tumeona hapa Bungeni wanafunzi waliofanya vizuri katika masomo yao ya kumaliza kidato cha nne na sita wakizawadiwa na kupewa tuzo na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kati ya wanafunzi hao, sita wanatoka katika shule za kata ambazo zipo vijijini na zinasemekana hazina vifaa vya kutosha, walimu waliofundisha wananfunzi hawa nao wangepewa motisha ili waongeze moyo katika kufundisha.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Kibaha Vijijini ni moja ya Majimbo ambayo hayana vivutio kwa wafanyakazi kwa kuwa uchumi wake ni mdogo na maendeleo finyu. Hakuna huduma za barabara safi, maji safi na salama, umeme, hospitali, shule zenye mandhari nzuri, vifaa, mabweni ya wanafunzi na hata nyumba za watumishi wanaopelekwa kufanya kazi kule. Kwa hali hii utaona kwamba wafanyakazi wanaotoa huduma katika Jimbo la Kibaha Vijijini wanafanya kazi kwa hali ngumu sana. Hali hii duni ya huduma za jamii, imepelekea watumishi wengi wanaopangwa katika Jimbo hili ama kutofika

kabisa kuripoti katika vituo vyao walivyopangiwa kufanya kazi au kufika kuripoti na kuondoka.

Naomba sana wakati wa utekelezaji wa Bajeti ya mwaka huu, Jimbo la Kibaha Vijijini liangaliwe kwa jicho la huruma ili kuwawezesha wafanyakazi waishi vizuri na waweze kufanya kazi kwa umakini bila msongo wa mawazo kutokana na kukosa huduma muhimu, maslahi duni na hali ngumu ya maisha. Naamini kwa kuboresha maslahi na huduma za jamii, wafanyakazi watatumia taaluma zao na kufanya kazi kwa bidii. Kwa kufanya hivi kutahatarisha maendeleo ya Jimbo lile.

Mheshimiwa Spika, naomba Jimbo la Kibaha Vijijini lipatiwe wataalamu zaidi katika maeneo yatakayobadili maisha magumu ya wananchi wa Jimbo lile katika kuendeleza kilimo, nishati na umeme, miundombinu, biashara, huduma za jamii, elimu, afya na wachumi watakao wawezesha vijana kubuni miradi itayodhibiti ukosefu wa ajira.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba, Bajeti hii ya mwaka 2011/2012, iliyolenga kukuza uchumi na kupunguza umaskini, kwa kumboreshea mfanyakazi maslahi yake nchi itakuwa na wafanyakazi wenye kujua uzalendo wa kweli kweli wenye taaluma, itapunguza ushawishi wa migomo na maandamano. Kutakuwa na uelewa wa utawala bora, kuondokana na vitendo vya rushwa na kuwa katika maadili ya kutoa na kupata huduma. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, utawala bora na maendeleo ya watumishi kielimu pamoja na matarijio ya kuendelea kuboreshewa hali zao na maendeleo yao kazini. Bajeti hii inatekeleza kwa dhati Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo inawajali na kuweka wananchi wake mbele. Maendeleo ya Taifa letu yanategemea wakulima na wafanyakazi na si vitu, naamini kama wafanyakazi wa umma wataondolewa kero mbalimbali kwa kuboreshewa mishahara yao, kupatiwa makazi na mafao bora basi nao watakuwa na moyo wa kufanya kazi zao kwa bidii na kutoa huduma bora kwa wananchi. Hii itapunguza tamaa za kujiingiza katika kudai rushwa, kutenda kazi kufuatana na maadili na kufuata taratibu zote zinazohuzu mikataba ya ajira zao.

Mheshimiwa Spika, nasikitika kusema kwamba kima cha chini cha shilingi 135,000/= ni kiasi ambacho kwa kweli hakikidhi mahitaji ya mfanyakazi hata kwa juma moja katika mwezi. Ukichukua mshahara huu kwa maana shilingi 135,000/- ukipiga mahesabu ya mahitaji ya mfanyakazi huyu kwa mwezi utaona kwamba mfanyakazi mwenye watoto wanne anayeishi Dar es Salaam sehemu za Temeke na kufanya kazi mjini katikati yanaweza kuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa chumba kimoja = Shs. 25,000/= hadi Shs. 40,000/= anahitaji vyumba vitatu tuchukue anapanga chumba Shs. 35,000/= x 3 = Shs. 105,000/=; nauli Shs. 1,000/= kwenda na kurudi kazini kila siku x 31 = Shs. 31,000/=; chakula, mavazi, ada ya shule, matibabu, *uniform* na mahitaji mengine ya kawaida katika jamii mfano, michango ya mazishi, harusi, sherehe na kadhalika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nafurahi kusema wale wote walioomba kuchangia wamemalizika na tukirudi saa 11.00 jioni wataanza kutoa ufafanuzi wa mambo mengi mliyosema na kwa sababu kuna Mawaziri watatu, watoa hoja walikuwa wawili na kawaida anakuwa Utumishi ndiyo anakuwa mtoa hoja rasmi zaidi, wana dakika 120, wamegawana, kwa hiyo ataanza Mheshimiwa Waziri Chikawe atafuatiwa na Mheshimiwa Wasira na mwisho Mheshimiwa Hawa Ghasia.

Sasa tutakapofika kwenye mshahara wa Waziri sio kila mshahara, tutakwenda mshahara wa Waziri wa Utumishi, ndiye atakayebeba mzigo huu. Sasa tunapotaka ufafanuzi katika Kamati ya Matumizi, Kanuni ya 101(3) inasema hivi:-

*"Mbunge atakayeamua kutumia Kifungu chenye mshahara wa Waziri, ataruhusiwa tu iwapo ataomba ufafanuzi wa suala mahsusi la sera na hatazungumzia zaidi ya mambo mawili ya aina hiyo".*

Kwa hiyo, hapa siyo kila kitu, tunapokosea ni kila mtu kuuliza jambo lilelile. Kama ni suala la sera, anaweza akauliza mmoja mwingine hataruhusiwa, hatu-*repeat*. Halafu maamuzi tuliyofanya hapa, utapewa muda wa dakika tatu, utaeleza jambo lako na ni vizuri ukajipanga jambo lako liwe mahsusi moja, sio unazungumzia kila kitu. Safari hii tume-*limit* hata Waziri atajibu kwa dakika tatu, ukishauliza hapo tumeshaondoka. Hauulizi tena kwa hiyo ataenda mtu mwingine. Kwa hiyo, muondoke hapa mkijua hivyo na *vote* tutakayotumia, mshahara wa Waziri ni *Vote 32*.

Waheshimiwa Wabunge, sina tangazo lingine, naomba nisitishe shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.58 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tulipositisha shughuli mchana, tulisema sasa wataanza wahusika kujibu hoja. Kwa hiyo, sasa nitamwita Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Utawala Bora, Mheshimiwa Chikawe, dakika 35.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii na mimi nichangie hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Utumishi.

Mheshimiwa Spika, naomba na mimi nizingatie protokali ya Bunge lako Tukufu, kwa kuanza kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa nafasi hii ya kusimama leo mbele yako na kuzungumza na Wabunge wenzangu. Niwashukuru wananchi wa Nachingwea, kwa kunichagua na kunipa imani kubwa sana, kunirudisha tena katika

Bunge lako Tukufu kwa mara ya pili. Nimshukuru mama yangu ambaye ndiye mshauri mkuu wangu katika mambo ya siasa na sababu ya mimi kuwepo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze mchango wangu ambao utakuwa katika kujaribu kujibu hoja za Wabunge mbalimbali zilizotolewa kwa maandishi na wale ambao walichangia kwa kuzungumza ndani ya Bunge lako Tukufu. Nianze moja kwa moja kujadili hoja zinazohusu utawala bora. Nitazungumzia hoja mbili. Kimsingi utawala bora ni mchakato wowote ule wa utoaji wa maamuzi na utekelezaji wake katika masuala yanayohusu umma kwa maslahi ya umma. Ni jinsi vyombo vya umma vinavyojiendesha na kutumia maslahi ya umma kwa manufaa ya umma.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa, utawala bora waliuwekea misingi nane ifuatayo:-

Mheshimiwa Spika, wanasema ni utawala ambao ni *concensus oriented.* Ni utawala ambao ni *participatory.* Ni utawala ambao unazingatia *Rules of Law.* Ni utawala ambao ni e*ffective* na *wfficient,* yaani makini. Ni utawala ambao uko *accountable,* uko *transparent,* uko *responsive* na *equitable* na e*nclusive.* Vipengele hivi nane ndio hasa wanavyozingatia wanaposema kuna utawala bora, hili ni zoezi pana sana, hakuna nchi yoyote duniani inaweza ikasimama leo hii ikasema inao utawala bora kamili. Tanzania na sisi tunajitahidi sana kuzingatia utawala bora kwa kuunda Taasisi mbalimbali ambazo zinasimamia vipengele hivi vyote vya utawala bora, tunajenga *democratic institutions* ambazo zinatuhakikishia kuwa tunazingatia misingi ya utawala bora.

Mheshimiwa Spika, kubwa katika jitihada za Serikali yetu ni kujenga demokrasia thabiti ambayo itahakikisha kuwa kuna ushirikishwaji mkubwa katika maamuzi na uendeshaji wa Serikali katika kutunga, kubuni na kutekeleza sera za maendeleo, kuongeza uwazi na uwajibikaji wa viongozi na kadhalika. Kubwa la pili ni utawala wa sheria na hili nalo watu wanalisema kila siku, *rule of law* lakini *rule of law is a legal maximum* ambayo ina misingi mitatu. Msingi wa kwanza katika *rule of law* unasema, hakuna mtu yeyote aliye juu ya sheria. Msingi wa pili unasema, hakuna mtu atakayeadhibiwa na Serikali ila tu kama amevunja sheria na msingi wa tatu unasema, hakuna mtu atakayekutwa na hatia ya kuvunja sheria ila tu kwa utaratibu ambao umewekwa na sheria na hii ni dhana ya siku nyingi. Hivi majuzi, nina maana karne ya 17, ndio majuzi kisheria, ndio imepata misingi hii hasa ya *Rex Lex* badala ya *Lex Rex. Rex,* Kilatini ni Mfalme, *Lex* ni Sheria. Zamani walikuwa wanaamini kwamba *Rex Lex* yaani Mfalme yuko juu ya Sheria lakini sasa baada ya hiyo Karne ya 17, tumefikia kusema kwamba ni *Lex Rex,* Sheria *above the King,* ambayo ndio tunatumia sasa. Ndio huu utawala wa sheria, hakuna aliyeko juu ya sheria. Hilo ni la kwanza la ujumla.

Mheshimiwa Spika, la pili la ujumla ambalo limezungumzwa na watu na pengine linahitaji ufafanuzi, ni *grand corruption.* Tunazungumzia *grand corruption* lakini tunapozungumzia *grand corruption* tunamaanisha nini? Tunamaanisha kesi ambayo labda ina vipengele hivi vitano ama kimoja ama chochote katika hivi vitano. Moja, kesi ambayo ina kiasi kikubwa cha fedha, *involved a billion* na kuendelea huko, unasema hii ni *grand corruption case.* Au kesi ambayo wahusika wake ni *influential figures, public*

*figures* hata *private figures* lakini *as long as* ni *inlfuential* katika jamii, tunasema hii kesi ni *grand corruption.* Halafu kesi ambayo labda ina *public interest* kubwa, hii nayo ina-*fall* katika hiyo. Kesi hizi pia zina tabia ya kuwa na *extra-territorial*, yaani zinavuka mipaka ya nchi. Inaweza ikafanyika hapa lakini inabidi iende mbali, ushahidi wake kuupata labda inabidi tuzunguke nchi nyingine nyingi, hii nayo tunai-*classify* kama *grand corruption case* na huwa nyingi zinachukua si chini ya miaka mitano kupeleleza tu. Kesi nyingi za aina hii kwa hapa kwetu zipo, tunaendelea kuzichunguza.

Mheshimiwa Spika, sasa nianze kujibu hoja labda mojamoja kama zilivyojitokeza na nianze na TAKUKURU na suala zima la rushwa. Taarifa ya Kambi ya Upinzani Bungeni, imeeleza kwamba TAKUKURU nchini imeendelea kuonesha udhaifu katika kukabiliana na tatizo la rushwa kwa mwaka 2010/2011, kwa kurejea taarifa za utafiti wa Haki za Binadamu za mwaka 2010 na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu *(LHRC).*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nasema taarifa hiyo kwanza sio sahihi. Sio malalamiko yote yanayopokelewa na TAKUKURU ni ya vitendo vya rushwa. Malalamiko yaliyo mengi hayahusiani na vitendo vya rushwa na kwa maana hii hupokelewa na kutolewa ushauri na mengine huhamishiwa kwenye Taasisi au Idara nyingine zenye mamlaka ya kuyashughulikia.

Mheshimiwa Spika, pili, katika kipindi cha mwaka 2008/2010 kwa mujibu wa takwimu zetu zilizopo kwenye tovuti ya TAKUKURU ambayo iko wazi na kila mtu anaweza kuipata, inaonesha kwamba jumla ya malalamiko yaliyopokelewa yalikuwa ni 17,752 na sio 14,426 kama ilivyoelezwa na Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni na malalamiko yaliyohusu rushwa katika hayo yalikuwa ni 2,682. Kati ya malalmiko 2,682 TAKUKURU iliweza kuchunguza na kukamilisha majalada 2,973 kwa maana ya kwamba malalmiko yote yaliyohusika yaliyohusu rushwa kwa mwaka huu yalichunguzwa na mengine 291 ya miaka ya nyuma, pia yalifanyiwa kazi. Kwa maana ya asilimia, utaona kuwa utendaji wa TAKUKURU hapa ulikuwa zaidi ya 100% kwa kuchunguza tuhuma zote za rushwa zilizowasilishwa na kupokelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Upinzani imeendelea kudai kwamba kwa kipindi cha mwaka 2008/2010, jumla ya kesi 101 tu kati ya kesi 424 zilizofikishwa Mahakamani ndizo washtakiwa walipatikana na hatia, ambazo ni sawa na 22.2%. Nayo taarifa hii pia sio sahihi. Kwa kipindi cha 2008 mpaka 2010 jumla ya kesi zilizoamuliwa na Mahakama zilikuwa ni kesi 382 na kati ya kesi hizo 139 Jamhuri ilishinda na washitakiwa walifungwa. Kesi zilizoshindwa ni 36.4% na sio 22.2% kama ilivyoelezwa na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni. Aidha, ieleweke kwamba kesi zikifikishwa Mahakamani, kushinda au kushindwa kwa kesi kunatokana na sababu mbalimbali kama vile upatikanaji wa mashahidi kwa wakati, uendeshaji kesi unaoongozwa na taratibu zake ambazo husimamiwa na Mahakama na mambo mengine mbalimbali kama uwepo wa pande zote mbili za kesi Mahakamani. Kutopatikana kwa mashahidi kwa wakati kwa sababu mbalimbali kama vile kuhamia eneo lisilojulikana na wakati mwingine kufariki, haya yote yanafanya kesi zichelewe. Pengine nitoe ufafanuzi kwamba sio kesi zote zinazofikishwa Mahakani kwa mwaka huo, zote zitatolewa uamuzi mwaka huo. Kwa

mfano, kipindi cha 2008 mpaka 2010, kesi zilizofikishwa Mahamani zilikuwa ni 593 na sio 424, lakini kesi zilizoamuliwa kwa kipindi hicho zilikuwa ni 382.

Mheshimiwa Spika, hoja kwamba TAKUKURU imekuwa ikiacha kazi yake ya msingi ya kuzuia na kupambana na rushwa na kubaki ikifanya zaidi kazi za Idara ya Polisi za Upelelezi wa Makosa ya Jinai *(CID).* Madai ni kwamba taasisi hii imekuwa ikijishughulisha sana na rushwa ndogondogo na kuwaacha wahusika wa rushwa kubwa, mfano mzuri ni jinsi taasisi hii ilivyojaribu kuwasafisha wahusika wa kashfa ya *RICHMOND* na Rada. Hoja hii haina ukweli. Ukweli ni kwamba sheria haibagui wala kuweka makundi ya walalahoi na vigogo. Rushwa ndogo au rushwa kubwa yote ni makosa machoni mwa sheria. Tofauti ya rushwa ndogo na rushwa kubwa ni kwamba penye rushwa ndogo, ushahidi ni wa hapohapo na hauchukui muda kwa kuwa unapatikana katika sehemu ya tukio tofauti na rushwa kubwa ambazo nilizieleza hapo mwanzo, hizi *grand corruption cases,* ushahidi wake huchukua muda, *minimum* miaka mitano na huhitaji kuupata ushahidi mwingine unaotoka nje ya mipaka ya nchi na hupelekea kazi hiyo kuchukua muda mrefu zaidi.

Mheshimiwa Spika, suala la *RICHMOND* lilizungumzwa. Nasema hili limekwisha na Bunge lako Tukufu lilishawahi kutoa maamuzi yake. Kesi ambayo inabidi labda niitolee maelezo kidogo, ni hii kesi ya Rada. Kesi ya Rada imezungumzwa sana na Wabunge ndani ya Bunge hili na mimi nataka nitoe maelezo kwamba kesi hii inapotoshwa sana. Ni kweli kwamba kumekuwa na madai mengi tena mengi sana dhidi ya aliyekuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Andrew Chenge, kuhusika na kashfa ya rada.

Mheshimiwa Spika, sasa ukweli ni kwamba uchunguzi na ushahidi uliopatikana na uchunguzi huu, sisi wenyewe tuliwatafuta *SFO (Serious Fraud Offences)* wa Uingereza, waje kutusaidia kuchunguza. Wakaja, wakachunguza wakishirikiana na *PCCB* wetu. Ushahidi uliopatikana umeonesha kwamba Mheshimiwa Andrew Chenge, hakuonekana katika sehemu yoyote katika mchakato wa malipo haya ya fedha za Rada zilizolipwa na Serikali ya Tanzania kwenda *BAES (British Aerospace Services).* Waliohusika kugawana zile 31% ya fedha za mkataba huo ni kama hawa wafuatao, tunawataja leo; Shailasi Vithrani ambaye ni Dalali wa *BAES*, Christopher Nakvi ambaye ni *Sales Manager* wa *BAES* na bwana Jonathan Mc Holman ambaye ni *Commercial Manager* wa *BAES.* Hawa ni Waingereza, walihusika na rushwa hii, walikula rushwa wao kama walikula rushwa, lakini Tanzania huku kwetu kutokana na ushahidi na uchunguzi uliofanywa na *SFO* na TAKUKURU, hakuna ushahidi wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nasema kama kuna mtu katika Bunge hili ama hata nje ya Bunge hili, ambaye kwanza labda hawa *SFO* anawaona hawafai na TAKUKURU pengine hawafai, anaweza akapata ushahidi, sisi tuko *open,* tutaupokea, tutam-*prosecute* huyo ambaye tutakuwa na ushahidi dhidi yake, tutafanya hiyo kazi siku hiyohiyo. Waheshimiwa Wabunge na nyie mnafahamu, hatuwezi kwenda Mahakamani kwa hisia. Wanasheria mnajua na wengi ninyi mnafahamu, ukienda Mahakamani unakwenda na ushahidi, sio ushahidi tu unakwenda na mikono safi. Huwezi kwenda kule na mikono michafu na huna ushahidi, unadai tu fulani namhisi kafanya kitu fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndio maana Serikali hii mpaka leo hatujamshtaki mtu yeyote, hususan huyo Mheshimiwa Chenge, hatuna ushahidi dhidi yake lakini kama yupo mtu, kama ipo *Organisation* mahali popote pale, inao ushahidi, ituletee, hatutasita. Tumewapeleka wengine na yeye tutampeleka kama tuna ushahidi. Kama hatuna ushahidi basi tufanye kama wanavyofanya Kanisani, jamani kuna mtu yeyote ana maneno dhidi ya huyu? Kama hamna nyamazeni msiseme tena, kama mnayo semeni sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni vema tukatambua kwamba Tanzania imepiga hatua kubwa sana katika mapambano dhidi ya rushwa. Hatua hizi ni pamoja na kuwa nchi ya kwanza Duniani kutunga Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, inayozingatia misingi ya Mkataba wa Kimataifa dhidi ya Rushwa, *United Nations Convention Against Corruption, 2003, African Union Convention on Preventing and Combating Corruption, 2003* na *SADC Protocal Against Corruption, 2001 a*mbayo imeiwezesha TAKUKURU kushirikiana na taasisi za nje katika kuchunguza na kukusanya ushahidi unaokuwa nje ya mipaka ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Taasisi ya Kupambana na Rushwa ya Botswana *(DCEC)* ambayo inasifika sana Barani Afrika kuwa taasisi mashuhuri na yenye uwezo mkubwa wa kupambana na rushwa, imekiri kwamba TAKUKURU ni chombo kilichokomaa na mwaka 2009 walileta watumishi wao watano kupewa mafunzo ya uchunguzi Tanzania na walipewa mafunzo hayo na TAKUKURU. Aidha, mwaka huu pia wameomba kuleta Maafisa wao wengine wapatiwe mafunzo hapa nchini. Aidha, nchi yetu ni nchi ya kwanza Barani Afrika ambayo imetekeleza masharti ya msingi ya Mkataba wa Kimataifa wa Kupambana na Rushwa *(United Nations Convention Against Corruption)* na TAKUKURU imewakilisha Tanzania katika majadiliano ya kuboresha utekelezaji wa mkataba huo wa Kimataifa unaoratibiwa na *UNOCD (United Nations Office On Crime and Drugs)* kule Viena, Austria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, TAKUKURU imeendelea kuisaidia Serikali ya Zambia kuanzisha Kamati za Uadilifu *(Integrity Committees)* katika sekta za umma. Kwa kupitia Taasisi yao ya Kupambana na Rushwa, *ZACC*, wameendelea kushirikiana na TAKUKURU kuwapa mafunzo mbalimbali watumishi wa chombo hicho. Aidha, *Malawi Anticorruption Bureau*, wamejifunza kutoka TAKUKURU namna ya kuandaa mkakati wa Taifa dhidi ya rushwa na kwa ushirikiano huo nao sasa wanao mkakati wa kitaifa dhidi ya rushwa nchini mwao. Kama TAKUKURU ingekuwa dhaifu kama tunavyodai ni vipi nchi nyingine zinakuja kujifunza TAKUKURU*? (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Bunge lako likubaliane na mimi kwamba utendaji kazi wa TAKUKURU ni mzuri pamoja na changamoto ambazo zipo. Tuache hii tabia ambayo inajitokeza sasa ya kuji-*over criticise*, kujidharau na kujidhalilisha, tujithamini, TAKUKURU *is good. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja kwamba rushwa ni ugonjwa mkubwa ambao unalitafuna Taifa letu na imekuwa vigumu sana kwa Serikali kulikabili tatizo hili kikamilifu, sababu

kubwa ikiwa ni wapokeaji wakubwa wa rushwa wako katika Serikali hii. Kambi ya Upinzani inashauri sasa, kuundwe Kamati ya Kudumu ya Bunge, inayosimamia vita dhidi ya rushwa na iongozwe na Mwenyekiti wa Kambi ya Upinzani. Ni kweli kwamba rushwa ni tatizo kubwa na sio hapa kwetu Tanzania tu, bali ulimwenguni kote. Kwa kutambua ukubwa wa tatizo hili, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kukabiliana na tatizo la rushwa. Baadhi ya jitihada hizo labda niziseme; mwaka 1930 wakati wa ukoloni, tulileteWa hapa *Indian Penal Code* ambayo ilikuwa inawaadhibu watumishi wa Serikali ya Kikoloni waliopatikana na hatia ya kupokea rushwa. Kwa hiyo, jitihada za kupambana na rushwa zilikuwepo toka wakati huo. Mwaka 1958, Sura Namba 400 ya Sheria ilirekebisha Sheria hiyo na kuiita sasa Sheria ya Kuzuia Rushwa. Mwaka 1971, baada ya uhuru, Sheria Namba 16 ilitungwa ya Kuzuia Rushwa na makosa manne yaliwekwa kwenye Sheria hiyo na Sheria hiyo ilikuwa inatekelezwa na Polisi.

Mheshimiwa Spika, kabla ya hapo tarehe 12/10/1965, Marehemu Mheshimiwa Rais wetu wa Kwanza, Julius Kambarage Nyerere, wakati akizindua Bunge alisema, nanukuu:-

*"Rushwa ni adui mkubwa wa haki, tusipoidhibiti itaangamiza Taifa letu."*

*This was 1965,* kwa hiyo mapambano yalianza na Viongozi walishaliona hili na ndio maana mwaka 1971 Sheria hii ikatungwa. Mzee Ali Hassan Mwinyi, katika awamu yake alipoingia na yeye alikuja na kampeni ya fagio la chuma, kama mtakumbuka. Fagio lile lilikuwa ni la kuwafagia wazembe, wala rushwa na wahujumu uchumi. Kampeni ile iliendelea na mpaka 1991 ni Mzee Mwinyi huyohuyo aliunda *Anti-Corruption Squad* kwa maana Sheria ya *Anti-Corruption* ya mwaka 1975 lakini hii sasa akabadilishwa kwa Sheria Na. 27 na kuanzishwa TAKURU. Mwezi Oktoba, 1995, miaka 30 baada ya Mwalimu Nyerere kusema, Rais Benjamini William Mkapa naye alisema kuhusu rushwa. Alisema hivi:-

*"Maneno matupu japo yawe matamu kiasi gani hayawezi kumaliza rushwa. Kushirikiana na kila mmoja kutimiza wajibu wake katika vita hii ndiyo mwanzo wa mafanikio"*.

Awamu hii tumeyafanya mengi, tumeona mwaka 2007, tumetunga Sheria ile Na.11 ambayo imefanya makosa yamekuwa mengi zaidi na kuipa TAKUKURU nguvu, tumefanya *institutional capacity building,* tumeijenga TAKUKURU, tumeiongezea uwezo mkubwa, sasa tumeitanua imekwenda kila Wilaya nia ni kupambana na rushwa. Tunatambua tatizo hili ni kubwa sana na tunatambua kwamba hata tukifanyaje, Serikali peke yake hata ikatunga sheria vipi pia hatutoweza kupambana nayo tukaishinda, ni jukumu la Watanzania wote, Waheshimiwa Wabunge mkiwemo, wote tukisema *no to corruption*, tutaendelea vizuri na nchi yetu tutakuwa tumeondokana au tumepunguza kwa kiasi kikubwa janga hili la rushwa.

Mheshimiwa Spika, kuiweka TAKUKURU chini ya Kambi ya Upinzani ili ifanye kazi vizuri, hii inapotosha ukweli ni kama vile kusema Kambi ya Upinzani yenyewe wako Malaika tu, hili si kweli. Juzi tu tumeona wakati ndugu zetu wanajaribu kuchagua

Wabunge wa Viti Maalum ilikuwa tabu kwelikweli walisema jamani kuna rushwa, wakavunja ule uchaguzi si mara moja, si mara mbili leo, nafikiri kusema hivyo si sahihi, maana mawazo haya hayaondoi ukweli wa hoja kwamba rushwa ni tatizo la dunia na Tanzania imeweka mikakati ya kukabiliana nalo na hata kama Kambi ya Upinzani itaongoza mapambano hayo, bado haitaondoa ukweli kwamba rushwa ipo kila mahali pamoja na humo ndani ya Kambi ya Upinzani. Tuungane jamani, nimesema tuungane pamoja, tulikabili tatizo hili la rushwa kwani utengano au makundi ya nani aongoze mapambano dhidi ya rushwa hayatakuwa na tija yoyote. Serikali wakati wowote ndiyo inaongoza jitihada zote za kukukabiliana na tatizo la rushwa kwa kushirikiana na wadau wote. Wadau wote tukikubali kuachana na mienendo mibaya isiyokuwa ya uadilifu tatizo litapungua kama siyo kuondoka kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu hili la Rada, tumeambiwa hapa kwamba fedha za Rada zitakapokuja zisiende Serikalini, walisema zipitie kwenye Kamati Maalum chini ya Bunge na *NGO* na nini na mimi nashangaa sana mawazo hayo, kwa sababu hii hoja ni dhaifu. Kwamba Serikali iliyoko madarakani isirudishiwe fedha za Watanzania, haibishaniwi kuwa fedha hizo zilitoka kwenye Hazina hiihii ya Watanzania na kulipwa kwa kampuni hii ya *BAES*. Kama nilivyosema hapo juu watuhumiwa wakuu wa kesi hii ni Waingereza pamoja na huyu Vithlani**,** si raia wa Tanzania japo anao urai wa Tanzania ndiyo maana hata Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, ilitoa hati ya kumkamata, Serikali ya Uingereza imeshindwa kumrejesha hapa nchini. Hoja hii ya kwamba fedha hizo zirejeshwe kwenye Akaunti Maalum ya *NGO* haina msingi, fedha hiyo ilitoka Hazina na ni lazima irejeshwe Hazina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inashangaza pia Kambi ya Upinzani inaleta hoja kuwa fedha hizo zikirejeshwa Bunge lijadili matumizi yake, ndiyo maana tunasema Kambi ya Upinzani hoja yake ni dhaifu. Kama ilivyokuwa hoja ya kampuni BAES, utajadili vipi jambo ambalo tayari mmekwishasema mnataka fedha hizi ziende kwenye *NGO* sasa mnajadili nini, mnasema hela zikija ziende kwenye *NGO*, ziende kwenye Kamati, sasa mnasema iletwe Bungeni tujadili tena, hii hoja kwa kweli naiona ni dhaifu.

Mheshimiwa Augustino Lyatonga Mrema, Mbunge wa Vunjo alisema hivi hatua zipi ambazo zimekwishachukuliwa katika uchunguzi wa kesi za uchaguzi za mwaka 2010. Tunasema hadi sasa kesi 18 zimefikishwa Mahakamani baada ya kesi nyingine tano kufikishwa Mahakamani hivi karibuni. Hatua hizo tumezichukua na bado uchunguzi unaendelea zikipatikana zingine zitaendelea kupelekwa Mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Henry Shekifu, alisema mfumo wa TAKUKURU uangaliwe kwa kina, anasema mamlaka ya viongozi wake wa juu na utaratibu wa kuwahoji na kuwaadhibu urekebishwe kwa sasa hufanya kazi kama miungu mtu, upo ubadhirifu na matumizi ya madaraka vibaya katika TAKUKURU. Pia TAKUKURU iimarishe usimamizi wa kesi Mahakamani. TAKUKURU inafanya kazi kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa na Utumishi wa Umma. Upo utaratibu wa wazi wa kuangalia uongozi wa juu wa TAKUKURU kama ilivyo kwa viongozi wengine wa Serikali. Aidha, utaratibu huo unaruhusu mtu yeyote kukata rufaa kwa Katibu Mkuu Kiongozi au Rais kama hakuridhika na uamuzi ambao utakuwa umetolewa na viongozi

wa TAKUKURU. Kama Mheshimiwa anao ushahidi wa ubadhirifu na matumizi mabaya ya madaraka, tungependa tuupate ili tuchukue hatua mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Tundu Lissu, alisema maneno aliyosema Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU kwa Maafisa wa Ubalozi wa Marekani, kupitia mtandao wa *Wikileaks* kama ni ya kweli basi Taifa hili limefikia pabovu. Hili ni tatizo kubwa na kama Wabunge tunapaswa kupambana nalo. Sasa kwanza madai yaliyonukuliwa katika mtandao huu wa *Wikileaks* hayana ukweli hata kidogo, madai hayo si ya kweli, si ya kweli yanatumiwa vibaya tu, yanatumiwa labda kama mtaji wa kisiasa na wale ambao hawamtakii mema Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU. Kama taarifa hizi zingekuwa ni za kweli, kwanza Serikali ya Marekani ingethibitisha na tunasema si kweli kwa sababu zifuatazo:-

(i) Kama Mheshimiwa Rais au Viongozi wa Juu wa Serikali wangekuwa wanamzuia Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU kutekeleza majukumu yake ni vipi basi kuna kesi ya Viongozi wa Serikali, X-Mawaziri wako Mahakamani leo hii, si wangemzuia, wangemwambia usimpeleke Mramba, bwana huyu ni komredi, hawakumzuia, amefanya kazi; na

(ii) Uchunguzi uliofanywa na Serikali umethibitisha kwamba taarifa hizi siyo za kweli na ndiyo maana Mheshimiwa Rais hakuchukua hatua yoyote dhidi ya Ndugu Hosea, Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU.

Mheshimiwa Spika, hii ya kumshambulia Hosea kama Hosea, *as an individual* haisaidii kuendeleza mapambano dhidi yetu, bwana huyu amejitoa, anapambana kwelikweli, tumsaidie, tumuunge mkono na tuwe naye pamoja. Madai ya *Wikileaks* yapuuzwe, hayana ukweli, yaacheni yalivyo. Afisa wa Kimarekani anapeleka taarifa kwao, anajipendekeza, hata sisi tunao Maafisa kama hao, wanaleta lakini ukichunguza unakuta huyu anatafuta kusema ame-*file report* si kweli.

Mheshimiwa Richard Ndassa, amesema Maafisa walioko Mkoani na Wilayani wamekaa kwa muda mrefu sehemu moja wahamishwe. Sisi tunasema utaratibu wa kawaida wa watumishi wa TAKUKURU kuhamishwa kutoka kituo kimoja kwenda kituo kingine ni kila baada ya miaka mitano. Hata hivyo, zoezi hili pia mara nyingi linakwama labda mara zingine kwa sababu ya kutegemea tu upatikanaji wa fedha lakini ni utaratibu wetu kuwahamisha wasizidi miaka mitano tunawapeleka vituo vingine ili wakafanye kazi. Anaomba wapelekewe vitendea kazi, tunajitahidi, tunawapelekea vitendea kazi, tunawapelekea magari na vitu vingine vya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, anasema TAKUKURU, Sekretarieti ya Maadili na *Controller and Auditor General* wafuatilie nyendo za viongozi wanaotumia nafasi zao kuliibia Taifa kwa kujinufaisha, TAKUKURU ifanye kazi kuliokoa Taifa. Tunakubali na ushirikiano baina ya vyombo hivi vitatu upo, ni wa karibu sana, tunashirikiana na *Controller and Auditor General* na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, pamoja na TAKUKURU, tunafanya kazi ya kufuatilia mienendo na tabia ya viongozi.

Mheshimiwa Sara Msafiri, Mheshimiwa Desderius Mipata wa Nkasi Kusini, wao walisema TAKUKURU ipewe meno, ipeleke kesi zake Mahakamani moja kwa moja bila kupitia kwa *DPP*. Wazo hili liliwahi kutolewa na Mheshimiwa Tundu Lissu kwenye Kamati yetu na tulisema kwa kweli ni wazo zuri lakini lilikuwa na tatizo moja tu dogo. Kwa sasa Waheshimiwa Wabunge tutakumbuka Polisi ndiyo walikuwa wanahisi mtu, wanamkamata, wanampeleleza, wakawa wanampeleka na Mahakamani. Baadaye Serikali ikaona kwamba aah, utaratibu huu unampa nguvu sana Polisi kwa hiyo tumnyang'anye utaratibu huu, tukamnyang'anya, sasa tumeanzisha utaratibu unaitwa *civilization, prosecution* zote zinafanywa na *State Attorney.* Sasa hapa tunaombwa tufanye yaleyale, tunampa huyu bwana uwezo wa kuhisi, kukamata, kupeleleza na kupeleka Mahakamani, nadhani *checks and balances* hazitakuwepo. Kwa hiyo, tunadhani utaratibu uliopo sasa ni mzuri na uendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesikia kengele, nataka nijaribu kutoa majibu ya harakaharaka kwenye hoja nyingine ukiondoa TAKUKURU. Ziko hoja zilijengwa kuhusu Usalama wa Taifa na hasa na Mheshimiwa Mnyika, alitaka kujua pesa zao ziko wapi, wanatumiaje na nini. Unajua chombo hiki, binadamu wote sisi tungependa kujua kinafanya nini, wanafanyajefanyaje kazi, lakini ukweli ni kwamba vyombo hivi duniani ni vyombo vya siri, hata taratibu zao za ajira ni za siri, matumizi yao ni ya siri, kama ingekuwa mambo yenyewe yanawekwa kwenye bajeti, si tungejua kiasi Marekani walichotumia kumuua bwana Osama, vitu vingine tukubali kwamba tuko hapa tumetulia mambo yetu yanakwenda vizuri kwa sababu ya usiri huo. Hayo ndiyo matokeo ya kazi ya Idara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Idara hii inafanya kazi nzuri, lakini alitaka ufafanuzi wa kifungu cha 30 kinachohusu matumizi ya kitaifa bilioni 130, ndiyo hayo Mheshimiwa, sasa ukitaka tuyaorodheshe hapa wanafanyaje, wamenunua gari ngapi, wamelipa mishahara mingapi, wamefanya *operation* gani itakuwa hatujitakii mema, hatuwezi kusema hayo lakini yapo matumizi ya kitaifa na yana-*guarantee* usalama zaidi.

Mheshimiwa Sabreena Sungura, alisema ili kuimarisha utawala bora, Serikali itunge sheria zitakazokuwa zinawajibisha Watumishi wa Umma pale wanapoenda kinyume ili iwe funzo kwa wengine? Nafikiri hizi sheria zipo, Mheshimiwa Hawa Ghasia anazijua sheria hizi atatuambia.

Mheshimiwa Mchungaji Natse alisema sheria mbili za mwaka 1970 na 1996 zinagongana, mimi nasema sheria hizi mbili, ya mwaka 1970 inaeleza nini usalama wa Taifa, makosa yake ni nini wakati Sheria ya mwaka 1996 inaunda chombo rasmi, hiki chombo kilikuwepo, lakini hakikuwepo kisheria, sasa ya 1996 inachofanya *simply* ni kukiunda tu, kwa hiyo hakuna mgongano wowote, ni sheria ambazo bado zinatumika.

Mheshimiwa Spika, kabla sijamaliza kabisakabisa nichukue nafasi hii kwanza kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, nyaraka za Serikalini ziko chini ya sheria za nchi hii *Chapter* 47, *National Security Act, section four* na *five* inazuia kukutwa na nyaraka za Serikali ambazo hustahili kuwa nazo, kuna adhabu. Hatungependa tuzitumie hizo kwa

Wabunge wetu, tulikuwa tunawaomba nyaraka zisizokuhusu achana nazo, unaenda kuzitafuta, mnazishika Bungeni, mnazitangaza, ukichukuliwa hatua unaweza kuja kusema ni mambo ya kisiasa lakini si ya kisiasa hata kidogo, yatakuwa ni mambo ya sheria tu, utakuwa umevunja sheria. Unaweza ukazipata zikakusaidia kujenga hoja, ukadhani hii ni siasa lakini hutakiwi kuwa nazo. Kwa hiyo mtu akija akiku-*challenge*, akikuambia bwana umeshikwa na nyaraka za Serikali tunakupeleka Mahakamani usije ukasema mimi Mwanasiasa, tuache. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge acheni tabia hizo si vizuri, sheria ipo tusiivunje sisi ndiyo tumezitunga sheria hizi tuziheshimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na niwaahidi Waheshimiwa Wabunge, kwa wale ambao sikuwataja na hoja zao sikuzizungumzia kwa sababu zilikuwa ni nyingi sana na muda ni mdogo, kama ilivyo kawaida yetu, majibu yote tutayaandika tutawapa Waheshimiwa Wabunge lakini mengine tutawasubiri kwenye vifungu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ghasia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, sasa nitamwita Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais inayohusika na Mahusiano na Uratibu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kukushukuru kwa kunipa fursa ili niweze kuhitimisha hoja ambayo niliileta hapa Bungeni jana. Awali ya yote, napenda niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wametoa michango katika maeneo yote ambayo mimi nayaratibu. Katika ofisi ya Rais, nashughulikia Tume ya Mipango, MKURABITA, TASAF, Mfuko wa Rais wa Kujitegemea na vilevile nashughulika na masuala yanayohusiana na mahusiano ya jamii. Hoja nitakazozijibu zitajikita katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, labda niwatambue Waheshimiwa Wabunge ambao wamesema katika maeneo haya, kwanza kulikuwa na Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omar Kigoda, Mbunge wa Handeni, Mheshimiwa Pindi Chana, Viti Maalum, Mwenyekiti wa Kamati Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Susan Lyimo, Viti Maalum na Mheshimiwa Mch. Israel Yohana Natse, Mbunge wa Karatu, Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengeya Kamani, Mbunge wa Busega, Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Deogratias Aloyce Ntukamazina, Mbunge wa Ngara, Mheshimiwa David Silinde, Mbunge wa Mbozi, Mheshimiwa Rose Kamili, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa John Mnyika, Mbunge wa Ubungo, Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa William Augustao Mgimwa, Mbunge wa Kalenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wafuatao wamechangia kwa maandishi, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mbozi Mashariki; Mheshimiwa Henry Daffa Shekifu, Lushoto; Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza, Buyungu; Mheshimiwa Augustino Lyatonga

Mrema, Vunjo; Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Busanda; Mheshimiwa Desderius John Mipata, Nkasi Kusini; Mheshimiwa Jadi Simai Jadi, Mkwajuni Zanzibar; Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mbozi Mashariki; Mheshimiwa Richard Ndassa, Sumve; Mheshimiwa Dkt. William Mgimwa, Kalenga; Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Viti Maalum; Mheshimiwa Dkt. Kebwe Stephen Kebwe, Serengeti; Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, Tarime; Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Viti Maalum na Mheshimiwa Nasir Yussuf Abdallah, Korogwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza mapema, nafarijika sana kwa michango mizuri iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge wote. Nitaeleza kwa muhtasari majibu ya hoja mbalimbali zilizotolewa, lakini kwa kweli kwa sababu ni nyingi na maeneo ni mengi sana itakuwa vigumu sana kuweza kujibu hoja ya kila Mbunge na dakika nilizonazo ni 45, kwa hiyo nitajikita zaidi katika maeneo ya jumla lakini nikipata muda nitajibu yale ambayo yanawezekana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo yako mambo machache ya jumla ambayo yamezungumzwa, moja linahusiana na Tume ya Mipango na ilikuwa ni kuhoji kwamba thamani ya shilingi inashuka, lakini mipango yetu ina bajeti maalum. Alitaka kujua inawezekanaje bajeti ile ikaendelea kuwa hivyo wakati thamani ya shilingi inashuka na alitaka kujua kwa nini thamani ya shilingi inashuka. Jibu la suala hili siyo gumu sana, ni kwamba suala hili ni suala linalotokana na uhitaji na upatikanaji, kwamba unakuwa na dola nchini kiasi gani na mahitaji ya nchi ni kiasi gani, kama mahitaji ni makubwa na kiwango cha dola kilichopo nchini ni kidogo basi kwa namna yoyote thamani ya shilingi inaweza kushuka, hiyo ni moja ya sababu. Sababu nyingine inatokana na mabadiliko ya thamani ya fedha tunazofanya biashara nazo. Kwa mfano, kama thamani ya dola itapanda thamani ya shilingi kwa namna yoyote itashuka. Kwa hiyo, hayo ni masuala ambayo imebidi tuyatolee ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, anauliza kwamba ili kuimarisha shilingi tunatakiwa kufanya nini? Jibu lake ni kwamba ni lazima ubadilishe *supply and demand* na kwa hiyo, unahitaji kuongeza zaidi mauzo nchi za nje. Ukiweza kuuza zaidi nchi za nje ukapata dola zaidi basi unaweza ukaimarisha thamani ya shilingi hapa nyumbani na kwa kuongeza thamani ya mazao yetu vilevile tutaongeza bei. Kwa hiyo, uwezekano wa kupata dola nyingi zaidi kwa mazao ambayo yameongezewa thamani ni kubwa zaidi kuliko kuuza mazao ghafi. Vilevile Benki Kuu kupitia Soko la Fedha za Akiba huwa inanunua na kuuza fedha za kigeni ili kuleta utulivu katika soko. Aidha, hatua nyingine ambazo zinafanyiwa kazi ili zitumike hapo baadaye ni pamoja na kuanzisha hifadhi ya kimkakati ya mafuta yatakayotumika wakati wa uhitaji mkubwa wa mafuta na mauzo ya bidhaa za thamani kubwa kama vile madini na fedha zake zikiwekezwa hapa nchini zinaweza zika-*stabilize* thamani ya shilingi. Hilo ndiyo swali moja kubwa lililokuwa limezungumzwa la ujumla kuhusu Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Spika, vilevile ikumbukwe kwamba kushuka kwa thamani ya shilingi siyo tatizo la mfumo wa uchumi bali ni tatizo linalozikumba pia nchi nyingi. Kwa mfano mwezi Januari 2011 dola moja ya Kimarekani ilikuwa inanunuliwa kwa shilingi 1,499.70/= na mwezi Juni ilikuwa shilingi 1,598.38/= sawa na 6.57% wakati dola

moja ilikuwa inanunuliwa kwa shilingi za Kenya 81.36 na baadaye ikashuka na kuwa shilingi 90 ambayo ni 10.62%. Kwa hiyo, ni *phenomenal* ya uchumi ambayo kusema kweli kwa maelezo niliyotoa ndiyo inaweza kufanya thamani ya shilingi ikawa siyo *stable*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu MKURABITA, suala lililohojiwa juu ya MKURABITA kwa kweli ni jambo la kutaka MKURABITA ipewe uwezo ili iweze kufanya kazi hii nchi nzima. Mimi nakubaliana na hoja hii kabisa na kwamba Serikali tutafanya kila tunaloweza kuisaidia MKURABITA ili iweze kupata rasilimali za kutosha za kuweza kufanya kazi ingawa siyo nchi nzima kwa mara moja lakini angalau nchi nzima kwa awamu ili kazi hii iweze kufanyika kwa sababu ukizungumzia juu ya kilimo kama kipaumbele na ardhi ndiyo rasilimali ya msingi kwa kilimo. Kwa hiyo, ukiwa na ardhi iliyopimwa na kuwawezesha wenye ardhi kupata mikopo, unaweza ukatekeleza Sera ya Kilimo Kwanza kwa ukamilifu zaidi kuliko kama ardhi yenyewe haina thamani na haiwezi kumwezesha mwenye ardhi kukopa. Kwa hiyo, tunaliunga mkono pendekezo hili na tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa *TASAF* hoja iliyozungumzwa ya jumla ilikuwa moja, kwamba *TASAF* ile ya awali yaani ya kwanza *TASAF I,* utekelezaji wake ulikuwa mzuri zaidi kuliko *TASAF II*. Hili limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi hapa na sababu zake ni kwamba *TASAF I* ilikuwa na mfumo tofauti wa kufikisha fedha, fedha zilikuwa zinakuja *TASAF* na miradi inakuja lakini TASAF yenyewe ilikuwa imewakilishwa kwenye Halmashauri za Wilaya. Kulikuwa na Wahasibu ambao walikuwa wanawajibika *TASAF* kwa hiyo, Wahasibu wale wakati wote walikuwa wanafuatilia kuona fedha zilizokwenda kwa jamii zimetumika kama zilivyokusudiwa na kutoa taarifa kwa haraka sana *TASAF* Makao Makuu.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi ilipokuja *TASAF II* tukabadili kwa sababu ya *D by D* tukaamua sasa kutumia uongozi wa Halmashauri na utendaji wa Halmashauri. Hii imebadilisha kidogo mfumo na imefanya mahali pengine mambo yamekwenda vizuri lakini mahali pengine siyo mazuri na *reporting* imekuwa inachelewa sana kuonyesha kiasi gani kimetumika na kwa kazi ipi. Kwa hiyo, napenda kusema kwamba kwa sababu sasa *TASAF II* imemalizika sasa tunakwenda *TASAF III* kuanzia mwakani, kwa hiyo, kwa kweli tutarudisha mfumo ule wa zamani wa *TASAF II* ili kuhakikisha kwamba jamii inatumia hizi fedha na tunapata *value for money* na kuhakikisha kwamba wananchi wanaoibua miradi yao na wanapata manufaa yanayostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wachangiaji wengine waliozungumzia hoja hii walikuwa ni Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Dkt. Abdallah O. Kigoda, nisingependa kupoteza muda kuzungumza mambo yaliyosemwa na Mheshimiwa Dkt. Kigoda kwa sababu alikuwa ametoa hoja nzuri sana na nyingi. Alikuwa anatuasa kwa kweli kuisaidia Tume ifanye kazi yake kwa ufanisi na sisi wote tungependa kuona hii Tume ambayo ni *think tank* ya Taifa inafanya kazi yake kwa ubora zaidi na wako wengine ambao vilevile walimuunga mkono kwa kusema tuipe Tume hii wafanyakazi tena wenye weledi, tuisaidie Tume hii ipate fedha za kutosha ili ifanye utafiti. Haya masuala yote yaliyozungumzwa yanahusiana na Tume kwa kweli tunakubaliana nayo na napenda

kuwahakikishia kwamba Tume hii ambayo Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Rais angependa kuona kweli ina-*perform*. Kwa hiyo, mawazo haya yatafika kwa Mwenyekiti wa Tume na kumuonyesha haya ndiyo mawazo ambayo Bunge hili linazungumza juu ya Tume hii. Mimi nina imani kabisa Tume hii itaimarishwa ili iweze kufanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Spika, siyo kwamba wataalamu watakaoingia kwenye ile Tume peke yao ndiyo watakaokuwa *think tank* na watafanya kazi zote za Tume, huwezi kuwa na wataalamu wa fani zote wanaishi mahali pamoja lakini kuna mfumo kwa mfano, tulipokuwa tunazungumza juu ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano tulikuwa tuna *contract* shughuli fulanifulani zinakwenda *University of Dar es Salaam* Kitengo cha Uchumi au *ESRF* wanafanya kazi hizo kwa niaba ya Tume. Kwa hiyo, siyo lazima kuwa na wataalamu wa kila fani lakini wale ambao ni *basic* itabidi wawepo na wataweza kufanya kazi na vyombo vingine vya hapa nchini ili tuone ni kitu gani kinaweza kufanyika.

Mheshimiwa Spika, Tume itafsiri Mpango ya Maendeleo wa Miaka Mitano kwa Kiswahili. Hii nayo ilikuwa ni hoja iliyotolewa na Mwenyekiti wa Kamati. Hiyo yote tunaendelea kushughulika nayo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, masuala yote yaliyosemwa na Mwenyekiti yalikuwa ni ushauri kwa Tume na kwa sababu tunafanya kazi kwa karibu sana na hii Kamati ya Fedha na Uchumi kwa hiyo, ushauri uliotolewa tunaendelea kuzungumza nao na tutakwenda kusimamia kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Tume na kwa upande wa maoni yaliyotoka Kambi ya Upinzani yaliletwa na Mheshimiwa Mch. Israel Yohana Natse. Alisema mipango ya kuinua uchumi na kupangia matumizi ya rasilimali tulizonazo ianzie ngazi ya chini na kweli mfumo wetu wa upangaji wa mipango ndivyo unavyotaka. Kwa mfano, mipango yote ambayo inapangwa kwa ajili ya Halmashauri za Wilaya ingestahili ianzie kwenye kijiji. Kwa hiyo, kwa kweli kitu ambacho tunaishauri Serikali za Mitaa ni kuimarisha *D by D* kwa kupeleka madaraka zaidi kwa wananchi kwa utaalamu na hata kwa fedha ili mipango iwe inaibuliwa kutoka kule. Sasa ipo mipango ya Taifa na mipango ya chini ya vijiji, ile mipango mingine mikubwa sana kama ya umeme, bandari na reli lazima itaibuliwa kitaifa lakini ile inayohusu wananchi, kilimo, ufugaji, uvuvi, barabara za vijijini na kadhalika ile lazima ianzie kule chini.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mch. Israel Yohana Natse nakubaliana naye, alisema bajeti ya 4.7 bilioni hazitoshi. Ni kweli lakini ndiyo iliyowezekana kwa mwaka huu. Tutashirikiana naye katika kudai zaidi ili mwakani iwe nzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, suala la kushuka kwa thamani ya shilingi nimelieleza katika masuala ya jumla na kwa kweli nadhani limeeleweka.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengine waliozungumza kuhusiana na suala la Tume ya Mipango walikuwa ni Mheshimiwa Godfrey W. Zambi yeye

alichangia kwa maandishi na Mheshimiwa Wiliam Mgimwa alichangia kwa kuzungumza. Tume ya Mipango iwezeshwe kwa kuwa na watumishi wenye weledi nimeshajibu. Serikali ihakikishe kuwa Tume ya Mipango inapewa pesa za kutosha ili iweze kutekeleza majukumu yake, nimeshaeleza na ninakubali.

Mheshimiwa Spika, moja ya kazi kubwa ya Tume ni kuibua na kufanya tafiti za kiuchumi lakini vifungu vya bajeti havithibitishi hivyo. Nakubali fedha zilizopo hazijatosha, tutajaribu kuisaidia Tume hii katika siku zinazokuja ili iweze kufanya kazi yake vizuri. Hayo vilevile yalisisitizwa na Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine ambaye alileta hoja yake kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa kwamba Tume ipewe kipaumbele na Serikali, tunakubali, hayo yalisemwa na Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, vinginevyo kazi ya kuwepo kwa Tume haitakuwa na maana kwani Tume imeundwa kwa ajili ya kutoa ushauri yaani *think tank* na Serikali lazima isikilize mawazo ya wataalamu katika kuendeleza nchi yetu.

Mheshimiwa Henry Daffa Shekifu alichangia kwa kuandika juu ya usimamizi wa mpango wa maendeleo na akataka uliopitishwa hivi karibuni ufanyike kwa umakini mkubwa. Nakubaliana naye kwamba iundwe Benki ya Maendeleo ambayo itasaidia fedha zote zitakazopatikana kwa kutekeleza mipango kamilifu. Hili ni wazo ambalo kwa kweli benki zipo na tunajaribu kuunda benki nyingine pengine haitakuwa lazima kuwa na benki maalum kwa sababu benki zilizopo zitakuwa zinasimamia kazi ya mpango huu.

Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengeya Kamani alisema Serikali ifungue matawi ya Benki ya Kilimo Mikoani badala ya kubaki Dar es Salaam. Hii Benki ya Kilimo inafanyiwa kazi sasa hivi na itakapofunguliwa haiwezi ikafunguliwa halafu ikaenda Mikoani moja kwa moja kwa sababu itabidi kwanza ijiimarishe hapo itakapokuwa. Inaweza ikafika Mikoani bila kufungua matawi kwa sababu tunazo benki kama *NMB*, unaweza ukafungua dirisha la kilimo katika *NMB* na mikopo ile ikawafikia wakulima kabla ile benki haijafungua tawi huko Mikoani.

Mheshimiwa Spika, pia alisema tafiti kuhusu namna Tanzania itakavyoweza kutumia fursa za kiuchumi katika Jumuiya ya kikanda zifanyiwe kazi. Kwa kweli tumeshaanza kuzifanyia kazi na kama unavyoona mwaka huu tunaanza kutazama suala la ajira kama fursa.

Mheshimiwa Tundu Lissu alizungumzia kwamba kuna upendeleo katika mgawano wa rasilimali fedha kwani kuna tofauti kubwa sana ya mgawano huo katika matumizi ya kawaida na ya maendeleo. Mheshimiwa Tundu Lissu kama kawaida alikuwa *militant* na akatishia kwamba kama hili halikutekelezwa basi mambo yataamuliwa mtaani. Nataka kumwomba Mheshimiwa Tundu Lissu awe anapunguza jazba na kwenda mtaani si lazima kwa sababu tunaamua mambo hapa na sisi wote tumetoka mtaani. Kwa hiyo, hakuna anayeogopa kurudi mtaani lakini nataka kumsaidia tu alikuwa ame-*cite* Mikoa fulanifulani kwamba ina bajeti kubwa zaidi kuliko Singida, alifanya Singida kama *base*. Sasa mimi nataka kumwambia tu kwamba Singida kuna *population* ya watu milioni

1,331,000, kuna *District Councils* nne, kuna wanafunzi wa Shule za Msingi 257,162, kuna wanafunzi wa *Secondary School 48,906, Secondary Schools* zilizopo Singida ni 154 na Shule za Msingi ni 503. Mbeya ambapo alisema wanapewa fedha nyingi sana kuna watu milioni 2,252,000, kuna Wilaya nane, kuna wanafunzi wa *Primary School 558,458* na wale ambao wako *Secondary School* ni 145,000 ni mara tatu ya Singida. Namba ya Shule za Sekondari ni 295, Shule za Msingi ni 1060 ambazo ni mara mbili ya zile za Singida. Halafu Mwanza kuna watu milioni 3,464,000 kuna *District Council* na *Municipal* jumla nane, wanafunzi 880,000 ambao ni mara tatu ya Singida na *enrolment* ya *Secondary School* ni 148,000. Namba ya shule ni 281 na wanafunzi wa Shule za Msingi ni milioni 1,232,000.

Mheshimiwa Spika, sasa ukigawa sawa rasilimali hizi hasa katika *recurrent* maana yake Mheshimiwa Tundu Lissu anatupa ushauri kwamba tufunge shule za Mwanza na Mbeya ili tugawe sawa, hiyo si sawa! Usawa huo hauwezi kutupeleka kule tunakotaka kwenda. Habari hizi zinamsaidia Mheshimiwa Tundu Lissu, hana haja ya kwenda mtaani maana hapa majibu yanapatikana. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, napenda kusema kwa ujumla tu kwamba Tume ya Mipango kuanzia mwaka huu wa nne itaanzia kutazama upya mgawo wa rasilimali. Shabaha yetu ni kuhakikisha tunapeleka maendeleo katika kila sehemu ya nchi yetu kwa sababu hata hivyo mgawo tunaouzungumza hapa ni wa *recurrent* inayopita Ofisi ya Waziri Mkuu yaani *Local Government* lakini ukitaka kuchukua migawo yote utakuta kwamba kuna bajeti kubwa sana inakwenda katika maeneo anayoyalalamikia kwa mfano kwa mwaka 2011/2012 Mkoa wa Singida utapata shilingi 40 bilioni kwa ajili ya kutengeneza barabara za lami na vilevile zipo fedha Mtwara ambazo zinafika 59 bilioni kwa ajili ya kutengeneza barabara inayotoka Masasi - Mangaka - Tunduru na kufungua maeneo ambayo bado yapo nyuma sana kwa mawasiliano kwa sababu kwa kufanya hivyo unakuza uchumi. Singida ina barabara inayopita pale kwenda Mwanza na barabara nyingine inatoka Babati inakuja Singida, kazi ya Viongozi wa Singida sasa ni kupanua barabara za vijijini ili ziweze ku-*link* na barabara kuu kwa ajili ya kukuza uchumi. Mambo ya kukuza uchumi na kufanana ni mambo magumu kwa sababu vilevile kuna *factors* nyingine za kiuchumi kwa mfano ukilinganisha Mbeya na Singida mazingira yanatofautiana sana kwani mvua ni jambo la kawaida tu lakini Singida mvua ni ya kuomba kwa Mungu. Kwa hiyo, lazima matatizo haya yatakuwa yanaifanya Singida na Mbeya ziwe tofauti sana na sidhani kama Mheshimiwa angependa na Mbeya ikose mvua ili zifanane na Singida, haiwezekani! *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka alisema mipango mingi katika nchi hii haifanikiwi kwa sababu haifuati utaratibu mzuri ni budi wananchi washirikishwe. Nakubaliana naye wala hatuna tatizo kabisa kwani ni lazima tushirikishe wananchi na nilisema wakati tunapitisha Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano kwamba lazima tuwashirikishe wananchi katika utekelezaji ili wawe sehemu ya mpango.

Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa alisema Tume inakusudiwa kuwa *think tank* lakini ni wataalamu wa aina gani ambao wapo wanaoweza kumsaidia? Nimesema tutaitazama Tume, tutaongeza idadi ya wataalamu, tumeanza mwaka jana, tuliajiri

wataalamu 22 na tutaendelea kuajiri wataalamu 38 mwaka huu wa fedha. Kwa hiyo, haya mambo yote yanafanyika Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa na alikuwa anaendelea kusema vipaumbele tulivyojiwekea ni lazima tuviheshimu, mimi nakubaliana naye. Kwanza, vipaumbele vile ni msingi kabisa, kwa miaka mitano huhitaji kuwa na vingine, ni miundombinu ambayo inahusisha bandari na barabara, ni kilimo ambacho kinahusisha mifugo mazao ya faida kubwa, miundombinu inayohusu barabara, bandari, viwanja vya ndege ambavyo vinaweza kusaidia kusafirisha mazao kutoka hapa nchini kwenda nje ya nchi. Vipaumbele vile tutaendelea navyo na hili vilevile lilikuwa limesemwa na Mheshimiwa Chacha Nyambari Nyangwine kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Yusuph Abdallah Nassir alisema Tume inahitaji kuajiri wataalamu, Wizara iandae hadidu za rejea kuona kama watatosheleza mahitaji. Wataalamu wanaohitajika ni wengi kuliko hawa watakaoajiriwa lakini tunakwenda hatua kwa hatua. Hayo ndiyo maelezo yaliyohusu Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Spika, maelezo mengine yalihusu MKURABITA, lakini kwa kweli nisingependa kupoteza muda mrefu kuzungumza juu ya MKURABITA labda nitumie nafasi hii niipongeze MKURABITA kwa ushindi iliopata kwa kupata tuzo ya Umoja wa Mataifa. Labda niseme kwamba hili ni wazo lilitoka nje la kuanzisha mfumo namna hiyo wa kurasimisha mali za wanyonge lakini sisi tulipolipata tukaliweka *into action*, kwa hiyo, walipokuwa wanashindanisha ubunifu kule Umoja wa Mataifa waliona MKURABITA ni *unique* kwa Tanzania kwa hiyo, hatukushindana na mwingine tulishinda bila kushindaniwa kwa sababu hakuna mtu mwingine anayefanana na sisi kwenye Umoja wa Mataifa, ndivyo tulivyoshinda. Kwa hiyo, mimi nadhani MKURABITA yale niliyoyasema ya jumla ndiyo yanaihusu MKURABITA kwamba tuisadie, tuitafutie rasilimali na ishirikiane na Wizara ya Ardhi ili iweze kufanya kazi ya kupima ardhi na kurasimisha mali ya wanyonge.

Ndugu yangu Mbunge wa Ubungo alikuwa amelizungumza hili kwa sababu tulisema kuna sehemu pale Dar es Salaam ambayo itapimwa na watu wapate hati za kimila, lakini akasema yeye anafahamu kwamba kuna tatizo la kampuni moja ambayo aliisema ina mfumo wa kifisadi.

Mheshimiwa Spika, nataka kusema kwamba hiyo kampuni ambayo anaisema Mheshimiwa John Mnyika ndiyo nimeisikia leo hapa Bungeni, kwa hiyo sikupata muda wa ku – *check* kujua hiyo ni kampuni gani. Namwomba aje anisaidie kuniambia ni ipi na tujue ina uhusiano gani na MKURABITA. Kama ina uhusiano na MKURABITA na kwamba tunakwenda kwa sababu ya hiyo tutaacha kwenda kwa muda, kwa sababu sisi hatuwezi kwenda kuweka *stand* kwa ujambazi wa namna yoyote, atupe *facts*, tutazifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo masuala yanayohusu MKURABITA, ambayo yalizungumzwa vile vile na Mheshimiwa Titus Kamani, Mheshimiwa David Silinde ambaye yeye alikuwa anahoji kama watu wa kule Tunduma na Kimara Baruti ya Dar es Salaam wameandaliwa kwa kazi hii? Nasema kabla MKURABITA hawajakwenda

itabidi kwenye *District Council* inayohusika wakashirikiane maana mara nyingi tunashirikiana na wadau, iwe ni Halmashauri ya Wilaya au wale ambao tunawapimia. Kwa hiyo na Mheshimiwa David Silinde nadhani atakuwa mdau, naye atakwenda kusaidia katika kuwaandaa kwamba kazi inakuja hapa Tunduma na Tunduma pale ni vizuri tupime, nimepita pale juzi pale ni *chaotic*, yaani magari yalivyopaki hata pa kupaki hapajulikani, hayaendi wala hayarudi, nyumba imekaa juu ya zingine, nafikiri tukirasimisha inaweza ikawa *a better* Tunduma kuliko ilivyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Deogratias Ntukamazina alizungumzia *TASAF* na MKURABITA na alisema ni vyombo muhimu sana na namuunga mkono, tuvitie moyo vifanye kazi yake. Niseme tu kwamba MKURABITA hii kwa kawaida inajenga uwezo wa Halmashauri, inafundisha vijana na inafanya kazi ya kupima iwe rahisi zaidi kuliko ukitumia ile *conventional way*, maana pale unafika unawafundisha halafu unafunza vijana wa *form four* na siku hizi wako wengi, unawapa vifaa vile *DPS* kwa ajili ya kupima, wanaweza wakapima halafu MKURABITA ikaja kutoa hati kwa kutumia ramani ambazo zimepimwa na vijana ambao wamefundishwa *locally*. Tukipata fedha tukafanya hivyo nchi nzima inaweza ikapimwa kwa muda mfupi unaokuja.

Mheshimiwa Spika, hii kampuni aliyoitaja Mheshimiwa John Mnyika inaitwa Twiga *Chemical*, kwamba kuna fidia na kuhamisha wananchi, ningependa kupata maelezo zaidi ya kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu MKURABITA vile vile Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza, alikuwa ametoa mawazo hayo ambayo yote yanaungwa mkono. Mheshimiwa Augustino Lyatonga Mrema alizungumzia juu ya umuhimu wa kupima na kuondoa mvutano wa ardhi katika maeneo hasa yale yaliyo na upungufu mkubwa wa ardhi kama Vunjo. Tunakubaliana nae kwamba suala hili likifanywa linaweza likasaidia maana mipaka ile itajulikana na migogoro inaweza ikamalizika.

Mheshimiwa Lolesia Bukwimba vile vile aliandika na sisi tunakubaliana naye, alisema jambo la pili ni huu Mpango wa Kurasimisha Raslimali za Biashara ya Wanyonge Tanzania (MKURABITA), utaratibu huu ni mzuri sana kwa kuwa wananchi wa kawaida wanapata nafasi ya kumiliki ardhi yao na hii ni kweli na ndiyo msingi mzima.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Desderius John Mipata, alisema MKURABITA iende nchi nzima, tumekwishajibu hilo. Mheshimiwa Jaddy Simai Jaddy, alisema ule mpango watu waelimishwe ili waujue. MKURABITA yenyewe ina programu ya kutaka kuwaelimisha watu ili waweze kujua na pia kuwepo na mawasiliano. Nakubaliana naye kwamba tukiwaelimisha kazi yetu itakuwa rahisi. Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye alikuwa ameandika na yeye ni mdau yuko Wizara ya Ardhi, kwa hiyo, tutashirikiana naye katika kuona haya mambo yanafanyika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *TASAF*, wana-*appreciate* kazi inayofanywa na *TASAF* ila mfumo huu tulioutumia tukiubadili nadhani *TASAF* III itakuwa sawa na *TASAF* I. Ningependa kuwashauri Waheshimiwa Wabunge kwamba *TASAF* wanaibua

miradi kutoka kwa wananchi wenyewe, halafu wananchi wenyewe wanachangia asilimia kadhaa kama wanavyochangia katika miradi mingine ya *Wold Bank* au Maji, wote tunachangia sasa tukiishachangia wananchi lazima tuwasaidie ili waone ule uchangiaji ni jambo la msingi, lakini tukisema tusichangie itakuwa ngumu. Wengine waliochangia katika eneo hili ni Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, Mheshimiwa Rose Kamili Sukum ambaye alisema iundwe Timu ya Wataalam kufuatilia *value for money*, tunakubaliana naye lazima uwepo mfumo unaofuatilia masuala ya namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, wengine ambao wamezungumzia *TASAF* kwa maandishi ni Mheshimiwa Godfrey Zambi na yeye nimekwishajibu habari zake. Hoja hii pia ilichangiwa kwa maandishi na Mheshimiwa William Mgimwa, Mheshimiwa Henry Shekifu, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mheshimiwa Desderius Mipata na pia Mheshimiwa Lolesia Bukwimba.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani walikuwa wanazungumzia Mfuko wa Rais wa Kujitegemea. Labda nielezee kuhusu Mfuko huu wa Rais wa Kujitegemea. Hii ni *concept* iliyoanzishwa mwaka 1983 na Marehemu Edward Moringe Sokoine. Ilikuwa nzuri sana lakini Mfuko huu una matatizo ya kutokuwa na raslimali za kutosha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, matatizo yote ambayo mnayasikia kwa kweli yanatokana na ukosefu wa rasilimali na nia ni nzuri, labda niseme tu kwamba Bodi ya huu Mfuko sasa hivi ina-*study* namna inavyoweza kuusaidia hata kama ikibidi kuupanua na kuona namna ya kuweza kuupatia raslimali ili uweze kufanya kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, yako mambo mengine yaliyosemwa ambayo na yenyewe nahitaji kuyatolea maelezo. Moja linahusu *NGOs*, hili lilisemwa kwa urefu sana lakini nataka niseme kwa ujumla kwamba, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu) haiandikishi *NGOs*, *NGOs* zinaandikishwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii na zingine zinaandikishwa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Hizi Wizara zote hazijasoma bajeti zao hapa Bungeni, kwa hiyo, ukitaka kupata majibu mazuri ya maswali yote yaliyoulizwa hapa kuhusiana na mahusiano ya asasi zisizo za Kiserikali, na baadhi ya wachangiaji akiwemo Mheshimiwa Susan Lyimo, walisema asasi hizi zinaonewa, mwingine akadai kwamba taarifa ambazo zinahusiana na mambo yanayotokea haziletwi Bungeni, ikazungumzwa habari ya nyumba za Loliondo na Taarifa ya Maji ya Sumu huko Mto Tigite, Tarime. Haya masuala yote mengine yamekwishashughulikiwa na Tume za utawala. Kwa mfano; Rais akiteua Tume kwenda kuchunguza habari ya Ihefu, ni yeye ndiye anapelekewa ile taarifa na anaweza akaiweka kwa nia ya kutaka achukue hatua lakini kwanza awe amejiridhisha juu ya mambo yaliyotokea.

Mheshimiwa Spika, sasa tukisema kila Tume iwe inakuja Bungeni, lakini kama kuna Mheshimiwa Mbunge yeyote ambaye anataka kujua chochote juu ya Tume, Bunge hili lina utaratibu wake wa kutoa taarifa. Anaweza ukauliza maswali juu ya Tume yoyote na Serikali itajibu itaeleza ni kitu gani. Lakini kuhusu hizi Tume kulikuwa na maneno yamesemwa hapa kwamba, wake za Marais wanakuwa na *NGOs* zao. Pia wanasema hizi *NGOs* zisiwepo, zinatumia raslimali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, hizi *NGOs* za Mama Anna Mkapa na Mama Salma Kikwete hazitumii raslimali za Serikali, hizi ni *NGOs* zao na kwa kweli dunia nzima *first ladies* huwa wanashughulika na jamii na ukitaka kuwa na uhakika kwa sababu mambo mengi huwa tunazungumza hapa kwa kufanya *reference* ya Amerika, hivi ungeweza ukamuacha *first lady* kama Hilary Clinton akakaa jikoni kwa muda gani? Lazima atakuwa na shughuli hivi ya kijamii anafanya, hata baada ya mume wake kutoka Ikulu anaendelea kufanya hivyo, licha ya Useneta pamoja na mambo mengine. Kwa hiyo, hizi *NGOs* ni muhimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna mwingine akasema *NGO* inaitwa *WAMA* ilitumiwa kufanya kampeni za uchaguzi. Jamani mambo ya kampeni yale yalikwisha, tukiendelea kusingiziana hapa tutapata matatizo. Eeh! Kwa sababu Salma Kikwete ni Mke wa Rais, halafu ni mwanachama wa CCM, ni Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa wa CCM, kwa hiyo na yeye alikwenda kama walivyokwenda wengine, hata Mheshimiwa Mgombea wa CHADEMA naye alikuwa na mke wake, anamuita mchumba wake walikuwa wote tu, kwa hiyo hapakuwa na tatizo. Sasa akienda Mushumbusi hakuna hoja, akienda Salma kesi, aah bwana acha hiyo. (*Kicheko*/*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nadhani hoja ni kwamba tulimaliza uchaguzi vizuri, tumeshinda na *actually* Watanzania ndiyo wameshinda, ndiyo maana wote tumo humu tu. Watanzania hawa ndiyo wamegawa nyie CHADEMA mtakuwa 23, CCM ngapi, sasa si wanagawa wakati ukifika watagawa tena? Sasa tusirudishe tena *politics* za uchaguzi humu Bungeni, tukaanza kuoneshana vidole, wewe ulikuwaje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kuzungumzia mambo mawili ambayo yatakuwa ya mwisho na nitayasema kwa ufupi.

Mheshimiwa Spika, udini, udini umesemwa humu na mimi nafurahi kweli kweli kwamba Waheshimiwa Wabunge wameona madhara yake. Wote waliosema humu walikuwa wanalalamikia udini, nataka niseme kwamba unafahamu tumepiga hatua kubwa sana nchini katika kujenga umoja na kwa kweli kama kuna *legacy* ya Wazee wale, Julius Nyerere na Mzee Karume ni kwamba walijenga msingi ambao kazi ya kuubomoa ni ngumu kweli. Mwaka jana wakati wa uchaguzi huo msingi ulitikiswa lakini ulishindikana kutikisika (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka vile vile niwatetee madhehebu ya dini kwamba hakuna dhehebu lolote ambalo lilikuwa limeamua rasmi kwamba, litafanya kampeni za siasa, halipo. Lakini madhehebu haya yanawakilishwa na watu wengi, ni kama vyama tu kila tawi sasa akitokea huko Kasisi akafanya vituko unaweza ukasema ni dhehebu, lakini ni Kasisi tu wa hapo. Makasisi hao walikuwepo, walifanya mambo ya ovyo kidogo, eeh Makasisi wa dini zote tu walifanya mambo ya ovyo, tunawajua na katika suala la mahusiano nimefanya mazungumzo na wao katika maeneo mengi kwa lengo la kuwasaidia kwa sababu umoja huu ndiyo msingi wa amani ya Tanzania. Wale wanaosema umoja hakuna, kuna utulivu, hata uuite nini umoja upo ndiyo maana umejengwa katika msingi imara kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema ukianza kuleta mgogoro wa kidini tofauti yetu haitakuwa kubwa na Ivory Coast, sisi wote ni Waafrika wala sisi siyo *specie special*, tumejengewa msingi mzuri na uongozi uliotutangulia. Kwa hiyo, tunasema na tumewaambia viongozi wetu wa kiroho tena kwa heshima kubwa kwamba tuache jambo hili kabisa na tulipige vita mpaka life. Hivi wewe ni Askofu au Imamu, uko msikitini unawaambia waumini nenda umpigie kura mtu wa dini yangu na wale watu wana vyama vyao ndani ya kanisa au Msikiti, sasa mle ndani Msikitini kwa sababu Imamu huwa haulizwi swali na Askofu haulizwi swali Kanisani, hakuna kunyoosha mkono mpaka amalize, lakini wakitoka nje wanaulizana sasa Askofu au Imamu leo amesema tupigie dini yetu, mbona yule mtu wa dini yetu siyo wa chama chetu? Nani anaamua huo ugomvi na Askofu au Imamu hayupo? *This is a serious problem* na Maaskofu wameniambia nenda uwambie wanasiasa wenzako ndiyo wanaotufuata fuata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Joseph Selasini alisema humu, nadhani alijua wanavyofuatwa fuatwa na amenituma niwaombe wanasiasa waache kuwafuata fuata watu wa dini.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nataka niombe vyombo vya habari vitusaidie katika kujenga nchi yetu yenye umoja, wasituharibie maana wakati mwingine wanasema mambo ambayo hayapo, muda sina lakini ningeweza nikawaambia. Kuna gazeti hapa linaitwa Mwananchi limeandika; ‘CHADEMA yaibwaga CCM kuhusu posho’ kulikuwa na mpira wa posho humu Bungeni? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nilileta hapa hoja ya Tume, ndani ya hoja mle ndani ya kitabu tumesema tutatazama upya posho mbalimbali kwa ajili ya kupunguza matumizi. Waziri wa Fedha amesema, sasa hoja ilikuwa iko wapi ambayo CHADEMA iliibwaga CCM? Uchochezi mtupu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, juzi Mheshimiwa Edward Lowassa alitoa maoni yake kama Mbunge tu wa Monduli, gazeti hili la Mwananchi linasema; “Vita ya Lowassa, Serikali ya JK sasa wazi’ Vita gani? Ipi? Hawa ni wachochezi na gazeti hili lina asili ya nje. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Sawa kabisa!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):** Labda angependa mambo ya nje yawe kama ya hapa, tunamwambia amechelewa, hapa hayawezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, juzi nilikuwa nimekaa pale alipokaa Mheshimiwa Samuel Sitta, lakini nilikuja hapa naumwa, nikapitia Zahanati ile pale wakanipa dawa ya mafua, ile dawa ya mafua inaweza kukufanya ukawa *drowse*, kesho nikakuta gazeti eti limenipiga picha kwamba nimesinzia. Sasa nawaambia wanipige picha niko *live* sasa. Wanafiki wakubwa hawa, wanachochea, wanataka kuleta mgogoro usiokuwa na msingi. (*Makofi*/*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi, naomba kutoa hoja. (*Makofi*/*Kicheko*)

**SPIKA:** Yako mengi, tunajitahidi kuwahimiza wajenge umoja wa Waandishi wa Habari za Bunge kwa sababu kwa kweli wanapotosha vitu vingi sana, zaidi ya hapo wanasema mimi naongoza Bunge lakini ni Mbumbumbu, sasa si unaona mambo yenyewe hayo, halafu napayuka payuka, sasa kazi yenyewe hii jamani… (*Kicheko*)

Lingine ambalo tunapenda lieleweke, Waheshimiwa Wabunge nawashukuru sana kwa sababu tunaanza kuwa pamoja, zungumzeni kwa nguvu zenu zote kujenga hoja, lakini mkitoka nje muwe marafiki, tusiwe na uadui baina ya mtu na mtu. Tukiwa humu ndani tuseme lakini tukifika huko nje tushikane mikono. Juzi tulicheza dansi na Tundu Lissu, wakasema mnaona hawa, niko kwenye gazeti mojawapo, sasa mtu wangu mmoja alikuwa anawasikiliza akaniambia aliwasikia wanasema, unawaona hawa waongo kabisa, kila siku anamwambia kaa chini, kaa chini, sasa unawaona wanachokifanya hapa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tuelewe kabisa kwamba hatuna uadui wala ugomvi ila tunataka watu wawakilishe watu kwa sauti yao na nguvu zao zote lakini tukitoka nje tunashikana mikono. Mheshimiwa Freeman Mbowe, huyu ameshiriki kwenye msiba wa mama yangu, amefika mwenyewe *physically* na wenzake wengi kule ndani Kijijini, unajua pale kijijini wanasemaje? Hawa wanasema Wapinzani, Wapinzani kitu gani? Mbona amefika kwenye msiba? Hivi kweli kwenye msiba hatuwezi kwenda? Mimi nitakwenda kwenye msiba wa mtu yeyote, sasa wananchi watuelewe tuko hapa tumeshinda, tumechaguliwa, tunakuja kuwawakilisha, tutashindana kwa hoja hapa, nje tutakaa pamoja, tutakula pamoja na tutatembea pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri asante sana, sasa mtoa hoja! (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Spika, napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niweze kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kwa mara nyingine kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa imani yake aliyoonesha kwangu kwa kuniteua kwa mara nyingine tena katika Ofisi yake na kuendelea kuniamini kufanya kazi katika kipindi kingine tena tangu alipoingia madarakani. Napenda kumuahidi kwamba nitajitahidi kufanya kazi kwa kadri ambavyo Mwenyezi Mungu amenijalia.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Lakini kabla sijaanza kuzijibu napenda nikupongeze kwa mara nyingine wewe binafsi kama mwanamke wa kwanza kuchaguliwa kuwa Spika katika Bunge hili. Tunajivunia sisi wanawake wenzako na hata wakati tunaomba kura tulitumia jina lako kama mfano wa wanawake wa kuigwa na sisi

tulichaguliwa ili tuchape kazi kama wewe. Kwa hiyo, hatuna wasiwasi kabisa na ufanyaji wako kazi na usirudi nyuma, kaza uzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati yetu na Wajumbe wote wa Kamati kwa mara nyingine kwa mchango wao katika kutusaidia na katika hoja ambazo wamezitoa. Pia napenda kuwashukuru Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira na Mheshimiwa Mathias Chikawe kwa ushirikiano wao mkubwa wakati wote tuliofanya nao kazi na pia kwa kujibu hoja nyingi ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge. Naomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia bajeti ya Ofisi ya Rais kwa kuzungumza na kwa maandishi. Aidha, napenda kutoa shukrani za pekee kwa Mwenyekiti na Makamu wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala pamoja na Wajumbe wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda niwashukuru wapiga kura wa Jimbo la Mtwara Vijijini kwa ushirikiano wao mkubwa walionipatia katika kuleta maendeleo ya Jimbo letu na pia napenda niwapongeze kwa ushindi ambao tumeupata katika Uchaguzi mdogo katika Vijiji na Vitongoji ambao tumefanya Jumapili ya juzi, hongera zao sana kwa sababu mimi sikuwepo, ni kazi zao. Napenda kuwashukuru wazazi wangu wapendwa, baba yangu mzee Abdurahman Mohamed Ghasia na mama yangu Kashu Balozi kwa malezi yao mema ambayo pia wanaendelea kunipatia. Mwisho, napenda kumshukuru mume wangu mpenzi Bwana Yahaya Muhata kwa mapenzi yake kwangu na watoto wote na uvumilivu katika kipindi cha uongozi wangu. Pia napenda kuwashukuru wanangu ambao wapo hapa Ina Ali, Seif Yahya na Nasra Yahaya kwa kuniunga mkono. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda sasa baada ya kutoa shukrani hizo niwatambue Wabunge wote ambao wamechangia katika hotuba yetu kuanzia hotuba ya Waziri wa Fedha hadi hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza, napenda nimtambue Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mwenyekiti wa Kamati na Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo, Waziri Kivuli, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa michango yao mizuri ambayo nina imani kabisa itatusaidia katika kuboresha utendaji wa kazi wa Ofisi yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda niwatambue Wabunge wote waliochangia kwa kuzungumza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa David Malole, Mbunge wa Dodoma Mjini; Mheshimiwa Sara Ali Msafiri, Mbunge wa Viti maalum; Mheshimiwa Dr. Titus Mlengeya Kamani, Mbunge wa Busega; Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Mbunge wa Rombo; Mheshimiwa Ernest Silinde, Mbunge wa Mbozi Magharibi; Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay, Mbunge wa Mbulu; Mheshimiwa Deogratias Aloyce Ntukamazina, Mbunge wa Ngara; Mheshimiwa Zainab Rashid Kawawa, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Magdalena Hamisi Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, Mbunge wa Viti Maalum. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Tundu Mughwai Lissu, Mbunge wa Singida Mashariki; Mheshimiwa Mchungaji Peter Simon Msigwa, Mbunge wa Iringa Mjini; Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido; Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa William Augustao Mgimwa, Mbunge wa Kalenga; Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Mbunge wa Kisarawe; Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mbunge wa Mkanyageni; Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Mbunge wa Korogwe Vijijini; Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi na Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mbunge Viti Maalum.(*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia kwa maandishi, naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Augustino Lyatonga Mrema, Mbunge wa Vunjo; Mheshimiwa Kapteni John Damiano Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi; Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki; Mheshimiwa Eng. Christopher Kajoro Chiza, Mbunge wa Buyungu; Mheshimiwa Prof. Peter Mahamudu Msolla, Mbunge wa Kilolo; Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi; Mheshimiwa Dr. William Augustao Mgimwa, Mbunge wa Kalenga; Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge Viti Maalum; Mheshimiwa Henry Dafa Shekifu, Mbunge wa Lushoto; Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mbunge wa Tumbe; Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mbunge wa Sumve; Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini na Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi, Mbunge wa Viti Maalum. (*Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Amina Abdullah Amour, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela; Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Jaddy Simai Jaddy, Mbunge wa Mkwajuni; Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Martha Moses Mlata, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Maselle Bukwimba, Mbunge wa Busanda; Mheshimiwa Ali Keissy Mohamed, Mbunge wa Nkasi Kaskazini; Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mbunge wa Masasi; Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Andrew John Chenge, Mbunge wa Bariadi Magharibi; Mheshimiwa Dr. Seif Seleman Rashidi, Mbunge wa Rufiji; Mheshimiwa Joyce John Mukya, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Mbunge wa Rombo. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Omary Ahmad Badwel, Mbunge wa Bahi; Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele, Mbunge wa Ngorongoro; Mheshimiwa Dr. Kebwe Stephen Kebwe, Mbunge wa Serengeti; Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha, Mbunge Viti Maalum; Mheshimiwa Mwigulu Lameck Madelu, Mbunge wa Iramba Magharibi; Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Mbunge wa Korogwe Vijijini; Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Omar Rashid Nundu, Mbunge wa Tanga Mjini; Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, Mbunge Viti Maalum; Mheshimiwa John Zefania Chiligati, Mbunge wa Manyoni Mashariki; Mheshimiwa

Felister Aloyce Bura, Mbunge Viti Maalum; Mheshimiwa Sabreena Sungura, Mbunge Viti Maalum na Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia wapo Mheshimiwa Said Arfi, Mbunge wa Mpanda Mjini; Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mbunge Viti Maalum; Mheshimiwa Subira Khamisi Mgalu, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mbunge wa Mkoani; Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza; Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagulla, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Mchungaji Dr. Getrude Rwakatare, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Seleman Saidi Jafo, Mbunge wa Kisarawe; Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo, Mbunge Viti Maalum; Mheshimiwa John John Mnyika, Mbunge wa Ubungo; Mheshimiwa Kuruthum Jumanne Mchuchuli, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine, Mbunge wa Tarime na Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine pia ni Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar, Mbunge wa Mfenesini; Mheshimiwa Stephen Julius Masele, Mbunge wa Shinyanga Mjini; Mheshimiwa George Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe; Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengeya Kamani, Mbunge wa Busega; Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge Viti Maalum; Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu, Mbunge wa Kilwa Kaskazini; Mheshimiwa Salome Daudi Mwambu, Mbunge wa Iramba Mashariki; Mheshimiwa Mussa Zungu Azzan, Mbunge wa Ilala; Mheshimiwa Augustino Manyanda Maselle, Mbunge wa Mbogwe; Mheshimiwa Aliko Kibona, Mbunge wa Ileje; Mheshimiwa Martha Umbulla, Mbunge Viti Maalum na Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vulu, Mbunge Viti Maalum. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna Mheshimiwa Dr. Faustine Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni; Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mbunge Viti Maalum; Mheshimiwa Abia Muhama Nyabakari, Mbunge Viti Maalum; Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki, Mbunge Viti Maalum; Mheshimiwa Prof. Kulikoyela Kahigi, Mbunge wa Bukombe; Mheshimiwa Sara Msafiri Ally, Mbunge Viti Maalum; Mheshimiwa Yusuph Abdallah Nassir**,** Mbunge wa Korogwe Mjini; Mheshimiwa Godluck Joseph Ole-Madeye, Mbunge wa Arumeru Magharibi; Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mbunge Viti Maalum; Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwe, Mbunge wa Kibiti; Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani; Mheshimiwa Modestus Dickson Kilufi, Mbunge wa Mbarali na Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa, Mbunge wa Kibaha Vijijini. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nianze kujibu hoja za Waheshimwa Wabunge kama ifuatavyo. Hoja ya kwanza ilitolewa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo ambaye alisema Serikali haijatenga fedha zozote za maendeleo katika mwaka huu wa fedha 2011/2012, kwa ajili ya teknolojia ya mtandao katika Utumishi wa Umma. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali huwa inatenga bajeti zake katika kila Wizara. Kwa ushahidi tu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma imetenga kiasi cha shilingi 2,071,470,000/= kupitia fungu 402 kwa ajili ya kutekeleza mtandao wa mawasiliano Serikalini. Pia

Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia imetenga kiasi cha shilingi 2,735,518,000/= kwa ajili ya mkongo wa Taifa na miradi mingine.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma tayari imeshaziunganisha Wizara ya Afya, Wizara ya Fedha, Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, Tume ya Mipango, Ofisi ya Bunge Dar es Salaam na Kituo cha Mafunzo kwa njia ya mtandao na mfumo wa Serikali mtandao. Sasa hivi tunaye Mshauri Mwelekezi ambaye anaainisha mahitaji halisi kwa ajili ya kuziunganisha Wizara zote Dar es Salaam na kuunganisha TAMISEMI Dodoma na Ofisi ya Bunge Dodoma. Ni matarajio yetu hadi kufika mwisho wa mwaka mwakani 2012 Taasisi zote za Serikali zitakuwa zimeunganishwa katika Serikali mtandao. Pia mkongo wa Taifa sasa hivi tayari umeshafika katika Mikoa 16 na Wilaya zake ikiwa ni awamu ya kwanza na sasa hivi tunaingia awamu ya pili ambapo tutahakikisha tunaunganisha Mikoa yote iliyobaki pamoja na Wilaya zilizobaki. Kwa hiyo, sio sahihi kama alivyosema Mheshimiwa Susan Lyimo kwamba hatujatenga chochote na hivyo Tanzania itaachwa nje ya TEHAMA. Napenda tusiwapotoshe wananchi wakati tunapochangia hoja zetu.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja ambayo imesemwa kwamba, mishahara haikidhi hasa kwa Walimu, Wauguzi na Waganga na kwamba wachangiaji wengi wamesema kwamba kada hizi zinalipwa mishahara midogo sana ukilinganisha na kada nyingine. Waliochangia katika hoja hii ni Mheshimiwa Susan Lyimo, Mchungaji Getrude Rwakatare, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay, Mheshimiwa Paul Philipo Gekul, Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Godluck Joseph Ole-Medeye, Mheshimiwa Yusuph Abdallah Nassir, Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki na Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa. Napenda niwahakikishie katika kufanya tathmini ya uzito wa kazi na majukumu katika Utumishi wa Umma wa kada hizi sasa hivi hasa Wauguzi na Waganga ndio watumishi wanaolipwa mishahara mikubwa ukilinganisha na watumishi wa kada nyingine wakifuatiwa na Walimu. Kwa hiyo, sio sahihi kusema kwamba wao wanalipwa mishahara midogo sana ukilinganisha na watumishi wengine.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja hapa ambayo imezungumzwa. Kwanza kuhusu kima cha chini cha mshahara, kwamba kwa nini sikutaja. Kwa mujibu wa makubaliano yetu na Vyama vya Wafanyakazi tumekubaliana kwamba kima cha chini cha mshahara ni siri yao, ni siri yetu tusikitangaze. Hata hivyo, kabla ya kufikia kima cha chini cha mshahara huwa tunakuwa na Baraza la Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma ambapo Serikali inawakilishwa na Vyama vya Wafanyakazi vyenyewe vinashiriki vikiwawakilisha wafanyakazi. Katika majadiliano yale tumekubaliana kima cha chini na ndicho hicho hicho ambacho kitalipwa. Kwa maana ya *TUCTA* wanafahamu kima cha chini cha mshahara ambacho tumekubaliana. Ndiyo maana katika bajeti yangu nikasema kima cha chini cha mshahara pamoja na mambo mengine tutazingatia mfumko wa bei lakini pia makubaliano ambayo tumefikia sisi pamoja na Vyama vya Wafanyakazi. Katika hotuba yangu pia nilisema kwamba ongezeko nililolizungumza la asilimia 40 ni kiasi cha pesa ukilinganisha na pesa ambazo tulitenga mwaka 2010/2011 ambacho ni

shilingi 9,038,000,000/=, ile ndiyo asilimia 40. Kwa hiyo, sio asilimia 40 kwamba ndio ongezeko la kima cha chini cha mshahara.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti mbadala ya Kambi ya Upinzani walisema kwamba kima cha chini kiongezeke mpaka shilingi 315,000/=. Baada ya kukokotoa na kuiangalia bajeti mbadala ya Kambi ya Upinzani mapato yao ya ndani walisema watakusanya shilingi trilioni 9,032,000,000/=, hiyo ilikuwa ni pamoja na mapato ya Halmashauri. Mapato tu yenyewe peke yake ya ndani ukiacha Halmashauri ni shilingi trilioni 8,681,000,000/= na mapato ya Halmashauri ni shilingi 351,000,000,000/= . Sasa kwa kulipa mshahara kima cha chini 315,000/= unachukua trillion 7,971,649,000/= sawa na asilimia 81 ya bajeti mbadala ya Kambi ya Upinzani. Katika mapato yao ya ndani Kambi ya Upinzani ukilipa mishahara inabaki shilingi trilioni 1,961,000,000/=. Hebu tujiulize kila mtu alivyokaa tunaweza kuiendesha nchi hii kwa shilingi trilioni1,961,000.000/=? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini katika bajeti yao mbadala walisema miradi ya maendeleo watatumia pesa za ndani shilingi trilioni 3,193,000,000/=. Sasa baada ya kulipa mshahara wamebakiwa na shilingi trilioni 1,961,000,000/= kabla ya matumizi mengineyo. Sasa athari za kutumia bajeti yao, bajeti mbadala ni kwamba, baada ya kulipa mishahara, nchi itakuwa imesimama, hatuweza kununua madawa, hatutaweza kununua chakula cha wagonjwa, hatutaweza kulipia umeme kwenye ofisi yoyote ya Serikali na baadhi ya watumishi ambao si wa umma tutashindwa kuwalipa mishahara na nchi haitakwenda. Nina wasiwasi kama Kambi ya Upinzani, kweli inao wachumi ambao walikaa kwa kweli, wakaijadili hii bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshangaa Mchumi mwenzangu na napenda ni-*declare interest* kwamba na mimi ni Mchumi. Niliipitia ile Bajeti, ni kiini macho ambacho wananchi walikuwa wanadanganywa wakiwemo Watumishi wa Umma kwamba wanaweza kuwalipa shilingi 315,000, walichukua tu namba wakazirundika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hoja nyingine sambamba na suala la mishahara ni suala la posho au kwa lugha nyingine ujira wa *mwia* kama ilivyoletwa na Mheshimiwa Shibuda. Katika utumishi wa umma tunao utaratibu wa kujadiliana kupitia Baraza la Majadiliano la Utumishi wa Umma na katika kuangalia posho zipi tuzihuishe na posho zipi tuziache tutapitia utaratibu huo huo, tutawashirikisha watumishi wa umma kupitia Mabaraza yao kama utaratibu ulivyo. Lakini kwa Waheshimiwa Wabunge napenda tuwe wakweli, tusiwe wanafiki, tusiwadanganye wananchi. Tunasema hapa hatutaki posho wakati hizo posho tumeshazikopea kwa miaka mitano. Posho zote tunazosema kwamba ziondoshwe tulishakopa na kuchukua mikopo ya shilingi milioni 200, zaidi ya asilimia 80 ya Waheshimiwa Wabunge, tunawadanganya wananchi kwamba hatutaki wakati mmeingia Mkataba na Benki mtalipa na nini na dhamana ya mikopo ile ni posho hizo ambazo leo mnajifanya mnazikataa. Ndiyo maana Serikali ikasema tutaangalia kama kutakuwa na ongezeko la mishahara ya kuweza kulipa hayo madeni tuliyokopa wakati huo huo tukaweza kuhuisha baadhi ya mambo. Kwa hiyo tuache kudanganya wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja ya kuanzisha mfumo ambao utalazimisha kila mtumishi wa umma kuonyesha majukumu aliyopangiwa na utekelezaji wake. Kuwepo mipango mikakati ambayo itafanya *OPRAS* kutekelezwa vizuri. Napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba kila Ofisi ya Umma inao mpango mkakati na upimaji wa *OPRAS,* sasa hivi umewekwa kisheria na pia tunao utaratibu wa kuwa na Mikataba ya Huduma kwa Wateja, lengo ni kuhakikisha tunawabana watumishi wa umma. Kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge tunapokwenda katika Ofisi za Serikali tuombe huduma kwa kufuata Mikataba ya Huduma kwa Mteja na pale ambapo mnaona tunababaishwa tusiogope kuwaumbua watumishi wa umma ambao wanatubabaisha au wanatoa lugha zisizo sahihi ili tuweze kuwachukua hatua zilizo thabiti.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi tunazungumza hapa, lakini mimi nakaa pale utumishi hakuna hata Mheshimiwa Mbunge mmoja anakuja ananiambia kuwa, nimekwenda ofisi fulani nimejibiwa vibaya, kila ofisi tunao Maafisa Malalamiko. Tunayo masanduku ya maoni ukifika hujahudumiwa vizuri tunaomba nendeni kwenye dawati la malalamiko, jazeni yale ambayo mmetendewa ambayo si haki ili tuweze kuwachulia hatua watumishi wanaohusika.

Mheshimiwa Spika, pia kuna hoja kwamba mazingira mengi katika Ofisi zetu sio rafiki kwa walemavu. Ofisi yangu imetoa mwongozo wa walemavu wa mwaka 2009 ambao unataka Ofisi zote za Umma zinazojengwa kuhakikisha kwamba inaweka miundombinu ambayo ni rafiki kwa walemavu na ofisi ambazo zimejengwa zamani na zenyewe huwa tunazitaka zihakikishe wanarekebisha miundombinu yao kuhakikisha kwamba walemavu wanaweza kupata huduma katika ofisi hizo bila usumbufu wowote.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja iliyotolewa kwamba jinsi tunavyoongeza mishahara tunaweka mishahara kwa ubaguzi. Napenda nilihakikishe Bunge lako kwamba si lengo letu kuwabagua watumishi katika kuwapangia mishahara. Katika kuweka vima vya mishahara vya kuanzia wanaotoka Vyuo Vikuu na wanaotokea katika vyuo mbalimbali huwa tunaangalia mambo mengi. Kwanza tunaangalia uzito wa kazi, tunaangalia muda alioutumia mtu katika kusomea ile kada yake. Mfano, Daktari anachukua zaidi ya miaka mitano, huwezi ukaja ukamlinganisha mshahara wake na labda Mchumi au Mhasibu ambaye amechukua miaka mitatu. Lakini pia katika kuangalia mishahara ya watumishi wa juu na wa chini na wa kada tofauti pia tunaangalia soko la ajira na pia tunaangalia uwezekano wa kuwabakisha watumishi hao katika utumishi wa umma. Katika siku za nyuma tumeona athari zilizojitokeza baada ya kuhakikisha kwamba watumishi wa kada tofauti tunawalipa mishahara inayofanana. Madhara yake ni kwamba, wataalam weledi wa kada zile ambazo ni adimu wengi wanaondoka katika utumishi wa umma. Kwa hiyo tunaweka mishahara hiyo tofauti tofauti, lengo ni kuhakikisha kwamba tunawabakisha na kuangalia katika soko la ajira wenzetu wanalipa nini?

Mheshimiwa Spika, pia Kamati ya Mheshimiwa Mbunge mwenzetu ya Mheshimiwa Ntukamazina walitushauri katika kupanga hii mishahara na kuangalia *gap* ya mishahara basi tuone uwezekano wa kuwaweka watumishi katika makundi mawili. Unaposema kima cha juu cha mishahara na cha chini basi umuangalie labda mshahara wa

Afisa Utumishi Daraja la Pili aliyetoka Chuo Kikuu na Katibu Mkuu labda kiongozi kwa sababu ndiyo nafasi ambayo tunategemea ataifikia kwa elimu yake aliyonayo na mhudumu wa Ofisi mshahara wake ulinganishe na kima cha juu cha *OS* ambayo ndiyo nafasi ya juu atakayoifikia. Sio sahihi kumlinganisha mhudumu mshahara wake na Katibu Mkuu Kiongozi au Mhudumu na Daktari aliye-*specialize* useme *gap* ya mshahara isiwe kubwa. Vinginevyo Madaktari wote watatukimbia. Nilipenda nionyeshe kiasi gani tunafanya hivyo na si lengo letu kuweka ubaguzi.

Mheshimiwa Spika, naomba niombe radhi kwamba nilimsahau Mheshimiwa Susan L. Kiwanga, ambaye alichangia kwa maandishi na napendas nimtambue.

**SPIKA**: Na Mheshimiwa Esther Matiko

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Na Mheshimiwa Esther Matiko, samahani naomba radhi na kama wapo wengine naomba wanieleze ili niweze kuwatambua.

Mheshimiwa Spika, pia tuliombwa kushusha kiwango cha *PAYE* kutoka asilimia 14 hadi asilimia tisa kwa kiwango cha chini na kutoka asilimia 30 hadi 27 kwa kima cha juu. Katika Baraza la Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma ambalo tulikaa, ajenda zetu mmojawapo ilikuwa kujadiliana kima cha chini lakini pia kuangalia uwezekano wa kupunguza kodi na ajenda hii tumekubaliana kwa mwaka huu tuache ili tuipe muda Serikali wa kuangalia kwa undani zaidi. Kwa hiyo, ni imani yetu kwamba, mwakani Serikali itaweza kuliangalia hili. Lakini pia ikumbukwe kwamba Serikali ya Awamu ya Nne katika kipindi cha miaka mitano tumeshusha asilimia hii kutoka 18 hadi kufikia asilimia 14 na ni lengo letu kuendelea kushusha hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Spika, kuna suala ambalo pia lilizungumzwa la tofauti zilizopo katika mafao zinazosababishwa na aina ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, kuwe na namna moja ya kukokotoa mafao ya watumishi. Hoja hii ilichangiwa na Mheshimiwa Godfrey Winston Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki na Mheshimiwa Susan Lyimo. Kwa kutambua tatizo hili Serikali imetunga Sheria ya Mdhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na jukumu kubwa la mdhibiti ni kuhakikisha kwa kadri inavyowezekana kuainisha na kuoanisha *formula* zinazotumiwa katika Mifuko mbalimbali ili kupunguza tofauti ya mafao na mpaka sasa hivi katika Mfuko wa *PPF* ambao ulikuwa unalalamikiwa kwa kiasi kubwa na sasa hivi kile kikokotoo kimebadilishwa kutoka moja ya mia tisa na sitini hadi moja ya mia sita. Hiyo ni mojawapo ya mafanikio ya Mfuko huo.

Mheshimiwa Spika, pia kuna hoja ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Susan Lyimo kwamba Serikali itafute fedha za dharura ili Wahadhiri wastaafu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine waanze kupata pensheni yao ya kila mwezi. Kwanza suala la Walimu wa Vyuo Vikuu ambao walikuwa wanalipwa kwa kile tunaita *SSS*, Mfuko huu ulikuwa ni Mfuko ambao ulikuwepo wakati bado tukiwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Baada ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuvunjika, Serikali ilianzisha Mfuko wa *PPF* na Wahadhiri ambao walikuwa katika Mfuko huo waliombwa waingie katika Mfuko wa *PPF* lakini kwa wakati huo kwa

sababu Mfuko huo wa *SSS* ulionekana ni *superior* ukilinganisha na *PPF,* Wahadhiri hao walikataa.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kuwa kulianzishwa Mfuko wa *PPF*, wanachama ambao walikuwa wanaajiriwa kama Watumishi walikuwa wanajiunga na *PPF*. Kwa hiyo, Mfuko huu sasa ukawa haupati wanachama, kwa hiyo, ukawa unadhoofika kifedha mwaka hadi mwaka. Baada ya malalamiko mengi ambayo yalitolewa na Wahadhiri Serikali ililiangalia hilo na kuamua Wahadhiri ambao bado wapo hawajastaafu waingizwe katika Mfuko wa *PPF* kwa Serikali kuchangia shilingi bilioni tisa ndani ya kipindi cha miaka kumi na ile pesa yao ambayo ilikuwa katika Mfuko huo wa mwanzo basi iingizwe kule iwe kama mchango wao na Serikali iwachangie ili kuhakikisha Mfuko wa *PPF* haufi na hii ni kuanzia mwezi Machi, 2011.

Mheshimiwa Spika, sasa kuna hoja kwamba waliostaafu nyuma na wenyewe waingizwe haraka. Hili si suala la dharura lakini pia ni suala la huruma ya Serikali. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge waiachie Serikali ilifanyie tathmini na kutafakari na kuona itakavyokuwa. Kwa hiyo, si suala la dhuluma kwamba kuna mtu alikusudia kuwafanyia dhuluma. Isipokuwa Wahadhiri wenyewe kwa kipindi hicho walikataa kuingia katika Mfuko ambao Serikali iliuanzisha. Kwa hiyo, sasa hivi yule Mdhibiti ndiyo anaufanya *actuarial valuation* Mfuko wa *PPF* na Mifuko mingine kuangalia uhai wake na kuona ni kiasi gani tunaweza kufanya huruma kwa yaliyopita.

Mheshimiwa Spika, pia kuna suala ambalo lilizungumzwa la kwamba kuna tofauti ya mafao katika Mifuko. Suala hili linafanyiwa kazi na Mdhibiti, lengo ni kuhakikisha pia si tu inatoa maslahi bora kwa kila Mfuko ambayo pia hayatofautiani lakini pia kuhakikisha kwamba, Mifuko hii inakuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limezungumzwa sana ni suala la kwa nini Serikali imeuza nyumba za Serikali ambazo zilijengwa kwa fedha za walipa kodi na kusababisha baadhi ya Mawaziri kukaa mahotelini kwa gharama kubwa. Nyumba nyingi za Serikali ambazo ziliuzwa miaka iliyopita zilikuwa katika hali mbaya na hivyo kufanya gharama ya kukarabati kuwa kubwa. Kwa hiyo, Serikali iliziuza nyumba hizo ili kuweza kujenga nyumba nyingine ikiwa ni pamoja na pesa zilizopatikana na Serikali kuongeza pesa zingine. Hadi sasa Serikali imekwishajenga nyumba 1,000 kati ya hizo 82 zimejengwa Dar es Salaam na bado tunaendelea na ujenzi wa nyumba katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya viongozi walioteuliwa walikaa Hotelini si kwa sababu wote Serikali haikuwa na nyumba, isipokuwa baadhi ya nyumba zilikuwa zinafanyiwa marekebisho kwa sababu Mawaziri ambao hawakupata fursa ya kuwa Mawaziri wakati huu walivyotoka haiwezekani mwingine aingie tu lazima urekebishe hapa na pale. Kwa hiyo, kikubwa tulikuwa tunafanya marekebisho ya nyumba hizo na ni imani yangu kwamba suala hili lilijadiliwa sana katika Bunge lako na naamini kwamba lilimalizwa.

Mheshimiwa Spika, suala la kuanzisha pensheni maalum ya wazee wote nchini wenye umri wa miaka 65 na kuendelea bila kujali walikuwa wanafanya kazi au la. Suala hili limechangiwa na Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Mariam R. Kasembe na Mheshimiwa Martha M. Mlata. Hawa wazee wamegawanyika katika makundi mawili, wapo wazee ambao wanapata pensheni kwa kuwa walikuwa wameajiriwa rasmi na kundi la pili ni wazee ambao hawakuwa na ajira rasmi. Kupitia Bunge hili nawaomba wananchi wote wawe na utamaduni wa kujiwekea akiba za uzeeni, lakini hata hivyo sasa hivi Serikali kama ambavyo wengine wametangulia kusema Mdhibiti naye katika mapendekezo yake ambayo ameyatoa ni pamoja na hili na Wizara ya Kazi pia ilishafanya uchambuzi wa hili. Kwa hiyo, Serikali inalifanyia kazi kuangalia ni gharama kiasi gani zitahitajika katika kuwapatia pensheni wazee ambao hawakuwa wanafanya kazi yoyote.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la uhamisho wa watumishi waliobainika kufanya kazi na kufanya makosa mbalimbali ya ukiukwaji wa kazi. Ofisi yangu ilishatoa Waraka kwamba ni marufuku kumhamisha mtumishi ambaye ameharibu eneo moja na kupelekwa eneo lingine. Wakati mwingine wanahamishwa tu kutokana na mwajiri au Mamlaka ya ajira iliyoko juu kwa kutokujua kama Mtumishi huyo alifanya kosa kule alikotoka. Lakini hata hivyo pale anapobainika huwa tunafuta uhamisho huo na kuhakikisha kwamba anarudi kule ambako amefanya makosa ili aendelee na mashtaka yanayomkabili katika eneo lile mpaka yatakapokwisha.

Mheshimiwa Spika, pia Waheshimiwa hao na Waheshimiwa wengine walisema kwamba uhamisho wa watumishi walio katika ndoa huwatenganisha na kusababisha uwezekano wa kupata UKIMWI hususan Walimu, ni vizuri sana tuepushe vifo vya Walimu kwa kuwaruhusu waungane katika ndoa zao. Ofisi yangu haijazuia kuwaweka pamoja walimu ambao ni wanandoa, wakati mwingine kinachogomba ni nafasi kule tu anakohamia kwa sababu wakati mwingine huwa tunataka atafute mtu abadilishane. Lakini wakati mwingine Dar es Salaam hapo hakuna nafasi na kila Mwalimu anakwambia yeye anahamia Dar es Salaam na ili kurahisisha uhamisho huo mwanzo tulikuwa tunaratibu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, suala hilo tumewaachia TAMISEMI ili walifanye kwa urahisi na sasa hivi malalamiko mengi sana yamepungua ukilinganisha na wakati ule ambapo sisi tulikuwa tunasimamia uhamisho huo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rose Kamili na Mheshimiwa Paulina Gekul walisema kwamba kuna suala la watumishi ambao wanaishi na Virusi vya UKIMWI na kwamba hawapatiwi stahili ambazo ofisi yangu ilitoa mwongozo kwamba wapatiwe.

Mheshimiwa Spika, ni jukumu la kila Mwajiri, kila Halmashauri, kila Wizara na kila Taasisi kuhakikisha kwamba inatenga pesa kwa ajili ya kuwahudumia watumishi ambao wameathirika na Virusi vya UKIMWI. Wanapotaka kwenda kutibiwa kama ni eneo anahitaji nauli, apewe, kama anahitaji kupewa *night,* apewe na kama anahitaji *special diet* apewe. Kwa hiyo, ni jukumu letu sisi Wabunge katika Halmashauri zetu kuhakikisha Watumishi ambao wameathirika na Virusi vya UKIMWI wanapata haki hiyo.

Mheshimiwa Spika, kila Halmashauri ninapotembelea kitu cha kwanza huwa nauliza kuhusu hilo, sasa hivi tumeweka mashindano, taasisi ambayo inawahudumia vizuri Watumishi wake ambao wamepata VVU huwa tunawapa tuzo kila mwaka kipindi cha kushughulikia suala zima la UKIMWI katika wiki ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la ucheleweshaji wa vibali vya ajira na kwamba tuliangalie upya, tumekubali kwamba sasa hivi tunaliangalia kwa sababu kuna Sekretariati ya Ajira, tunaangalia ni kwa kiasi gani tunaweza tukarahisisha.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limezungumzwa sana ni kuhusu suala la Sekretariati ya Ajira kwamba ni kwa nini tumeamua kuanzisha Sekretariati hiyo na hasa kuchukua majukumu ya Serikali za Mitaa. Sekretariati ya Ajira inafanya usaili kwa taasisi zote za Serikali siyo Halmashauri tu, ni Wizara, Wakala za Serikali zote. Lengo ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na utumishi wa umma wenye mtazamo wa Kitaifa, kwa sababu ilifika mahali sasa Utumishi wa Umma umekaa kikanda, umekaa kikabila, umekaa kidini. Kuna baadhi ya Wizara ilikuwa ukienda unajua kwamba Wizara hii ni ya kabila fulani na Wizara hii ni Kabila fulani. Lakini hata kwenye Halmashauri huku maeneo mengi mnalalamika kwamba walioajiriwa pale ni ma-*expert,* ni kwa sababu Wakurugenzi na Maafisa Utumishi walikuwepo pale walikuwa wanahakikisha wanaajiri ndugu zao ambao wengi siyo wa maeneo yale. Hata maeneo mengine tulikuwa tunagawana Mwenyekiti, Madiwani na kadhalika bila kufuata vigezo vya kuajiri.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kwamba tunarahisisha tutafungua Ofisi za Sekretarieti za Ajira kila Mkoa. Sasa hivi tunazo ofisi hizi kila Kanda. Tutakapokuwa tunafanya usaili kabla hatujafungua hizo ofisi kwa sababu sasa hivi tunazo ofisi za Kanda, tutafuata eneo hilo hilo. Hata sasa hivi wanapoomba kazi tunaomba waoneshe wako wapi, ili tunapowapangia vituo vya kufanyia usaili kama wewe umesema upo Mwanza tutakupangia kituo kilichopo karibu na Mwanza. Kama umesema upo Dar es Salaam wakati upo Kigoma ndiyo unajitesa mwenyewe lakini lengo ni kuhakikisha kila mtu anafanyiwa usaili katika eneo lililo karibu na yeye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka nilizungumzie ni suala la Watumishi hewa. Ni kweli tumefanya uhakiki wa watumishi hewa tumegundua mpaka sasa hivi zaidi ya bilioni saba zimetumika kulipa Watumishi hewa, ni tofauti na Mheshimiwa Gekul aliyesema trilioni mbili, hapana, nadhani ilikuwa tatizo katika kutofautisha namba hizo katika trilioni na bilioni.

Mheshimiwa Spika, ni hatua gani tumezichukua mpaka sasa hivi? Kwanza, wale wote ambao walibainika bado wanaendelea kulipwa mishahara hewa tumewaondoa kwenye *payroll*.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa*
*muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ni kengele ya pili hiyo.

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Kama nilivyosema tunaanza kutumia ule utaratibu tuliokubaliana, atakayetaka kutumia mshahara wa Waziri ni Kifungu cha 32 halafu tutatumia dakika datu, ukishauliza Waziri pia atajibu dakika tatu, halafu haurudii tena. Ukitaka kutoa shilingi ni hivyo hivyo dakika tatu, utaungwa mkono na wenzio dakika mbili, halafu utakapojibiwa utatumia dakika mbili.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**FUNGU 20-OFISI YA RAIS IKULU**

Kif**.** 1001 *Admnistration and General…Shs*. 8,524,917,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo Juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**VOTE 30- OFISI YA RAIS NA SEKRETARIETi YA BARAZA LA MAWAZIRI**

Kif.1001 *Admn. and General*................Shs.196,403,880,000/=

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru, Fungu la 30, Kifungu ya 1001, *programme* ya 10, Kasma 229900, *operating expenses*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliomba ufafanuzi kuhusu matumizi ya kifungu hiki, kwa kuwa kwanza Kanuni za Bunge zimekiukwa kwamba hatukupewa randama yenye ufafanuzi wa matumizi, lakini kwenye maelezo ya Waziri amesema kwamba nimetaka kujua matumizi ya bajeti ya Usalama wa Taifa. Kwenye maelezo yangu sikuomba matumizi ya bajeti ya Usalama wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kwa undani wake kinahusu TAKUKURU shilingi bilioni takriban 43, ukiangalia kwenye Randama, kinahusu matumizi ambayo yameitwa Matumizi ya Kitaifa, bilioni 135 bila kutolewa maelezo yoyote, na kinahusu ardhi milioni 18, Mazishi milioni 12, *Consultancy* milioni 15 na matumizi mengineyo.

Mheshimiwa bado nahitaji ufafanuzi kuhusu bilioni 135 zilizopo kwenye kifungu hiki. Kwa kuwa pamoja na masuala ya Usalama wa Taifa, naelewa kwamba Kifungu hiki ndicho kinachotumika vibaya kwenye matumizi mengine ya anasa na ubadhirifu.

Naomba maelezo kuhusu kifungu hiki ambacho kina shilingi takriban bilioni 135 kwa sababu maelezo ambayo yametolewa na Waziri hayajitoshelezi kabisa. Kama maelezo yatakayotolewa hayataniridhisha nitaomba kutumia Kifungu cha kushika shilingi ili tupewe maelezo ya kina ili Bunge lisije likatumika kama *rubber stamp* kupitisha kifungu hiki.

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maelezo kuhusu kifungu hicho 229900, ni kweli kifungu hiki kinacho jumla ya shilingi 179,506,554,000/=. Katika mgawanyo wa pesa hizi zipo za TAKUKURU, ambazo ni kama bilioni 43 na zipo hela za Idara ya Usalama wa Taifa ambazo ni shilingi mia moja thelathini na tano na milioni mia saba, *breakdown* ya pesa hizi hatukuziweka na hatutaziweka kwa sababu siyo busara kuwekwa kwa matumizi ya pesa kwa idara yetu hadharani kama hivyo. Ni idara ambayo pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Mnyika kwamba kuna *extravagance* lakini siyo kweli, hakuna matumizi mabaya, hakuna matumizi ya anasa, ni matumizi ya kazi, malipo ya mishahara ya vijana wanaofanya kazi hii, *operating expenses* ya magari, nyumba na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza pesa hizi kwa kweli siyo nyingi na wala hazitoshi kuendesha idara hii.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja ya kuondoa shilingi kwenye kifungu hiki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge ni dakika tatu endelea.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru, nakubali kabisa kwamba masuala ya Idara yetu ya Usalama ni ya siri, hilo nalikubali kabisa. Lakini Bunge lako Tukufu linajadili bajeti ya Jeshi hatuingii kiundani sana, lakini maeneo ya kimsingi ya bajeti huwa yanapitiwa, lakini pili kwenye Kamati huwa wanapewa *briefing* pamoja na kwamba wananyang'anya makabrasha lakini huwa wanapewa *briefing*. Lakini kwa kifungu hiki taratibu hizo hazikufuatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetaka maelezo vile vile, kwamba kwa nini Kanuni za Bunge zimekiukwa kwa sababu nimeelewa kilichopo kwenye Randama. Lakini Wabunge wengine wengi hapa pengine walikuwa hata hawaelewi kwamba TAKUKURU ipo kwenye kifungu hiki, nimehoji vile vile kwa nini Kanuni za Bunge zimekiukwa Wabunge hatukupewa nakala ya Randama ili tunapojadili matumizi ya Serikali tujadili tukiwa na taarifa zote zilizokamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu na la msingi sana, Bunge lina wajibu wa kuisimamia Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 63, kwa mambo yote iwe mambo ya Jeshi au Ulinzi, kuna mipaka ya taarifa, lakini kuna taarifa za msingi za kiutekelezaji. Hotuba ya Waziri wa Mahusiano ambayo kwa mujibu wa *instrument* iliyotolewa na Rais kuhusu majukumu yake, hotuba ya Waziri wa Mahusiano, hotuba ya Waziri wa Utumishi, hawakuzungumza chochote kuhusiana na utendaji kazi wa Idara ya Usalama wa Taifa

kama sehemu ya Utekelezaji wa majukumu ya Serikali ya mwaka uliopita. Ndiyo sababu bado nasisitiza sana, kwa niaba ya wananchi, kwamba pamoja na usiri wote wa Usalama wa Taifa na kila kitu, lakini ni lazima kwa sababu nilihoji mambo ya msingi, kwamba Usalama wa Taifa ulikuwepo kwenye Tume ya Kuchunguza Migogoro ya Ardhi Dar es Salaam, Tume iliyoundwa na Mkuu wa Mkoa wakati huo akiwa Mheshimiwa Lukuvi, ndani ya taarifa ile ya Tume pamoja na siri ina mapendekezo ya mambo ambayo Usalama wa Taifa inatakiwa kufanya, nikahoji mambo mengine ni *public*, Usalama wa Taifa umeyafanyaje yale ambayo ni ya wazi ya umma, sikupewa ufafanuzi. Hapa ndiyo sehemu ambayo tunahoji utekelezaji wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nitaomba kupata ufafanuzi kuhusu kifungu hiki lakini kuhusu kukiukwa kwa Kanuni na kuhusiana na wajibu wa Usalama wa Taifa katika kulinda mali za wananchi iwe ni viwanja, iwe ni nini, kama ambavyo nimeeleza kwenye sakata la viwanja vya wazi kule Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo.

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti naomba kutoa maelezo yafuatayo kuhusu suala la Randama; tumeambiwa na Ofisi ya Bunge tulete Randama nakala kumi, tumeleta. Nafikiri Wizara zote zitaambiwa hivyo hivyo wanaleta kumi kumi na sisi tumeleta zetu kumi. Sasa kama Mheshimiwa hakupewa ama hakustahili kupewa sijui, kwa sababu hatukuambiwa tugawe kwa kila mtu, tunagawa kumi na tumeleta kumi kama tulivyoelekezwa na Ofisi ya Spika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naambiwa pia Randama yenyewe ilipokelewa kwa mujibu wa taratibu. Kwa hiyo, suala la randama kwa kweli halipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Bunge hili kupima utendaji kazi wa Idara hii sijui tunapimaje, nadhani turidhike na hali hii ya usalama wa nchi yetu ambayo ipo, ni kielelezo tosha cha jinsi gani Idara hii inafanya kazi vizuri. Hatuwezi tukakaa tunapima maana hakuna vigezo hivyo, anayejua kazi zao na kuzipima ni nani kati yetu humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mara yangu ya pili kuingia ndani ya Bunge hili na huko nyuma nilikuwa nakuja kama Afisa, sijawahi kuona hata siku moja Wabunge wote mahiri waliokuwepo wakihoji kifungu hiki. Kwa mara ya kwanza leo nasikitika, tunalazimika hapa kuieleza dunia ni nini Idara yetu ya Usalama inafanya, hatustahili kufanya hivyo. Tunatakiwa tuwe wazalendo ndugu zangu, Idara hii inatulinda sisi ni kwa ajili ya usalama wetu sisi na usalama wa nchi yetu. Hatuwezi kutoa hizi zote *otherwise* tutakuwa hatuna haja ya kuwa na Idara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ambayo mnasema ni ya siri leo ghafla sasa inakuwa kila mtu anajua, ninapozungumza hivi wananiona hata Ulaya.

**MWENYEKITI**: Tumemaliza, kwa sababu kinachotakiwa ni kwamba mwenye hoja alishasimama angeungwa mkono, hakuungwa mkono, sasa hivi ni yeye tu ataweza kujibu basi.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa nashukuru. Kwanza kuhusu Randama, Kanuni ya 99(4) imeeleza bayana utaratibu wa uwasilishaji wa Randama, kwa mujibu wa taratibu za Kibunge ambazo naamini Mwenyekiti ana uzoefu nazo sana, hati ikishawasilishwa mezani ni *public* na inatakiwa kutolewa kwa Wabunge wote, jambo ambalo halijafanyika. Kwa hiyo, hili ni jambo ambalo ni Wizara ikakiri udhaifu na kuahidi kwamba itarekebisha kwenye bajeti zinazofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pili, sijaomba kazi za siri za ndani za majukumu ya ki-*intelligency* …

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, kwanza kabisa nielezee kuhusu Randama. Kwa mfano, kesho Wizara ya Makamu wa Rais itasoma hotuba yake, kwa hiyo, Randama ilitakiwa iwekwe leo, kwa hiyo, tutaangalia kama jana hatukuweka Randama za Ofisi tulizosoma leo. Lakini wakati huo huo, Mbunge anapopewa Randama kama kweli ana jambo lake anatakiwa atukumbushe, kwamba hatujaona kitu kama hicho mpaka tulipofikia *stage* hii hatukupata taarifa, kwa hiyo, kwa sababu ya hoja hii tumekubaliana kwamba baada ya hapo tunapiga kura.

Waheshimiwa Wabunge sasa tunapiga kura kwamba Mheshimiwa Mbunge shilingi yake akae nayo ama airudishe. Kanuni haisemi zaidi ya hapo. Kwa hiyo tunapiga kura kuhusu fungu hili.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mjumbe aliyetoa hoja alipaswa aungwe mkono, je aliungwa mkono?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, hapana. Kwenye shilingi hawaungi mkono isipokuwa kama akishatoa yeye kama mtu angetaka kuchangia angesimama akachangia lakini haungwi mkono kwa maana ya watu kumi. Hii haihusiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya Mheshimiwa John J. Mnyika ilikataliwa na Bunge)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo Juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif.1002 - *Finance and Accounts*…………Shs.407,689,000/=

Kif. 1003 - *Policy and Planning*……………Shs. 404,607,000/=
Kif.1004 - *Internal Audit Unit*……………......Shs.263,991,000/=
Kif.1005 - *Information and Comm.*
*Technology Unit.............................Shs. 226,334,000/=*
Kifungu 2001 – *Cabinet Secretariat*………………..Shs. 1,337,511,000
Kifungu 2002 – *Government Communication* …….Shs. 340,270,000
Kifungu 2003 – *Good Government*…………………..Shs. 469,377,000
Kifungu 2004 – *Public Service Appeal*………………..Shs. 383,685,000
Kifungu 2005 – *Public Sector Reform*
*Coordination Unit*..................................Shs. 282,379,000

**FUNGU 32 – OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA**

Kifungu 1001 - *Administration and HR Mgt. Divisio*....Shs. 9,049,230,060

**MWENYEKITI:** Naomba niwaandike wote. Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Tundu Lissu, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mheshimiwa David Silinde, Mheshimiwa John John Mnyika, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Susan Kiwanga, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, kila mara nakusahau. Kuna mwingine? Tunaanza na Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri juu ya namna gani Sekretarieti ya Ajira inavyofanya kazi na mipango yake na matarajio ya kufungua Ofisi za Sekretarieti ya Ajira katika Mikoa yote Tanzania. Lakini *vote* hii haikupangiwa fedha za maendeleo. Kwa hiyo, nilitaka nijue kwamba Mheshimiwa Waziri, atoe matumaini kwamba ni kweli hizi ofisi zitafunguliwa katika Mikoa yote Tanzania? Ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ufafanuzi kwamba ni kweli tutahakikisha kwamba tunafungua hizo ofisi kwa kuomba majengo katika Ofisi za Serikali na pale ambapo tutashindwa tumeweka fedha kwa ajili ya kukodi kwa kuanzia. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi, naelewa kwamba Mheshimiwa Waziri hakupata muda wa kumaliza masuala mengi ambayo Kambi ya Upinzani tulikuwa tumeomba tupatiwe maelezo.

Labda naomba kuuliza suala moja tu kuhusu suala zima la watumishi hewa. Suala la watumishi hewa ni suala ambalo limeendelea kutafuna uchumi au fedha za wananchi ambao ni walipa kodi.

Mheshiimwa Waziri, nilitaka atueleze wanakuja sasa na mkakati gani kwa sababu mimi naamini hakuna watumishi hewa, fedha hizo lazima kuna mtandao mkubwa wa

watumishi na walipaji. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kujua kama wamefanya utafiti wamejua ni watu gani na watu hawa wamechukuliwa hatua gani na Serikali, sasa inakuja na mkakati gani ili kuhakikisha kwamba tunapoingia katika mwaka huu wa fedha hatutakuwa tena na huo msamiati wa watumishi hewa. Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taasisi ambazo tayari tulishafanya uhakiki wa watumishi hewa, tuliwapelekea wenzetu wa TAKUKURU na walikwenda kwa sababu tulianza na Wizara ya Elimu na Wizara ya Afya. Wizara ya Elimu ilikuwa ni sekondari zote nchi nzima na tayari wameshamaliza hiyo kazi ya kupita wana *trace* ni akina nani wamehusika kwa Tanzania na wameunda kikosi kazi ambacho na chenyewe kilikuwa kinafanya *forensic audit* kwa kuangalia fedha zilizotoka hazina na mtiririko mzima kwa sababu maeneo mengine wamesema wamerejesha na kuangalia ni akina nani waliohusika na tumekubaliana sasa hivi kwa sababu wameshafikia hatua ya juu wawe wanatupa taarifa kila robo mwaka ili wale waliomaliza tuwe tunachukua hatua.

Lakini pia ili kuhakikisha kwamba suala hili halijirudii, tuna uboresha mfumo wetu wa kuwaingiza watumishi katika *payroll* na sasa hivi tunafanya usafishaji wa taarifa za kiutumishi katika taasisi zote za Serikali, tunafanya *data cleaning* wanakuja taasisi moja baada ya nyingine. Baada ya hapo kila taasisi watakuwa wanawaingiza wenyewe wale watumishi, sisi Utumishi tutakuwa tuna *approve* na hazina sasa hivi hawata-*process payroll* tutakuwa tunafanya sisi utumishi ili kupunguza mtawanyiko wa *risk* ya kuwa na watumishi hewa. *(Makofi)*

**MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maslahi na hili jambo ninalolisema. Kwanza naomba radhi naona haya kusemea ndani ya Bunge hili kwa jambo linalonihusu binafsi ni kutokana na kwamba sioni msaada wowote ninaoupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1993 mpaka mwaka 1995 Mheshimiwa Rais Ali Hassan Mwinyi, aliniteua kuwa Naibu Waziri Mkuu. Nilifanya kazi kubwa kama kujenga vituo vya polisi, sungusungu na Watanzania wote wanajua utumishi uliotukuka nilioufanya. Mimi sikufukuzwa kazi, Rais aliondoa tu ile dhamana aliyonipa akanipa kazi nyingine. Ninachoshangaa wenzangu ni kwamba naona hawatambui ule utumishi nilioufanya, hakuna maslahi ninayopata, hakuna posho wala hakuna kitu chochote. Sasa nataka niulize kwa nini nilitumikishwa kwa miaka miwili bila kupata mafao? *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Hoja imeeleweka nani anajibu?

**MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA:** Limeeleweka?Ahsante sana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala lake ni zito na tumelipata kwa mara ya kwanza katika Bunge hili na ni la kisheria zaidi, namuomba Mheshimiwa Mbunge atuachie tulitafakari na tutawasiliana naye kwa majibu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Lakini maslahi ulipata ving'ora vilikuwepo bwana. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi naomba nipate ufafanuzi. Nilipochangia nilisema kwamba kuna maeneo mengi ambayo hayana watendaji. Kazi zimesimama kwa sababu Serikali imesimamisha ajira. Sasa nataka ufafanuzi je, ni kwa namna gani shughuli za maendeleo zitaendelea kama hakuna watendaji katika Halmashauri zetu? Niliseme vijiji vingi havina watendaji wa kata wa vijiji hata hatuna Mkurugenzi. Sasa nilitaka ufafanuzi na mimi hili nitatoa shilingi.

**SPIKA:** Toa shilingi sasa, kama haina tofauti sana isipokuwa tutapiga kura.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nipate ufafanuzi wa watendaji ambao hatuna katika Halmashauri nataka kwanza nipate ufafanuzi nikiridhika sitatoa shilingi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ufafanuzi kwa masuala yake, kwanza katika mchango wake kaweka mambo mawili, kwanza ni la kukaimu Wakuu wa Idara na Wakurugenzi. Napenda nimhakikishie kwamba tutachukua hatua za haraka iwezekanavyo kwa sababu hakuna sababu ya kukaimu. Kama waliopo hawana sifa tutahakikisha tunatoa sehemu nyingine.

Suala la watendaji wa vijiji na kata nalo kwenye Bajeti tumeweka makisio ya kuajiri zaidi ya watumishi 64,000 nadhani watendaji wa vijiji na kata na wenyewe wamo. *(Makofi)*

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu wa maandishi nilizungumzia suala la *TASAF*. Kwa hiyo, ningependa nipate maelezo ya ufafanuzi wa kisera juu ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* kwa hoja zifuatazo, katika kitabu cha hotuba yake Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa 28 ameelezea juu ya jukumu kubwa la *TASAF* ambalo ni kuleta maendeleo endelevu katika ngazi za Vijiji, Shehia na Wilaya. Lakini *TASAF* baada ya kutoa hicho wanachotoa katika miradi yake hujiondoa kabisa. Kwa hiyo, miradi ile huwa inapata matatizo huwa haina msaada wowote. *(Makofi)*

Lakini vile vile kuna suala kubwa la *ceiling* ndogo, katika *TASAF* kuna *ceiling* ndogo sana. Katika sehemu ambayo mimi natoka, kiwango cha juu kabisa ni shilingi milioni 40 kuna mingine shilingi milioni 10, shilingi milioni 15. Lakini kubwa zaidi ni kwamba kuna masharti magumu yaliyowekwa katika mfuko huu wa *TASAF* nadhani na *World Bank* kitu kama hicho. Sasa masharti hayo ni kwamba lazima asilimia 75 ya fedha zile ziende kwenye *labour* na asilimia 25 kwenye vifaa kutokana na kwamba vifaa ni ghali mno. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa swali ni lipi maana dakika tatu siyo nyingi, Mheshimiwa Waziri umeelewa juu ya *TASAF* na wewe pia ni dakika tatu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kifungu anachoulizia hakihusu *TASAF* kwa sababu tumekwishapitisha vifungu vya *TASAF* chini ya *President's Office*, lakini kwa sababu mimi namheshimu sana itabidi maelezo mafupi tu kwamba *TASAF* kwa kawaida inapata miradi yake kutokana na jamii. Iko miradi ya namna mbili, moja ni ya ujenzi wa ki-*facilities* na nyingine ni ya kusaidia jamii kuongeza kipato hasa kwa jamii maskini sana. Kwa hiyo, tunapopeleka fedha pale na ule mradi matumaini ni kwamba ukishakuwa *empower* basi watauendeleza wananchi wenyewe kwa sababu *TASAF* inawa-*empower* inawasaidia halafu inawaacha wapige hatua zaidi kutoka pale.

Sasa mimi sielewi tatizo hasa ni nini kwa sababu kama ni mradi haujamalizika nimesema katika maelezo kwamba tumepeleka fedha katika Halmashauri ya Wilaya ili ule ambao haujamalizika uweze kumaliziwa ndio wananchi waendeleze. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi niliomba tu Mheshimiwa Waziri kupitia Wizara yake aniambie kwamba ni utaratibu gani Ofisi yake itaweka kuhusu dhana au tabia ya unyanyaswaji wa kijinsia kwa watumishi katika maeneo mbalimbali ambapo wamekuwa wakitishiwa ama kupewa adhabu hasa wanawake. Anapokuwa amemkataa ama bosi wake ama anayemzidi katika ofisi yake anaweza akakosa vitu kwa mfano labda kwenda kusoma au kupandishwa cheo au wakati mwingine anapewa ahabu hata ya kuhamishwa kupelekwa maeneo ambayo inasemekana ni adhabu kali. *(Makofi)*

Sasa wamekuwa wakinung'unika chini chini hakuna utaratibu wa kuweza kuripoti kwa sababu masuala haya ni ya siri sana. Je, Ofisi yake inaweka utaratibu gani ili kuweza kukomesha vitendo hivi ambavyo wanawake wengi wamekuwa wakiumia wanashindwa waripoti wapi na wananyanyasika bila hata msaada. Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi kwanza hilo ni kosa na kama mwanamke yeyote labda ananyanyaswa kijinsia na anayemfanyia ni bosi wake, akaripoti kwa bosi wa juu yake, lakini kama anaombwa rushwa ya ngono sasa hivi karibu kila Wilaya TAKUKURU imefika. Lakini hata kama TAKUKURU haipo mimi nina imani tunayo maeneo ya kwenda kulalamika na katika taasisi zote za Serikali tunayo madawati ya malalamiko. Kama wapo anawajua na wananyanyasika kwa sababu hiyo na hakuna mahali pa kwenda kusema tunaomba Mheshimiwa Mbunge atupatie majina. *(Makofi)*

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi niliomba ufafanuzi kuhusu wafanyakazi wa Mashirika ya Umma hususan Shirika la Hifadhi ya Taifa ambapo watumishi hawapewi likizo yao ya kustaafu, inatolewa tu kama likizo ya mwaka ambavyo unafahamu kwamba hivyo ni vitu viwili

tofauti na hiyo ni haki yao ya msingi. Sikupata majibu na naamini wafanyakazi wanasubiri kusikia hili. Ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, likizo ni haki ya msingi ya kila mtumishi na huwa inatolewa kila baada ya miaka miwili na ile likizo ya kustaafu haimo miongoni mwa mtiririko wa likizo ya kawaida. Kwa hiyo, hata kama alishakwenda likizo yake ya kawaida anapokaribia kustaafu ni lazima apewe likizo yake ya kustaafu kwa sababu inamsaidia yeye kufanya maandalizi yake ya kustaafu ikiwa ni pamoja na kukusanya kumbukumbu ambazo zitamsaidia katika kufuatilia mafao yake. Kwa hiyo, ni likizo muhimu wapewe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 104(1) nitaongeza dakika 30 kuanzia 1.45 mpaka saa 2.10 kama hatujafanya basi tutapitisha kwa *guillotine*. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru watumishi wengi waliostaafu wametumikia nchi hii kwa uaminifu mkubwa sana. Lakini pensheni wanayolipwa kwa mwezi bado ni kiwango kidogo nadhani ni shilingi 51,000. Serikali ina kauli gani kuangalia upya kiwango hiki ili waweze kupandishiwa? Lakini sambamba na hilo tupunguze hata muda wa kuwalipa maana sasa hivi tunawalipa miezi sita na mimi niliokutana nao wamenituma niiombe Serikali iangalie walau ipunguze miezi sita walau iwe hata miezi mitatu, kama ni fedha kidogo lakini kwao inawasaidia sana, Serikali ina kauli gani juu ya hili? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, pensheni ndogo sana sana sasa hivi ni kwa wale ambao walistaafu miaka ya nyuma kipindi mishahara ikiwa midogo. Lakini kama Serikali huwa tunajitahidi kuangalia pale hali inaporuhusu kuiangalia na kuboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kupokea kwa kipindi cha miezi sita, sita lilitokana na wenyewe baada ya kuona kwamba kwa kwenda kila mwezi wakilinganisha na kiasi walichokuwa wanakipata walikuwa wanasema kwamba inaishia kwenye nauli. Kwa hiyo, tukaona iwe kwa miezi sita ili angalau kupunguza zile gharama. Lakini hata hivyo kama tutapata ridhaa yao kwamba tupunguze iwe ni miezi mitatu, mitatu sisi kama Serikali hatuna matatizo yoyote. *(Makofi)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Katika mchango wangu nilikuwa nimezungumzia suala la vita ya rushwa na suala mahususi la kashfa ya rada. Sasa katika maelezo yake Waziri amemkosha hapa aliyekuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na mimi sijaridhika na maelezo ya Mheshimiwa Waziri kuhusiana na jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina barua iliyoandikwa na msimamizi wa kesi ya uchunguzi wa kesi hiyo ya rada kutoka London, Uingereza ambayo inasema kwamba katika kipindi cha miezi sita kati ya mwaka 1997/1998 Andrew Chenge alipokea jumla

ya dola za Marekani milioni 1.5 katika *account* yake iliyokuwa katika Kisiwa cha *Jersey*, Uingereza. *(Makofi)*

Mchunguzi huyu anasema kwamba hii *account* ya Chenge, ilipokea hizo fedha kutoka Kampuni inayoitwa *Evans International* inayomilikiwa na mtu anaitwa Shylesh Viflani aliyekuwa *agent* wa *Bae Systems* katika hili sakata la rada, pili mchunguzi huyu huyu anasema kwamba baada ya kupokea hizo fedha, Andrew Chenge ali-*authorise* zitoke *pound* za Kiingereza laki sita ziende kwa mtu anaitwa Idris Rashid aliekuwa Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania katika kipindi ambacho huu mgogoro wa rada ulikuwa unaamuliwa. Sasa hii barua inasema…, nitaondoa shilingi Mheshimiwa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifungu chenyewe anachokizungumzia tumepita, lakini kama anao ushaidi, naomba akabidhi huo ushaidi wake kwa TAKUKURU ili wafanyie kazi au amkabidhi Mheshimiwa Mathias Chikawe au anaweza kupeleka Mahakamani anao uhuru huo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mimi naomba usitoe shilingi kwa sababu hata tungefanyaje hapa dakika tatu kwa kweli hatuwezi kutoa *justice to this thing.* Alivyosema Mheshimiwa Waziri nadhani tufuate huo utaratibu. Ndiyo, yaani umeshasema, sasa ukitoa shilingi ni dakika tatu hizo hizo wala hatuwezi kubishana.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa *record* naomba nitoe shilingi na naomba niseme kwamba hili suala sio dogo kama ambavyo upande wa Serikali unataka kulifanya. Fedha za walipa kodi wa Tanzania zaidi ya shilingi bilioni 40 sijui, zimepotezwa, zimeibiwa kwa kushirikisha Maafisa wa Serikali Shylesh Viflani hakuwa Afisa wa Serikali, hao Waingereza waliotajwa kwamba ndiyo wezi wao sio Maafisa wa Serikali na huu ushaidi wa maandishi unasema kwamba walioshiriki katika ngazi zote za mjadala wa rada alikuwa Andrew Chenge na Idris Rashid, kwa nini hawajashitakiwa? Naondoa shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tumesikia umeondoa, Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivyokuwa natoa maelezo kuhusu suala hili nilisema wazi, tunataka kwenda Mahakamani tukiwa na ushahidi. Sasa nashukuru kama Mheshimiwa anao ushaidi, naomba atuletee twende Mahakamani, hatuwezi kwenda Mahakamani kwa hisia hisia tu, kama anao ushaidi huo anaosema anao, atupe leo tutakwenda Mahakamani kesho, hii ni ahadi nampa. *(Makofi)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii habari ya kana kwamba nina ushaidi ni habari ya kudanganya Watanzania. Hii barua ya *Serious Fraud Office* imeandikwa kwa *Attorney General of the United Republic of Tanzania*, ni ya kwao, wanayo. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya Mheshimiwa Tundu Lissu ya kutoa shilingi ilikataliwa na Bunge)*

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mimi ningependa Waziri atoe maelezo ya ziada kuhusu watumishi wa Vyuo Vikuu vya Dar es Salaam na Sokoine waliokuwa chini ya utaratibu wa *SSS.* Labda kwa taarifa tu kwa Wabunge ambao hawafahamu utaratibu huu. Utaratibu huu ulikuwepo kabla ya kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977, kwa mujibu wa utaratibu huu mtumishi anapostaafu anapata malipo ya mkupuo mmoja tu, hapati pensheni ya kila mwezi, kulikuwepo na majadiliano kwa muda mrefu baina ya Vyama vya Walimu, Vyuo Vikuu na Serikali. Serikali ikawa inaahirisha ahirisha uamuzi toka miaka ya 1980 jambo hili limekuwa likijadiliwa, watu wamekuwa wakistaafu, wengine wanapata shilingi 300,000 tu kwa mkupuo mmoja na hiyo imetoka. Naomba Waziri ajibu vizuri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani nilishamjibu tena kwa kirefu sana kwamba hao wahadhiri walikuwa katika utaratibu huo ambao ulikuwa chini ya Chuo Kikuu cha Afrika Mashariki na baada ya kuvunjika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Serikali ilianzisha Mfuko wa *PPF* ambapo waliombwa wajiunge wakakataa na kwamba kwa wakati huo ilikuwa kule kunaonekana nadhani kulikuwa kuzuri kuliko ilivyokuwa *PPF*. Baada ya kuonekana kwamba kule kunayumba waliomba kuingizwa *PPF* na Serikali kwa sababu kwa kipindi chote wao walikuwa hawajaichangia *PPF,* kwa hiyo Serikali ilikuwa inalifanyia kazi na wao na Mheshimiwa anajua kwamba Mdhibiti amekwenda Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, amezungumza nao na katika kulimaliza hilo, Serikali imekubali kutoa shilingi bilioni tisa kuchangia *PPF* na hao wahadhiri na wenyewe kile kilichopo kwenye *SSS* kitaingizwa kwenye Mfuko wa *PPF* kwa wale ambao wapo kuanzia Machi, 2011 na wale ambao wamestaafu nimesema iachwe Serikali ifanye tathmini ione ni kwa kiasi gani inaweza ikawasaidia kwa sababu walishastaafu na walishapewa mkupuo wao. *(Makofi)*

Hata mimi mwenyewe ninaezungumza nilikuwa kwenye Mfuko wa *LAPF* ukiwa *Provident Fund*, nimeondoka na shilingi milioni tatu wakati naingia kwenye siasa, sina pensheni yoyote ninayopokea. Kwa hiyo, mambo mengine ni huruma lakini walioanza kuanzia mwaka 2007 kama sikosei, Serikali imeubadilisha ule mfuko kuwa pensheni kwa kuchangia shilingi bilioni 103 kwa kipindi cha miaka kumi, lakini haikutubeba sisi ambao tulikuwa kule nyuma. Kwa hiyo, kutokana na hali ilivyo naomba tuiachie Serikali iangalie huruma na uwezekano wa kulifanyia kazi, tunafanya tathmini. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza nataka ufafanuzi hasa kuhusu ajira za Taasisi za Muungano kwa miaka mingi ambazo tunazikosa na tukizipata chache mno na hakuna ofisi yoyote Zanzibar hadi leo,

Waziri utatueleza nini na hawa vijana ambao siku zote wanaulizwa lazima uzoefu, uzoefu vijana wetu waliomaliza shule, la kwanza.

La pili, urasimishaji haujafanyika Zanzibar hata mara moja, ni wakati mmoja tu kulikuwa na *attempt* ya kujenga Ofisi Kiungoni katika Shehia ya Kiungoni na mapaka leo jengo hilo halijafikia popote, tunataka tuelezwe MKURABITA una mpango gani katika Bajeti hii katika kufanya shughuli zake Zanzibar na hasa katika Jimbo la Mkanyageni, naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na la Sekretarieti ya Ajira aliloanza nalo kwamba kama nilivyosema kwenye majibu yangu tutafungua ofisi moja kila mkoa na kwa upande wa Zanzibar tayari Katibu wa Sekretarieti alishakwenda kuzungumza na wenzetu wa Zanzibar kwa sababu tulishakubaliana katika vikao vyetu vya Muungano kufungua ofisi na kwa kuanzia tumeomba watutafutie ofisi na kama watashindwa watutafutie japo ya kukodi, hilo linaanza haraka na kwa sasa hivi usaili tunaenda kufanyia kule kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uzoefu. Kwa nafasi zote za kuanzia hakuna mtu anayeulizwa uzoefu, tatizo kwa vijana wetu akimaliza *degree* ya kwanza akiunganisha na *Masters* basi akiona nafasi ya Mkurugenzi anaomba, akiona nafasi ya Mwanasheria Mwandamizi anaomba, Afisa Daktari aliye *specialize* au mwandamizi anaomba, wakati nafasi hizo ndizo zinazohitaji uzoefu. La MKURABITA naomba Mheshimiwa Wasira amalizie. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):** Meshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyoelezwa katika hotuba ya Ofisi ya Rais Utumishi ambaye ndiye aliye-*present issue* za MKURABITA, tulisema kwamba MKURABITA inafanya kazi katika sehemu zote za Muungano. Kwa hiyo, katika Bara kuna Wilaya kama tano ambazo zitaingizwa kwenye programu ya mwaka unaokuja. Lakini katika eneo la Zanzibar kutakuwa na Wilaya mbili na zimetajwa kwenye ile hotuba, Pemba imo na Mjini Unguja. Sasa kama anazungumza habari ya Jimbo lake, tutafika huko baadae lakini kwa mwaka huu hatufiki kwa sababu hata Majimbo ya huku Bara hatufiki yote umesikia tunaeleza. Kwa hiyo, tutakwenda pole pole, tutafika mpaka Mkanyageni. *(Makofi)*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi pamoja na pongezi nyingi nilizompa Mheshimiwa Hawa Ghasia kwa kazi nzuri, nilikuwa nimehoji suala la watumishi wengi kupoteza kumbukumbu zao maofisini hatimaye kusababisha kupoteza malipo yao ama kuchelewa kupata malipo yao, niliomba dawa itolewe katika hili ili likome.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kupoteza kumbukumbu na kuchelewesha kupata mafao, kama nilivyosema kwamba tunauboresha mfumo wetu wa malipo na mishahara na mfumo huu sasa hivi hata wale walioajiriwa tunawaingiza upya

wote na unaweka viambatisho vyote kama *attachment,* unaweka barua yako ya kuajiriwa, ya kuthibitishwa kazini, wategemezi wako, warithi wako, kwa hiyo, ni mategemeo yetu mtumishi akistaafu hata kama amepoteza barua zake kumbukumbu zote sisi tutakuwa nazo, lakini si hivyo tu kama mtumishi amestaafu na amepoteza baadhi ya kumbukumbu chache ambazo zinamfanya asipate mafao yake, tunao utaratibu wa kumuomba Mheshimiwa Rais kupitia kwangu kama mwajiri wake anaweza kuomba kwetu na sisi tukamuomba tukamuomba Mheshimiwa Rais asamehe baadhi ya vipengele ili mstaafu yule aweze kupata pensheni yake bila ya kuwepo baadhi ya viambatisho ambavyo vinahitajika. Naomba tutumie fursa hii ili kuwaondolea kero wastaafu. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN L. B. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Katika mchango wangu pamoja na mambo mengi, lakini inaniruhusu nizungumzie jambo moja kwamba kuna matatizo mengi sana kuhusu walimu wapya na walioajiriwa muda mrefu. Wengine kutokupandishwa madaraja kwa hiyo muda mwingi wanatumia kufuatilia mafao yao na kusababisha kutokufundisha darasani na matokeo mabaya ya watoto wanaomaliza kidato cha nne. Sasa hivi wana mpango ina maana wanataka kufanya mgomo kwenye chama chao, wana madai ya shilingi bilioni 13, naomba anithibitishie Waziri je, kwenye Bajeti hii hizo hela za walimu zimetengwa? Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la upandishwaji wa vyeo, tulivyoingia kipindi cha miaka mitano ni eneo ambalo tumelishughulikia sana kuhakikisha kwamba walimu wote ambao walirundikana katika chuo kimoja kuhakikisha kwamba tunawarekebishia madaraja yao na kuwapanga kwa mujibu wa miundo yao. Sasa hivi malalamiko makubwa yako kwa upande wa sekondari na mwaka jana tuliziagiza Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha kwamba wanafanya zoezi maalum za kuwapandisha vyeo. Bahati mbaya ni wachache sana tuliwashughulikia kwa sababu ma-*file* yao yalikuwa hayajapelekwa kwenye mamlaka nyingi za Serikali za Mitaa. Mwaka huu tuna walimu wengi sana wa sekondari ambao watapandishwa vyeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madai ya watumishi na walimu, kwanza sijui Mheshimiwa hizo takwimu amezipata wapi kwa sababu mwaka 2009 tulihakikisha madai yote ya walimu na watumishi wengine tunayalipa na kusema kwamba tusizalishe madeni mengine mapya na madai yote ya watumishi ambayo bado hayajalipwa yako kwenye Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuna kawaida ya kuzungumza na wenzetu, viongozi wa vyama vya wafanyakazi, suala la mgomo ni la mwisho sana baada ya kutoa *notice* ya miezi miwili na mpaka sasa hivi sina *notice*, sasa Mheshimiwa Susan naomba nikushauri kuwa walimu wana utaratibu wao wa kugoma wana utaratibu wao wa maandamano mpaka sasa hivi sina *notice,* sasa naomba usiwashawishi kugoma, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Je, sasa Serikali inaweza kuwatajia Watanzania ni nani aliye andaa Mkataba wa kuingia kwenye

ununuzi wa rada na ni nani ambaye aliweka saini katika ununuzi wa rada ili Watanzania wamjue na ashitakiwe katika mahakama zetu kwa uzembe kazini, uhujumu uchumi na kutia hasara Serikali kama ambavyo tumeona katika kesi za Daniel Yona, Basil Mramba pamoja na Gray Mgonja ambao wanashitakiwa kwa uzembe kazini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, kama swali limezungumzwa katika vifungu halirudiwi tena, hili limeshazungumzwa. Mheshimiwa Mnyika. *(Makofi)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika mchango wangu nilizungumza kuhusu rushwa kubwa kubwa na masuala ya TAKUKURU, sasa katika majibu ya Waziri amezungumza kwamba tuzipuuze taarifa za kwenye mitandao kama *Wikileaks* na ripoti nyingine, lakini mimi nina gazeti hapa la ndani ya Tanzania na nimesikitishwa sana na kauli ya Waziri kuhusiana na gazeti la Mwananachi, lakini gazeti hili ni la *This Day* sio la Mwananchi, linasema; *"UK reports slams Lowassa*, *Rostam highlights of involvement of the two politicians in Richmond's and several other dubious deals"* na ndani ya ripoti kunazungumzwa kuhusu *Richmond* pamoja na Kagoda na hii ni ripoti ya wataalamu ambayo ilifadhiliwa na Shirika la Maendeleo ya Uingereza *(DFID)* na ripoti ambayo imekwishaanza kujitokeza kuwa *public*. Ndani ya ripoti hiyo wanasema moja ya kikwazo pamoja yale ambayo yalizungumzwa kuhusu *Wikileaks* ya kupeleka kesi hizi Mahakamni ni TAKUKURU kuzuiwa na Sheria, naomba kuondoa shilingi katika jambo hili nipewe maelezo ya kina kama maelezo hayataridhisha. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumzia masuala mawili, masuala ya Kagoda ambayo nataka nimuhakikishie TAKUKURU inaendelea kuchunguza suala la Kagoda mpaka sasa, suala linalo-*involve* mambo ya ndani na nje, suala la *Richmond*, Bunge lako Tukufu lilishamaliza jambo hilo, lilitoa maelekezo na yametekelezwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya toa hiyo shilingi yako.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Lakini naomba kuondoa shilingi katika jambo hili kwa mambo mawili. La kwanza, ripoti ya wataalam inasema kwamba TAKUKURU inalalamika vilevile moja ya kikwazo cha wao kupeleka *cases* Mahakamani ni Ofisi ya *DDP* kwamba ni lazima *DDP* atoe kibali na kadhalika. Kwa hiyo, hapa kuna hoja kwamba sheria inapaswa kubadilishwa ili kutoa mamlaka ya moja kwa moja ya TAKUKURU kuweza kushitaki kama ilivyo kwa Katiba mpya ya Kenya, ilivyo kwa sheria za Ghana, Kenya, Zambia na Ethiopia. Sasa nataka kauli ya Serikali kama sasa iko tayari kurekebisha sheria ili kuipa mamlaka TAKUKURU kushitaki moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo zito sana kwa Taifa kwa sababu mimi nina taarifa kwamba kutokana na kesi ile ya *EPA* kulikuwa kuna mpango kazi kati ya Serikali na Wahisani, na sasa hivi Wahisani wanalalamika kuhusiana na kesi hizi na kuna uwezekano wakapunguza kusaidia msaada wa Bajeti kwa sababu hii. Kwa hiyo,

ningeomba kauli ya Serikali kwa ajili ya kuwawezesha Watanzania kupata pesa za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba ufafanuzi kutoka Serikalini kuhusu jambo hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Mnyika kwa kusema alivyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nadhani tunayo fursa nzuri sana iliyopatikana kutokana na jinsi Serikali ilivyoamua kwamba kuna mambo mengi sana yanatakiwa yashughulikiwe katika Katiba Mpya. Huo ndiyo mchakato ambao utawezesha mambo mengi sana kuyaweka sawa. Kwa kuheshimu muda wa Bunge ningewasihi ambao wana masuala kama hayo wangetulia kwanza, tutapata fursa hiyo na nadhani wote kwa pamoja kama Taifa bila kujali vyama tutaweza kufanya mapendekezo yatakayozaa sheria na taratibu zinazoweza kuwa bora zaidi na kuzuia baadhi ya mambo ambayo yametuletea shida. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, dakika mbili.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Nashukuru kwa maelezo ya ufafanuzi ya Mheshimiwa Samuel Sitta. Mheshimiwa Waziri na naelewa na natambua umuhimu wa mchakato wa Katiba na kweli kwamba Katiba itawezesha mfumo wa utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wakati tukisubiri Katiba kuna hatua ambazo tunapaswa kuzifanya za kawaida kabisa, mathalani tunajadili hotuba ya Rais sasa hivi, tunajua kwamba Rais aliwahi kulihutubia Bunge kuhusu hili suala la Kagoda na *EPA.* Lakini mpaka leo ile hotuba ya Rais iliporudishwa Ikulu kukarabatiwa mpaka leo haijaletwa tena Bungeni. *(Makofi)*

Mimi ningeshauri kwamba hotuba ile iletwe lakini twende sambamba na kuangalia kwa Sheria zilizopo hivi sasa tuna uwezo wa kufanya marekebisho ya Sheria ya TAKUKURU na Sheria iliyompa mamlaka *DPP* bado tukafanya kesi hizi zikapelekwa mahakamani mapema zaidi kabla ya kuwa na Katiba mpya mwaka 2013 au 2014. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya Mheshimiwa John Mnyika ya kutoa shilingi ilikataliwa na Bunge)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunapoweka Siwa hatuzungumzi, tunasimama *still.* Siyo mnaanza kuzungumza. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu litengue Kanuni zake kwa mujibu wa Kanuni ya 28(v) ili kuwezesha kuongeza muda wa dakika 30 ili kukamilisha kazi iliyobaki.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Bunge liliafiki utekelezwaji wa kutengua Kanuni tajwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kama tulivyosema bahati yetu mbaya kwamba Wizara kubwa kama hii tulikuwa na dakika 45 kupitia vifungu kwa sababu ya ukubwa wa Wizara yenyewe. Sasa mimi hoja hii tunaomba muda wa nusu saa kusudi tuingie kwenye vifungu vile vya maendeleo na sehemu nyingine ambapo mnaweza kuhoji na hii nusu saa ninayoomba ni kuanzia saa 2.15 kwa hiyo itakwenda mpaka saa 2.45 usiku yaani nusu saa baada ya hapa. Kwa sababu sasa hivi tunatumia ule muda ninaoongeza mimi kwa mujibu wa Kanuni ya 104. Kwa hiyo, ziliongezwa dakika 30 ili tuweze kumaliza vifungu vinavyotakiwa. *(Makofi)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**FUNGU 32 – OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA**

Kifungu 1001 **–** *Administration and*
*HR Mgt. Division*..................................Shs. 9,048,230,060
Kifungu 1002 **–** *Finance and Accounts Unit*…………Shs. 205,827,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1003 **–** *Information, Edu. and Comm.* ....…Shs. 572,788,946

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *sub-vote 1003* kifungu kidogo *220500 military supplies and services.* Natambua kwamba masuala ya *military* yanakuwa ama kwenye Jeshi ama kwenye Wizara ya Afya kuendana na masuala mazima ya kampeni labda wana kampeni fulani fulani. Sasa nilikuwa naomba kujua kifungu hiki hapa kinahusu nini hasa. Ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kinahusu ukodishaji wa maturubai ambayo huwa tunatumia wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma na maturubai *SS code* inapatikana kwenye jeshi ambao ni *tent.* Kwa hiyo, hiki ni kifungu ambacho kinapatikana kwenye jeshi lakini matumizi yetu lazima yaende kwa *S code.* Kwa hiyo, kwa vifungu vyetu sisi tusingeweza kuichukua. Kwa hiyo, ni hivyo Mheshimiwa Mbunge.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1004 – *Procurement Management Unit*……Shs. 214,551,000
Kifungu 1005 – *Internal Audit Unit*…….........…………Shs. 105,984,000
Kifungu 1006 – *Planning Division*…….........…………Shs. 331,577,000
Kifungu 2001 – *Policy Development Division*………Shs. 434,477,000
Kifungu 2002 - *Management Services Division*……Shs. 324,579,000
Kifungu 2003 – *Establishment Division*………………Shs. 723,016,000
Kifungu 2004 – *Ethic Promotion Division*………………Shs. 153,154,994
Kifungu 3001 – *Human Resources Dev. Division*…Shs. 2,375,525,000
Kifungu 3004 – *Development Mgt. Unit*………………Shs. 141,359,000
Kifungu 4002 – *Mgt. Information System Division*…Shs. 743,619,000
Kifungu 4003 – *Records and Archives Division*………Shs. 647,489,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 33 – SEKRETARIETI YA MAADILI**

Kifungu 1001 – *Administration and General*…………Shs. 851,135,200
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts*………………Shs. 188,287,100

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1003 - *Policy and Planning* ………………Shs. 1,047,467,200

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi niliomba ufafanuzi kuhusiana na kupanda kwa kiwango kikubwa kwa kasma za posho kwenye Bajeti ya Sekretarieti ya Maadili na Viongozi wa Umma. Sasa

nazungumzia *vote* hiyo ya *33 programme 10 sub-vote 1003* kasma *210300 Personal Allowances (Non-Discretionary)* ambayo inaonyesha kwamba mwaka wa fedha 2009/2010 ilikuwa shilingi milioni 40 ikaja ika-*shoot* mpaka ikapungua ikafikia shilingi milioni 28 halafu imeongezeka ghafla kutoka shilingi milioni 28 mpaka shilingi milioni 237. Ningeomba maelezo tu ni kwa nini kiwango hiki cha posho kimeongezeka kwa kiwango hiki? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la posho katika Sekretarieti ya Maadili ni kutokana na mambo mawili, kwanza ongezeko la wastaafu wamekuwa wengi. Tumefungua ofisi sehemu mbalimbali na *of course* ongezeko la mishahara, kupandisha stahili za watu ambao wanastahili kulipwa posho. Kwa hiyo, ongezeko hili ni kutokana na tu wa wingi wa *staff* na haki zao. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Kanuni inakataa kurudia jambo ambalo limezungumzwa nilikuwa na jambo ambalo Mheshimiwa Mnyika amelizungumza.

**MWENYEKITI:** Ahaa, basi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1004 – *Information, Edu. and Comm.*…………Shs. 93,214,000
Kifungu 1005 – *Procurement and Mgt. Unit*……………Shs. 80,879,500
Kifungu 1006 – *Internal Audit* ................………………Shs. 108,239,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 66 – OFISI YA RAIS – TUME YA MIPANGO**

Kifungu 1001 – *Admn and HR Mgt. Division*...........Shs. 1,276,940,000
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts*………………Shs. 219,350,000
Kifungu 1003 - *Planning and Monitoring Division*……Shs. 324,501,000
Kifungu 1004 – *Information, Edu. and Comm. Unit*…Shs. 280,982,000
Kifungu 1005 – *Internal Audit Unit* ........………………Shs. 186,421,000
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*…Shs. 165,891,000
Kifungu 1007 – *Library and Documentary Unit*……Shs. 121,693,000
Kifungu 1008 – *Management Information System*…Shs. 192,476,000
Kifungu 2001 – *Micro Economy Cluster*……………Shs. 1,166,460,000
Kifungu 2002 – *Productive Sector Cluster*……………Shs. 845,765,000
Kifungu 2003 – *Infrastructure and Services Cluster*…Shs. 812,480,000
Kifungu 2004 – *Social Service and Demographics Cluster*……...…………Shs. 817,300,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2005 – *International Trade and Econ. Relations C*.................................…Shs. 779,300,000

**MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kifungu kidogo *220900 Training -Foreign.* Hapa katika kazi za *international trade and economic relations* kwa nini katika miaka hii iliyopita kulikuwa na umuhimu wa kusafiri na kwenda kufuata uzoefu sehemu zingine. Hapa sasa hivi hawatataka kwa ajili ya *inter change relationship* na *understanding* na sehemu za nje. Kwa nini wakati bado biashara hiyo inahusika?

**MWENYEKITI:** Kuna *zero money* kwamba hii hakuna haja. Umeiona Mheshimiwa Waziri wa Nchi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo fedha zipo kwenye kifungu cha 221100 ambacho ni *travelling out of the country,* watakwenda kufanya mafunzo ya namna hiyo. Ni *study tour* zaidi. Kwa hiyo, *covered* na hicho kifungu.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 67 – SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA**

Kifungu 1001 – *Admin and HR Mgt. Division*….......Shs. 1,336,318,000

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nilikuwa nataka nipate ufafanuzi katika kifungu 220700 kuna *rent expenses* kwa gharama ya shilingi milioni 300.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi hii sasa hivi wapo pale Magogoni tunabanana katika zile Ofisi tulizokuwa nazo na hazitoshi. Sasa hivi tunategemea waongeze watumishi wengi zaidi. Kwa hiyo, tunategemea watapanga na ni matarajio yetu kwamba si mikoa yote watafanikiwa kupata Ofisi za Serikali. Kwa hiyo, tunategemea pia na kwenyewe watapanga, ndiyo maana kiwango hiki kimekuwa kikubwa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts*………………Shs. 306,549,000
Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation*.............................................…Shs. 101,300,000

Kifungu 1004 – *Edu., Information and Comm.*………Shs. 26,025,000
Kifungu 1005 – *Legal Services*……..................…………Shs. 21,021,000
Kifungu 1006 – *Procurement Management*…………Shs. 150,761,000
Kifungu 1007 – *Mgt. Information Systems*……………Shs. 140,947,000
Kifungu 1008 – *Internal Audit*……………...................……Shs. 21,192,000
Kifungu 2001 – *Recruitment Mgt. Division*……………Shs. 684,041,000
Kifungu 2002 – *Quality Control*……..............…………Shs. 151,496,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 94 – TUME YA UTUMISHI WA UMMA**

Kifungu 1001 – *Administration and General*………Shs. 2,306,713,000
Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation Unit*……..................………… Shs. 300,094,000
Kifungu 2001 – *Civil Service*……………...................……Shs. 226,974,000
Kifungu 2002 – *Local Government Service*…………Shs. 274,023,000
Kifungu 2003 – *Teachers" Service*……………......……Shs. 4,760,914,000
Kifungu 2004 – *Fire and Immigration Service*………Shs. 163,066,000
Kifungu 2005 - *Health Service*……..............…………Shs. 183,223,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 30 - OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA BARAZA LA MAWAZIRI**

Kifungu 1003 - *Policy and Planning* ……….......………Shs. 66,769,353,00

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan Lyimo na Mheshimiwa John Mnyika. Sasa muangalie, akisema mwenzio kifungu, wewe hatukuruhusu.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kifungu kidogo 6339. Wakati nachangia hotuba ya Waziri Mkuu, nilihoji matumizi makubwa ya ukarabati wa Ikulu ya Rais, lakini naamini sasa ipo katika kitabu hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitoa takwimu kuanzia miaka 10 iliyopita...

**MWENYEKITI:** Dakika tatu tu unazo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukarabati umetumia takribani shilingi bilioni 53 na mwaka jana tu Bunge lako Tukufu lilipitisha shilingi bilioni 7.2 lakini mwaka huu wanaomba shilingi bilioni 10.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu ni kwamba nataka nijue *value for money*, mwaka jana walikarabati kitu gani na mwaka huu ni kwa nini wanaomba fedha nyingi kiasi hicho? Lakini kibaya zaidi fedha zote zinatoka ndani! Nilikuwa naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, *GFS Code* hii inaandikwa Ukarabati wa Ikulu. Ukarabati wa Ikulu ulianza na ulikuwa na awamu tatu, ulianza mwaka 2001, jengo lenyewe la Ikulu ukaisha mwaka 2006. Baada ya hapo ukarabati umeendelea wa Ikulu ndogo ndogo zote pamoja na ya Chamwino hapa Dodoma, Tanga, Nachingwea, Tabora, Arusha, Moshi, Mwanza na Shinyanga, zote hizi zinakarabatiwa na zinaingia kwenye *Code* hii moja. Kwa mwaka huu pamoja na hii ni majengo mapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Cabinet Secretariat* sasa hivi inajengwa Ofisi mpya. Hapo hapo kunajengwa pia Jumba la Mkutano pale Ikulu, hakuna vyumba vya kutosha vya Mkutano kwa hiyo linajengwa lingine. Shilingi bilioni 10 hizi ni kwa ajili hiyo na bado zitaendelea kwa sababu bado hazijakamilika na bado hali ya Ikulu hizi ndogo ndogo nyingine si nzuri sana kwa hiyo, itabidi tuendelee. Kwa hiyo, sio jengo lile moja, ni Ikulu kwa ujumla wake.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru ni kasma katika Kifungu hicho, kasma ya 4921, *Property and Business Formalisation Program* ambayo naamini ndio ya MKURABITA. Katika kuchangia nilihoji ni kwa nini kiwango cha MKURABITA cha Bajeti kimeshuka kutoka shilingi bilioni sita mwaka wa fedha uliopita mpaka shilingi bilioni tatu mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikupewa ufafanuzi na hili linaathiri utekelezaji wa mpango wa MKURABITA na wakati ule nilisema kwamba mpango kwa Dar es Salaam, umetajwa mtaa mmoja tu wa Kimara Baruti sio hata Kata kwa hiyo, pesa hizi ni kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sitapewa ufafanuzi wa kutosha, nitaomba nitumie Kifungu cha 102 cha Kanuni, unipe fursa niweze kutoa hoja tufanye *reallocation* kutoka kwenye Fungu hilo hilo la Ukarabati wa Ikulu ambalo limeongezeka kwa shilingi bilioni tatu ili lirudi fungu la zamani la shilingi bilioni sita ili tuweze kupima ardhi na kurasimisha mali za wanyonge wengi zaidi ambao inaweza kuwasaidia kukwamua umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba ufafanuzi wa kina kutoka kwenye Serikali na hili linawezekana kabisa kuhamisha hicho kiwango cha shilingi bilioni tatu, kwa sababu kwa maelezo ya Waziri, inaonesha tunaendelea na ujenzi mwingi sana Dar es Salaam wakati CCM imesema inataka kuhamia Dodoma.

Sasa kwa maneno mengine basi mimi sioni kama kuna ulazima wa kuongeza kutoka shilingi bilioni saba za mwaka jana za Ukarabati wa Ikulu mpaka shilingi bilioni 10 nyingine wakati ambapo sehemu kubwa ya pesa hizi zinatumika Dar es Salaam.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, MKURABITA kwa takwimu nilizonazo ipo sehemu mbili. Katika *Vote 30* ambayo tumeshaipitisha ipo katika Kifungu 270850, ambayo kuna shilingi 3,170,554,700 na pia ipo katika hiyo ya Maendeleo ambayo kuna shilingi bilioni tatu. Ukijumlisha unapata takribani shilingi bilioni 6.6 hivi, kwa hiyo hakuna tofauti sana na mwaka jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nahisi kuwa Mheshimiwa amechanganya vitu vingi sasa hata sijui, anataka hapo hapo tufanye *reallocation,* hapo hapo tukajenge Ubungo, sina hakika! Lakini nasema kwa mwaka huu MKURABITA angalau inakuwa sasa hivi na zaidi ya shilingi bilioni sita. *(Makofi)*

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu, Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 102...

**MWENYEKITI:** Aah, hukutoa hoja, ulikuwa unatuambia unataka kufanya hivyo na...

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilinde!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, naomba tukae tuelewane. Lengo lako lilikuwa kwamba ikiwezekana uhamishe hela nyingine upeleke huku. Tumeshaambiwa kwamba katika *Vote 30* zipo na hapa zipo, kwa hiyo, zimeongezeka zipo shilingi bilioni sita, ndio maana tunaendelea. Kifungu hiki nimeshahoji, tunaendelea.

**FUNGU 32 - OFISI YA RAIS – MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA**

Kifungu 1001 - *Adminstration and Mgt. Division*……Shs. 2,886,800,000
Kifungu 1003 - *Information, Edu. and Comm.*……….Shs. 100,000,000
Kifungu 1004 - *Procurement Mgt. Unit*......…………….Shs. 50,000,000
Kifungu 1006 - *Planning Division* …...........…………Shs. 1,797,000,000
Kifungu 2001 - *Policy Dev. Division* …….......……….Shs. 1,336,955,000
Kifungu 2002 - *Mgt. Services Division*……..........……….Shs. 700,000,000
Kifungu 2004 - *Ethic Promotion Division* …………….Shs. 170,000,000
Kifungu 3001 - *Human Resourses Dev. Division*…….Shs. 1,612,000,000
Kifungu 3004 - *Diversity Mgt. Unit* …............…………Shs. 380,000,000
Kifungu 4002 - *Mgt. Information System Division*….Shs. 2,071,470,000
Kifungu 4003 - *Records And Archives Division*…….Shs. 6,234,045,000

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 33 - OFISI YA RAIS – SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI**

Kifungu 1001 - *Adminstration And General*....……….Shs. 910,000,000

**FUNGU 66 - OFISI YA RAIS – TUME YA MIPANGO**

Kifungu 1003 - *Planning And Monitoring Division*…….Shs. 200,000,000

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa John Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika mchango wangu niliomba ufafanuzi kuhusiana na *Sub Vote* hiyo, Kasma ya 650 – *UNDP Support,* shilingi 200,000,000 kwa ajili ya Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliomba ufafanuzi kuhusu mambo mawili, kwanza inaonesha pesa za maendeleo, kwa upande wa mipango inategemea pesa za wahisani peke yake, kwa hiyo, ningeomba maelezo ni kwa nini hatujapanga pesa za ndani kwa ajili ya Tume ya Mipango?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa Serikali itatoa ufafanuzi kama ule wa mwanzo wa kwamba pesa zipo kwenye mafungu mengine. Ieleweke yale mafungu ni mafungu ya Matumizi ya Kawaida ya mishahara, posho na kadhalika, sio ya maendeleo, hapa tunazungumzia Fungu la Maendeleo. Lakini la pili…

**MWENYEKITI :** Ngoja kwanza. Ikiwa kwenye shughuli za maendeleo, hatu-*discuss policy.* Wewe unauliza hizi shilingi 200,000,000 ni za kazi gani ? Ndio swali lenyewe, hatujadili hapa.

**MHE. JOHN J. MNYIKA :** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi ni ya kazi gani ?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka ufafanuzi vilevile kama katika kuzitumia hizo shilingi 200,000,000 kwa kazi wanayoifanya, kama Tume ya Mipango itahusisha wataalamu wa Vyuo Vikuu vyenye *element* ya Mipango kama Chuo cha Mipango Dodoma na Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, katika kufanya kazi yake ya utafiti na utekelezaji wa kazi ya Tume ya Mipango, hilo naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mradi maalum wa Tume ya Mipango, unagharamiwa na fedha kutoka nje kwa ajili ya kushughulikia masuala ya ongezeko la watu *(population).* Ni hiyo peke yake tu ndio shughuli yenyewe.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu, kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Mheshimiwa Mtoa Hoja, Taarifa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo basi, naliomba Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naafiki! *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Utawala Bora na Ofisi ya Rais – Uhusiano na Uratibu kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Mawaziri wa Nchi Ofisi ya Rais wote waliohusika katika kazi hii. Lakini pia niwapongeze Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu mmefanya kazi vile inavyotakiwa na ninadhani kwa kadri tutakavyoendelea basi mtafanya vizuri zaidi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa jioni hii nawashukuru kwa kukubali kuongeza muda kwa sababu tumefikia angalau sehemu ile tuliyokuwa tunataka tupitie kuliko kufanya *guillotine.* Tunaendelea kutathmini huu utaratibu wetu tuone kama tunakwenda nao vizuri namna gani, lakini mpaka hivi sasa nashukuru angalau tumefikia kupitisha vifungu kimoja hadi kingine. *(Makofi)*

Kwa kuwa, sina matangazo mengine, napenda kuahirisha Kikao hiki mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 2.43 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano,*
*Tarehe 6 Julai, 2011 saa tatu asubuhi)*